

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 5 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MHE. REGIA E. MTEMA - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA: Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Kazi na Ajira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 373

Kuboreshwa kwa Maslahi ya Madiwani

MHE. FELISTER A. BURA aliuliza:-

Madiwani ni nguzo muhimu katika kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na nia ya Serikali ni kuboresha maslahi ya Madiwani il waweze kutimiza wajibu wao ipasavyo:-

Je, ni lini maslahi ya Madiwani yataboreshwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) aliibusu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Waheshimiwa Madiwani ni nguzo muhimu katika kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa kuzingatia Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi (*D by D*), majukumu ya Waheshimiwa Madiwani ya kusimamia maendeleo ya Wananchi yameongezeka hivyo Serikali inatambua umuhimu wao na

majukumu makubwa waliyonayo. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imekuwa ikiboresha posho na stahili mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Waheshimiwa Madiwani wanalipwa posho ya shilingi 120,000 kutoka shilingi 60,000 ya awali, ambayo hata hivyo haitoshelezi. Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anahitimisha hoja ya Bajeti yake ya Mwaka 2011/2012, alieleza kuwa, kimsingi, Serikali inakubali kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani na itayafanyia kazi na kuyazingatia wakati wa kufanya Mapitio ya Bajeti ya nusu mwaka (*Mid - Year Review*). Aidha, kutokana na ukweli kwamba, Bajeti ya Mwaka 2011/2012 imeshajadiliwa na kupertishwa, utekelezaji wa maamuzi hayo utakuwa mgumu kufanyika katika mwaka huu wa fedha. Hivyo, tunategemea kwamba, utekelezaji utanza Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba, Waheshimiwa Madiwani, wanalipwa kiasi kidogo sana cha fedha; na kwa kuwa kazi wanayofanya ni kubwa ya kufuatilia maendeleo ya Wananchi katika maeneo yao; na kwa kuwa wanapofuatilia maendeleo hayo wanatembea kwa miguu katika vijiji ambavyo viko ndani ya Kata zao:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuwadhamini Waheshimiwa Madiwani katika mikopo ya vyombo vya usafiri?

(b) Kwa kuwa Bajeti ya Serikali hutegemea makusanyo ya kodi na mambo mengine na katika mwaka huu bajeti imeshapita lakini kuna *Mid-Year Review* ya Bajeti ya Serikali; je, Serikali iko tayari kuongeza posho kidogo baada ya *review* ya bajeti katikati ya mwaka huu? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala analolizungumza la vyombo vya usafiri ni jambo la msingi kwa maana ya ufuatilaji na Kata nydingine ni kubwa, unakuta Diwani hawezi kwenda kokote kama alivyoeleza hapa. Ninachosema ni kwamba, wakati tunapoipitia maelekezo tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, hatuangalii suala la posho tu, ametoa maelekezo kwamba, tuangalie pia vyombo vya usafiri na mambo mengine ambayo yanahu maslahi ya Madiwani.

Mheshimiwa Mbunge pia amezungumzia makusanyo katika Halmashauri kwa maana ya *own source*. Sana sana ambalo linakuja katika mazungumzo wakati tunapoandaa mpango huu ni kuona jinsi ambavyo Halmashauri zenyewe zinaweza zikawadhamini Madiwani ili waweze kuchukua mikopo katika vyombo vya fedha; ndicho kinachozungumzwa hapa. Zipo Halmashauri ambazo zimeanza kujaribu kufanya hilo.

Kwa hiyo, kama anavyosema, tunapoandaa sasa ile mipango ambayo tunafikiri tutaipitisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili nalo tutaliangalia tuone jinsi ambavyo hawa Waheshimiwa Madiwani wetu wanaweza wakasaidiwa kwa njia hiyo niliyoizungumza ya kuweza kupata vyombo vya usafiri, kwa maana ya Halmashauri kuchukua dhamana. (*Makofii*)

Swali la pili kuhusu tutakapoanza *Mid-Year Review* je, hatuwezi tukaangalia namna ya kuongeza kidogo pale; maamuzi yote ya fedha hapa yanavyotumika yanafanywa na Bunge hili. Tukienda kwenye *Mid-Year Review Program* na ikaonesha kwamba, tunaweza kupata hicho kiasi kidogo kikasaidia, sisi tutamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu ili hilo liweze kufanyika. *There is no problem, mimi sioni problem yoyote, kwa hiyo, review itakwambia kama una uwezo au huna.* (*Makofii*)

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, swali kuuliza kuhusu posho na maslahi ya Madiwani lilikuwa ni la kwanza, nililiuliza toka tulipoanza Bunge na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mmekuwa mkituunga mkono. Ukitazama hapa unaona kama Serikali inapiga chenga na kupiga danadana na mimi inanipa shaka Mheshimiwa Waziri huko kwako hakuna Madiwani wanaopata tabu; kwa nini usiwaongezee posho na maslahi Madiwani wetu? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nimweleze ndugu yangu Deo Filikunjombe kwamba, ninachosema ni msimamo wa Serikali, sisemi msimamo wangu kwa Madiwani wangu wa kule Siha. Madiwani wangu wa kule Siha ninawapenda sana na tena hapa kama mngewaongezea mkasema kila mmoja apate milioni moja huko waliko watafurahi sana. Sasa ndugu yangu Filikunjombe, mimi hapa ninachosema ni *conduit* ya kipitisha haya mambo, mkipitisha hapa Waziri Mkuu akaniambia kesho asubuhi watangazie kila mtu atapata milioni mia, haraka haraka ninamwambia Mkurugenzi lipa.

Ninachotaka kusema hapa ni kweli kabisa ninajua kwamba ni uchungu alionao moyoni, anajua kwamba hawa Madiwani wanaozungumzwa hapa ni wasaidizi wetu na sisi tunapenda tuwasaidie katika jambo hili na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuja hapa wakati anakamilisha bajeti yake, alitamka waziwazi kwamba, kimsingi tunakubaliana na jambo hili.

Mimi nina hakika kwamba, jambo hili litakwenda vizuri kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wetu. Tusisahau pia kwamba na Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ana Madiwani kule kwake, naye hivyo hivyo angependa haraka haraka awapitishie, lakini ufinyu wa bajeti ndiyo unakwamisha. Sasa ndiyo maana amesema kwenye *Mid-Year Review* na kwenye kipindi kinachokuja, tunategemea mambo yatakuwa mazuri na aliiweka vizuri. Ukitoma Hotuba yake inajieleza vizuri kabisa. Kwa hiyo, tunakubaliana na Mheshimiwa Filikunjombe kuhusu hilo analolisema, pia kuhusu uchumi. (*Makofî*)

Na. 374

Mkutano wa Cancun, Mexico kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi

MHE. MARTHA M. MLATA aliuliza:-

Suala la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi ni jambo linalogusa nchi zote duniani na hivi karibuni kulikuwa na Mkutano wa Cancun, Mexico juu ya mabadiliko ya tabia nchi (*climate change*):-

- (a) Je, hiyo Cancun ni nini na inahusiana vipi na mazingira?
- (b) Je, Tanzania imefaidika nini na hiyo Cancun?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi, mwaka 1992 Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Mabadiliko ya Tabia Nchi na kila mwaka nchi Wanachama hukutana katika nchi au Mji unaokubaliwa ili kujadili masuala ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Mkutano wa kwanza ulifanyika Geneva mwaka 1995, wa pili Berlin (1996), wa tatu Kyoto – Japan (1997) na kadhalika. Mkutano wa Kumi na Tano ulifanyika Copenhagen (2010) na wa Kumi na Sita ulifanyika Cancun Nchini Mexico, kuanzia tarehe 29 Novemba – 10 Desemba, 2010.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, Cancun ni Mji wa Kitalii nchini Mexico, ambako Mkutano wa Kumi na Sita wa Mabadiliko ya Tabia Nchi ulifanyika. Mkutano wa Kumi na Saba utafanyika mwaka huu (2011) Desemba katika Mji wa Durban – Afrika ya Kusini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imefaidika na Mkutano wa Cancun kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutetea maslahi ya nchi yetu kwa kuhakikisha kuwa msimamo uliopitishwa na Baraza la Mawaziri Tanzania, kuhusu kuunda Mfuko wa Fedha wa Dunia ili kusaidia nchi zinazoendelea kupunguza gesi joto unazingatiwa.

(ii) Tanzania imeteuliwa Mwenyekiti Mwenza, Mwenyekiti mwingine ni New Zealand wa kusimamia majadiliano (*negotiations*) kuhusu upunguzaji wa gesi joto hasa kwa nchi zilizoendelea.

(iii) Kuhakikisha nchi zinazoendelea zinashiriki kikamilifu kwa kupata fedha na teknolojia katika mpango wa Kimataifa unoitwa hatua mwafaka za Kitaifa za kupunguza gesi joto (*Nationally Appropriate Mitigation Actions - NAMAs*), maandalizi ya utekelezaji yameanza.

(iv) Nchi zinazoendelea kupata fedha kiasi cha US \$ billioni 100, ifikapo mwaka 2020 ili kutekeleza mipango ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi. Kwa sasa Tanzania inaandaa Mkakati wa Kitaifa pamoja na mpango kazi wake ili kunufaika na fedha hizi. Miradi mingi niliyoordhesha katika Hotuba yangu ya Bajeti, mmeipitisha hapa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania kwa sasa ni Makamu wa Rais wa Afrika wa Mkutano wa Mawaziri wa Mazingira (*African Ministerial Conference on Environment – AMCEN*) na kwa hivi sasa mimi ni Makamu wa Rais wa Mazingira Afrika. (*Makofii*)

Ninapenda pia kuwajulisha kwamba, aidha, mwaka 2012 – 2014, Tanzania itakuwa Rais wa *AMCEN* na Mkutano ujao (2012) wa *AMCEN*, utafanyika hapa Tanzania. Ikimpendeza Mheshimiwa Rais, mimi nitakuwa Rais wa Afrika mwaka kesho. (*Makofii*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza Waziri kwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, pia ninamshukuru kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano kama hii imekuwa ikifanyika kama yeye aliyosema mingi sana duniani, lakini sijawahi kuona Tanzania inafaidika kwa kiasi gani. Sasa labda niulize tu kwamba; kuna mkutano kama huu pia ulifanyika Rio de Janeiro Brazil mwaka 1992 na Nchi za Nordic wenyewe walitekeleza Maazimio yale na wakafaidika:-

(a) Ninapenda kujua je, Tanzania ilifaidika vipi na hasa kwa kuwahusisha Wananchi?

(b) Nilikuwa ninapenda kujua hizo *Carbon Funds* Wananchi wa kawaida wanafaidika vipi hasa katika kurekebisha au kutimiza azma ya kutunza mazingira kwa wakataji wa mkaa, kutumia mkaa na mambo mengine; Tanzania inafaidika vipi? Ahsante. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mkutano wa Kimataifa ulifanyika Rio de Janeiro mwaka 1992, lakini katika hiyo suala muhimu ni kwamba, tunazishawishi nchi zilizoendelea ziweze kupunguza hizo gesi joto, kwa sababu gesi joto zinazalishwa na wenzetu ambao wameendelea, wenyewe viwanda vikubwa. Sisi mchango wetu ni mdogo sana.

Kwa kuwa huwezi kuzuia wingu lisihame na gesi joto kutoka America kwenda Afrika, kwa hiyo, mambo haya yanafanyika kwa pamoja. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi nchi zilizoendelea bado hazijakubaliana mia kwa mia kutoa mchango mkubwa ili kupunguza hizi gesi joto. Ndiyo maana unakuta hii mikutano imeanza tangu mkutano wa kwanza mpaka mwaka huu tunaingia mkutano wa 17 na hatuwezi kuacha, kwa sababu athari zake zinatudhulu zaidi sisi watu tulokoo katika nchi maskini, kwa sababu wenzetu wana fedha nydingi na teknolojia ya kukabili athari. Kwa hiyo, bado tunaendelea na mipango hiyo ya kuwashawishi wenzetu waweze kuchangia.

Kwa kiasi fulani, wameshaanza kukubali kwa sababu ambayo hii nitaijumuisha na swali la *part b*, ambayo inasema tunafaidika vipi na *Carbon Fund*? Manufaa tunayo, kwa mfano, katika Hotuba yangu nilishasema tuna mradi wa kwanza wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo zalishi ya Ukanda wa Pwani, ambapo Tanzania imepata *US Dollar* milioni 3.1 na fedha hizi zilitolewa kwa ajili ya nchi maskini. Kwa hiyo, nchi maskini

zimeanza kupewa hizo fedha. Mradi mwingine ni utekelezaji wa vijiji vya mfano, *Equal Village*, pamoja na kujenga kituo nilichosema kwamba, tutajenga kituo cha mabadiliko ya tabia nchi Kilimanjaro. Kwa hiyo, tayari tumeshaanza kufanya mpango na tayari zimeshaanza kutolewa *Euro 2.2 milioni* na *European Unit*. Pia kuna mradi wa kujenga uwezo wa nchi katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi, ambapo kuna *US Dollar* milioni moja zimetolewa na Danida na kadhalika. Kwa hiyo, tunaendelea kuwashauri na tayari tumeshaanza kupata mafanikio na kuhusu *Carbon Fund* bado tunaendelea kuwasisitiza ili Wananchi wanaouza misitu waweze kufaidika na hela hizi. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Swali hili limetuchukua muda mrefu, tunaendelea na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel.

Na. 375

Ujenzi wa Chuo cha Ufundı - Bahi

MHE. OMARY A. BADWEL: Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwa mujibu wa Kanuni ya 41(B) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inasema; Mbunge anayeuliza swali anaweza kulinondo swali lake wakati wowote kabla hajajibwa. Iwapo swali husika tayari limewekwa kwenye Orodha ya Shughuli, kwa kusimama mahali pake, jina lake linapoitwa wakati wa maswali na kutamka kuwa analiondoa swali lake na kueleza kwa kifupi sababu ya kufanya hivyo. Wakati swali langu hili likisubiri majibu hapa Bungeni, tayari nimeridhika na utekelezaji wa Wizara husika na mimi nimeamua kuliondoa. Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofii*)

SPIKA: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Omary Badwel na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wengine muige mfano huo. Swali linalofuata la Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine, Mheshimiwa Livingstone Lusinde atamwulizia.

Na. 376

Wanafunzi wa Vyuo kupata Mikopo na Ajira

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE (K.n.y. MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE) aliuliza:-

Je, Serikali inatumia utaratibu gani ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wa Vyuo wanapata mikopo na baada ya masomo yao wanapata ajira ili waweze kulipa mikopo yao?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za utoaji mikopo huanza kwa wanafunzi kujaza fomu zenyé taarifa muhimu za waombaji pamoja na wazazi au walezi wao. Taarifa hizi zinahusu kiwango cha elimu na ufaulu wa mwombaji mkopo, shule alizosoma na kiwango cha elimu, kazi na mahali wanapoishi wazazi au walezi wake. Taarifa hizi husaidia mfumo wa utoaji mikopo kubaini uwezo wa kiuchumi wa mwombaji pamoja na wazazi au walezi wake.

Baada ya utambuzi huu kufanyika, mwombaji hupangiwa daraja la mkopo wake kuanzia asilimia sifuri hadi asilimia 100. Jukumu la Serikali ni kutoa elimu bora kwa Wananchi wake ili waweze kujajiri na kuajiriwa katika Taasisi, Mashirika na Serikalini. Katika soko huria la ajira ni jukumu la vyuo vyetu vya elimu ya juu kuwapa wanafunzi stadi za ujasiriamali ili baada ya kuhitimu waweze ama kujajiri au kuajiriwa na hivyo kuwa katika nafasi ya kulipa mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, urudishaji wa mkopo unafanyika kwa kuzingatia makubaliano kati ya Bodi ya Mikopo, Mwombaji pamoja na Mwajiri. Kwa wahitimu waliojajiri wenye, makubaliano yanakuwa kati ya aliyenufaika na mkopo pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi

wa Elimu ya Juu. Changamoto ya Serikali ni kuwabaini wahitimu sehemu zote wanazofanya kazi ili kuwezesha taratibu za kurejesha mikopo hiyo.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Wanafunzi wangapi mpaka sasa hivi wameweza kurejesha mikopo tangu utaratibu huu umeanza?

(ii) Serikali inawasaidiaje wanafunzi wanaotoka kwenye Shule za Sekondari za Kata ambao wanafaulu halafu wanashindwa kutafuta fomu na kuijunga na Vyuo Vikuu kwa sababu kule wanakosoma hakuna kompyuta wala umeme?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la kwanza kwamba ni wanafunzi wangapi ambao wameshalipa mikopo yao mpaka hivi sasa; ningependa kulijibu kwa fedha badala ya namba, kwa sababu namba sina lakini idadi ya fedha ninayo; kwamba, hivi sasa Serikali imeshakopesha jumla ya shilingi bilioni 630.6 kwa ajili ya wanafunzi kuweza kujigharimia katika elimu ya juu. Kati ya hizi, shilingi bilioni 636 bilioni 100.6 zimeiva kwa ajili ya kurejeshwa. *Installment* ambazo zilikuwa zinahitajika mpaka tarehe 30 mwezi wa sita mwaka huu, ziwe zimerejeshwa ni jumla ya shilingi bilioni 25.9. Kwa bahati mbaya tulizomudu au Bodi ilizomudu kuzikusanya mpaka hivi sasa ni bilioni 8.9.

Kwa hiyo, katika zile pesa ambazo zilikuwa zinatakiwa zirejeshwe hivi sasa kwenye Bodи ni bilioni 8.9, ambazo zimerejeshwa kati ya bilioni 25.9. Hii ni changamoto, lakini tupo tumejipanga kwa ajili ya kuifanya kazi changamoto hii, baada ya Tume ya Rais ambayo imemaliza kazi hivi karibuni kutoa *recommendations* kadhaa ambazo ndiyo tunazifutilia ili kuweza kurekebisha hali hiyo ngumu ambayo inaweza iksitisha uwezo wetu wa kuweza kutoa mikopo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu fomu za mikopo; wenzetu wa Bodи ya Mikopo wamepiga hatua moja zaidi kwamba, sasa hivi unaweza ukaomba mikopo kwa njia ya kompyuta, *on line application system*, wanaita *loan application system* ama *OLAS*. Sasa hii imeongezea katika taratibu ile ya makaratasi ya kujaza fomu zenyewe kama ilivyo makaratasi hayo unajaza na unayapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipindi ambacho mtu anaweza akaomba ni kirefu. Tuna kipindi cha miezi miezi zaidi ya kufanya kazi hiyo. Hata ingebidi mwanafunzi atoke kijiji chochote Tanzania kwenda Bodи ya Mikopo, hakuna sehemu Tanzania ambayo sasa hivi haifiki ndani ya miezi miwili na vijana wetu hawa waliosoma, wamesoma vizuri ni wajanja waelewa na maeneo mengi wanamudu changamoto hii ya kuweza kujaza fomu zao kwa wakati. (*Makof*)

MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninataka kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mara nyangi Serikali hutumia fedha nyangi sana kuwasomesha vijana hawa nje ya nchi na ndani ya nchi; na kwa kuwa tegemeo la Serikali ni kuwaona vijana hawa baadaye wanarudi na kuja kusaidia katika Wizara mbalimbali tulizonazo hapa nchini; je, Serikali huchukua hatua gani kwa wale wanafunzi ambao huamua kubakia ughaibuni au kukimbia nchi baada ya kupata elimu hiyo kutohana na mkopo unaotolewa na Serikali?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika taratibu za kutoa mikopo, hivi sasa tunamfunga yule ambaye anapewa mikopo baada ya *grace period* aanze kulipa mkopo wake. Sasa kuna baadhi ya wanafunzi ambao tunawafundisha nje ya nchi, kufuatana na mikataba ambayo tunaandikiana na nchi wahisani au washirika wa maendeleo mbalimbali. Wale ambao wanarudi, tunawabana kuweza kulipa mikopo yao kama inavyotakiwa. Wale wanaobaki kule wakiweza kulipa wakiwa huko sisi tunashukuru tu. Wanapata mafunzo na baadaye tunategemea wanarudi, lakini wanapoacha kulipa taratibu za kisheria zinafuatwa ili kuhakikisha kwamba, aidha, tunawarejesha au tunawashtaki Mahakamani ama wadhamini wao

ambao wamedhamini wao kupewa mikopo ile kuwachukulia hatua za kisheria ili mikopo ile tuweze kuirudisha.

Na. 377

Ahadi ya Kupeleka Umeme Kijiji cha Nyashimba

MHE. AZZA H. HAMAD (K.n.y. MHE. AHMED A. SALUM) aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Nyashimba na Puni – Shinyanga Mashariki wakati alipoongea na Wananchi hao akielekea Kahama kikazi mwaka 2007 na tayari maombi juu ya ahadi hiyo yalishawasilishwa ofisini kwake:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa wakati alipokuwa katika ziara kikazi Mkoani Shinyanga akielekea Wilaya ya Kahama, Serikali ilifanya tathmini kwa ajili ya kujua gharama za ujenzi wa njia kupeleka umeme katika Vijiji nya Nyashimba na Puni. Tathmini hiyo ilianza Februari, 2011 na kukamilika mwezi Machi, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na matokeo ya tathmini hiyo, kila kijiji kitahitaji *transformer* moja ya ukubwa wa KVA 100 na njia ya usambazi umeme ya msongo wa KV 04, yenye urefu wa kilomita mbili kwa kila kijiji. Umeme utambazwa kwenye vijiji hivyo kutoka kwenye njia ya umeme inayotokea Ibadakuli, Shinyanga Mjini, kupitia kwenye vijiji hivyo kuelekea Wilaya ya Kahama. Gharama za mradi katika kila kijiji ni milioni 69.566, yaani kama milioni 70 hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliafikiwa kwamba, kazi hii ifanywe na *TANESCO*. Hata hivyo, Shirika la *TANESCO* halikuweza kutenga fedha ya mwaka 2011 kutohaka na uhaba wa fedha unaolikabili Shirika. Wizara yangu imeielekeza *TANESCO* iwasilishe maombi haya na tathmini hiyo iliyofanywa kwa *REA* ili iweke kwenye orodha ya miradi itakayoweza kufadhilliwa na *REA*.

MHE. AZZA H. HAMAD: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Pamoja na majibu ambayo yanakatisha tamaa Wananchi wa Puni na Nyashimbi, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa ahadi hii imekuwa ni ya muda mrefu toka mwaka 2007 na mpaka hivi tunavyoongea haipo kwenye bajeti; Mheshimiwa Waziri huoni kwamba unapoteza imani ya Mheshimiwa Rais kwa Wananchi wake?

(ii) Je, ni lini Serikali itawapatia umeme Wananchi wote wanaopitiwa na nguzo za umeme wakati wao wakibaki kuwa watazamaji tu na kutohuka huduma hiyo; mfano Kijiji cha Msalala na Kijiji cha Welezo vilivyopo katika Jimbo la Solwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya umeme Mkoa wa Shinyanga ni kwamba, Shinyanga inahitaji kama *megawatt* 60 wakati wa *pick*. Katika *megawatt* 60 watumiaji wakubwa kama wanenamia kama *megawatt* 50, kwa hiyo, utaona matumizi ya umeme ya Shinyanga yako *very secured*. Kwa kuzingatia hayo, Serikali ilieelekeza *TANESCO* kwa makusudi kabisa ifanye mkakati maalum wa kuongeza usambazaji wa Miradi ya Umeme Shinyanga na Miradi hiyo kwa bahati nzuri na hatua zilizofikiwa zote ziko hapa; ni Miradi mingi, ninadhani jumla itafika kama bilioni 1.3. Kwa hiyo, ni Miradi midogo midogo mingi kwa ajili ya

kuongeza usambazaji kwa Mkoa wa Shinyanga, ambao kusema kweli umeme wake ume-concentrate kwenye ile Miradi mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Miradi ni mingi na hii ahadi ya Mheshimiwa Rais imechelewa kidogo. Nilichosema ni kwamba, ahadi yenye ni milioni 140, inaweza ikapatiwa ufumbuzi kuitia *REA* kwa sasa hivi matatizo ya *TANESCO* sisi wote tuyafahamu, tumeyapeleka *REA* na tutahimiza ipate utekelezaji haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, ninawaomba Wananchi wa Nyashimbi na Puni wabaki na matarajio kwamba, katika muda mfupi tutalipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Wananchi wote wanaopitiwa na umeme, nyaya zinazopita juu, inategemea kwanza na nyaya gani zinazopita. Pale Ibadakuli inayopita ni KV 33; kwa hiyo, inawezekana kuweka transformer ya KVA 100 ukawasambazia watu umeme. Hata hivyo, napo pana gharama na inategemea kama inakidhi vigezo. Kwa kuwa hilo ndiyo lengo, ninaomba nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeweka makisio haya kwamba, kila unapopita umeme na tunaweza tukaushusha chini na Wananchi wapo na wanakidhi vigezo tufanye hivyo.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Ninashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa katika ziara hiyo Rais akiwa MJINI Kahama aliagiza kwamba ukuaji wa Mji wa Kahama lazima uende sambamba na usambaji wa umeme katika Mji wa Kahama kwenye maeneo kama Shunu, Mungula, Ukondamoyo; na kwa kuwa agizo hilo halijaanza kutekelezwa; je, Waziri anawahakikishia Wananchi wa Mji wa Kahama kwamba atakuja kushuhudia kutokutekelezwa kwa agizo hilo la Rais na kwamba asimamie maelekezo ya utekelezaji wa agizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ziara hiyo ni kweli kwa sababu alikuwa anaelekea Kahama kuna ahadi zilizotolewa; kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, kuna Miradi hapa ya Kahama ambayo utekelezaji wake unaendelea Shinyanga kwa gharama kubwa. Tuna Miradi kama sita, saba hapo hapo Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa James Lembeli tukutane. Ninakubali tutakwenda kukagua utekelezaji wa Miradi hii inayofanyika na kuhimiza utekelezaji wa ahadi hizo kwa maeneo kama ya Mbulu na Mwendakulima ambapo hapa ipo. Inaonekana hapa *Sub-Station* ilikuwa inafanyiwa kazi, lakini kama kuna kazi ya ziada ni ahadi ambayo pia ilikuwa inahusisha kutoa umeme Buzwage na maeneo mengine. Kwa hiyo, ninaifahamu vizuri, tutakwenda tutafanyia kazi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke kwamba, Bajeti ya Wizara hii bado tumeishika mkononi, inabidi tumpe pesa akafanye kazi hizi tunazotaka.

MHE. SAID M. MTANDA: Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kitomanga ina umbali wa kilomita 15 kutoka Makao Makuu ya Jimbo ambako ndiko kuna umeme; je, Serikali ipo tayari sasa kupeleka umeme Vijiji vya Kilangala, Kitomanga na Mkwajuni ambavyo vina umbali wa kilomita 15 tu kutoka Makao Makuu ya Jimbo ambako ndiko kuna umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, umeme katika maeneo ya Mchinga, Mradi unahusiana na Mradi wa *Mtwara Electricity Project*, ambao unahusiana na kupeleka umeme Lindi na Mtwara.

Kwa hiyo ni kweli katika usambazaji uliokusudiwa pale Mchinga, Mradi ule ulifikia kukwama kidogo na hali hiyo pia ipo Ruangwa, Nachingwea na Tandahimba. Tulikwenda kule mwezi wa kwanza, tumeionna hii hali na tumekubaliana kwamba, tutafute hela ya ziada. Sasa kazi hizi zitafanywa na *TANESCO*, mwanzoni zilikuwa zifanywe na watu wa *ARTUMAS*, lakini tumegundua kazi hiyo hawaiwezi, tumekubaliana ifanywe na *TANESCO*. Kilomita 15 ni nyngi kidogo, kwa tathmini iliyofanywa ni kama milioni 350 au 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tulipokwenda kule tunajua hii hali ya Kitomanga na Mkwajuni na maeneo ya pale jirani, kwa sababu yanahusisha pia na Miradi ya Tandahimba, Newala na Masasi mpaka kule Mangaka kwa Mheshimiwa Mkapa. Kuna *network* ni Mradi mkubwa kidogo. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira wakati ninatafuta ufumbuzi wa namna ya kupanua *Mtwara Electricity Project* kwa Wananchi wote wa maeneo hayo.

Na. 378

Ujenzi wa Barabara ya Iringa – Mtera – Dodoma

MHE. CHIKU A. ABWAO aliuliza:-

Kwa kuwa Barabara ya Iringa – Mtera – Dodoma imekuwa kwenye mpango wa kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa kipindi kirefu sasa:-

Je, Serikali bado inafanya upembuzi yakinifu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Chiku Abwao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haifanyi kazi ya upembuzi yakinifu kwa Barabara ya Dodoma na Iringa. Kazi ya usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara hii ya Iringa – Mtera – Dodoma, yenye urefu wa kilomita 260, ilikamilika mwaka 2008. Mikataba kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Iringa mpaka Migori yenye urefu wa kilomita 95.2. Migori mpaka Fufu kilomita 93.8 na kutoka Fufu mpaka Dodoma kilomita 71 imesainiwa tarehe 13 Januari, 2011 na kazi za ujenzi kwa sehemu zote tatu zilanza rasmi tarehe 15 Machi, 2011. Mradi huu unagharimiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Shirika la Maendeleo ya Japan (*JICA*) na mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

(i) Kwa kuwa Barabara hii imekuwa katika mipango ya muda mrefu sana; na kwa kuwa niliwahi kuizungumzia toka Awamu ya Kwanza ya Mheshimiwa Mkapa wakati Mheshimiwa Anna Abdallah akiwa Waziri wa Ujenzi; je, Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu yenye matumaini makubwa atawezza kututamkia wazi watusika wa hii barabara kwamba itakamilika lini?

(ii) Kwa kuwa ni kawaida barabara inapoengwa hutoke waathirika ambao wengine wanaweza wakawa na haki ya kupewa fidia na wengine kukosa haki hiyo ya kupewa fidia. Je, Mheshimiwa Waziri, atanieleza ni wangapi watalipwa fidia na ni wangapi ambao hawatalipwa fidia kwa faida ya Wakazi wa Ismani, Mtera, Dodoma na Iringa pia?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chiku Abwao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza anaulizaBarabara hizi zitakamilika lini. Ninapenda kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kipande kifupi cha kutoka hapa Dodoma mpaka Fufu, chenye urefu wa kilometra 71, kitakabidhiwa kwetu kikiwa kimejengwa, mwanzoni kabisa yaani mwezi Aprili, 2013. Vipande viwili viliviyobaki kutoka Fufu mpaka Migori, Migori mpaka Iringa, tutakabidhiwa mwezi Januari, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii lake la pili la fidia; kiasi kilicholipwa mpaka sasa kama fidia ni jumla ya shilingi 414,151,500 na Wananchi walolipwa mpaka sasa ni 303. Wananchi watatu hawajachukua fidia yao mpaka sasa; mmoja nina taarifa anasema kwamba, fidia ni ndogo ya milioni mbili na kitu, lakini wawili hawajulikani walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo taarifa kwa sasa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukifuatilia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukiachia mbali ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya kutoka Likuyufusi kwenda mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, Mkenda; Mheshimiwa Rais, wakati akihutubia mikutano ya kuomba kura aliwaambia Wananchi wa Jimbo la Peramiko, Barabara ya Makambako – Songea, ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami miaka mingi sana iliyopita, itafanyiwa matengenezo upya.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri aniambie utekelezaji wa ahadi hiyo; kwanza ya Killani; pili ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuanza kuitengeneza Barabara hiyo kwa kiwango cha lami upya; utekelezaji wake utaanza lini kwa kuwa naona kupo kimya kama maji kwenye mtungi?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la msingi lilikuwa Barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa, kilometra 260; Mheshimiwa Mhagama, amechomekea swali la kutoka Makambako kwenda Songea. Sasa ninachotaka tu kusema ni kwamba, Bajeti ya Wizara imepitishwa; yale yaliyoandikwa yote kwenye Hotuba yetu na kwenye kitabu kilichopitishwa tutayazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile ahadi ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais, tunafahamu zipo kwenye llani ya Uchaguzi kuanzia ukurasa wa 72 hadi wa 82. Tutazitekeleza kwa kipindi cha miaka mitano.

Na. 379

Mawasiliano Ya Simu Katika Jimbo la Lushoto

MHE. HENRY D. SHEKIFU aliuliza :-

Mawasiliano ya simu ni muhimu sana katika Dunia ya leo:-

Je, ni lini mawasiliano ya simu yatafikisha katika Kata za Mlola, Kilole, Kwekanga, Malibwi na Makanya katika Jimbo la Lushoto ambako kuna watu wengi walio na uwezo kiuchumi?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, pamoa na Wananchi wa Jimbo la Lushoto, kwa juhudzi zao kubwa za kuharakisha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika Jimbo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango na juhudzi za Wananchi katika kuleta maendeleo, Wizara yangu inaendelea kuchukua juhudzi za makusudi kukabiliana na changamoto zinazokabili upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo Jimbo la Lushoto. Juhudi hizo zinahitaji ushirikiano wa karibu kati ya Serikali, Kampuni za Simu pamoa na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, jithihada hizo za pamoa zinaendelea chini ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote na kwamba, katika kipindi cha miaka miwili ijayo, maeneo mbalimbali nchini yasiyokuwa na huduma za mawasiliano, yakiwemo yale ya Jimbo la Lushoto, yatakuwa yamefikiwa na huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mlola na nydingine za jirani, tayari zimewekwa kwenye mpango wa kufanyiwa tathmini yakinifu na Kampuni ya *Airtel* kabla ya mwisho wa mwaka 2011. Kwa taarifa nilizonazo sasa hivi, Wataalamu wa Kampuni ya *Airtel*, wameondoka jana na sasa hivi wapo Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kampuni ya *Vodacom* imeahidi kufanya utafiti wa maeneo yaliyotajwa ili kuona uwezekano wa kupanua mtandao wake Wilayani Lushoto. Utafiti huu unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu ya *Zantel* pamoja na Kampuni ya Simu ya *TTCL*, zimeahidi kuweka katika mipango yake, kuhakikisha kwamba, maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yanafikiwa na huduma za mawasiliano.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda kutoa shukrani za Wananchi wa Jimbo la Lushoto, kwa Wizara hii. Ninaomba Waziri akubali kupokea shukrani za Wananchi wa Jimbo la Lushoto, hasa Kata ya Mlola, ambayo watu wa *Airtel* wameshaonesha mfano kwa kwenda kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru kwa sababu amejibu kwamba, watu wa *Airtel* wako Lushoto. Wananchi hawa walijawa na wasiwasni kwa sababu *Airtel* walifika katika eneo la kujenga mnara na kwa bahati mbaya wakaondoka. Ninashukuru ye ye mwenyewe ametamka wapo Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali; Wananchi wa Kata zinazozunguka Mlola ambazo ni Malibwi, Kilole na Kwekanga, nao baada ya kuona wenzao wanapata mnara wameanza kuhamasika. Waziri anasema nini ju hili ili Wananchi hawa nao wakae mkao wa kupata simu?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunapokea pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, mtani wangu, mjukuu wangu, lakini vilevile niwahakikishie Wananchi wa Lushoto walio karibu na Kata ya Mlola, ikiwemo Kata ya Kilole, Kwekanga, Malimbwi, Makanya na Kinjumbi, wote nao wapo katika mpango na *Airtel* katika safari hii watapita maeneo hayo yote. Walikwenda kule tarehe 23 Mei, 2011 kuangalia na wakaona kwamba, hakuna *coverage* katika maeneo yao. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Lushoto kwamba, mawasiliano yako njiani.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya mawasiliano yaliyoko katika Kata zilizotajwa kwenye Jimbo la Lushoto, yanafanana sana na matatizo yaliyoko sehemu ya Katumba Wilayani Kyela pamoja na Wilaya ya Ileje. Ukipika maeneo hayo unaambiwa *welcome to Malawi*. Sasa je, Serikali ina mpango gani ama ina mkakati gani kuhakikisha kwamba maeneo hayo niliyoyataja ; Wilaya ya Ileje na Wilaya ya Kyela, yanapata mawasiliano mazuri? Ninaomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu spika, maeneo ya Katumba katika Wilaya ya Kyela pamoja na Wilaya ya Ileje, yapo katika mpango ule ule ambao nimeusema kwamba, katika kipindi cha miaka miwili tutajitahidi kuhakikisha kwamba, maeneo yote yamefikiwa. Kwa hivyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na sisi na kama nilivyowaomba siku ya bajeti yetu, atuletee maeneo kwa kutaja Wilaya, Kata na Vijiji, ambavyo anadhani kwamba, havina mawasiliano ili tuweke katika mpango ambao utahakikisha kwamba, Wananchi wa maeneo hayo wamefikiwa na mawasiliano.

Na. 380

Hitaji la Mawasiliano ya Simu – Ibumba na Izimbili

MHE. SAID J. NKUMBA aliuliza:-

Kutokana na matengenezo mazuri yaliyofanyika katika Barabara ya Tujuo – Izimbili – Ufuke, Wananchi wengi wamejenga pembezoni mwake na wengine kuitumia kwa ufanisi:-

Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na makampuni ya simu ili kuhakikisha kuwa maeneo ya Ibumba na Izimbili yanakuwa na mawasiliano ya uhakika kwa ajili ya usalama wa wakazi wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mhesihmiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ninapenda kujibu swali la Mhesihmiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mhesihmiwa Naibu Spika, ninapenda kumtaarifu Mhesihmiwa Mbunge kuwa, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya Ibumba na Izimbili na itazihimiza kampuni za simu kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote na hata kuendelea kuzishawishi kampuni za simu kwa kutumia bajeti zao, waweze kupeleka mawasiliano ya uhakika katika maeneo yaliyotajwa na Mhesihmiwa Mbunge.

Mhesihmiwa Naibu Spika, maeneo ya Ibumba na Izimbili yapo katika mpango wa kufanyiwa tathmini yakinifu na Kampuni ya Mawasiliano ya *Airtel* katika mwaka huu ili kuweza kufikisha mtandao wa mawasiliano ya simu za mkononi na hivyo basi kusaidia Wananchi wa maeneo hayo kuwa na mawasiliano ya uhakika.

Mhesihmiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Vodacom* ina mikakati ya kuweka mitambo katika maeneo ya Tutuo na Ipole pamoja na ninavyozungumza hivi sasa, nimeambiwa tayari wameshawasha. Pamoja na kufanya utafiti ili kuweza kuimarisha mawasiliano katika maeneo yaliyoainishwa na Mhesihmiwa Mbunge; Kampuni ya Simu ya *Zantel* imeahidi kupanua mtandao wake kupitia miundombinu ya kampuni nyingine ili kufikisha mawasiliano katika maeneo aliyoataja.

Mhesihmiwa Naibu Spika, aidha, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), kwa upande wake imeahidi kuyaweka maeneo yaliyotajwa na Mhesihmiwa Mbunge katika Mpango Mkakati wake wa Mwaka 2011 – 2013.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mhesihmiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhesihmiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa tathmini yakinifu zimekuwa zinachukua muda mrefu sana vikiwemo vikwazo vilevile vyta *NEMC*, kwa maana ya athari za mazingira katika maeneo mbalimbali ambayo yanaainishwa kufanyiwa kazi ya kuweka minara: Je, Wizara sasa ina mkakati wa haraka sana kuhakikisha kwamba vikwazo hivi vinaondolewa haraka ili shughuli hizi ziweze kwenda haraka na Wananchi waweze kujipatia mawasiliano wanayoyahitaji katika maeneo mbalimbali nchini?

(ii) Kwa kuwa Mhesihmiwa Naibu Waziri umetoa majibu mazuri sana hapa wakati ukinijibu kwa niaba ya Wananchi wa Sikonge. Upo tayari sasa kunipatia maelezo yako hayo kwa maandishi ili baadaye kama mambo hayatakuwa mazuri tuweze kukamatana vizuri sana?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mhesihmiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhesihmiwa Nkumba, kama ifuatavyo:-

Mhesihmiwa Naibu Spika, ninakubaliana na yeze kuwa kweli kumekuwa na matatizo katika kuhakikisha kwamba, vibali vinatolewa kuweka minara kutoka *NEMC*. Nimhakikishie tu kwamba, wakati ninakuja hapa Ofisini, swali hili *nillili-anticipate* na hivyo nilizungumza na Katibu Mkuu wangu na Katibu Mkuu wangu ameahidi kuwaita wadau wote ikiwemo Makampuni ya

Simu, *NEMC* pamoja na *TAMISEMI*, waweze kuzungumza, waone ni kwa namna gani tunaweza kuharakisha hii *process* ya kuweza kuweka minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii lake la pili, anauliza nipo tayari kumpa kwa maandishi; ninadhani nimhakikishie tu kwamba, haya niliyoyasema yanawekwa kwa maandishi katika *Hansard* yetu ndani ya Bunge hili. Pamoja na hayo, kama anahitaji barua kutoka Wizarani, basi tupo tayari kufanya hivyo na nimhakikishie tu kwamba, nitakapotoka hapa, nitampa *e-mail* niliyoipokea leo kutoka *Airtel*, ikisema maeneo hayo yatafanyiwa uchambuzi yakinifu mwezi Septemba mwaka huu.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo ya mawasiliano ya Sikonge kwa Mheshimiwa Said Nkumba, yanafanana sana na matatizo ya mawasiliano katika Jimbo langu la Chambani hasa katika Ukanda wa Mashariki ambapo Mheshimiwa Waziri amewahi kufika kule na kuona hali halisi; je, ni lini basi Serikali itafikisha mawasiliano katika Ukanda wa Mashariki hasa katika Viji viya Matele, Chwale, Kekewani, Mapape na Mambani ili nao waweze kufaidika na mawasiliano ya simu?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulizungumza kuhusu habari hii na nikamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni lazima niende kwanza nikathibitishe. Baada ya kuthibitishe kwamba kweli hakuna mawasiliano, baadaye tutapeleka mawasiliano haraka inavyowezekana.

Na. 381

Wimbi la Mauaji na Ujambazi - Zanzibar

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA aliuliza:-

Kumekuwepo na wimbi kubwa la mauaji na ujambazi katika Mji wa Zanzibar:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya vitendo hivyo na kuhakikisha kuwa havitokei tena?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba lipo wimbi kubwa la mauaji na ujambazi katika Mji wa Zanzibar; hali ya uhalifu katika Mji wa Zanzibar ni ya kawaida sana na ni ndogo ikilinanishwa na miji mingine ya Tanzania.

Aidha, takwimu nilizonazo zinaonesha kwamba, matukio ya mauaji na ujambazi Zanzibar, hivi sasa yamepungua sana kutohana na juhudhi kubwa zinazofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Wananchi na Wadau wengine kuititia Mpango wa Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Jeshi la Polisi Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla, litajitahidi kukabiliana na matukio ya mauwaji na vitendo vya ujambazi.

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hali ya uhalifu katika Mji wa Zanzibar ni ya kawaida; na kwa kuwa Zanzibar ongezeko la watu wanaoingia

linakua siku hadi siku; je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ule utaratibu uliokuwa unatumika zamani wa *Passport* kwa wageni urudie tena ili kuepusha vitendo vyatya uhalifu kukua zaidi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa maoni yangu, ninadhani kwa hapa tulipofika hakuna ulazima sana wa kutumia *passport* kwenda Zanzibar, maana Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mtanzania yeoyote anayo haki ya kwenda sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya kuwekewa vikwazo. (*Makofii*)

Kama swali la msingi hapa ni kumjua nani anaingia Zanzibar, nani anaingia Dar es Salaam, nani anaingia Tabora, ninafikiri utaratibu ambaa Zanzibar wameuanzisha kuwa na vitambulisho vyatya Ukazi wa Zanzibar ni hatua muhimu. Kama tunavyojua kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara yangu sasa hivi ipo mbioni kutayarisha utoaji wa Vitambulisho wa Taifa. Ninadhani utaratibu huo ukitekelezwa, utawasaidia sana kujua Mtanzania gani anaondoka sehemu moja na kwenda sehemu nyngine. Ninarudia, ninadhani kwa hatua ambayo tumefikia, hakuna umuhimu wa kutumia *pass* ya kusafiria kwenda Zanzibar. (*Makofii*)

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kuniona, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hali ya ujambazi ambayo ilikuwa inajitokeza Zanzibar inafanana sana na hali ambayo inajitokeza katika Jimbo la Ukonga kwa siku za hivi karibuni hasa katika Kata za Majohi, Chanika, Msongola pamoja na Kitunda kwamba majambazi wanaigia katika sehemu za biashara na makazi ya watu kuanzia saa kumi na mbili hadi saa nne usiku na kunyang'anya mali za Wananchi. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba inafanya utaratibu wa kurudisha usalama wa mali na watu wanaoishi katika Kata nilizositaja?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwaiposa kama ifuatavyo:-

Kama unavyoolewa, Jeshi letu la Polisi limepeewa dhamana Kikatiba na Kisheria, kusimamia ulinzi wa usalama wa raia na mali zao. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jeshi la Polisi linachukua hatua tatu kama ifuatavyo:-

(i) Jeshi letu la Polisi linashirikiana na Wananchi kwa kupitia dhana ya Polisi ya Jamii na Ulinzi Shirikishi. Lengo lake ni kuliwezesha Jeshi la Polisi kupata taarifa mapema za vitendo vyatya uharifu, kwa sababu tunaamini waharifu tunaishi nao, tunakula nao na tunazungumza nao.

(ii) Kupeleleza na kupata taarifa za vitendo vyatya uharifu kabla hata havijatokea ili Jeshi la Polisi liweze kuchukua hatua mapema; lakini pale ambapo vitendo vyatya uharifu tayari vimeshafanyika, Jeshi la Polisi linafanya upelelezi ili wawapate watu wanaohusika na vitendo hivyo ili tuweze kuwachukulia hatua za kisheria.

(iii) Kufanya doria na misako ya waharifu mbalimbali.

MHE MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninaomba kuuliza swali. Kwa kuwa Zanzibar sasa imetulia haina mvutano tena; na kwa kuwa takwimu za Wizara ya Mambo ya Ndani zinaonesha bado ujambazi na mauaji yanaendelea; je, Mheshimiwa Waziri haioni sasa kwa sababu ya usalama tulionao Zanzibar, Raia wa Zanzibar waruhusiwe kumiliki silaha ndogo ndogo kama Watanzania wengine?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, kaka yangu, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama alivyosema, vitendo vyatya mauaji na ujambazi vimepungua sana Zanzibar na labda tu nitoe taarifa kwa faida ya Wananchi na wasikilizaji kwa ujumla: Mwaka 2008, kulikuwa na matukio ya mauaji Zanzibar 15, vitendo vyatya ujambazi 15; mwaka 2009, matukio ya mauaji

mbalimbali 22, ujambazi 6; mwaka 2010, matukio mbalimbali ya mauaji 15, vitendo vya ujambazi kitendo kimoja; na mwaka huu wa 2011, mpaka hapa tulipofikia, mauaji ya aina mbalimbali matano, lakini ujambazi ni tukio moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii inadhihirisha ile kauli niliyosema kwamba, hali ya usalama imeimarika sana na ninakubaliana na kauli ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa Zanzibar imetulia. Ninaona Mheshimiwa Mbunge anajichanganya, ye ye amesema anakubaliana nami kwamba, hali imeimarika sana. Kama hali imeimarika, anasema wapatiwe silaha ndogo ndogo sasa, ninaona Mheshimiwa anajichanganya, lakini hata hivyo Wizara italitafakari na kuchukua hatua inayostahiki. (*Makofi*)

Na. 382

Sababu Mojawapo Inayosababisha Ajali Barabarani

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA (K.n.y. MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE) aliuliza:-

Ajali za barabarani zinaendelea kuwa tishio kubwa kwa maisha ya Watanzania na moja ya sababu zinazochangia tatizo hilo ni madereva kutozingatia alama za barabarani ambazo zimewekwa kisheria, je, ni lini Watanzania watafundishwa na kutakiwa kutumia na kuzingatia alama sahihi za barabarani?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, moja ya sababu zinazochangia ajali za barabarani ni madereva na watumiaji wengine wa barabara kutozingatia alama za barabarani. Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi, pamoja na wadau wengine, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa Wananchi juu ya matumizi sahihi ya barabara. Kwa sasa Jeshi la Polisi linatoa elimu kwa kupitia vyombo vya habari ikiwemo televisheni na redio.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, Jeshi la Polisi hususan Kikosi cha Usalama Barabarani huwatumia maofisa wake kwenda kwenye Shule za Msingi na Sekondari kutoa elimu ya usalama barabarani ikiwemo matumizi ya alama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zinazofanyika, utafiti unaonesha kwamba, baadhi ya madereva huvunja Sheria za Usalama Barabarani kwa makusudi na wala si kwa sababu ya ukosefu wa elimu. Hii inatokana na tabia ilioanza kujengeka katika jamii yetu ya Wananchi kutopenda kufuata sheria. Kwa kulitambua jambo hili, Serikali kupitia Jeshi la Polisi, itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria madereva wanaovunja Sheria za Usalama Barabarani. Miongoni mwa hatua hizo ni kuwashtaki madereva mahakamani na kuwanyang'anya leseni kwa wale watakaposababisha vifo na majeraha. Suala la kubadilisha tabia za wanadamu siyo jambo rahisi sana na haliwezi kufanywa na Jeshi la Polisi peke yake. Kwa kupitia Bunge Iako Tukufu, ninawaomba Watanzania wenzangu wote wajenge tabia ya kufuata sheria.

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa sisi ambao tumeendesha Mjini Dar es Salaam kwa muda mrefu, dereva unajaribu kutokuwa karibu na daladala kama inawezekana kwa sababu wanaweza wakaamua kukatiza au *ku-overtake* kushoto au kulia wakati wowote ulti. Nilitaka kujua kama waendesha daladala wana sheria tofauti za kuzifuata na kama siyo hivyo; Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna mikakati ya kutoa elimu; je, mnaweza mkalichukua hili kundi kama kundi maalum na muwape elimu ya kuendesha kwa usalama barabarani? (*Makofi*)

(ii) Ni tabia iliyozoleka kwa magari yanayoharibika kwenye Barabara Kuu wenyewe magari huwa wanatandaza matawi makubwa barabarani kwa kuashiria kwamba kuna gari bovu pale mbele. Katika uhai wangu katika Bunge hili Serikali imekemea mara nyangi lakini bado inaendelea; nilitaka kujua kama Serikali imehalalisha hilo na kama halijafanya hivyo kuna mikakati gani mipya kwa sababu tumewahi kuahidiwa kwamba hili litakomeshwa?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Prof. Mwakyusa, maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

La kwanza, ninakubaliana naye kwamba, wapo baadhi ya madereva wa daladala Dar es Salaam, ninadhani siyo Dar es Salaam tu, miji mingi na maeneo mengi katika nchi yetu, wapo madereva ambao hawaftati taratibu na Sheria za Usalama Barabarani. Ninakubaliana naye kwamba, Wizara yangu ifanye juhudhi na mkakati maalum wa kupambana au kuwaelimisha madereva hao wa daladala, lakini siyo madereva tu wa daladala, lakini mpaka wapanda pikipiki nao wanaingia kwenye mkumbo huo, tutafanya kila lillo katika uwezo wetu kuwaelimisha watu hao.

Pili, ni kweli upo utamaduni wa baadhi ya madereva ambao wanaharibikiwa na magari yao kuweka matawi makubwa kama kielelezo cha kuonesha kwamba, sehemu fulani kuna magari ambayo yameharibika. Sasa taratibu hizi hazikubaliki kisheria hata kidogo. Kwa maana hiyo, tunaliagiza Jeshi la Polisi, kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, maana Wizara ya Ujenzi wana sheria maalum ambayo inakataza juu ya jambo hilo, magari ambayo yanaharibika barabarani yaondoshwe haraka iwezekanavyo, siyo suala tu la usalama kwa Wananchi na vyombo ambavyo vinapita barabarani, lakini hata kwa usalama wa barabara, maana magari yanayoharika barabarani yakikaa muda mrefu yanamwaga mafuta barabarani, jambo hili husababisha hasara kubwa na uharibifu mkubwa kwa barabara zetu. Kwa maana hiyo basi, tunayo kila sababu sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tukishirikiana na wenzetu Wizara ya Ujenzi, tufanye kila lillo katika uwezo wetu kuhakikisha kwamba, magari hayakai barabarani muda mrefu ili yasisababise ajali, lakini pia yasisababise uharibifu mkubwa kwa barabara zetu hizi ambazo tunatumia fedha nyingi sana kuzigharimia.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tuwiane radhi muda wetu umepita sana. Ninaomba niende kwenye kutambulisha wageni; nianze na wageni wa Mheshimiwa Waziri Kabaka, ambao ni pamoja na Maofisa wa Wizara ya Kazi na Ajira Makao Mkoo, wakiongozwa na Katibu Mkoo Fredrick Shitindi; Naibu Katibu Mkoo, Bibi Edin Mangesho; Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu; Kamisa Mwakyesa; Kamishna wa Kazi, Sauli Kinemela, Mkurugenzi wa Ajira, Ernest Ndimbo; Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Haji Janabi; Mkurugenzi wa Fedha Joshua Masaka; na Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, Doroth Wilson. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nitawataja kwa haraka haraka, Viongozi wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii, ambao ni pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya *NSSF*, Abubakari Rajabu; ahsante sana Katibu Mkoo wetu wa zamani; Mkurugenzi Mkoo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), Ramadhani Dau; karibu sana Ndugu Dau; Mkurugenzi Mkoo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi za Jamii (*SSRA*), Irene Isaka; Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi wa Umma (*SMA*), Cosmas Msigwa; Kaimu Mkurugenzi Mkoo wa Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), Alex Ngata; Mkurugenzi wa Wakala wa Huduma za Ajira (*TaESA*), Elieza Mwasele; na Kaimu Mtendaji wa Shirika la Tija la Taifa (*NIP*), Leonida Rwejuna. (*Makofi*)

Viongozi wa Vyama vya Waajiri (*ATE*) ni pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania, Bibi Hilderguard Mziray; Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania, Dkt. Aggrey Mlimka pia wapo *TUCTA*; Makamu wa Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi *TUCTA*, Robert Maskini; na Kaimu Katibu Mkoo wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania, Nicholaus Mgaya. Mwenyekiti wa TUGHE Taifa, Dkt. Diwani Mrutu; karibu sana na pia tuna wageni kutoka *TACO*, Muungano wa Washauri Elekezi Tanzania, ambao ni pamoja na Katibu wa *TACO*, Ibrahim Kachale; Makamu Mwenyekiti Profesa Kessy na Mjumbe Dkt. Damas Mbogolo. (*Makofi*)

Baada ya wageni hao wa Mheshimiwa Waziri, sasa nimirambulisha mgeni wangu ambaye ni Dkt. John Lusingu, yeye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watanzania wote waishio Nchini Uingereza, tuliwahi kuwa pamoja pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, ambaye ni Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, ambaye ni Ndugu Florence Mahanga; Florence simama sijamaliza kukutambulisha. Huyu ni mke wa Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga; karibu sana mama. Katibu Mkuu wa TUGHE, Ali Kibwana Kiwenge; karibu sana. (*Makofii*)

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Regia Mtema, Waziri Kivuli wa Kazi na Ajira, ambao ni Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu wakiongozwa na Ndugu Remija Esteratus Mtema; pacha wa Mheshimiwa Regia; karibu sana Remija, pacha wako anafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge Ukumbini ni pamoja na Wenyevitani wanane wa Mitaa kutoka Kata za Segerea na Kimanga Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Mtaa wa Kimanga Darajani, Ndugu Chacha Mwenge. Karibuni sana, wako hapa juu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni kutoka *World Vision*, Shinyanga wakiongozwa na Meneja wa Kanda wa *World Vision*, Ndugu Mashimba Ndaki, ni wageni wa Mheshimiwa James D. Lembeli. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Diwani wa Kata ya Kabutuka, Ndugu Moses Bilamfanye. Karibuni sana. Kata ya Kabutuka naamini ni Kigoma. (*Makofii*)

Wageni wengine waliofika Bungeni ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi ambao ni wanafuzi kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari Morogoro, wako 75. Karibuni sana mjifunze jinsi Bunge lenu linavyofanya kazi zake. (*Makofii*)

Wengine ni wanakijji 40 wa Shamba Darasa, wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Sanjaranda, Mheshimiwa Elphas Lwanji, watakuwa ni wageni wa Mheshimiwa John P. Lwanji, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia kuna wafanyakazi 25 wa *World Vision* kutoka Shinyanga, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia kuna kikundi cha *VICOBA* kutoka Ikundi, jimbo la Singida Mashariki, Mheshimiwa Tundu Lissu, siwaoni hawa wageni, lakini karibuni sana. (*Makofii*)

Wanafunzi 60 na Walimu tisa kutoka Shule ya Msingi Msalato Dodoma, karibuni sana wanafunzi na Walimu kuona jinsi Bunge lenu linavyofanya kazi. (*Makofii*)

Pia kuna wanafunzi 70 kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri iliyopo Dodoma, wao wako *basement*. Karibuni sana wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Jamhuri, ni moja kati ya shule zinazofanya vizuri zilizopo hapa Dodoma yenye Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, naendelea sasa na matangazo ya kazi, kutoka kwa Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yaa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, wajumbe wake wanaombwa wakutane katika ukumbi namba 227, saa 7.00 kwa muda mfupi baada tu ya kumaliza shughuli za hapa.

Mheshimiwa John J. Mnyika, Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anawaomba Wabunge wote wakutane leo saa 9.00 alasiri, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala, ukumbi namba 219.

Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kutakuwa na semina kuhusu elimu ya masuala ya UKIMWI kesho Jumamosi tarehe 6 Agosti, 2011. Semina hiyo itaanza saa 4.30 asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 6 Jumamosi kutakuwa na mechi ya mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na Timu ya *British Council*. Mechi hii ni mechi kubwa na dhununi kubwa la mchezo huu wa

siku ya Jumamosi ni kuzindua programmu ya michezo inayoitwa *International Inspirations* yenyelengo la kuinua na kuhamasisha michezo kwa watoto na vijana wa rika zote bila kujali jinsia na ulemavu. Hivyo Wabunge wote hasa wanawake wanaombwa kuhudhuria michezo huu utakaoanza saa 9.00 jioni.

Pia katika michezo huo ambapo itakuwa ni timu za mpira wa miguu na *netball*, katika mpira wa miguu kutakuwa na ushiriki wa Wabunge wanawake katika timu ya upande wa Bunge ambapo *goalkeeper* wa timu ya Bunge kesho kwa mpira wa miguu atakuwa ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, namba tano ni Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko, beki ni Mheshimiwa Maria I. Hewa. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia kwamba leo mtakapokuwa mnatoka, nyuma ya jengo la utawala kuna maonyesho ya kazi zinazofanywa na Wizara ya Kazi na Ajira na huduma ambazo zinatolewa na Wizara hiyo. Kwa hiyo, Wizara inawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote kutembelea maonyesho hayo kwenye viwanja vya Bunge.

Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, anawaomba Wabunge wote ambaa ni wawakilishi wa Bunge hili katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini saa 7.00 mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, wakutane pale Ukumbi wa Msekwa kwa kikao kifupi.

Mheshimiwa Moses Joseph Machali, nadhani ndiye Katibu hakuandika cheo chake lakini anaomba Wabunge wote wa *NCCR Mageuzi* wakutane saa 7.00 mchana mara baada ya shughuli za Bunge, chumba namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, naomba kuwatangazia kwamba Mheshimiwa David M. Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, hivi sasa amesafiri kwenda Afrika Kusini ambako atatunukiwa Shahada ya Uadtari yaani *Honorary Doctorate* kutambua mchango wake katika kazi za jamii ambazo amezifanya katika maisha yake. Atakaporudi tutafafanua ni kwa nini amepata zawadi hiyo. (*Makofi*)

Kwa kumalizia naomba niseme yafuatayo. Liko gazeti moja leo limetoe moja ya *heading* inayosema 'Bunge ni nguvu ya Soda' na mpo wanafunzi wetu mnaojifunza kuwa Waandishi wa Habari, napenda kuwaambia wote wanaohusikana na masuala ya habari na hasa wanaoandika vichwa vya habari vya aina hiyo kwa kweli jambo hili ni utovu wa nidhamu. Bunge ni nguzo ya nchi na ni chombo muhimu kabisa katika utawala wa nchi yetu, hawezi mtu kwa maoni yake tu akaamua kukashifu Taasisi kubwa na nzito, yenyenafasi muhimu katika nchi kama Bunge. Kwa hiyo, pamoja na uhuru wa uandishi wa namna hii unaishia kwenye *contempt of Parliament*. Kwa hiyo, napenda kuwakumbusha Waandishi wetu wote kwamba wajichunge sana wanapokuwa wanaandika habari za Bunge pamoja na kukosoa kinachoendelea jambo ambalo hatuwazui, lakini nao kujizua kukashifu Taasisi kama hii ambayo ina namna mbalimbali za kuweza kuchukua hatua dhidi ya watu wa aina hiyo. (*Makofi*)

Lakini kwa kumalizia, baadhi yetu sisi humu ndani ndiyo vinara wa kukashifu Bunge. Kwa hiyo na sisi tuwe mfano mzuri zaidi ili walio nje yetu wasiweze kuvuka mipaka. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 - Wizara ya Kazi na Ajira

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kabla sijaanza kutoa hoja yangu, naomba nichukue fursa hii kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Wanawake wa Mkoo wa Mara wa UWT kwa kumpoteza Mwenyekiti wa UWT wa Wilaya ya Serengeti, Ndugu yetu na rafiki yetu, Tereza Macarius. Naomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii illyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kwa kuzingatia taarifa hizo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili Mpango wa Kazi na kuitisha Makadirio ya

Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo kuiongoza nchi yetu katika Uchaguzi wa mwezi Oktoba 2010. Aidha, napenda kumpongeza kwa kuendelea kutuongoza na kutoa maelekezo katika utekelezaji wa kazi katika Sekta ya Kazi na Ajira. Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kusaidia hatua zitazowezesha kutatua tatizo la ajira hususan kwa vijana. Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio makubwa sana. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuja nchini kwetu na wadau wa maendeleo kuona haja ya kuendelea kutuunga mkono. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu kwa miaka mingine mitano ambapo nina uhakika Watanzania watampa ushirikiano wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Ghalib Bilal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi, kwa kuteuliwa tena na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu lilipokutana hapa Dodoma mwezi Novemba 2010, llimchagua Mheshimiwa Spika wa kwanza mwanamke wa Bunge letu Tukufu Mheshimiwa Anne S. Makinda na wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kuwa Naibu Spika. Nachukua nafasi hii kuwapongeza sana. Aidha, niruhusu vilevile niwapongeze Wenyeviti wetu wote watatu waliochaguliwa na Bunge hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote mliochaguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwezi Oktoba 2010 na wale wote mlioteuliwa na Mheshimiwa Rais akiwemo Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawapongeza kwa dhati Wabunge wenzangu wote mlioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Wilson Mukama, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Aidha, nawapongeza waheshimiwa John Chiligati, Vuai A. Vuai, Mwigulu Nchemba, January Makamba na Nape Nnauye kwa kuteuliwa kwao katika nyadhifa nyeti ili waiongoze Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete kwa imani kubwa aliyointyesha kwangu na kunikabidhi Wizara hii ambayo ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu ili niweze kuiongoza. Nami napenda kusema imani huzaa imani na hivyo naahidi kwamba nitajitahidi kila niwezavyo kuifanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mbunge wa Kilosa, kwa Hotuba zao nzuri zilizolezea vema mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. Malengo, maelezo na vigezo vilivymo kwenye Hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyezeki wake mahiri, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyezeki wa Kamati, Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia Mbunge wa Kondoa Kusini, iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya

Wizara yangu tarehe 30 Mei, 2011. Wizara yangu imezingatia ushauri walioutoa na ambao umesaidia sana kuiboresha bajeti hii ninayoiwasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya awali, naomba sasa kuelezea mapitio ya utekelezaji wa maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, utekelezaji wa Mpango na Kazi kwa mwaka 2010/2011, Mpango wa Kazi wa mwaka 2011/2012 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kazi kwa mwaka 2010/2011. Utekelezaji wa mpango kazi wa Wizara ya Kazi na Ajira na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka 2010/2011 umezingatia Sera, Mpango na Mikakati ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, na Mkakakti wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Katika kipindi hiki Tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Wizara ya Kazi na Ajira. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi na ukaguzi wa viwango vya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sheria za Kazi, ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu za kazi, kuboresha hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2010/2011, Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) iliidhinishwa jumla ya shilingi 16, 965, 919,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 8,381,419,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 1,993,843,000/= kwa ajili ya malipo ya mishahara na shilingi 6,590,657,000/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Wizara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 9,626,012,267.81 sawa na 92.78% ya shilingi 10,375,262,000/= zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida. Aidha, Wizara ilitumia jumla ya shilingi 2,143,278,210.81 sawa na 32.52% ya shilingi 6,590,657,000/= zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya maendeleo. Kazi zilizotekeliza ni pamoja na:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi. Kufanya ukaguzi sehemu za kazi. Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Aidha, Wizara imeendelea kuwa karibu na Wafanyakazi na kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Wizara imeendelea kuhimiza maelewano mema baina ya Waajiri na Wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuza wa migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kufanya kaguzi sehemu za kazi pamoja na kutoa elimu ya Sheria za Kazi ili kuboresha utekelezaji na uzingataji wa Sheria za Kazi na kuchukua hatua stahiki pindi haki za Wafanyakazi zinapokiuwa. Wizara imefanya kaguzi 3,003 katika sehemu mbalimbali za kazi nchi nzima kwa lengo la kuona namna Sheria za Kazi zinavyozingatiwa na kutekeleza na Waajiri na Waajiri sehemu za kazi. Aidha, kaguzi hizi zinasaidia kuongeza uelewa na kubaini ukiukwaji wa sheria, kuzuia migogoro na kuboresha mahusiano mema mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imekamilisha dodoso litakalotumiwa na maafisa kazi, wakati wa kufanya kaguzi katika maeneo ya kazi ili kulinda haki za mama mjamzito na anayenyonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu ya Sheria za Kazi katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Jumla ya wafanyakazi 8,988 na Waajiri 450 wamenufaika na zoezi hili. Aidha, vitini 4,000 vya uelimishaji vimechapishwa na kuzambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uundaji wa vyombo vya ushirikishaji wafanyakazi. Wizara imeendelea kusimamia uundwaji na uimarishwaji wa vyombo vya ushirikishaji wa Wafanyakazi ili kuwawezesha kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayowagusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia dhana ya UTATU (*Tripartism*), Wizara imeunda na kuteua wajumbe wa Bodi za Mishahara za kisekta kumi na mbili. Bodi hizo ni za sekta za Ujenzi, Mawasiliano, Shule binafsi, Madini, Viwanda na Biashara, Ulinzi Binafsi, Afya, Maji, Majumbani, Mahoteli, Kilimo na Usafirishaji. Bodi hizi zitaishauri Wizara yangu kuhusu viwango vya chini vya mishahara katika sekta mbalimbali hapa nchini kulingana na hali ya uchumi wetu.

Aidha, Wizara imeratibu vikao viwili vya Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii (*ESCO*) ambavyo vilijadili na kushauri kuhusu masuala ya kanuni za Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, umuhimu wa ushirikishwaji wa Wafanyakazi katika uandaaji na utekelezaji wa Sera zinazogusa maslahi yao na migogoro sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia kwa Wafanyakazi. Wizara imekamilisha uandaaji wa Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Act*) Na. 20 ya mwaka 2008 ambapo Sheria hii inakusudia kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Pamoja na mambo mengine mfuko utatathmini na kuboresha viwango vya fidia vitakavyolipwa kwa Wafanyakazi wanaoumia, kupata magonjwa, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini. Maandalizi ya kuanzisha mfuko huu yamekamilika ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwa Sheria na Kanuni za Sheria hiyo kupitia Tangazo la Serikali Na.105 na Na.106.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi. Wizara imeendelea kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa usalama na afya mahali pa kazi, ambapo Rasimu ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Rasimu ya Sheria Mpya ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi zimeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya ajira ya mtoto na mazingira hatarishi ya kazi. Wizara inatekeleza Mpango wa Kutokomeza Ajira mbaya ya Mtoto katika Wilaya 18 za Tanzania Bara na Wilaya mbili za Tanzania Visiwani chini ya mradi uliofadhliliwa na idara ya kazi ya Serikali ya Marekani (*USDOL*) kupitia Shirika la kazi Duniani (*ILO*). Aidha, kamati ya kitaifa ya kuratibu masuala ya utumikishwaji wa Mtoto iliwezeshwa kutekeleza majukumu yake ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Brazil kupitia Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) yenye lengo la kusaidia utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa kutokomeza ajira ya mtoto hususan katika lengo la utoaji elimu kwa wadau katika Wilaya 128 za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha na kuendeleza hifadhi ya jamii nchini. Wizara imefanikisha uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) ambayo imeanza kufanya kazi mwezi Oktoba, 2010. Bodi ya mamlaka hii ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi Machi 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa mamlaka hii kutasaidia sana katika kupanua wigo wa huduma ya hifadhi ya jamii nchini na kuweka utaratibu wa kudhibiti sekta ya hifadhi ya jamii. Aidha, kuwepo kwa Msimamizi na Mdhibiti wa Hifadhi ya Jamii, kutasaidia sana kupunguza malalamiko ya watumishi wa sekta mbalimbali kuhusu mafao yanayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria sita za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kuziwianisha na Sheria Na.8 ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha mazingira wezesi ya uwekezaji na biashara. Wizara inafanya marekebisho katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya mwaka 2004 ili kuondoa vikwazo vya biashara kwa Wawekezaji. Lengo likiwa ni kuwapa fursa Waajiri ili waweze kuajiri Wafanyakazi katika mkataba wa muda maalum kwa kada na taaluma zote.

Aidha, rasimu ya Sheria ya Ajira imeandaliwa ambayo itaratibu na kurahisisha upatikanaji wa vibali vya ajira kwa wageni na kuchukua hatua za kinidhamu pindi yanapotokea makosa ya kiutendaji. Kwa ujumla hatua hizi zitasaidia kuwavutia wawekezaji lakini pia itaimarisha nafasi yetu ya ushindani wa kibiashara na nchi nyingine katika soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuzaji wa ajira nchini. Wizara imeendelea na uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira 2008 kwa kusambaza nakala 4,025 za Sera hiyo zikiwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa Wadau mbalimbali. Aidha, imekamilisha rasimu ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na vile vile imekamilisha rasimu ya Sheria Mpya ya Huduma za Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya kukuza Ajira nchini. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kushughulikia matatizo ya ajira kwa kutekeleza programu ya kitaifa ya kukuza ajira. Programu hii imeainisha maeneo makuu manne yanayopelekea kuongezeka kwa ajira ambayo ni:-

(i) Kukuza ajira kwa kuhamasisha uwekezaji katika sekta binafsi yenyewe uwezo wa kuibua fursa nyingi za ajira;

(ii) Kukuza ajira kwa kuimarisha uwekezaji wa Umma kwa kupitia Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi;

(iii) Kukuza ajira kwa kuongeza ujuzi wa nguvu kazi na upanuzi wa vyuo vya mafunzo na matumizi ya teknolojia (Teknohana) kama nyenzo ya kazi; na

(iv) Kujenga uwezo wa Taasisi zinazohusika na ukuzaji wa ajira ili kuweza kuratibu na kusimamia mpango mzima wa kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga fursa za ajira hasa kwa vijana. Wizara imeendelea kuhamasisha na kushirikiana na sekta zote za kiuchumi kuhuisha masuala ya ajira katika sera na programu zao za maendeleo. Wizara imeziwezesha Wizara sita (6) kufanya uchambuzi utakaowezesha kufahamu idadi ya ajira mpya zitakozosalishwa kutoptana na mipango yao ya maendeleo. Wizara zilizowezeshwa ni Kilimo, Chakula na UShirika, Viwanda, Biashara na Masoko, Mambo ya Ndani, Ujenzi, Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) chini ya Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa wa "ONE UN Joint Program (JP 1)", imefanikisha uanzishaji na uimarishaji wa kamati za kukuza ajira kwenye Wilaya zote za Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imeweza kutekeleza mradi wa majaribio unaoitwa 'Kazi Nje Nje', ambao unawajengea vijana uwezo wa mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kujiajiri na kuwasidia vijana wenzao waweze kujiajiri. Mpaka kufikia mwezi Februari, 2011 jumla ya vijana 50 wamehitimu mafunzo ya awali na kusambazwa katika Mikoa ya Pwani, Mbeya, Tabora, Singida, Mwanza, Mtwara, Lindi, Tanga, Arusha na Dar es Salaam kwa majaribio. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila kijana anasaidia angalau vijana wengine 100 kuanzisha shughuli ya kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira kwa kutayarisha Mwongozo wa kukusanya, kuchambua na kuhifadhi taarifa hizo ambao ukikamilika utawezesha Taifa kuwa na takwimu sahihi za matumizi ya Nguvu Kazi. Aidha, Wizara imeshirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa na Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango katika kufanya matayarisho ya utafiti wa Nguvu Kazi (*Manpower Survey*).

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti na ukaguzi wa vibali vya ajira za wageni. Wizara imeendelea kuimarisha taratibu za usimamizi, utoaji na ukaguzi wa vibali vya ajira za wageni kwa lengo la kulinda nafasi za ajira za Watanzania. Jumla ya maombi 2,776 ya vibali vipyta vya ajira za

wageni walioomba kwa mara ya kwanza yalipokelewa, ambapo maombi 1,880 yalikubaliwa, maombi 629 yalikataliwa, maombi 219 yalisitishwa kwa uchunguzi zaidi na maombi 48 yalipelekwa Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) kwa uhakiki. Aidha, maombi ya kuongeza muda yalikuwa 1,061, ambapo maombi 863 yalikubaliwa na 146 kukataliwa, maombi 48 yalisitishwa kwa uchunguzi na maombi 4 yalipelekwa *TIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya kagazi za vibali vya kazi katika makampuni 72 yaliyopewa vibali hivyo katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza, Kagera na Dar es Salaam. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani imefanya utafiti wa masuala ya Uhamaji nguvu kazi ambapo matokeo ya utafiti huo yataapelekea kuundwa kwa Sera ya Uhamaji Nguvu Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka 2010/2011 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Maombi mapya matatu ya usajili wa Vyama vya Wafanyakazi kutoka sekta ya usafirishaji na ya utalii yalipokelewa na kushughulikiwa. Vyama hivyo ni Tanzania "Union of Tourist Porters" (TAUTOPO), "Tanzania Road Transport Workers Union" (TARWOTU) na "Voice of Workers Association of Tanzania" (VOWOTA). Aidha, ombi moja la Waajiri lilipokelewa la kusajili umoja unaojulikana kama "East African Employers Organization" (EAO);

(ii) Kagazi 65 za kumbukumbu za Wanachama wa Vyama vya Wafanyakazi zilifanyika katika Mikoa 13 ya Tanzania Bara, ambayo ni Mwanza, Kigoma, Lindi, Mtwara, Mara, Shinyanga, Tanga, Kagera, Kilimanjaro, Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Katika kagazi hizo ilibainika kuwa Vyama vingi vinazingatia utunzaji wa kumbukumbu za Wanachama kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ushauri ultolewa kwa wale waliodhihirika kutozifahamu taratibu na kutakiwa kuzizingatia; na

(iii) Malalamiko kutoka Vyama vya Wafanyakazi yalipokelewa na kushughulikiwa. Vyama vilivyohusika ni Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Chama cha Wafanyakazi wa Mtandao wa Simu Tanzania (TEWUTA), Chama cha Wafanyakazi wa Ujenzi na Migodi (TAMICO), Chama cha Wafanyakazi Walinzi Binafsi (TUPSE), Chama cha Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani (CHODAWU) na Chama cha Mabaharia (TASU). Malalamiko mengi yalihusu kutozingatiwa kwa Sheria na Kanuni zake, Katiba za Vyama kutozingatiwa na kutoridhishwa na huduma mbalimbali zinazotolewa na Vyama kwa Wanachama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga uwezo wa Wizara. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kujenga uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kuratibu utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa Watumishi 21 wa Wizara wa kada mbalimbali. Aidha, mafunzo ya maadili, utawala bora sehemu za kazi na vita dhidi ya rushwa yalitolewa kwa Watumishi 87 wa Wizara;

(ii) Watumishi 124 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo, Watumishi 37 walioajiriwa wamethibitishwa kazini na Watumishi 20 wapya wameajiriwa;

(iii) Kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na kuwahudumia watumishi wa Wizara wanaoishi na virusi vya UKIMWI; na

(iv) Kujenga na kukarabati ofisi tano (5) za kazi zilizopo kwenye Wilaya za Korogwe, Lushoto, Tabora, Lindi na Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za Taasisi sita za Umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA), Shirika la Tija la Taifa (NIP), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii

(NSSF), Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) na Tume ya Usulu hishi na Uamuzi (CMA). Utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2010/2011 kupitia Taasisi hizi ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umeendelea kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwa kufanya kaguzi sehemu za kazi 5,376 za kawaida sawa na asilimia sabini na saba (77%) ya lengo na kaguzi maalum 9,591 sawa na asilimia sitini na tisa (69%) ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kaguzi hizo ilibainika kuwa baadhi ya Waajiri hawatoi taarifa za ajali zinapotoka, hawasajili sehemu za kazi, hivyo kusababisha ajali na kuhatarisha usalama na afya za Wafanyakazi. Jumla ya Waajiri 16 walichukuliwa hatua ya kutozwa faini na mashtaka dhidi ya Waajiri 23 yapo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa uchunguzi na hatua zaidi. Wakala inaandaa vigezo vitavyowezesha kutangaza Waajiri bora wanaozingatia na Waajiri wasiozingatia usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala pia imekuwa ikitoa elimu na ushauri kwa Waajiri na Wafanyakazi kuhusu usalama na afya mahali pa kazi. Wakala imetoa mafunzo kwa Maafisa wa usalama na afya mahali pa kazi 78, mafunzo kwa wafanya biashara wadogo wadogo na kati 105 kutoka Mikoa ya Ruvuma, Iringa na Singida na jumla ya Wafanyakazi 10,181 sawa na asilimia 101.8 ya lengo walipimwa afya zao ili kubaini matatizo na athari wanazopata kutohana na maeneo wanayofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala imeendelea kujitangaza kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo nya habari na tovuti yake ya www.osha.go.tz. Aidha, siku ya kimataifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Kitaifa iliadhishwa mkoani Ruvuma, tarehe 28 Aprili, 2011 kwa kauli mbiu "Mifumo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini: Nyenzo ya uboreshaji endelevu wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi".

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwahudumia jumla ya wateja 6,113, kati ya hao watafutakazi walikuwa 5,556 na Waajiri 557. Watafutakazi 845 waliunganishwa kwa Waajiri nchini. Aidha, Wakala ilisimamia na kuratibu ajira za Watanzania nchi za nje, ambapo watafutakazi 286 waliunganishwa na Waajiri, kati ya hao 279 nchini Oman na 7 katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE);

(ii) Wakala imefanya mawasiliano na nchi mbalimbali ili kuwezesha Watanzania kuajiriwa katika nchi za nje. Baadhi ya nchi hizo ni Kenya, Uganda, Rwanda, Qatar na Umoja wa Falme za Kiarabu. Tayari duru fu ya makubaliano (*bilateral agreement*) na Umoja wa Falme za Kiarabu imefanya; na

(iii) Wakala imeanzisha tovuti yenye jina la www.taesa.go.tz ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kutangaza huduma mbalimbali zitolewazo na Wakala na hivyo kuwafikia wadau wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Tija la Taifa (NIP) liliendelea kutoa mafunzo mbalimbali pamoja na ushauri ili kuinua tija sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika lilitoa mafunzo kwa washiriki 1,150 kuhusu tija kutoka Taasisi 77 sawa na asilimia 96.3 ya lengo liliopangwa. Aidha, Shirika liliifanya tafiti mbili (2) sawa na asilimia 50 ya lengo na kutoa huduma za ushauri elekezi katika kukuza tija kwa wateja 17 sawa na asilimia 57.0 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Shirika limeweza kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni 591,331.5 sawa na asilimia 85.1 ya lengo ambazo zimetumika katika kulipa mafao ya Wanachama, kuwekeza katika vitega uchumi, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo; na

(ii) Limeendesha semina 297 kwa Waajiri na Wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii. Vilevile kwa mara ya kwanza Shirika lilifanya Mkutano Mkuu wa wadau mwezi Februari 2011 huko jijini Arusha ambao ulihudhuriwa na wadau wapato 556.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la NSSF limechangia katika shughuli za maendeleo ya nchi yetu kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali muhimu kama ifuatavyo, naomba muendelee kuangalia katika *screen* miradi hiyo itakuwa inaoneshwa.

- (i) Ujenzi wa awamu ya pili wa majengo kwa ajili ya wanafunzi 15,000 wa Chuo cha Sayansi ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Dodoma, unaohusisha mabweni, madarasa, mabwalo ya chakula, majengo ya ofisi na viwanja vya michezo;
- (ii) Awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 87 huko Mtoni Kijichi Dar es Salaam ambao upo katika hatua za mwisho, ambapo awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 215 imeanza. Aidha, mradi wa ujenzi wa nyumba za Bugarika mkoani Mwanza upo katika hatua za awali;
- (iii) Ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi unaendelea katika Mikoa ya Kigoma na Arusha na katika Wilaya za Njombe na Kahama. Aidha, ujenzi wa majengo mengine katika Mikoa ya Morogoro, Arusha, Mbeya na Shinyanga umeanza;
- (iv) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambalo mnalionia hapo kwenye runinga, unaotarajiwa kuanza kabla ya mwisho wa mwaka 2011. Michoro imekamilika ambapo mkandarasi wa ujenzi anatarajiwa kupatikana mwezi Novemba 2011;
- (v) Ujenzi wa Chuo cha Nelson Mandela Arusha na ofisi za Wakala wa Ufilisi na Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA) unaendelea. Aidha, ujenzi wa jengo la Mzizima (*Ex-Aisco*) jijini Dar es Salaam na hoteli ya kisasa huko jijini Mwanza upo katika hatua za awali na Mkataba wa makubaliano na India wa ujenzi wa Hospitali ya Apolo umesainiwa;
- (vi) Uwekaji wa kompyuta katika ofisi za Shirika za Mikoa na Wilaya na kuziunganisha katika mtandao wa Shirika umekamilika;
- (vii) Ujenzi wa vituo vya kumbukumbu katika Mkoa wa Dodoma umekamilika na ujenzi kama huo unaendelea katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mara; na
- (viii) Ujenzi wa makazi na ofisi katika eneo la Mchikichini Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Imesajili Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii nchini na kuifanya tathmini ya awali mifuko husika;
- (ii) Imetayarisha Kanuni mbalimbali za uendeshaji wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii ili kuwianisha mafao na kuboresha uhai wa mifuko;
- (iii) Imeboresha mafao ya Wanachama kwa kuwezesha Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*) kutumia fomula moja badala ya mbili;

- (iv) Imefanikisha kuhamishiwa wanataaluma waliokuwa katika mfumo wa "Senior Staff Superannuation Scheme - SSSS" na kwenda katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) ili kuboresha mafao yao ya pensheni, ambapo Serikali itatoa Shilingi bilioni tisa (Tsh.9,000,000,000/=) katika kipindi cha miaka 10 kufidia michango yao;
- (v) Imesambaza nakala 6,000 za Sheria na Sera ya Hifadhi ya Jamii kwa wadau mbalimbali nchini; na
- (vi) Imetoa elimu na kufanya semina mbalimbali za wadau kuhusu majukumu ya Mamlaka na masuala ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*Commission for Mediation and Arbitration*) ni chombo chenye jukumu la kusuluhisha na inapolazimu kuamua juu ya migogoro ya kikazi. Upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Tume unaweza kupeleka shauri hilo Mahakama ya Kazi. Vilevile, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya Sheria za Kazi na uimarishaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu15), iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 2,320,879,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi 900,250,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Shilingi 744,129,000 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 676,500,000/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Tume ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 1,641,532,061 sawa na asilimia 99.83 ya shilingi 1,644,379,000/= zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida. Aidha, Tume ilitumia jumla ya shilingi 596,200,000 sawa na asilimia 88.13 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Tume iliendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Kazi zilizotekeliza ni pamoja na:-

- (i) Kusajili migogoro 8,177 ambapo migogoro 6,904 sawa na asilimia 84 ilisikilizwa na kupatiwa ufumbuzi. Migogoro 4,132 sawa na asilimia 60.9 ilimalizika kwa njia ya usuluhishi na migogoro 2,772 sawa na asilimia 39.1 kwa njia ya uamuzi. Migogoro 1,273 sawa na asilimia 16 inaendelea katika hatua mbalimbali ikiwemo kwenda Mahakama ya Kazi;
- (ii) Kusajili Mabaraza ya Wafanyakazi 141 na kutoa mafunzo kwa Taasisi 99 kuhusu matumizi sahihi ya Sheria za Kazi Na. 6 na Na. 7 zote za mwaka 2004, na kutoa ushauri juu ya faida ya ushirikishwaji Wafanyakazi katika sehemu za kazi kwa Taasisi 40;
- (iii) Tume kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imetengeneza kitabu cha rejea cha maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Volume I*) yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi;
- (iv) Mchakato wa kuandaa Kanuni za huduma muhimu (*Essential Services Rules*) umeanza;
- (v) Tume imeajiri jumla ya Watumishi wapya 55 wa kada mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi. Pia Tume imewaendeleza Watumishi katika fani za sheria, uhasibu na utunzaji wa kumbukumbu ili kuongeza ufanisi wa kazi; na
- (vi) Ofisi za kanda ya Dar es Salaam na Ofisi za Mikoa ya Iringa na Mbeya zimefanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia sheria na viwango vya kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi,

kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Utekelezaji kwa mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa kufanya ukaguzi sehemu za kazi, ili kuhakikisha kwamba Waajiri na Waajiriwananazangatia wajibu wao na kuwepo kwa mazingira bora ya kufanya kazi. Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kufanya kaguzi za kazi 6,200 katika maeneo mbalimbali ya kazi na kutoa elimu kwa Wafanyakazi na Waajiri juu ya utekelezaji wa Sheria za Kazi;
- (ii) Kuratibu na kukuza majadiliano ya UTATU kupitia Bodi za Mishahara za Kisekta na Baraza la Ushauri katika Masuala ya Uchumi, Kazi na Jamii (*LESCO*);
- (iii) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera hiyo ili kuboresha na kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii nchini;
- (iv) Kuratibu uhuishaji wa Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa lengo la kuboresha huduma za Hifadhi ya Jamii;
- (v) Kukamilisha taratibu za kuridhia Mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO Conventions*) kuhusu masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi;
- (vi) Kusimamia uanzishwaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara wakiwa kazini;
- (vii) Kusimamia na kuratibu mipango ya utokomezaji wa utumikishwaji wa mtoto; na
- (viii) Kuratibu ushiriki wa wajumbe wa Tanzania katika mikutano ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuifanya marekebisho Sekta ya Hifadhi ya Jamii ili iweze kuwanufaisha zaidi Wanachama na kupanua wigo ili Watanzania wengi zaidi waweze kufaidika. Wizara itaendelea na Programu ya maboresho ambayo yatekelezwa kwa awamu kuanzia mwaka 2010/2011. Maboresho hayo yanahusisha marekebisho ya Sera, Sheria za Hifadhi ya Jamii na utafiti wa kuongeza wigo wa Watanzania walio katika sekta isiyo rasmi na hata Wazee kutambuliwa katika Mfumo wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukuza ajira za staha nchini, katika mwaka 2011/2012 Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kuhamasisha uanzishaji wa Kamati za kukuza ajira katika Mikoa nane (8) ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Mwanza na Kamati 46 za Miji/Manispaa/ na Halmashauri za Wilaya;
- (ii) Kukamilisha na kuchapisha Sheria mpya ya Kukuza Ajira pamoja na kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ajira hususan kwa vijana;
- (iv) Kushughulikia maombi ya vibali vya ajira za wageni na kufanya kaguzi kwenye Kampuni zilizoajiri wageni kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*);
- (v) Kutayarisha na kusambaza kwa wadau Mwongozo wa kuhuisha masuala ya ajira kwenye mipango ya nchi;
- (vi) Kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira na vilevile kukamilisha mwongozo wa kukusanya na kutathmini taarifa hizo;

- (vii) Kushiriki kwenye maandalizi ya utafiti wa Nguvu Kazi katika Sekta Isiyo Rasmi;
- (viii) Kufanya tathmini ya mpango wa kuwezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
- (ix) Kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali wadogo katika maonesho ya kila mwaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Nguvu Kazi/Jua Kali yanayotarajiwa kufanyika nchini Uganda mwezi Novemba 2011;
- (x) Kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Uhamaji wa Nguvu Kazi (*Labour Migration Policy*); na
- (xi) Kufanya tathmini na mapitio katika Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri katika mwaka 2011/2012, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kushughulikia maombi ya usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri na kuwaelimisha wadau juu ya taratibu za kujunga na Vyama na umuhimu wa Vyama hivyo kwa Wanachama;
- (ii) Kufanya kaguzi 80 za kumbukumbu za Wanachama na fedha katika Mikoa 15 na matawi ya Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri; na
- (iii) Kushughulikia malalamiko mbalimbali ya Vyama na kutoa ushauri stahiki kwa lengo la kujenga mahusiano mazuri baina ya Chama na Chama na pia Wanachama na Viongozi wa Vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujenga uwezo wa Wizara katika mwaka 2011/2012, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Watumishi wa Wizara ili kutoa huduma bora na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Utendaji Kazi (*OPRAS*);
- (ii) Kufanya tathmini ya mahitaji ya ukarabati na uboreshaji wa ofisi saba (7) za kazi na ajira katika Wilaya za Dodoma Mjini, Musoma, Sumbawanga, Ifakara, Moshi, Singida na Mbeya;
- (iii) Kukarabati na kuboresha ofisi nne (4) za kazi na ajira ikiwa ni pamoa na ununuzi wa vitendea kazi na samani katika Wilaya za Dodoma Mjini, Musoma, Sumbawanga na Singida;
- (iv) Kuratibu ushirikishwaji na kuimarisha mahusiano bora kwa Watumishi wa Wizara kwa kufanya Mikutano ya Wafanyakazi na kushiriki shughuli za michezo; na
- (v) Kujenga ufahamu kwa Watumishi wa jinsi ya kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI na vita dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA). Ili kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala utatekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kufanya kaguzi 7,000 za kawaida na 14,000 maalumu za usalama na afya sehemu za kazi na kupima afya za Wafanyakazi 13,000 katika sehemu mbali mbali za kazi;
- (ii) Kutoa mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi hususani namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Usalama na Afya Mahali pa Kazi;
- (iii) Kukamilisha uandaaji wa Sheria mpya ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi pamoja na Kanuni zake. Vilevile kukamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi;
- (iv) Kuratibu utekelezaji wa kuridhia Mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO Conventions*) kuhusu masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, ambayo ni Mkataba Na.155 (*Occupational Safety and Health Convention, 1991*), Mkataba Na. 167 (*Safety and Health in Construction Convention, 1988*) na Mkataba Na. 187 (*Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) umepanga kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuboresha ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa Taarifa za Soko la Ajira; na
- (ii) Kuwaunganisha Watafuta kazi na Waajiri ndani na nje ya nchi na kufanya utafiti wa upatikanaji wa fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Shirika la Tija la Taifa limepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuendesha mafunzo 80 ya uongozi kwa watumishi 1,300 kutoka Taasisi za Umma na binafsi;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa wateja 30 katika sekta za Umma na binafsi;
- (iii) Kufanya tafiti nne katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) litatekeleza kazi zifuatizo:-

- (i) Kukusanya jumla ya Shilingi milioni 833,553.7 na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya Wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo;
- (ii) Kuimarišha uandikishaji na ukusanyaji michango ya Wanachama, kuendelea na ukusanyaji wa madeni na pango. Vile vile kuboresha huduma kwa wateja na kujenga uwezo katika Shirika na kutafuta vyanzo vingine vya kugharamia miradi ya muda mrefu inayohitaji fedha nyangi kwa njia ya ubia (*Joint venture*);
- (iii) Kuendelea kutoa elimu kwa Wanachama, Waajiri na Umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii;
- (iv) Kuendelea kufanya upembizi yakinifu ili kuangalia upya mahitaji ya Wanachama kulingana na mahitaji ya sasa ya Hifadhi ya Jamii;
- (v) Kukamilisha utekelezaji wa mradi wa uzalishaji umeme wa megwati 300 katika eneo la Mkuranga ambapo Mshauri Mwelekezi amepatikana. Inatarajiwa kuwa mradi huu ukikamilika utazalisha umeme utakaoingizwa katika gridi ya Taifa;

- (vi) Kukamilisha ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Njombe na kuendeleza ujenzi katika Mikoa ya Morogoro, Arusha, Mbeya, Shinyanga na Wilaya ya Kahama. Aidha, Shirika litaanzisha ujenzi wa majengo ya ofisi katika Wilaya ya Temeke na llala;
- (vii) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni, Hospitali ya Apollo jijini Dar es Salaam, Chuo cha Nelson Mandela Arusha, ofisi za Wakala wa Ufilisi na Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), jengo la Mzizima (*Ex-Aiscc*) jijini Dar es Salaam, Hoteli ya kisasa Mwanza na ujenzi wa kijiji cha kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu "*Farm*");
- (viii) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Udongo na Miamba (*College of Earth Science*) na Chuo cha Sayansi na Hisabati (*College of Mathematics*) katika Chuo Kikuu cha Dodoma na ujenzi wa nyumba za Polisi awamu ya tatu endapo majadiliano ya udhamini wa Serikali yatakuwa yamekamilika;
- (ix) Kukamilisha ujenzi wa ofisi za kumbukumbu katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mara; na
- (x) Kuendelea na ujenzi wa makazi, biashara na ofisi katika eneo la Mchikichini, Manispaa ya llala jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) itaendelea na hatua za kuboresha sekta ya Hifadhi ya jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuandaa Kanuni zitakazotoa mwongozo wa kuwezesha malipo ya pensheni kujipwa kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa kipindi husika pamoja na uwekezaji katika vitega uchumi;
- (ii) Kuandaa Mikakati ya kuongeza wigo wa hifadhi ya Jamii ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi na kuongeza uelewa wa hifadhi ya jamii kwa wananchi;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa uhuishaji wa Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa lengo la kuboresha huduma za Hifadhi ya Jamii;
- (iv) Kuwezesha tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kaguzi mbalimbali ili kupima utekelezaji wa mageuzi;
- (v) Kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi kwenye sekta ya Hifadhi ya Jamii;
- (vi) Kufanya tafiti mbili kwa lengo la kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii na kutoa pensheni kwa wazee;
- (vii) Kutoa elimu kwa Umma ikiwa ni pamoja na kuanzisha wiki ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2011/2012, Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 18,148,986,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wake wa mwaka. Kati ya fedha hizi Shilingi 12,204,111,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 5,944,875,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, Tume imeweka kipaumbele katika kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kusuluuhisha na kuamua migogoro ya kikazi na kuandaa taarifa;

- (ii) Kufanya utafiti juu ya malalamiko ya Wafanyakazi ambayo hayajatolewa taarifa katika Tume na kuyashughulikia;
- (iii) Kusimamia uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi sehemu za kazi;
- (iv) Kuendesha mafunzo ya uelewa kwa Waajiri na Wafanyakazi juu ya matumizi sahihi ya Sheria za Kazi;
- (v) Kujenga uwezo wa Tume kwa kuwaendeleza watumishi, kutembelea nchi zinazoendesha shughuli za utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na uamuzi kwa lengo la kujifunza;
- (vi) Kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*);
- (vii) Kuboresha mazingira ya uandaaji na utunzaji taarifa kwa njia ya Elektroniki (*Digitization of filing system*);
- (viii) Kutengeneza juzu ya pili ya kitabu cha rejea ya maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Volume II*) yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kwa matumizi ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2011/2012, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inaomba jumla ya Shilingi 2,814,780,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,810,280,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,004,500,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, tangu nilipoteuliwa katika Wizara hii nimefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu na Taasisi zake. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudhi zao kubwa walizonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga (Mb), kaka yangu na Naibu Waziri wa Kazi na Ajira kwa ushirikiano na ushauri wake wa karibu. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Eric F. Shitindi pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Bibi Edine E. Mangesho. Aidha, nawashukuru sana Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Bodi zao kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii. Kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru sana Mwalimu wangu wa kwanza katika Wizara hii kuhusu masuala ya *labour* ambaye ni msaidizi wangu Bwana Fugara Mwanjali ambaye mpaka sasa anaendelea kunisaidia sana katika kumudu kazi zangu katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii – (*LESCO*), Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia mara kwa mara katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo Tumeshirikiana nazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya Washirika wa Maendeleo ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na Washirika wa maendeleo mbalimbali ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yetu. Hivyo, napenda shukrani za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani (ILO), UNDP, UNICEF, UNFPA,

Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark (DANIDA), Idara ya Kazi ya Marekani na Benki ya Dunia (WB). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi, namshukuru Spika na Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. Natoa pia shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango, ushauri wao na ushirikiano mkubwa wanaonionyesha tangu nilipoteuliwa kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Mara walionipigia kura kwa moyo wao wote na kwa mara ya pili wakanizezesha kuwepo Bungeni ambapo Mheshimiwa Rais aliniteua katika nafasi hii. Nawashukuru sana, naahidi nitaendelea kuwa pamoja nao katika kuwatumikia kwa uaminifu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, familia yangu imekuwa nguzo kubwa sana katika kuniwezesha kumudu mikikimikiki ya maisha na kwa wakati huohuo kunipa faraja kubwa ambayo imenisaidia sana kumudu kazi nilizonazo ambazo nimekabidhiwa na Taifa. Katika nafasi hii, naomba nimshukuru sana binti yetu Patricia Robi pamoja na mume wake Joel pamoja na wajukuu zangu Tina na Angelo kwa faraja kubwa na usaidizi mkubwa wanaonipa. Pia nawashukuru sana wadogo zangu Modesta, Veneranda na Albinus kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendelea kumlea mama yetu na kwa hili najua Mungu atawaongezea maisha hasa duniani na baadaye kheri huko mbinguni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu na kazi kwa mwaka 2010/2011 na Mpango wa Kazi kwa mwaka 2011/2012, Wizara inawasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 na Fungu 15 kama ifuatavyo:-

(a) **Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira**

(i)	Matumizi ya Kawaida Shilingi	12,204,111,000.00
(ii)	Miradi ya Maendeleo Shilingi	<u>5,944,875,000.00</u>
	Jumla Shilingi	<u>18,148,986,000.00</u>

(b) **Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

(i)	Matumizi ya Kawaida Shilingi	1,810,280,000.00
(ii)	Miradi ya Maendeleo Shilingi	<u>1,004,500,000.00</u>
	Jumla Shilingi	<u>2,814,780,000.00</u>

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ndiyo inashughulikia Hifadhi ya Jamii kwa ujumla. kwa hivyo leo, pamoja na NSSF, lakini pia tunasimamia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya GEPF ambao wameleta maonyesho yao hapa. Mfuko wa GEPF uko mstari wa mbele katika kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii hasa kutumia sekta isiyo rasmi. Hivyo nawakaribisha Waheshimiwa Wabunge waangalie maonyesho haya na washawishike kuijunga na hifadhi hizi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja illitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka kwa hotuba nzuri. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii au Msemaji wake.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 na Kanuni ya 114 za Bunge (2007), nachukua nafasi hii kwa kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Majukumu ya Kamati hii ni pamoja na kufikiria na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira Dar es Salaam tarehe 30 Mei, 2011 na kupata maelezo ya Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, (Mb) Waziri wa Kazi na Ajira, ambayo yalihusu utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2011/2012, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2010/2011 na Malengo yaliyomo katika Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika kufikiria taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira ya mwaka 2010/2011 na Bajeti ya mwaka 2011/2012 ilizingatia miongozo muhimu ya Wizara ikiwa ni pamoja na dira, dhima, majukumu na malengo ya Wizara. Katika kikao hicho Kamati ilhoji utekelezaji wa sekta mbalimbali za Wizara ya Kazi na Ajira. Aidha, Kamati iliipitia Bajeti ya mwaka 2011/2012, malengo yaliyowekwa na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Bajeti ya mwaka 2010/2011. Katika mwaka wa Fedha uliopita wa 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali na hasa katika maeneo yafuatayo:-

- (a) Serikali iweke mikakati ya kuboresha mafao ya Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Aidha, mifuko itafute njia bora ya kusaidia Wanachama hata kabla ya kustaifu;
- (b) Serikali iharakishe mchakato wa kuridhia mkataba utakaowezesha Shirika la NSSF kutoa fedha ya ujenzi wa daraja la Kigamboni mapema iwezekanavyo;
- (c) Serikali iweke muda wa kuanza kazi ya ujenzi wa daraja hili (*timeframe*) badala ya kuendelea kusema kwamba ipo kwenye mchakato.
- (d) Mara kazi ya ujenzi wa daraja itakapoanza Serikali iweke mikakati ya kukabiliana na changamoto ili kazi ya ujenzi iweze kuwa na manufaa kwa taifa;
- (e) Ili mradi huu uweze kuwa na manufaa kwa taifa, Serikali iweke mikakati ya kujenga barabara za kuunganisha daraja la Kigamboni na mji wa Dar- Es Salaam;
- (f) Serikali na uongozi wa OSHA uweke mikakati madhubuti ya kukamilisha utaratibu wa kufanya marekebisho katika Sera ya Usalama na Afya mahali pa Kazi na kutunga Sheria ya kutekeleza Sera hiyo;
- (g) Serikali itenye fedha za kutosha na kuwezesha OSHA kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuanzisha Ofisi za kanda 6 nchi nzima na kuweza kushughulikia na kudhibiti matatizo mbalimbali yanayotokea katika viwanda na maofisi mbalimbali;
- (h) Shirika la OSHA watoe taarifa ya ukaguzi wa viwanda 10 bora vinavyozingatia usalama na afya mahali pa kazi na viwanda 10 visivyozingatia;

- (i) Mifuko mingine ya hifadhi za jamii kama vile *PSPF*, *LAPF*, *PPF* ione uwezekano wa kuanzisha ujenzi wa nyumba za bei nafuu na kupunguzia wananchi adha ya kukosa makazi bora; Aidha, Serikali itoe dhamana kwa mifuko hiyo ili kuipa mazingira mazuri ya kufanya kazi hizo kwa ufanisi zaidi;
- (j) Serikali iweke sera bora ya kuboresha mafao ya Wanachama wa hifadhi za jamii na pia mifuko itafute namna ya kumhudumia Mwanachama wake hata kabla ya kustaafu na kufariki; na
- (k) Serikali kupitia Hal mashauri ya Jiji la Dar es Salaam iharakishe kukamilisha taratibu za kukabidhi jengo la *Machinga Complex* kwa uongozi wa Wafanyabiashara ndogondogo ili waweze kulitumia na kuachana na biashara za kutangatanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa ufanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi na Ajira kuhusu maagizo ya Kamati, Wizara imejitahidi kutekeleza maeneo kadhaa na mengine bado Kamati inahitaji kujua zaidi utekelezaji wa maagizo yaliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 Wizara iliidhinishiwa na Bunge Matumizi ya shilingi 16,769,578,000/=; na Tume ya Usuluhishi na Uamuji iliidhinishiwa Shilingi 2,316,294,170/=. Mheshimiwa Waziri allieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011. Baadhi ya shughuli zilizotekeliza na mafanikio yake ni kama ifuatavyo:-

- (i) Watumishi 124 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo, watumishi 37 walioajiriwa wamethibitishwa kazini na watumishi 20 wapya wameajiriwa;
- (ii) Wizara imeratibu utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi 21 wa Wizara wa kada mbalimbali;
- (iii) Ukaguzi wa mapato na matumizi ya Wizara umefanya katika Ofisi za kazi za Mikoa na Wilaya pamoja na Makao Makuu ya Wizara;
- (iv) Wananchi wameelimishwa kuhusu shughuli za Wizara kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mikutano ya waandishi wa habari;
- (v) Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani imekamilisha dodoso litakalotumiwa na Maafisa kazi wakati wa kufanya kaguzi katika maeneo ya kazi ili kulinda haki za mama mjamzito na anayenyonyesha;
- (vi) Wizara imesambaza nakala 4025 za Sera ya Taifa ya Ajira kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa wadau mbalimbali;
- (vii) Wizara imefanya kaguzi za vibali vya kazi katika makampuni 72 yaliyopewa vibali hivyo katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza, Kagera na Dar es Salaam;
- (viii) Malalamiko kutoka Vyama vya wafanyakazi vikiwemo Chama cha Walimu Tanzania (CHAWATA), Chama cha wafanyakazi wa Ujenzi na Migodi (TAMICO), Chama cha Mabaharia (TASU), Chama cha Wafanyakazi walinzi binafsi (TUPSE) yalipokelewa na kusikilizwa; na
- (ix) Wizara kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuji ilisajili migogoro 6612 ambapo migogoro 4778 sawa na asilimia 72.2 ilisikilizwa na kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake, kwa Mwaka 2011/2012 imeomba shilingi 20,963,766,000 kati ya hizo shilingi 18,148,986,000 ni kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 na kiasi cha Shilingi 2,814,780,000 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 15. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali ijitahidi kuongeza fedha katika Wizara hii ili kuwezesha Taasisi za kusimamia kazi na ajira kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Wizara ya Kazi na Ajira inasimamia sekta muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa kama vile sekta za Kazi, Ajira, Hifadhi ya Jamii na kadhalika. Hivyo basi, ni vema sekta hizi zikaangaliwa kwa umakini kutokana na ukweli kwamba maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla yanategemea sana mazingira bora ya utekelezaji wa viwango vya kazi, usawa na kazi za staha na nafasi za ajira za kutosheleza mahitaji nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wafanyakazi. Ziko Sheria kadhaa zinazohusu kazi na ajira mfano, Sheria na 6 ya Mwaka 2004 ya Ajira na Mahusiano Kazini, pamoja na Sheria hizo bado kumekuwepo na migogoro inayojitokeza mara kwa mara hasa katika baadhi ya Viwanda, Makampuni na Mashirika mbalimbali nchini kutokana na Waajiri kutotekeleza baadhi ya Sheria na Kanuni za Ajira. Kamati inashauri Serikali kuendeleza juhudhi zake za kutoa elimu kwa Waajiri kuhusu Sheria na Kanuni za Ajira na kuhakikisha zinafuatwa. Hatua hii italeta amani sehemu za kazi kwa kulinda haki na wajibu wa wafanyakazi na Waajiri.

Aidha, Kamati inashukuru Serikali kwa kuendelea kupandisha mishahara ya wafanyakazi japo Kamati inashauri Serikali kuangalia njia ya kudumu ya kufanya hivyo. Migogoro mingi ya wafanyakazi wa sekta binafsi na Serikali imekuwa ikitokea kutokana na kudai mishahara na marupurupu. Kumekuwa na migomo na migogoro mingi nchini inayohusu wafanyakazi na wakati mwingine migogoro au migomo hiyo imepelekea usumbu mkubwa kwa wafanyakazi na hata wananchi kwa ujumla kwa kukosa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza Serikali ione umuhimu wa kuanza kuitambua migogoro yote ya ajira iliyopo nchini, ya muda mrefu na muda mfupi na kuitengenezea mpango kazi ili kuitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Wafanyakazi. Vyama vya Wafanyakazi vipo kwa mujibu wa Sheria za nchi na lengo kubwa ni kusaidia kuleta tija katika kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Vyama vya wafanyakazi visimamie maslahi ya wafanyakazi kwa kuwaelimisha kuhusu haki zao za msingi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Ajira. Kama hili litazingatiwa, itasaidia kupunguza uonevu, migomo na migogoro mbalimbali sehemu za kazi hivyo kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama na afya mahali pa kazi. Suala la usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi ni la muhimu na Kamati imebaini bado kuna upungufu katika utekelezaji na kwa kuwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ndio mhusika anayepaswa kufanya kazi ya ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi, Kamati inaagiza kwa mara nyininge OSHA iendelee kufanya kaguzi za viwanda na makampuni mbalimbali nchini na kuleta taarifa ya ukaguzi huo unaohusu usalama na afya mahali pa kazi. Aidha, Serikali longeze bajeti katika eneo hili ili kufanikisha kaguzi hizo. Hii italeta chachu na changamoto kwa viwanda vingine na Mashirika kujenga tabia ya ushindani katika kuimarisha mazingira ya kazi na afya za wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha usalama na afya mahali pa kazi, Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuhakikisha Waajiri wanafuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Usalama mahala pa kazi. Hii ni pamoja na kuhakikisha wafanyakazi hasa wa viwandani, wanapatiwa vifaa maalum vya kujikinga mahali pa kazi (*Personal Protection Equipments*) kama vile *masks, gloves, safety boots* na *overalls* kwani afya ya Watanzania wengi ziko katika hatihati na tusipozingatia suala hili Taifa gharama kubwa ya kutibu afya ya Watanzania kwa kutokana na madhara haya. Aidha, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuhakikisha Uongozi wa Viwanda na makampuni unaweka utaratibu wa kupima afya za wafanyakazi mara kwa mara ili kubaini afya za wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa siku ya tarehe 28 Aprili kila mwaka ni siku ya usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi na kwa kuwa maeneo mengi ya viwanda na kazi hasa binafsi si salama kwa wafanyakazi na jamii inayowazunguka, Kamati inashauri Serikali kutumia siku hiyo kutoa elimu kwa Umma kuhusu masuala mbalimbali ya usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Jamii Nchini. Hifadhi ya Jamii huunganisha Sera na Mipango katika kupunguza umaskini na kumlinda Mwanachama na tishio la kupungua kwa uwezo wake kiuchumi na vile vile kumhakikishia kipato baada ya kukosa uwezo wa kufanya kazi.

Hifadhi ya Jamii kama ilivyo katika nchi nydingine, ni kinga dhidi ya majanga mbalimbali kama vile ugonjwa, ulemavu na kukosa ajira, na kwa kiasi kikubwa hifadhi ya jamii inasaidia kujenga usawa katika jamii na kuondoa umaskini. Nchi yetu imekuwa bado inatatizo kubwa la umasikini wa kipato kwani pengo kati ya walionacho na wasionacho ni linazidi kuwa kubwa. Tunaipongeza Serikali kwa juhudhi mbalimbali za kuondoa tatizo hilo, nchi nydingi duniani hutumia mifumo ya hifadhi ya jamii kuwaondolea kero mbalimbali wananchi wake. Hata hivyo, bado wananchi wana uelewa mdogo kuhusu hifadhi ya Jamii na ni jukumu letu Wabunge na Serikali kwa ujumla kuhakikisha wananchi wetu wanaelimishwa kuhusu jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibit wa Hifadhi ya Jamii. Tunaishukuru Serikali kuitia Bunge kwa kuitisha Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibit wa Hifadhi ya Jamii (Sheria namba 8 ya Mwaka 2008). Mamlaka hii ndio mdhibiti rasmi wa kusimamia Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii na kuhakikisha kwamba Mifuko inaendeshwa kwa kufuata kanuni na taratibu za kisheria za mafao na maslahi ya Wanachama. Aidha, Mamlaka inakusudia kuongeza wigo wa hifadhi za jamii kwa makundi ambayo hayajafikiwa na huduma hii kama vile wakulima, wafugaji na wananchi wa vijijini na kuwajengea uelewa kuhusu hifadhi ya Jamii. Kamati ina imani kuwa Mamlaka kwa kutumia sheria itaweza kurekebisha kasoro ya kutokuwepo kwa ushindani ulio sawa kati ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibit wa Hifadhi ya Jamii (Sheria namba 8 ya Mwaka 2008) inaonekana kuwa na upungufu na kwa kuwa Mamlaka imeanza mchakato wa kufanya marekebisheso, Kamati inashauri marekebisheso hayo yafanyike haraka iwezekanavyo ili kuisaidia Mamlaka kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibit wa Hifadhi ya Jamii bado ni mpya na inahitaji kujitangaza na kwa kuwa Mamlaka hii inahitaji Bajeti kubwa ili kumudu kuijendesha na kutoa elimu kwa jamii kuhusu kazi zake, Kamati inashauri Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii itenye fedha kwa ajili ya kuiwezesha kufanya kazi zake ipasavyo kwani Bajeti ya Serikali pekee haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayoiweka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii chini ya Wizara tofauti inaleta vikwazo kwa Mamlaka kufanya mawasiliano na kuratibu Mifuko inavyotakiwa, mfano PPF, PSPF na GEPF zipo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, NSSF ipo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, LAPF ipo chini ya TAMISEMI na NHIF ipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kufanya Marekebisheso ya Sheria ili mifuko yote iwe chini ya Wizara moja. Aidha, Kamati inashauri sera zote zinazohusu hifadhi ya Jamii zihusianishwe na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo uliopo sasa hauruhusu Mwanachama mmoja kuhamia mfuko mwengine, Kamati inasisitiza kwamba, kwa kuwa Sheria Namba 8 ya Mwaka 2008 inaitaka Mamlaka kuweka utaratibu wa Mwanachama kuhama kutoka mfuko mmoja kwenda mwengine. Kamati inashauri mchakato wa kuanzisha utaratibu huu uanze mapema iwezekanavyo ili kuwanufaisha Wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pensheni kwa Wazee. Pamoja na juhudhi kubwa za Serikali katika kuwashudumia wazee kama vile matibabu ya bure, bado wazee wanakabiliana na matatizo mengi ukizingatia asilimia 53 ya yatima nchini wanalelewa na wazee. Aidha, wazee hawana mikopo na huugua mara kwa mara. Ni asilimia nne (4%) tu ya wazee milioni mbili hapa nchini ambao wako katika mfumo rasmi wa pensheni. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira ameonyesha kuanza kusimamia suala hili kwa karibu na kwakuwa utafiti umeonesha uwezekano wa kulipa pensheni kwa wazee wote kumeonyesha mabadiliko makubwa katika nchi nydingi zilizoanzisha utaratibu huu kama vile:-

- (i) Wazee wenyewe wamenawiri;
- (ii) Gharama za Serikali kutibu wazee zimepungua;
- (iii) Uchumi wa vijijiini umeimarika;
- (iv) Mzunguko wa fedha hasa vijijiini utaongezeka na kuongeza ajira kwa vijana;
- (v) Lishe na elimu vijijiini vitaimarika; na
- (vi) Jamii itaongeza upendo kwa Serikali yao.

Kamati inaagiza kuwa mwakani Serikali ianze kutoa pensheni kwa wazee kwani Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaahidi Serikali kuanza kutoa pensheni kwa wazee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazee wanapata tabu sana, wanateseka sana na ukizingatia wazee ni watu muhimu sana. Kamati inaomba sana Serikali isaidie kufanikisha azima hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Takwimu zilizopo hivi sasa zinaonyesha kuwa, kati ya nguvu kazi inayokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 20 ya Watanzania wote, ni takriban asilimia sita tu ndiyo wanapata huduma za Hifadhi ya Jamii. Takwimu hii inadhiihirisha kuwa bado kuna uelewa mdogo wa hifadhi ya jamii kwa watunga sera, Waajiri, Waajiriwa, Wanachama na wananchi kwa ujumla. Kamati inashauri elimu kwa Umma kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) iendelee kutolewa kwa jamii hasa katika maeneo ya Wilayani na vijijiini. Hii itasaidia wananchi wengi wa sekta binafsi ikijumuisha wakulima, wavuvi na wachimbaji wadogo wa madini kupata uelewa na kujunga katika mifuko hii kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla na hasa katika kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* ni Shirika lilioweza kufanya vizuri hapa nchini na hasa katika uwekezaji kwa manufaa ya nchi yetu na hii inajidhihirisha katika uwekezaji mbalimbali na hasa Chuo Kikuu cha Dodoma, Serikali imekuwa ikiingia mikataba na Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) katika ujenzi wa miradi mbalimbali, hata hivyo Serikali huchukua muda mrefu kuanza kulipa gharama za miradi hiyo baada ya kukabidhiwa. Kamati inashauri Serikali kusaini mikataba ya ujenzi na kulipa madeni yake kwa utaratibu uliopangwa ili kuwezesha mfuko kumudu kuendelea na kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waajiri wamekuwa hawawasilishi michango ya wafanyakazi kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa na wengine wamekuwa hawawasilishi kabisa. Kamati inashauri Waajiri na wafanyakazi waendelee kupewa mafunzo kuhusu sheria za uchangiaji katika uhifadhi wa jamii, vilevile Waajiri ambao hawachangii kabisa wawaibishwe kisheria kwani tatizo hili limikuwa likisumbua sana uendeshaji wa mifuko na hata *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inalipongeza Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2011/2012, Shirika linataraja kuanza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika eneo la Kigamboni, hii itasaidia wananchi wengi wenye kipato cha chini kupata makazi bora. Vilevile, Kamati inalipongeza Shirika kwa kujenga ofisi na vitega uchumi katika Mikoa ya Kigoma na Arusha na katika Wilaya za Njombe na Kahama. Hata hivyo, Kamati inashauri Shirika kuendelea kujenga vitega uchumi katika Wilaya hasa ambazo zinaonekana kuwa nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ajira. Tatizo la ajira linazidi kukuwa kwa kiasi kikubwa hapa nchini na linaendana na ongezeko kubwa la watu kwa mfano, asilimia 47 ya Watanzania wote ni walio chini ya umri wa miaka 15, na zaidi ya asilimia 49 ya Watanzania ni vijana na watu wazima kati ya umri wa miaka 15-64 na asilimia nne (4%) iliyobaki ni wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama nchi nyingine zinazoendelea, uchumi wake unategemea kilimo. Takribani asilimia 69 ya wanawake na asilimia 62 ya wanaume wanategemea

kilimo. Ni asilimia 17 tu ya wanawake na asilimia 13 tu ya wanaume wako katika ajira rasmi ambazo ziliJulikana toka mwanzo kama *white colour jobs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wamekuwa wakimaliza masomo katika Vyuo na Taasisi mbalimbali lakini wameshindwa kupata ajira. Hili ni tatizo kubwa kwani hatutaweza kufikia malengo ya millennia wala kupunguza au kuondoa umaskini kama hatutatua tatizo la ajira. Tunaomba Serikali sasa katika mambo ya kushughulikia kama kipaumbele ni pamoja na tatizo hili la ajira na hasa kwa vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri uwekezaji katika sekta ya mawasiliano, sekta binafsi, *human capital, domestic mobilization* na *informal sector* utakuwa ni suluhisho kubwa la tatizo la ajira. Hata hivyo, nchi nyingi za Ulaya na Amerika zimeongeza uhitaji wa vyakula vya kiafrika na hii ni kutokana na ongezeko la waafrika wengi katika nchi hizo. Mwanya huu ukitumiwa vizuri ni njia nyingine ya kuongeza ajira. Kamati inashauri Serikali kutambua hali ya mazingira tuliyonayo kama mito na mabonde na kuleta kilimo cha kisasa ili kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za wageni. Kwa muda mrefu sasa tumeshuhudia kuwepo kwa malalamiko mengi ya kuashiria kuwa hali si njema sana katika mfumo wa ajira hasa zisizo rasmi, wageni wengi wameonekana kuwa na ajira katika maeneo ya hoteli, viwanda na kadhalika, wageni wameshika nafasi nyeti na za juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa Kamati wangependa kufahamu kama ni kweli vijana wetu wasomi na waliomiliza Vyuo vikuu wameshindwa kweli kuandaliwa kushika nafasi hizo katika nchi yetu? Kama kuna udhaifu au matatizo ni wakati muafaka wa kuangalia hayo, kwa sasa sekta ya mawasiliano inafunguka sana, soko la pamoja la Afrika Mashariki nalo haliko nyuma na mianya mingine mingi ya kibashara, ingawa bado mataifa ya kigeni yameendelea kuvamia hata sekta isiyo rasmi ya biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri ni lazima sasa tuwaamshe vijana wetu na tujamshe wenyewe ili tufanikiwe katika mipango yetu ya upatikanaji wa ajira kwa vijana wetu nchini na nje ya nchi na kuhakikisha vijana wetu wananaufalka na mianya yote ya ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla.

- (i) Bado kuna tatizo kubwa la ajira kwa watoto katika sehemu mbalimbali kama vile katika migodi, bandari na maeneo ya uvuvi, Kamati inashauri Wizara zote husika zitafute njia ya kukomesha ajira hizi haramu na Serikali itenye Bajeti maalum ili kuokoa watoto hawa;
- (ii) Kuanza kufikiria namna njema ya kutambua mchango wa wanawake wanaposhughulika na kazi za nyumbani katika kuongeza pato la Taifa;
- (iii) Kuchukua hatua za Kisera na za Kisheria ili kuwawezesha wanawake na watu wenye ulemavu kupata ajira sawa kwa vigezo vinavyotumika katika kutoa ajira;
- (iv) Kuboresha na kuwzesha Sera ya Sekta Binafsi ili kuongeza ajira za kutosha;
- (v) Kutumia sensa ijayo ya Taifa kupata takwimu sahihi za watafutaji na watoaji ajira kwa kutumia vyanzo tulivyonavyo sasa;
- (vi) Kuratibu shughuli za ujasiriamali ili kuwzesha vijana na wanawake kujajiri;
- (vii) Kuhakikisha mpango wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kunaleta ukuaji wa ajira;
- (viii) Serikali ifuatilie kwa karibu uhalali wa raia wa kigeni wanaofanya kazi za kawaida nchini na kuwachukulia hatua stahili wale waliokiuka taratibu hizo; na

(ix) Kuna Waajiri wengine hubadilisha mikataba ya wafanyakazi kutoka mkataba wa muda mrefu au msimu na kuwa mkataba wa muda. Tatizo hili ni kubwa na limeonekana katika kiwanda cha sukari Mtibwa ambapo zaidi ya wafanyakazi 2000 waliokuwa wa msimu sasa wamekuwa wafanyakzi wa muda. Hii inawakosesha wafanyakazi hao kukosa mafao yao ya *NSSF*. Kamati inashauri Serikali kusimamia na kuhakikisha Waajiri wanafuata Sheria za Kazi na Ajira ili kuondoa tatizo hili kwani limewakumba wafanyakazi wa Kiwanda cha Jambo *Plastic* pamoja na viwanda vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu, pia namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, (Mb) Waziri wa Kazi na Ajira, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, (Mb) na wataalam wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Eric Francis Shitindi kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2010/2011 na Bajeti ya Mwaka 2011/2012., Kamati inawashukuru na kuwatachia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Ninapenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa majina:-

- | | |
|--|--------------|
| 1. Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mb, | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. John Damian Komba, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mb | " |
| 5. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb, | " |
| 6. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb | " |
| 7. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb | " |
| 8. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb | " |
| 9. Mhe. Donald Kelvin Max, Mb | " |
| 10. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | " |
| 11. Mhe. Hamad Ali Hamadi, Mb | " |
| 12. Mhe. Abdallah Sharia Ameir, Mb | " |
| 13. Mhe. Salum Khalfan Barwany, Mb | " |
| 14. Mhe. Mariam Salum Msabaha, Mb | " |
| 15. Mhe. Assumpter Nshunju Mshama, Mb | " |
| 16. Mhe. Asha Mohamed Omari, Mb | " |
| 17. Mhe. Ramadhani Haji Salehe, Mb | " |
| 18. Mhe. Rebecca Michael Mngodo, Mb | " |
| 19. Mhe. Said Mohamed Mtanda, Mb | " |
| 20. Mhe. Abdallah Haji Ally, Mb | " |
| 21. Mhe. Hussein Mussa Mzee, Mb | " |
| 22. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb, | " |
| 23. Mhe. Naomi Kaihula Mwakyoma, Mb | " |

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah na Ofisi yake kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Vilevile makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Grace Bidya kwa kuratibu kazi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. REGIA E. MTEMA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuniilinda, kunipa Uzima na Afya njema na kuniwezesha kusimama hapa kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge (Toleo la mwaka 2007), kifungu cha 99 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kunipigia kura kwa wingi kwenye uchaguzi wa mwaka jana bila kujali Ulemavu wangu, Jinsia na uwezo wangu kifedha. Kwa mujibu wa matokeo ya Tume nilipata kura 38,550 sawa na asilimia 45 ya kura zote zilizopigwa. Natambua kwamba sote tulifanya kazi kwa pamoja, kwa nguvu, kwa bidii na kwa moyo katika hali ngumu ya kifedha na kimazingira ili kuhakikisha ninashinda Jimbo hili. Kama TAKUKURU Wilayani Kilombero ingefanya kazi yake vizuri katika kipindi kile cha Uchaguzi leo hii ningekuwa ni Mbunge wa Jimbo hili. Ninawashukuru sana kwa heshima kubwa mliyonipa. Hivyo basi ninawiwa kuwatumikia, kuwapigania, kuwatetea na kusimimia maslahi yenu ndani na nje ya Bunge kama Mtanzania muwajibikaji. Hakuna Kulala Mpaka Kieleweke! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Ukoo wote wa kina Mtema na Kihauli; wazazi wangu Dkt. & Mrs. Estelatus Mtema na ndugu zangu wote kwa upendo wao mkubwa. Kwa namna ya pekee, namshukuru sana pacha wangu mpenzi nihayefanana naye Bi. Remija Mtema, kwa Upendo na msaada mkubwa kwangu. Hakuna raha duniani kama kuzaliwa mapacha hasa mnaofanana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru viongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani; Mheshimiwa Freeman Mbobe, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa kuniamini na kunituea kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Naahidi sitawaangusha hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa rafiki yangu mpendwa, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo kwa Kunilea vema, kunifundisha ujasiri, uchapakazi na uadilifu wakati tukiwa tunaiongoza Idara ya Vijana CHADEMA Makao Makuu. Hivi nilivyo leo ni sehemu ya malezi yake. Nakushukuru sana Kamanda! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakutana leo ikiwa imebaki miezi minne tu kuelekea kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Tangu Uhuru, wafanyakazi wa Tanzania wamekuwa na mchango mkubwa katika siasa na ujenzi wa Taifa. Tanzania tunayoiona hii leo isingwezekana kama si kwa mchango wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa wapigania haki za wafanyakazi kama marehemu Mzee Rashid Mfaume Kawawa, Mzee Abdul Sykes, Mzee Dosa Aziz na Michael Kamaliza hauwezi kusahaulika kwani wameacha alama ya kudumu katika historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote humu ndani, tunasimama katika mabega ya mashujaa wafanyakazi waliotutangulia, pamoja na wale ambao leo bado wanatoka jasho kulisimamisha Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wao mkubwa kwa Taifa hili, wafanyakazi wa Tanzania bado hawavuni kile walichopanda, bado hawajafaidi vizuri matunda ya jasho lao, wala matunda ya uhuru wa nchi yao. Madai mengi ya wafanyakazi yanahusiana na mambo ya maslahi, usalama, haki, usawa na utu wao. Madai haya mengi ni ya muda mrefu na yanapaswa kupatiwa ufumbuzi. Hatuwezi kujenga Taifa la kisasa kwenye nchi ambayo wafanyakazi wamekata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya wafanyakazi. Mwezi Aprili, 2010, aliyejikuwa Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, alitoa tangazo la kupandisha mishahara ya wafanyakazi wa sekta binafsi kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, licha ya kutolewa kwa tamko hilo, Kambi ya Upinzani imebaini kuwa bado wafanyakazi wengi wa sekta binafsi hawajapandishiwa mishahara yao hadi hii leo.

Wafanyakazi wengi wa sekta binafsi viwandani, migodini, mahotelini na sehemu zinazofanana na hizo bado wanalipwa mishahara duni mno ukilinganisha na fedha wanazozalisha kinyume kabisa na tangazo hilo la Waziri. Kwa wastani, wafanyakazi wa kada ya chini wamekuwa wakilipwa shilingi 80,000 kwa mwezi. Hiki ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na hali halisi ya gharama za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa *Geita Gold Mine* hulipwa kiasi cha sh. 500,000/= kwa mwezi wakati wa kigeni hupokea dola 2,000 kwa wiki sawa na dola 8,000 kwa mwezi nje ya mshahara, hupeana fedha hizo kwa ajili ya matumizi ya mwisho wa wiki. Hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa hivi karibuni na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kushindwa kusimamia kupanda kwa mishahara yenewe, pia ni wazi kuwa Serikali imeshindwa kuingilia kati ubaguzi huu unaofanywa dhidi ya wafanyakazi wa Kitanzania walio katika sekta binafsi. Ukweli kuwa Serikali imeshindwa kusimamia viwango vya upandishwaji wa mishahara ya sekta binafsi kwa kuwa hata yenewe imeshindwa kulipa kima cha chini cha mshahara wa sh. 315,000/= kwa watumishi wake wa sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tuliitaka Serikali ipandishe kima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma hadi kufikia sh. 315,000/= ili kuwawezesha wafanyakazi kumudu gharama za msingi za maisha. Cha kusikitisha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na mambo mengine, alisema kuwa baada ya kukokotoa Bajeti Mbadala ya Upinzani, alibaini kuwa wafanyakazi wote wa umma wakilipwa kima cha chini cha sh. 315,000/=, Serikali italazimika kutumia jumla ya shilingi Triliioni 7,971,649,000/= kwa mishahara tu na kwa hiyo itakuwa imebakila na fedha kidogo ambazo hazitatosha kununulia madawa na kugharamia huduma nydingine muhimu kwa wananchi zinazotolewa na Serikali. Ukweli ni kuwa, kauli hii ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi haikuwa na dhamira njema ya kuwasaidia wafanyakazi waliopendekeza ongezeko hilo la mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akihitubia wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam, mwezi Aprili, 2010, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, katika maelezo yake alisema wafanyakazi wote wa sekta ya umma wanakadiriba kuwa 350,000. Hata tukisema kuwa ndani ya mwaka mmoja uliopita idadi ya wafanyakazi wa sekta ya umma imeongezeka hadi kufikia wafanyakazi 400,000, bado kima cha chini cha sh. 315,000/= kikilipwa, Serikali haiwezi kutumia jumla ya shilingi triliioni 7.9 kama alivyodai Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimahesabu, tukichukua mshahara kama kikokotozi cha gharama, Serikali ikilipa kima cha chini cha shilingi 315,000 kwa wafanyakazi 400,000, bila kuzingatia asilimia 15% ya makato ya akiba (kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii – *PPF, PSPF, LAPF* na *NSSF*) na asilimia 3% ya makato Bima ya Afya (*NHIF*), itatumia jumla ya shilingi triliioni 1.512 tu kwa ajili ya mishahara na sio shilingi Triliioni 7.9 alizodai Mheshimiwa Waziri! Huu ni ukweli wa kihisabati. (*Makoti*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama kima hicho cha sh. 315,000/= kitalipwa kwa wafanyakazi 400,000 pamoja na kujumuisha asilimia 15% ya makato ya akiba (kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii – *PPF, PSPF, LAPF* na *NSSF*) na asilimia 3% ya makato ya Bima ya Afya (*NHIF*), kwa pamoja (na gharama za huduma nydingine – *OC*), bado gharama nzima ya kulipia mshahara huo, haiwezi kuzidi shilingi triliioni mbili! Huu ni ukweli wa kihisabati na si vinginevyo (Hii ni kwa mujibu wa hesabu zilizopigwa na wataalam wazalendo wa Vyuo vyetu Vikuu vya ndani na kuthibitishwa na Kambi Rasmi ya Upinzani).

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama tukiweka na kima cha juu na cha kati wanachopata watumishi wa umma bado hakiwezi kuzidi shilingi triliioni tatu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasilitiza kuwa Serikali ina uwezo wote wa kupandisha mshahara huo ikiwa tu itadhamiria kwa dhati kuwajali wafanyakazi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanaharakati wa Masuala ya Haki za Binadamu Mary Rose McGready aliwahi kusema, nanukuu: “*There is no greater joy, nor greater reward than to make a fundamental difference in someone’s life*” kwa tafsiri isiyu rasmi kwamba ni hakuna furaha na thawabu kubwa ambayo mtu atapata kama atafanya mabadiliko makubwa katika maisha ya mtu. Serikali ya Tanzania inapaswa kufanya haya kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira. Kwa mujibu wa kitabu cha hali ya uchumi cha 2010, kinaonyesha kuwa Nguvu Kazi nchini ni milioni 18.8 na kati yao watu milioni 16.6 wameajiriwa na milioni 2.2 hawajaajiriwa. Lakini wengi wa waajiriwa hawa hawako katika ajira rasmi. Takwimu

hizi zimewahusisha mpaka Wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama Machinga kama vile wauza maji na wengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya utafiti na kuja na takwimu sahihi za walioajiriwa nchini. Itenganishe walioko kwenye ajira rasmi na isyo rasmi na walioko kwenye sekta ya umma na sekta binafsi. Wakala wa Huduma za Ajira Nchini (*TaESA*) wawe wanatoa hali za ajira kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu ajira hafifu katika mfumo rasmi, kuna sababu tatu za msingi zinasababisha uhaba wa ajira ya uhakika hapa nchini, ambazo ni ukuaji mdogo wa uchumi, uzalishaji duni viwandani na ukosefu wa maarifa na stadi stahiki mionganoni mwa vijana. Ili kuongeza ajira na kuboresha ujira, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuweka mkazo katika mambo yafuatayo:-

- (i) Kuinua uchumi kwa kutekeleza mipango mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu;
- (ii) Kupanua na kuimarisha viwanda vidogovidogo hasa vijiji ili kupunguza idadi kubwa ya vijana kuhamia mijini bila kuwa na uhakika wa kupata ajira;
- (iii) Kuimarisha elimu ya ufundi na stadi za maisha kwa vijana hii ni pamoja na kuimarisha vyuo vya *VETA* kwa kuwa vijana wengi hasa kutoka shule za Kata wanashindwa kabisa kuingia katika mfumo wa ajira nchini na hii ni kwa kuzingatia hali halisi ya ufaulu kwa shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa. Kwa mujibu wa taarifa za watumishi wenye ulemavu zilizokusanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Disemba 2007, inaonesha kuwa ni asilimia 0.2 tu ya watumishi wote wa umma walioajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hali ni hiyo kwenye utumishi wa umma basi hali ni mbaya zaidi kwenye sekta binafsi kwani waajiri wengi binafsi wamekuwa wakikwepa kuajiri watu wenye ulemavu kutokana na visingizio mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo ili kuongeza ajira kwa wenye ulemavu:-

- (i) Serikali kufanya utafiti na kupata takwimu za watu wenye ulemavu waliooko katika soko la ajira na walioajiriwa kwenye sekta binafsi.
- (ii) Serikali kuimarisha na kuboresha miundombinu kwenye ofisi na maeneo ya kazi kote kwa sekta ya umma na binafsi.
- (iii) Serikali kuharakisha utungwaji wa Kanuni za Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya 2010 ili sheria hii iweze kutekelezwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vya Ufundi (*VETA*) ni vyuo pekee nchini vinavyotoa elimu na ajira kwa pamoja. Katika Vyuo hivi ndipo Vijana wenzangu wengi wanaweza kupata stadi stahiki za kazi, ujuzi pamoja na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa huko nyuma *VETA* ilikuwa chini ya Wizara ya Kazi na Ajira lakini baadaye ikaondolewa na kupelekwa Wizara ya Elimu na Ufundi ambako *VETA* imedorora kabisa hivi sasa. Mpaka hivi sasa nchi yetu ina vyuo nane tu vya *VETA* nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mbunge kijana ambaye naguswa sana na tatizo la ajira kwa vijana wenzangu namwomba Mheshimiwa Rais kuridhia ombi langu la kurejesha Vyuo vya *VETA* chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ili kuongeza ufanisi wa Vyuo hivi na kupunguza tatizo la ajira kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili chuo kimoja cha VETA kiweze kukamilika kwa ujenzi pamoja na mahitaji yote inahitaji shilingi bilioni saba tu na ili kila Halmashauri ya Wilaya ipate chuo chake, zitahitajika jumla ya ahilingi bilioni 875 tu ambapo napendekeza Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011-2016, itafute pesa hizi iwe kwa kukopa ama kwingineko ili Vyuo hivi vipate uhai na hatimaye tupunguze tatizo la ajira nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubuni mbinu mpya na za kudumu za kutatua ajira kwa wanafunzi wanaohitimu Vyuo Vikuu. Imekuwa ni kawaida siku hizi kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu kukaa muda mrefu bila kupata ajira za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mzigo wa kodi kwa mfanyakazi. Kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi kumepunguza uwezo wa matumizi. Pamoja na malalamiko yote ya wafanyakazi hapa nchini, bado wafanyakazi ndio walipa kodi wakubwa na wazuri. Wanalipa kodi mbalimbali ikiwemo kodi ya mshahara (*PAYE*) ambayo ni kubwa sana ukilinganisha na hali halisi ya gharama za maisha. Kambi ya Upinzani tunatambua kuwa, kodi hii ni chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali. Kuna haja ya kuzirahisisha kodi hizi ili ziweze kumpunguzia mzigo mkubwa wa kodi mfanyakazi ambaye hata hivyo kipato chao ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi hii ni mzigo mkubwa kwa mfanyakazi wa Tanzania na kwa mwaka huu wa fedha tulipendekeza na tunapendekeza tena kiwango hicho cha kodi kifanyiwe marekebisho na kishushwe mpaka asilimia tisa kwa kiwango cha chini na asilimia 27 kwa kiwango cha juu. Uamuzi huu utawezesha wafanyakazi kubakia na fedha toka kwenye mishahara yao na hivyo kuishi vizuri katika kuweza kuyamudu maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria za Kazi na Haki za Wafanyakazi. Pamoja na uwepo wa Sheria za Kazi kama vile Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na 6 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na 7 ya 2004, bado nchi yetu ina ukiukwaji mkubwa wa sheria hizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kutozingatiwa kwa masharti ya ajira (*employment standards*) kama vile muda wa saa za kazi, likizo na siku za mapumziko. Waajiri wengi hasa wa sekta binafsi wamekuwa hawaheshimu masharti haya. Hili limeshuhudiwa katika baadhi ya migodi kama vile Geita *Gold Mine*, *Resolute Gold Mine*, kwenye viwanda kama vile Jambo *Plastic* cha Dar es Salaam, Kiwanda cha Sukari Kilombero (Illovo), Kiwanda cha nguo cha KTM cha Mbagala, Dar es Salaam, Kiwanda cha Nguo cha *Sun Flag* cha Arusha, Kilombero *Plantation Limited*, Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Dar es salaam na vingine vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, waajiri wa viwanda hivi au makampuni haya wamekuwa wakiwafanyisha kazi wafanyakazi wao kwa muda mrefu zaidi kupita muda rasmi wa kazi, bila kuwalipa posho ya ziada (*Overtime allowances*). Wafanyakazi wa viwanda na makampuni haya hawapewi likizo, wanapouqua hawawalipi posho za matibabu na baadhi yao hawana mapumziko ya mwisho wa wiki na hata wanawake wajawazito wamekuwa hawapewi likizo ya uzazi (*Maternity leave*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wafanyakazi wamekuwa wakiachishwa kazi kiholela bila ya kujali haki za waajiriwa kwa mujibu wa sheria. Waajiri kwa maslahi yao wamewaachisha kazi wafanyakazi kwenye viwanda vyao au makampuni yao bila kufuata sheria za kazi na ajira zinavyosema. Hili limetokea hivi karibuni kwenye Viwanda vya Jambo *Plastic* na Urafiki ambapo wafanyakazi wameachishwa kazi kienyeji, Mgodi wa Geita *Gold Mine* umewaachisha kazi zaidi ya wafanyakazi 50 kinyume na taratibu na Kampuni ya Zantel imewaachisha wafanyakazi 80 kwa kipindi cha miezi minne tu tangu Aprili mwaka huu mpaka sasa baada ya Idara ya Rasilimali Watu (*Human Resource*) kuchukuliwa na mgeni kinyume na Sheria za Kazi inayotaka Idara hii kuongozwa na Wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi rasmi ya Upinzani ina taarifa kuwa malalamiko yote haya yalishafikishwa Serikalini na wafanyakazi wa Geita *Gold Mine*, Wafanyakazi wa Zantel, *Jambo Plastic*, Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Kampuni ya *Caspian* na wengineo. Miongoni mwa vyombo vya Kiserikali vilivyotaarifiwa ni Idara ya Uhamiaji, Idara ya Kazi, Mamlaka ya Usuluhishi na Maamuzi

(CMA), lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hata Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikwenda kwenye Kiwanda cha Jambo *Plastic*, lakini hakuna hatua zozote madhubuti zilizochukuliwa kuhakikisha malalamiko ya wafanyakazi hawa yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa kwa Serikali hii inayoongozwa na Chama kinachojita Chama cha Wakulima na Wafanyakazi, kushindwa kuchukua hatua za kuwanusuru wafanyakazi hawa na kampuni nyngine zinazonyanyasa wafanyakazi. Tunataka malalamiko yote ya wafanyakazi wa viwanda hivi yashughulikiwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kumekuwa na wimbi la kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi wa nchi nyngine wanaoingia kwa mgongo wa wawekezaji kinyume cha taratibu na ambao hufanya kazi za kawaida ambazo Watanzania wana uwezo nazo. Wafanyakazi wetu wengi wanaonekana kuwekwa pembedi, si kwa sababu hawana uwezo bali kwa sababu waajiri wanaleta watu wao toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uwekezaji Na. 26 ya mwaka 2007, Sura 38, Kifungu cha 24, inaruhusu Mwekezaji kuleta wataalam wasiozidi watano kutoka nje ya nchi. Aidha, iwapo Mwekezaji ataona kuna haja ya kuongeza wataalam zaidi kutoka nje ya nchi, atapaswa kuwasilisha maombi maalum Kituo cha Taifa cha Uwekezaji ambacho kitawaruhusu ikiwa tu itathibitika hakuna Mtanzania hata mmoja mwenye utaalam husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume kabisa na sheria hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kuwa migodi na kampuni nyngi nchini, wamekuwa wakajiri raia wengi wa kigeni. Miongoni mwa makampuni na taasisi ambazo zinalalamikiwa kwa kuajiri wageni wengi kinyume cha sheria, ni *Sun Flag, Tanzanite One Mererani, Geita Gold Mine, Ausdrill Limited, Murza Oil Company* na Kampuni ya Simu ya Zantel.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imekuwa ikiwanyima Watanzania wengi fursa ya kuajiriwa wakati kumbe nafasi zipo, lakini wanapewa wageni kinyume kabisa cha sheria. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Wizara hii, kufanya ukaguzi maalum katika migodi, viwanda na mashirika yote yanayolalamikiwa kuajiri wageni kinyume cha sheria (yakiwemo tuliyoyataja), ili kuhakikisha sheria husika inaheshimiwa na Watanzania wazawa wananaufaika nayo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu, akijibu swali la papo kwa hapo kuhusu makampuni mengi kuajiri wageni wengi hata kwa nafasi zinazoweza kujazwa na Watanzania, pamoja na mambo mengine, alisema hali hiyo inasababishwa na Watanzania kutojali sana kazi, kuwa wavivu na kutoa visingizio vingi ikiwemo kuumwa na hivyo kuwafanya waajiri wengi kupendelea kuchukua wafanyakazi wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa, kauli hiyo ya Waziri Mkuu inaweza kuwa na ukweli lakini kauli hii isitoe mwanya zaidi kwa waajiri kuwanyanyasa wafanyakazi na kuajiri wafanyakazi kutoka nje ya nchi kinyume cha sheria. Hakuna mfanyakazi ambaye hawezikufiwa, kuuguliwa, au hata kupatwa na matatizo yeeye mwenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafanyakazi walioachishwa kazi. Wapo Wafanyakazi waliopunguzwa au kufukuzwa kazi bila kupewa mafao yao. Kiwanda cha Sukari Kilombero (Illovo) wakati kinabinafishwa mwaka 2000 kilipunguza Wafanyakazi, lakini mpaka sasa wengi wao hawajapewa mafao yao. Ni miaka zaidi ya kumi sasa bado Watanzania hawa wanadai mafao yao lakini hawapewi. Ni aibu kwa Taifa kushindwa kusimamia maslahi ya Wafanyakazi hawa Wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo pia Wafanyakazi waliowahi kufanya kazi Serikalini ambao mpaka leo bado hawajalipwa mafao yao. Vile vile wapo Wafanyakazi walioumia kazini na wengine kupata ulemavu, lakini bado hawajapata haki zao na wengine wamenyimwa kabisa haki zao, majina ya wafanyakazi hawa tunayo kwenye kumbukumbu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kusimamia na kuhakikisha wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Sukari Kilombero wanaodai mafao yao na wale

wote waliokuwa watendaji Serikalini wanapata haki zao haraka iwezekanavyo na wale walioumia na kupata ulemavu kazini wote wapatiwe stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ni muhimu sana katika kulinda maslahi ya wafanyakazi pindi wanapostaifu. Yapo malalamiko ya siku nyingi kuwa pamoja na Mfuko huu kufanya vizuri katika uwekezaji lakini mafanikio yake hayawanufaishi moja kwa moja wachangiaji wa Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani inapendekeza kuwa, sehemu ya faida inayotokana na uwekezaji igawiwe kwa wanachama kulingana na michango yao. Aidha, Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa Tanzania inatumia mfumo wa kutoza kodi michango ya wanachama na mapato yatokanayo na uwekezaji (*TEE*). Nchi Nyingine hazitozi kodi kabisa katika maeneo yote (*EEE*). Hii inapelekea mafao ya wastaifu kupungua sana. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuondoa kodi kwenye mapato yatokanayo na uwekezaji (*Investment Income*) ili tuwe na mfumo wa (*TEE*) katika michango, mapato yatokanayo na uwekezaji na mafao kwa wanachama. Hii itafanya mifuko kutoa mafao makubwa zaidi kwa wastaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*). Bunge lilipitisha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii mwaka 2008 kwa lengo la kuangalia ni jinsi gani Mifuko hiyo inavyofanya uwekezaji kwa kutumia fedha za wanachama wake. Aidha, kuna umuhimu mkubwa kwa mamlaka hii kuharakisha kupatanisha (*harmonize*) mfumo wa malipo ya *pension* kuwa shilingi 80,000 kwa mwezi kwa Mifuko yote, kwani mahitaji muhimu kwa wastaifu hao ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dhana ya hifadhi ya jamii ni pana sana, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuzingatia pendekezo letu kuweka mfumo utakaowafanya wazee wote kupata pesheni (*Universal pension*) kila mwezi kwa kiasi cha shilingi ishirini elfu kwa kuanzia, ili kuwapunguzia wazee wetu hasa waishio vijijini gharama kubwa za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiunganisha Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii na kubaki miwili tu. *PPF* na *NSSF* iunganishwe na kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta Binafsi, na *LAPF*, *PSPF* na *GEPF* iunganishwe na kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta ya Umma. Pia, Kambi ya Upinzani inapendekeza Mifuko yote iwekwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ili kuongeza ufanisi na tija. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la Vyama vya Wafanyakazi toka vianzishwe mwaka 1929 liliikuwa ni kutetea maslahi ya wafanyakazi, lakini hadi leo ambapo Tanzania inakaribia kutimiza miaka 50 ya Uhuru, bado wafanyakazi wanakabiliwa na matatizo yaleyale yaliyopelekea kuanzishwa kwa vyama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zetu zinazoratibu masuala ya kazi ikiwemo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na 7 ya mwaka 2004, zinaruhusu wafanyakazi kuunda umoja wao illi kuwa na sauti moja katika kutetea maslahi ya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo waajiri wengi ambao hawataki kuona Vyama vya Wafanyakazi vinaanzishwa kwa kuwa wanajua kwa kufanya hivyo, wafanyakazi watakuwa wamepata sehemu ya kipeleka kero na hatimaye kupata mtetezi. Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*), mfano wa waajiri wanaowakataza wafanyakazi wao wasianzishe wala kujihusisha na Vyama vya Wafanyakazi ni Geita *Gold Mine*, Mgodi wa North Mara na baadhi ya Viwanda na Makampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baadhi ya wafanyakazi wanatishiwa kufukuzwa kazi pale ambapo wanataka kupata wasaa wa kujadili matatizo katika maeneo yao ya kazi. Kambi ya Upinzani tunaitaka Wizara kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko haya na kuyatafutia suluhisho na pia kuwahoji waajiri hao ni kwa nini wanawanyima wafanyakazi hao fursa ya kufanya mikutano kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hata Serikali yenyewe imekuwa ikitoa vitisho mara kadhaa kwa Vyama vya Wafanyakazi pindi vinapotaka kufanya migomo ya kushinikiza kutimizwa kwa madai yao. Ni vema ikaeleweka kuwa migomo ni haki ya wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria za Kazi, kifungu cha 75(a) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004 na kifungu namba 26(i) cha Sheria ya Majadiliano katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya wafanyakazi kufuata taratibu zote za kisheria pindi wanapotaka kuandamana au kugoma ili kushinikiza madai yao, bado Serikali imekuwa ikitumia mabavu kuwakandamiza wafanyakazi na vyama vyao. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha mara moja kutumia mabavu katika kushughulikia madai ya wafanyakazi, kwani kufanya hivyo ni kukiuka haki za binadamu na sheria halali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, John F. Kennedy alikuwa Rais wa Marekani aliwahi kusema, nanukuu: "*A nation that is afraid to let its people judge the truth and false hood in an open market is a nation that is afraid of its people.*" Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kuwa Taifa ambalo linaloogopa watu wake wasijadili ukweli na uongo katika uwanja wa wazi, ni Taifa linaloogopa watu wake, ni wazi kuwa Serikali yetu inaogopa nguvu ya wafanyakazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuanzishwa kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), bado Wafanyakazi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu yasiyozingatia usalama wa afya zao. Taasisi hii haijafanya kazi vya kutosha ili kulinda usalama wa afya za wafanyakazi kazini. Ni muhimu kuweka utaratibu wa kuhalikisha mashirika, taasisi na makampuni yote nchini yanatekeleza matakwa ya *OSHA* na kuongeza adhabu kwa taasisi ambazo hazizingatii taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *OSHA* ya mwaka 2003 imeweka mwanya mkubwa kwa wafanyakazi kushindwa kutoa taarifa za uvunjifu wa Kanuni za Afya na Usalama Kazini. Kifungu cha 99(1) sehemu (d) na (e) vya sheria hiyo, vinawataka wafanyakazi ambao wameguswa na matatizo ya afya na usalama kutoa taarifa kwa mlolongo mrefu kwenda kwa mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, japo ni vizuri kwa wafanyakazi kufanya hivyo kwa maana ya kujaribu kutatua tatizo, lakini mahali ambapo pana uvunjaji mkubwa na wa wazi wa kanuni za usalama na afya kumwambia mwajiri ni sawa na kujifukuzisha kazi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilete mapendekezo ya mabadiliko ya sheria hiyo ili kuwalinda wafanyakazi hawa. Hivi ndivyo ilivyo kwenye nchi zilizoendelea kama Marekani ambapo wafanyakazi wa nchi ile huweza kutoa taarifa kwenye taasisi zao bila hata kulazimika kutaja majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hayo, yapo malalamiko ya wafanyakazi wa sekta ya madini kuhusu matumizi ya mionzi. Suala hili illisharipotiwa humu Bungeni, lakini kutokana na taarifa zilizopo bado hali hiyo inaendelea na wafanyakazi hao wanaendelea kupata athari hizo pamoja na majibu mepesi kuwa mionzi hiyo haina athari kwa wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kambi ya Upinzani inapendekeza *OSHA* iongezewe fedha ili iweze kujidesha yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*) ni muhimu sana kutokana na majukumu yake katika kutatua migogoro sehemu za kazi kwa ufanisi, usawa na kwa haraka tofauti na ilivyo kwa Mahakama za kawaida. Pamoja na Tume kuwa na jukumu hilo kuu, bado yapo malalamiko mengi sana juu ya utendaji wake hasa katika kutoa haki sawa baina ya mwajiri na mfanyakazi au baina ya wafanyakazi na vyama vyao vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi ni kukosekana kwa haki katika maamuzi ya Tume kutokana na waajiri wengi kuwa na nguvu ya fedha. Pia waajiri wengi wanatumia mwanya wa baadhi ya wafanyakazi ambao hawana uelewa wa masuala ya kisheria ambapo maamuzi ya Tume hawazingatii na badala yake baadhi ya wafanyakazi hufukuzwa kazi mara tu maamuzi yakishatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa wito kwa watendaji wa Tume hii kuzingatia weledi katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua waamuzi ambao hawazingatii taratibu za kazi pamoja na kutoa haki pale inapostahili. Aidha, vyombo vingine vya Kiserikali ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia kwa karibu Tume hiyo na mamlaka zingine za wafanyakazi ili kudhibiti mianya ya ujisadi katika utetezi wa haki na maslahi ya wafanyakazi. Hata hivyo, bado kuna changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na Tume kuwa na mashauri mengi ambayo hayajafanyiwa maamuzi au usuluhishi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) ni chombo muhimu kinachowenza kulisaidia Taifa katika kuhakikisha shughuli zinafanyika kwa tija ikizingatiwa uchache wa rasilimali tulizonazo. Shirika hili likitumiwa vizuri litapunguza upotevu wa fedha za umma unaofanyika katika nyanja za mafunzo toka kwa taasisi ambazo baadhi hazina nyenzo na uwezo wa kutoa mafunzo yenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa shughuli zote za mafunzo kwa taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma zifanywe na Shirika hili. Vile vile Shirika la NSSF lifikirie upya kudhamini ujenzi wa jengo la shirika (*Maarifa House*). Mwisho kabisa, Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali iliwezeshe shirika hili ili liweze kujindesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TaESA*) ni chombo muhimu sana katika ustawi wa watafuta ajira nchini. Chombo hiki kimekuwa kikiwezeshwa na Serikali kila mwaka tangu kuanzishwa kwake ili kufanya kazi kwa ufanisi na tija. Lakini tangu kuanzishwa kwake *TaESA* hajajitangaza vya kutosha kiasi kwamba chombo hiki muhimu hakijulikani kabisa wakiwemo baadhi ya Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni aibu kwa Taifa chombo kinachowezeshwa na Serikali Waziri hakifahamu. Kambi ya Upinzani inahoji kama Waziri hakifahamu itakuwaje kwa mwananchi wa Tanganyika Masagati kule Kilombero anayetafuta ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitembelea tovuti ya *TaESA* hivi karibuni na kukuta tangazo la kazi kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha nne. Kambi ilishangazwa na namna tangazo hilo liliyokuwa, halikuweka wazi aina za kazi zilizopo na ilimtaka anayetafuta kazi kufika mara moja kwenye ofisi zao. Kambi ya Upinzani inahoji hivi ni Watanzania wangapi wanaweza kufikiwa na kutumia mtandao na wanavyoambiwa kuwa wafike kwenye ofisi hizo Dar es Salaam. Je, ni Watanzania wangapi wanaweza kufanya hivyo? Je, shirika hili ni kwa watu wa Dar es Salaam peke yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa *TaESA* ipewe fedha za kutosha na ijitangaze zaidi vijijini kwani walioko vijijini ndio wana matatizo zaidi ya kupata taarifa za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waziri mwenzangu mama Kabaka kwa ushirikiano mkubwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Makongoro Mahanga kwa kuwa mwelesi kila ninapomwomba akafanye kazi huwa anakwenda haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Regia Mtema Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Kazi na Ajira natumaini ndugu yako Remidia amekuona. Sasa Waheshimiwa Wabunge Wizara hii tunatakiwa tuitendee haki leo, kwa hiyo, muda wetu ni mdogo sana sina hakika tutachukua wachangiaji wangapi. Lakini watakuwa ni wachache mno. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kairuki.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia. Sikutegemea kama nitapata fursa hii lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwani leo wachangiaji ni wachache na ni vema tuweze kuitendea haki Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali hususan kwa kuunda Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibit wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Usimamizi huu wa *SSRA* utaiwezesha Mifuko hii kuwa endelevu na itawezesha Mifuko hii kuwatendea haki na kuwapatia taarifa wachangiaji muhimu ambao ni wafanyakazi. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kwamba Mifuko hii imekuwa na wigo finyu wa huduma ya Hifadhi ya Jamii nchini. Ni takriban asilimia sita tu ya Watanzania ndiyo wanaopata huduma ya Hifadhi ya Jamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kiwango hiki ni kidogo sana hususan ukizingatia wenzetu wa Uganda wanachangia kwa asilimia nane na wenzetu wa Kenya wanachangia kwa asilimia 15. Niiombe Serikali iweze kufanya jitihada ili kiwango hiki na uwigo huu uweze kuongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010-2015 pamoja na Katiba yetu kupitia Ibara ya 11(1) inaitaka Serikali kuhakikisha inafanya jitihada ili watu wengi zaidi waweze kupata Huduma ya Hifadhi ya Jamii. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko mengi ya tofauti kubwa katika mafao hususan katika eneo hili niwaongelee Wahadhiri wa Vyuo Vikuu. Kumekuwa na Wahadhiri ambao unakuta wana elimu sawa, wana uzoeufi sawa na wamekaa kazini kwa muda ambao ni sawa pia, lakini unashangaa inapofika wakati wa kustaafu malipo yao yamekuwa yakinotautiana hadi kufikia hata mara tatu baina ya mfanyakazi mmoja na mfanyakazi mwagine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, viwango vya pensheni vimekuwa pia vikitofautiana sana. Hivi ni kwa nini Serikali yetu isiangalie uwezekano wa kuwa na *formula* moja sawa baina ya Mifuko yote hii ya Hifadhi ya Jamii? Vile vile, Mifuko hii kuhusiana na *qualifying period* kuna Mifuko mingine ambayo inataki miaka 10 na kuna Mifuko mingine inataki miaka 15 ndipo unaweza ku-*qualify* kupata mafao yako. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo la kuingiliana kwa mafao, nitolee mfano wa *NSSF* pamoja na *NHIF*, unakuta mtumishi mmoja amekuwa akichangia *NSSF* na wakati huo huo amekuwa akikatwa kwenye *NHIF* kupata mafao ya matibabu. Kwa kweli, huu ni uonevu mkubwa kwa wafanyakazi na pia inaongeza gharama kubwa kwa mwajiri. Ningependa tatizo hili liweze kufanyiwa uchunguzi na ikiwezekana litatuliwe haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna tatizo la muundo wa kisheria baina ya Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii, tunayo Mifuko sita ya Hifadhi za Jamii kama ambavyo tumesikia kutoka kwenye taarifa ya Kamati kama ulivyowasilishwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama. Katika Mifuko hii sita kuna Mifuko ambayo inawajibika chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kuna ambayo inawajibika kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, pia kuna ambayo inawajibika chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (*TAMISEMI*). Ilishatajwa, hivyo, sina haja ya kurudia kuiainisha Mifuko hiyo mmoja mmoja. Hali hii ni kinyume na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003 ambayo inataki Mifuko yote iwe chini ya Wizara inayohusika na masuala ya hifadhi ya jamii yaani Wizara ya Kazi na Ajira. Hivyo basi, naishauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha tatizo hili linarekebishwa na Sheria iweze kurekebishwa ili iweze kuendana na Sera ya Hifadhi ya Jamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa wakati Waziri anajumuisha Hotuba ya Wizara hii atueleze endapo *SSRA* imekwishafanya tathmini ya matatizo yanayoikabili Mifuko yetu kama vile matatizo ya ulinganifu wa mafao ya pensheni na kutathmini afya za Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa ambalo *SSRA* itatakiwa kulitatua na Serikali kwa ujumla ni tatizo la gharama kubwa za uendeshaji wa Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii. Hii inapunguza sana ubora wa mafao na imani ya wanachama ambao ni wafanyakazi kwenye Mifuko hii. Wastani wa kuendesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Tanzania ni asilimia 12. Wakati kiwango cha Kimataifa kinachoruhusiwa ni asilimia tano au chini ya hapo. Sasa iweje kuwe na tofauti kubwa ya asilimia saba, tunashindwa kuelewa. Kwa kweli tunaomba suala hili liangaliwe ili tuone kweli kama Sera za Uwekezaji na gharama nyingine ni za msingi na za lazima ili mwanachama wa Mifuko aweze kufaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kwenye Hifadhi ya Jamii, ambalo ningependa kulizungumzia ni ukosefu wa Hifadhi ya Jamii kwa wazee. Kama sote tunavyofahamu, wazee katika jamii yetu wana ushiriki mkubwa na muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi. Inakadiriwa kwamba asilimia 73 ya wazee wetu ambaao ni takriban milioni mbili bado wanashiriki katika shughuli za kiuchumi na kwa mujibu wa tafiti ambazo zimefanywa na *ILO* pamoja na *Help Age International* na Wizara ya Kazi na Ajira inawezekana kabisa kutoa fao hili la hifadhi ya Jamii kwani endapo litatolewa għarama yake haizidi asilimia 1.28 ya pato la Taifa letu. Ilikadiriwa mwaka 2010 kwamba ikiwezekana itolewe shilingi 16,586 kila mwezi kwa kila mzee ambaye ana miaka 60 au zaidi. Napendekeza Serikali iħarakishe mfumo huu wa kutoa Hifadhi hii ya Jamii kwa wazee kwani italsaidia Taifa kupunguza umaskini na kwa wazee wenywew kwa asilimia 11.9. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la *maternity protection*. Tanzania ilisaini Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Afya ya Uzazi, Mkataba Namba 183 wa Mwaka 2000. Inashangaza hadi kufikia leo hii Mkataba huu bado haujaridhiwa na nchi yetu. Ningependa Waziri anapofanya majumuisho awaeleze wanawake wa Kitanzania ni kwa nini Mkataba huu mpaka kufikia leo hii haujaridhiwa na ni lini sasa nchi yetu itaridhia Mkataba huu. Sheria yetu ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba (6) ya Mwaka 2004 inakataza kabisa ubaguzi wa aina yoyote kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika maeneo ya viwanda ya *EPZ* kuna wasichana wadogo wadogo wengi sana ambaao wamekuwa wakajiriwa katika maeneo hayo. Lakini kwa kweli, wamekuwa wakibaguliwa na kudhalilika sana na haki zao za uzazi zimekuwa zikivunjwa. Msichana huyu anayefanya kazi Viwanda vya wa *EPZ* anapopata mimba anafukuzwa, hapo hapo nchi hii ya Tanzania ndio tunajivuna kwamba tunalinda na kuhifadhi masuala na haki za kijinsia. Kweli tunatetea na kulinda usawa wa kijinsia kama mfanyakazi huyu wa kike ambaye ana haki yake ya msingi ya kuweza kujifungua watoto na halindwi? Kweli inashindikana vipi kumhakikishia mfanyakazi huyu ambaye anapata ujauzito na kwamba pindi anapopata ujauzito akienda kujifungua atarudi na atapata marupurupu yake na ajira yake bado itatunzw? Ningependa Serikali ijibu hili na ielete imepata takwimu za watu wangapi ambaao wamepata matatizo haya na inachukua hatua gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ingawa wengine linaweza lisiwfurahishe ni la maslahi ya wafanyakazi wa majumbani. Kundi hili la wafanyakazi, ni kundi muhimu na kubwa sana. Tuna takriban ya wafanyakazi wasiopungua 400,000 katika nchi yetu ambaao ni wa majumbani. Wafanyakazi hawa ni wasichana wa ndani na wavulana wanaofanya kwenye bustani zetu, madereva pamoja na makundi mengine. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Rais wetu Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa *ILO* Geneva kwenye Mkutano wa 100 mnamo tarehe 15 Juni, 2011 amba po kwa kweli altambua mchango mkubwa unaofanya na wafanyakazi hawa wa majumbani. Sasa niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mkataba huu utakapokuja kuridhiwa kwa kweli muwaunge mkono wafanyakazi hawa na hususan niwapongeze sana wafanyakazi wa nyumbani, Angelina pamoja na Angela, wanaotokea Taasisi ya Kivulini, Mwanza na Musoma ambaao kwa kweli waliwawakilisha vizuri wafanyakazi wenzao wa majumbani na walitoa mchango mkubwa sana katika Mkutano huo. Nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati sasa haki za wafanyakazi hawa majumbani zikatambuliwa, wafanyakazi hawa wamekuwa wakichukuliwa kama watumwa kwa muda mrefu hili ni tatizo kubwa sana. Endapo tutaridhia Mkataba huu wa kuwalinda wafanyakazi wa majumbani wataweza kupata fursa ya kuingia mikataba halali na waajiri wao ambaao wengine ni ninji, Mikataba hiyo itaainisha aina za kazi wanazotakiwa kuzifanya kama wafanyakazi wa majumbani, mazingira wanayofanya kazi yatatakiwa kuwa yenye staha, usalama wa afya zao kazini utapaswa kuzingatiwa, ukomo wa masaa ya kazi na kadhalika. Hapa naomba nisisitze, kuna wengine mmekuwa mkiwatumi kisha watumishi wenu wa majumbani kwa zaidi ya masaa 12 mpaka 18. Wengine mmekuwa mkiaweka *on standby*, unakuwa unakwenda kwenye shughuli zako, unakunywa pombe na shughuli zingine yeye anakuwa *on standby*, kukaa kusubiri kukufungulia mlango. Je, na haya unahesabu kama ni masaa yake ya kazi? Mfanyakazi huyu anastahili kuwasiliana na familia na ndugu zake, mfanyakazi huyu anastahili kupata fursa ya

kujiburudisha na mfanyakazi huyu pia anatakiwa mara moja kwa wiki apate muda wa kupumzika na si lazima umlazimishe apumzikie nyumbani kwako kwani wengi wamekuwa Jumapili wakiwaacha wawe huru kidogo kupata *leisure* lakini bado mmekuwa mkiwaweka *on standby*, muache awe huru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine pia wamekuwa hawawalipi wafanyakazi wao mishahara na wengine mmekuwa mkiwalipa mishahara hii kupertia mtu wa tatu (*third party*), wewe umemwajiri mtu wa tatu au unafanya kazi na yule mfanyakazi. Kwa kweli, tabia hii ikomeshwe na ningelomba Serikali ihakikishe inachukua jitihada za makusudi kufanya ukaguzi majumbani kubaini ni wafanyakazi wangapi amba ni wafanyakazi wa majumbani na kubaini endapo haki zao za msingi kama wafanyakazi zinalindwa kwani ni muhimu kuthamini utu wao na haki zao za msingi kama binadamu mwingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwa haraka haraka, ni ajira za wafanyakazi wa kigeni. Kumekuwa na tatizo kubwa la ajira za wafanyakazi wa kigeni amba wengi wao wamekuwa wakipewa vibali bila ya kufuata utaratibu, wengi wao wamekuwa wakija hawana elimu wala uzoefu. Kuna mara kadhaa wafanyakazi wa Kitanzania wamekuwa wakiwfundisha kazi wafanyakazi hawa wageni na pindi wanapopata uzoefu kidogo tu, wamekuwa wakigeuka na kuwa *supervisors* wa wafanyakazi wa Kitanzania. Kwa kweli, hii ni aibu kubwa na tatizo hili linatakiwa likomeshwe haraka kwani ni kuwanyonya wafanyakazi wa Kitanzania, wakati ajira zingine zina uwezo kabisa wa kufanya na mfanyakazi wa Kitanzania. (*Makof*)

Nitoe mfano wa Mgodi wa Marmo Granito Mines (Tanzania) Limited ulioko Mbeya. Mgodi huu una wafanyakazi wasiopungua 32 amba kada zao ni za kawaida kabisa, mfano mafundi mchundo, madereva, walinzi, wapokea fedha, *welders* na mafundi seremala pamoja na mafundi chuma amba ni wageni. Hivi kweli hata mlinzi na mfunga mlango tuna haja ya kuwa na mgeni? Hivi kweli Mtanzania hawezi kufanya kazi zingine kama ufundi chuma? Kwa kweli ni aibu na hatuwezi kukubali huku kila siku tunaiomba Serikali yetu itueleze ina mkakati gani wa kupunguza tatizo la ajira nchini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika Kampuni ya Barrick wanaye *welder* wa Kitanzania ambaye analipwa shilingi laki nane. Lakini hapo hapo, kuna *welder* wa Kighana analipwa shilingi milioni 11 kwa mwezi. Kwanza ajira hii inatakiwa ifanywe na Mtanzania lakini isitoshe tofauti ya mshahara ni kubwa mno. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nitachangia kimaandishi na niwapongeze sana wafanyakazi wote kwa ujumla, tuko pamoja, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Makofi hayo Mheshimiwa Angellah Kairuki yanakubali mchango wako nilitamani nikuongezee muda hasa baada ya kuwatetea sana Ma-house *girl* ukasahau ma-house *wife*. (*Kicheko*)

MHE. ASAA OTHMAN HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nami fursa hii na kwa unyeti wa Wizara hii niweze kuzungumza machache kwani ndugu yangu mchangiaji aliyejita amefanya kazi nzuri hasa kwa eneo ambalo nilitarajia i niliongelee kwa uwezo wangu wote. Hata hivyo, tumefika mahali katika nchi yetu tuone ni aibu mzalendo kudhalilishwa ndani ya ardhi aliyozaliwa. Ajira ya wageni hatuikatai pale inapoheshimu sheria na taratibu na taratibu za nchi. Lakini itakuwa ni jambo la fedheha sana mzalendo kudhalilishwa na mgeni ndani ya ardhi yake. Kwa hili, tunaiomba sana Serikali ijenge utaratibu basi wa kuwaona kwamba wageni wana nafasi zao lakini wazalendo kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie moja kwa moja kwenye suala la ajira. Tumebarikiwa sana Tanzania. Tumebarikiwa kwa kuweza kuwa na mambo mawili makubwa kati yale manne aliyataja Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna watu na la pili tuna ardhi lakini ni kubwa yenyе rutuba nyingi, sijui tatizo tumejikwaa wapi. Ndugu yangu jana Kafulila alisema kwamba wazee kule wamechoka. Sitaki niseme wamechoka kadri ninavyomuona kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi anaonekana bado yuko imara. Lakini nadhani kuna neno la kujikwaa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asaa yale maneno ya Kafulila tulyaondoa kwenye *Hansard*. Endelea rafiki yangu.

MHE. ASAA OTHMAN HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kuna kujikwaa na kujikwaa siyo kuanguka. Nadhani bado muda upo wa kuweza kusimama na kufanya mazuri. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ni tegemeo la Taifa letu. Leo vijana hawa kwa kiasi kikubwa tunawapoteza kwa majanga mbalimbali yanayowapata na hii ni kutokana na kwamba kuwadhibiti bado hatujamudu vile ipasavyo. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaingia kwenye majanga mazito yanayopoteza maisha yao, lakini yanatupotezea sisi kama Taifa la Tanzania. Vijana wanaangamia na ubugiaji wa unga, uvutaji wa bangi na majanga mazito ambayo yanawapoteza maisha yao. Haya ni mengi tunayajua Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kila maeneo tunayotoka kwenye Majimbo yetu tunayaona, hivi basi nadhani wakati umefika sasa hii nguvu kazi ya Taifa tusiipoteze kama inavyoendelea sasa kupotea. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi tutamudu kuibua ajira? Ajira ya Tanzania kwa asilimia kubwa ni lazima turudi kwenye kilimo. Mheshimiwa Rais, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete amekiita Kilimo Kwanza kina tafsiri pana, muda huu hautoshi. Lakini niseme kwamba kilimo *per se* mifugo na uvuvi kwa ujumla wake hapa ndipo kwenye ukombozi wa Mtanzania kwenye ajira. Kwa kijana unapompeleka kwenye *power tiller* kama lilitivo utamkosa. Lakini utaweza kumchukua kijana kama utampeleka kwenye viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo, utaweza kumpata kijana kwenye kusarifu mazao ya mifugo, utamchukua kijana umwekee kusarifu mazao ya baharini. Maeneo yote haya Tanzania si maskini. Hatuko maskini wa ardhi, hatuko maskini wa mifugo, hatuko maskini wa bahari, hatuna umaskini wa watu. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pale tulijikwaa ndio tatizo letu. Sasa turudi tuone kwamba tumejikwaa wapi na tufanye nini ili tuondokane na hali inayotukabili sana. Hali ni mbaya inaumiza sana wazazi wanateseka kwa vijana wao. Lakini na Taifa nasema linapoteza nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni lazima tuweze kuvitunza, kuvienzi na kuvijenga. Labda nitoe rai tujenge viwanda, viwanda vyetu ni vidogo vidogo na viwanda vya katil. Lakini viwanda hivi vikae kwenye maeneo yale ambayo Kanda ya Ziwa wana maziwa ya kuvua samaki lakini pia kuna ufugaji mkubwa kwa hiyo, mazao haya mawili kwa pamoja yaweze kusarifiwa na vijana kuweza kupata ajira huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ya Kusini yenyе mazao mengi ya kilimo, tunataka kusarifu mazao ya kilimo, mazao ya kilimo tutaongeza tija kama tutayasarifu na kama si kuyauza kama yalivyo. *Juice*, inakuwa na thamani zaidi, ile *juice* ya embe ama ya chungwa baada ya kupatikana *juice* yenye we kuliko kuiiza lile chungwa kithamani yake. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matunda mengi Tanzania. Tuna mazao mengi ya kilimo, tuna mazao mengi ya mifugo. Tukiyataja maziwa ya ng'ombe, maziwa tunapoyasarifu kuna aina nyingine zaidi ya nne au ama tano kutokana na maziwa haya haya pamoja na kwamba leo bajeti hii tunazungumza ni sungura mdogo, inaweza ikawa hivyo na mimi nakubali, lakini sungura mdogo huyu huyu, tusije tukamchinja tugawana nyama, ni vema sungura tumlee aweze kuzaa matunda, tutaendelea kupata watoto hao hatimaye mwaka kesho tutazungumzia mbuzi. Tunakoondokea mbuzi wa maziwa anazaa watoto watatu na wawili ni faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuweze kuitumia vizuri sana bajeti hii ya mwanzo ya sungura mdogo kusudi bajeti ya tatu 2013 mama yangu pale Mheshimiwa Waziri tuzungumzie bajeti ya ng'ombe wa maziwa, tutakuwa tumepiga hatua kubwa ya kuwa na ng'ombe wa maziwa na kuhakikisha tunapata maziwa, tunasarifu maziwa na mazao yake, tunasarifu ngozi, tunapata nyama ya kula, lishe kwa mama, wazazi, wajawazito na wale wanaonyonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mada kuu ni ajira, ajira hii tutaweza kuikuza kwa kuwaita wawekezaji. Nataka nimalizie, tuhamasishe wazalendo kwenye suala la uwekezaji. Lakini na taasisi zetu za fedha sasa ziwe tayari Serikali hebu ifanye iwezavyo, taasisi za fedha ziweze kutoa mikopo nafuu kwenye masuala ya uwekezaji. Watanzania wana akili, Watanzania wana elimu, Watanzania wana uwezo, sikubaliani na kwamba hatuna uwezo wa kufanya kazi ama ni wavivu, hili siliweki kwenye mantiki. Lakini tutawezaje ni suala la kuwekeza kwenye viwanda vya kwetu vidogo vidogo, viwanda vya katilisimili ya ndani ya nchi ndio itaweza kutukomboa kwenye suala zima la ajira, vijana wanaangamia na Taifa linapoteza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyeti wa Wizara hii na kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge waweze kuchangia vizuri suala hili, naomba niheshimu muda huu na nakushukuru lakini niseme kwamba wazalendo namba moja. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Napenda kutumia nafasi hii pia kumpongeza sana Mbunge mwenzangu mwakilishi mwenzangu wa wafanyakazi Mheshimiwa Angella Kairuki kwa namna ambavyo ameweza kuwasilisha wafanyakazi wenzetu wa aina zote vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, basi utakapoletwa ule mkataba wa (*domestic workers*) wafanyakazi wa ndani sote tuungane pamoja tuupitishe ili tuwajengee wafanyakazi wote mazingira mazuri ya kufanya kazi zenye staha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba majukumu ya Wizara hii ni mengi na ni mazito. Lakini na malalamiko ya wafanyakazi nayo yamekuwa mengi sana, sikutaka kuyagisia leo. Lakini yamekuwa mengi mno. Niwaombe Waheshimiwa Mawaziri, hebu timizeni wajibu wenu, nendeni mkakague kwenye makampuni haya, mtambue kero za wafanyakazi, msisubiri mpaka sisi tuje tuwaumbue watu ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kampuni inaitwa *TANALEC* wanasema imeajiri Wakanya watupu, Watanzania waliopo pale wanakuwa *frustrated* siku hadi siku ili mradi tu waache kazi. Mazingira ya kazi makampuni ya migodi hao ndio wanawa-*frustrate* wafanyakazi vibaya mno, wanawazuia hata kujunga na Vyama vya wafanyakazi. Hebu basi angalau huyu wakala anayeitwa *OSHA* hebu tumwezeshe aende akakague vizuri hayo maeneo, msisubiri mpaka sisi tuwalettee taarifa humu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nije sasa na ya kwanza. Nataka nianze na kumnikuu bwana Juan's Somavia ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *ILO*, yeye anasema hivi naomba nitumie kanuni ya 60 ili niweze kusoma hii nukuu yake. Anasema: "We know that work is the best root of poverty but one can not legislate employment in and poverty out. It is a long and complex process that requires all elements of society to work together. The Government, employers, and workers each have a unique and crucial role to play in defining a positive consensus". (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba ajira ndio kigezo kikubwa cha kuondoa umaskini duniani kote. Katika nchi zilizoendelea hata Marekani leo raia wanawapima viongozi wao kwa kiwango gani wanaweza kupunguza tatizo la umaskini kwa kuongeza ajira. Wizara hii kwa kweli ndio Wizara mama inayoweza kupunguza tatizo la umaskini kama itafanya kazi yake ipasavyo. Hatuna kasoro yoyote kwa sababu nilikuwa naangalia na wenzetu wanafanyaje, nikakuta kwamba kumbe katika nchi za wenzetu nazo wana Wizara hii ya kazi na majukumu ya Wizara hii ni haya haya tu. Kusimamia sheria za kazi, kutatua migogoro ya

wafanyakazi, kutengeneza mazingira mazuri ya kazi, kutangaza soko la ajira. Lakini sisemi kwamba hatujapiga hatua, tumepeiga hatua kubwa sana. Kwa nini nasema hivi zamani tulikuwa tuna sheria takriban nane za kazi, zile sheria kila jambo lilikuwa lina sheria yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Trade Unions Act, Severance Allowance Act* na kadhalika tukaja tukazi-compile zile tukatengeneza sheria mbili, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba (6) ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi namba (7) ya mwaka 2004. Lakini sheria hizi zinatoa pia fursa ya mfanyakazi kudai haki yake kwa uhuru zaidi. Mfanyakazi anakuwa na uhuru wa kuijunga na Chama cha Wafanyakazi kule ndio kwenye kisemeo chake cha madai yake. Sasa hoja yangu ya msingi ninayotaka kuisema hapa ni nini? Sheria tunazo lakini malalamiko ni mengi, sheria hizi zinawalinda wanaolalamika, hebu tutimize wajibu wetu. Hata hivyo, tumekuwa tuki-concentrate sana na matatizo ya wafanyakazi sikatai, wana haki yao ni lazima tuwatendee haki. Lakini tunalo bomu kubwa sana la ukosefu wa ajira kwa vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo naona ni bomu kubwa kuliko hata yale matatizo ambayo yapo ya wafanyakazi ambaao tayari wamekwishaajiriwa. Kwa nini mtu yeoyote ambaye ana ajira huwezi ukamlinganisha na mtu ambaye hana ajira. Mtu ambaye anaamka asubuhi hajui atakula nini, ana watoto wanamtegemea, hajui atawavalisha nini, hajui hata ile siku itaishiaje, hajui mtu huyu. Vijana tuliokuwa nao wanategemewa na familia zao. Wana vigezo vya kuajiriwa na ni wengi lakini hawana ajira. Wizara ya Kazi na Ajira ndio Wizara inayotakiwa na ndio yenye wajibu wa kutengeneza soko la ajira. Timizeni wajibu wenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunasema moja ya kazi za Wizara hii ni kutangaza soko la ajira, lakini hata takwimu hauna. Nilikuwa naangalia *National Statistical Bureau*, siyo tu ya Tanzania na zingine zote hazina hata takwimu. Lakini nataka niwaambie na ndio maana nasema sisi hatuna kasoro yoyote, ni basi tu hatutimizi wajibu wetu kwa sababu majukumu tuliyonayo ya Wizara yetu yanafanana hata na nchi zingine. Hii *National Statistical Bureau* hata Taiwan wanayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakusomea taarifa iliyopo kwenye *National Statistical Bureau* ya Taiwan anasema *table* ya kwanza hizi ni takwimu, hizi *important indicators based on manpower survey*. Yaani hii ni *survey* ya nguvu kazi iliyopo Taiwan. *Important indicators based in seasonably adjusted series*. Ya tatu anasema, *labour force participation rate by educational attainment*. Hizo ni takwimu. Takwimu nyngine ni za *labour force participation rate by age*. Takwimu nyngine za *employed persons by industry*. Takwimu zingine *employed persons by occupation*. Takwimu zingine zinasema *employed persons by class of workers*. Takwimu zingine zinasema *employed persons by reason why in an employment* nyngine anasema: "An employment rate by educational attainment. Nyingine anasema an employment rate by age. Lakini ya mwisho takwimu zinasema *persons not in the labour force by reason why not?* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini sisi tunashindwa kuyafanya haya? Tunayo *National Statistical Bureau*, lakini haifanyi kazi yake. Leo utatangaza soko la ajira wakati wewe mwenyewe hujui una *manpower* kiasi gani? Hivi una uzalendo kweli na vijana wazawa katika nchi yako? Watu wataacha kuajiri watu waliokuwa nje kwa sababu hawaoni takwimu. Hebu timizeni wajibu wenu bwana tafadhali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuongelea tatizo la ajira kwa watoto. Hili lipo kisheria. Lakini hivi wale watoto wanaombaomba kule barabarani hii siyo ajira kwa watoto? Au ajira kwa watoto kwetu sisi tunaipa tafsiri ipi? Wale ni watoto, wana mama zao. Mama zao wanawatumwa wale watoto nenda kasimame kwenye gari ile kaombe pesa. Usipoomba pesa leo sikupi chakula. Kwa hiyo, ni *contract* kati ya mama na mtoto, mtoto aende akalete pesa kwa ujira wa kulipwa chakula. Mnashindwa nini kui-*define* hii? Kwani hili hamlioni kama ni tatizo? Mnasubiri mpaka Mheshimiwa Mama Sophia Simba ahangaike na Wizara yake wakati Sheria za Kazi zipo na zinapinga ajira kwa watoto. Timizeni wajibu wenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kidogo katika upungufu, hapana siyo wa Wizara. Kuna *point* moja nill-note hapa nilisema namna ambavyo sheria zetu hazitoi mwanya wa kuwafundisha kazi hususan wakandarasi. Tunao wakandarasi wa nchini China wanaokuja kujenga barabara. Wakandarasi hawa hebu tuwawekee utaratibu hata kwenye sheria tu ile ya manunuzi,

tuwape masharti kwamba mnapoondoka hapa muwe mmewafundisha Watanzania wetu, wazawa wetu amba mnaawaajiri kwa muda, angalau waweze kujua kumwaga lami kwenye barabara. Ili na sisi tuwe tuna *skills* itatusaidia kupunguza gharama ya kuleta wakandarasi. Lakini vile vile kuna tatizo lingine nataka niliseme hapa ambalo ni yale yale tu, tunao raia wa kigeni wanaingia nchini na makampuni yao ya samaki katika Kanda ya Ziwa wenye asili ya Kiasia, wanaajiri Waasia wenzao, wanawaingiza kinyemelanyemela, wanawapa ajira, wanawafungia ndani mle mle kwenye ma-godown, wakishajua Kiswahili kidogo tu ndiyo wanatoka nje. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, timizeni wajibu wenu. Nataka niwaseme sasa wafanyakazi. Tunao wajibu wa kudai haki zetu. Lakini hakuna haki isiyokuwa na wajibu. Wafanyakazi hatutimizi wajibu wetu. Kila mmoja kwa nafsi yake anajifahamu. Rushwa, kuvujisha siri za Serikali, huko ni kutotimiza wajibu kwa mfanyakazi. *Poor customer care!* Wafanyakazi hawajui *customer care* hata kama wanafundishwa, lakini *practically* Watanzania wengi hawajui *customer care*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikwenda Nane Nane pale, kuna banda moja la EPZ nafikiri lile. Kijana tu, sijui akafikiri na mimi ni kijana mwenzie. Ndiyo maana wenzetu huwa wanasema *do not judge the book by looking at its cover*. Anajibu jibu tu, tena anasonya. Wala sikuwa na haja ya kumwambia mimi ni nani, kwa nini nimwambie? Mimi ni Mtanzania mwenzake. Mteja, nahitaji huduma, anatoa tu majibu ya ujana ujana. *Poor customer care*, bado ni tatizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ukiyachanganya ndiyo yanayofanya hata wenzetu wa nje waajiri watu wengine. Lakini si hivyo tu, ndiyo yanayofanya hata baadhi yetu Watanzania hata kazi ya *domestic, ma-house boy, ma-house girl*, siku hizi tunawaajiri Wamalawi. Ndiyo. Mtu anaona bora Mmalawi kwa vile anajua kutimiza wajibu wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Naibu Spika, muda umekwisha?

NAIBU SPIKA: Ndiyo, ndiyo.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka niambiwe katika ile programu ya kukuza ajira kwa vijana imetengewa fedha kiasi gani.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Zainab Kawawa. Nakushukuru sana kwa mchango wako na kwa kweli Wabunge akinamama leo mmetuonesha mfano nzuri sana wa namna ya kuchangia. Mheshimiwa Zitto nitakupa nafasi baadaye. Lakini tuliwekeana utaratibu, ulikuwa umesafiri. Huwashi hiyo *microphone* mpaka nikuruhusu kwanza kusema ndiyo unaanza kusema. Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kazi na Ajira. Kwanza, niwapongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Kairuki na Mheshimiwa Zainab Kawawa na Mheshimiwa sijui jina. Wameongea *point* nzuri, nydinge hizo ambazo ningeongea lakini nitakazia na nitaongeza zingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni fedheha sana kwa Taifa letu kwa nchi yetu ya Tanzania kuona kwamba tunasomesha Watanzania, tunaanzisha hata *VETA* ili vijana wetu wapate ujuzi na kujajiri na kwamba waweze kuajiriwa na tuna sera kwamba tunaleta *foreign investors*, tija mojawapo katika ya nydingi tuzitarajazo ni kutoa ajira nydingi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia gazeti la *The African Toleo* la tarehe 1 Agosti, ambalo limebeba *heading*, *Barrick undermines Tanzania workers*. Naomba kwanza kuchangia unyanyasaji wa wafanyakazi wazawa kwenye hii kampuni na makampuni mengine mengi ambayo ni ya kigeni, kuna unyanyasaji mkubwa sana. Ila naomba nifanye *case study* ya *Barrick* ingawaje Mheshimiwa Angellah aligusia tu kwa kutoa mfano wa yule Ghanaian ambaye

ameletwa analipwa milioni 11 *point something* na ambaye kuna Mtanzania au Watanzania *with the same experience analipwa laki nane.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa makampuni hayo hayo ambayo yapo Bulyanhulu, Tulawaka, Buzwagi na kule kwetu North Mara yamekuwa yakiwatumia wazawa kufanya hizo kazi zote. Watanzania hao wanafanya kazi zaidi kuliko huyo *expatriate* au hao ma-*expatriate* wanaotoka Ghana, South Africa na kwingineko, lakini hao ma-*expatriate*wanapata *credit at the expense* ya hawa wazawa ambao wanalipwa laki nane tu. *On top of that* hawa wazawa hawapati hata ile *allowances* ya kununua maziwa kwa sababu tunajua kazi za *mines* kwa wale wanaochimba madini wanatumia *materials* ambazo ni *toxic* ina maana afya yao inakuwa *in danger* hawa ma-*expatriate* wanapewa laki nane au dola 800 kwa wiki kama *allowance* ya maziwa na vitu vingine kuweza *ku-exhale* ile sumu. Lakini Watanzania wenzetu hawapewi hata senti tano. Ina maana wala hawapati hata ile *packet* ya maziwa kila siku kuweza kutoa ile *toxic materials* ambazo wamekuwa wamezivuta, wakiwa kule kwenye migodi chini. Hii inatia fedheha sana na inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ambayo tumekuwa tukijiliza, na nimekuwa nikijuliza naomba Mwenyezi Mungu anipe muda nichangie. Ni kwamba hawa *expatriate* wanaokuja wana-*submit CV* zao ili waweze kupata *work permit*. Nataka njue Idara husika ikipitia hizo *CV* na vyeti vyao vingine inajidhihirisha vipi kwamba kazi wanazoomba hamna Mtanzania mwenye sifa kama hiyo na hadi inapelekea kutoa *post* hizi kwa hawa wageni. Kwa hiyo, napenda sana Waheshimiwa Mama yangu Kabaka na kaka Makongoro, Mawaziri wa hii Wizara wanipe majibu kwa haya kwamba ni vigezo vipi wanatumia kuweza kutoa hizi *posts* kwa wageni tena ambao hawana sifa kama hayo Ghanaian ambapo tuna Watanzania ambao wanaweza kufanya kazi hizo na mbaya zaidi ndio hao ambao wanazifanya na kwa nini wasiweze *ku-create* hiyo iwe kama ni ajira kwa Watanzania na ni lini watasitisha hiki kitendo cha wageni kufanya kazi zinazoweza kufanya na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa Mawaziri kama waniambie waliweza kupata nafasi ya kusoma hili gazeti la *The African* kwa maana imeandika maovu mengi. Kama walipata ni hatua gani wamechukua kufuatilia katika hizi *institution* ambazo zimekuwa *ear marked* hapa. Kwa hiyo, katika majumuisho yao ningependa Wizara husika itoe majibu kwa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuongelea kuhusu wafanyakazi ambao unakuta wanapata ulemavu wakiwa kazini na wengine wanapelekea hata kuacha kazi, lakini hawapati *compensation* yoyote ile na wanakuwa wametelezewa. Napenda Wizara husika iniambie *statistically* imefanya uchunguzi au kuitia kwenye taasisi nydingine zozote zile za *private* na za *Government* kwa sababu tuna kesi nyangi ambazo wafanyakazi wa Serikalini wamepata ulemavu wameacha kwa sababu wamekuwa *disabled*, hawawezi kuendelea na kazi, lakini aidha, wamepata malipo finyu au hawajapata kabisa. Kwa hiyo, pia nitapenda kupata ufanuzi kwa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine napenda kuzungumzia kuhusu wafanyakazi 92 ambao walikuwa wakifanya kazi kwenye Kiwanda cha Urafiki cha Dar es Salaam ambao waliachishwa mwaka 1999. Wafanyakazi hao wali-*file case* wakidai mafao yaoambayo ni zaidi ya bilioni 1.8. Walishinda kesi, Serikali ikakata rufaa, lakini pia Serikali bado ilishindwa kesi. Kuanzia mwaka 1999 mpaka leo ni takriban miaka 11, hawa wafanyakazi hawajalipwa, *despite* ya kwamba kuna barua imeandikwa na Msaidizi wa Rais *iki-instruct* hawa watu walipwe, lakini mpaka leo hii bado hawajalipwa. Kwa hiyo, napenda Wizara iniambie hawa wafanyakazi 92 waliokuwa wakifanya kazi kwenye Kiwanda cha Urafiki, Dar es Salaam watalipwa lini? Hiyo 1.8 bilioni ita-*accumulate interest* maana yake miaka 11 mingi na ikizingatiwa maisha ni magumu kama tujuavyo kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si waathirika wa Urafiki tu pia kuna wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi kwenye Kiwanda cha Sukari Kilombero walioachishwa mwaka 2000 wakati kiwanda kinabinafishwa. Mpaka leo hii na wenyewe hawajalipwa stahiki zao. Napenda Wizara pia iniambie kwa hili. Ni lini hawa watu watalipwa stahiki zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majumuisho yote naomba pia kuiuliza Wizara na Idara zinazohusika kwenye utoaji wa vibali ingawa nili-site Barrick lakini pia kuna makampuni ambayo *management* zao zinaongozwa na wageni. Nataka kujua *post* kama *human resource*, *post* kama *public relations*, na *post* zingine nyngi ambazo tuna Watanzania wenye *qualification* tena wengine wana *masters degree*, kuna wengine wana *degree* ya kwanza kuna wengine mpaka wana *PhD* wanawenza wakafanya hizi kazi, lakini *yet ukienda kwenye hayo makampuni unakuta ni wageni ndiyo wapo, it is an absurd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *Baclays Bank* leo *all the management team* ni watu wa nje. Hivi hatuna Watanzania kweli wanaoweza kufanya hizi kazi. Kwa nini tunaruhusu hii halilitee. Ukienda leo *Zantel* menejimenti yote pale ni watu wa nje. Kwa kweli inatia uchungu sana na ina-*demoralize* Watanzania wanaosoma. Kwa sababu unabaki tu kuwa mtaani, usipokuwa na *security* ya kwenda kukopa benki uanzishe kabiashara kako unakuwa ni mtu ambaye uko mtaani. Napenda sana nipate majibu kwa haya, wakati wa kufanya majumuisho yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu makampuni makubwa, wajaribu pia kutembelea hizi *workshop* za magari. Ukienda kwenye magereji mengi ya Wachina utakuta zile *post* nyngi ni Wachina wapo na kwenye hiyo *garage*, unakuta wameweka kama kahimaya kao, ambapo wanaishi humo humo, kama alivyosema Mheshimiwa Zainab Kawawa, ingawa yeye ame-*site* Wahindi. Naomba ni-*site* Wachina. Wanakuwa wako ndani na mle, wanamchukua labda Mtanzania mmoja ambaye atawafundisha Kitanzania kidogo, then *after* wanatoka wakiwa wanaelewa lugha kuongea na wateja. Ina maana ajira haiwezekani hata umakenika tusipatie Watanzania wenzetu hizi *post*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo. Naomba nitoe nafasi kwa wengine. Ila naomba katika majumuisho nipate majibu kwa yote mliyosema. (*Makofii*)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Wizara hii. Nilifikiri kwamba Wizara hii jukumu lake kubwa kama si jukumu pekee ni kutengeneza nafasi za ajira. Nafasi za kazi kwa Watanzania kwamba, jukumu kubwa la Wizara hii liwe ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata kazi na ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inaitwa Wizara ya Kazi na Ajira. Sasa nimeangalia kwenye kitabu cha bajeti, *Volume IV*, kitabu cha Nne ukurasa unaohusu Wizara hii ina ukurasa kama mbili hivi, siyo nyngi. Lakini imepewa kama shilingi bilioni moja, Wizara nzima kwenye mafungu ya maendeleo ina shilingi bilioni moja. Sasa najiuliza hii Wizara itafanya kazi namna gani? Wamesema bilioni sita, bilioni tano, milioni tisa, hizi tano ni za nje, ni *forex* misaada itakayokuja, wafadhili na mikopo na huenda isije, hela ya ndani iliyotengwa ni shilingi bilioni moja. Wizara haiwezi kufanya kazi namna hiyo. Ndiyo maana pale Mheshimiwa Zainab Kawawa amesema kwamba haungi mkono hoja mpaka aambiwe kile kifungu cha *youth employment programme* kina shilingi ngapi? Kina sifuri kwenye *local* kina sifuri kwenye *foreign*, yaani hakina kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na vifungu vingi ndani ya Wizara hii ni sifuri, sifuri, sifuri, havina pesa. Sasa hili jukumu la kutengeneza ajira litafanyika vipi bila pesa. Kwa hiyo, najiuliza, lakini pia nafikiri tunafikiria sasa ajira za kuajiriwa kwenye Serikali, kwenye Idara za Serikali, Mashirika ya Umma, maana yake hatupanui wigo. Hotuba ya Waziri imezungumzia kidogo mambo ya kilimo, mambo ya ufundi na mengine. Lakini hotuba yenye haielezi kwa kina, haina mkakati wowote wa kupanua ajira kwenye maeneo haya. Nafikiri ajira kubwa katika nchi hii ni kwenye kilimo. Asilimia karibu 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, mwajiri mkubwa ni kilimo, lakini Wizara hii haina mkazo huko. Haielezi inaboresha vipi mambo ya kilimo ili kupanua ajira kwenye sekta hii. Hadi leo tunalima kwa jembe la mkono. Huwezi ukasema umejjajiri kwenye kulima kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea Wizara hii itoe mipango, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara nyngine kuboresha ukulima wa kisasa. Tupanue tuwe na wakulima wakubwa. Niishauri Serikali hivi, wakulima wakubwa waje, wawekeze hapa, wana mitambo, matrektu, wana *planters, harvester, mashine* za kupalilia, wanaweka mbolea vizuri, wanaajiri wananchi wengi.

Tunapanua ajira kwenye kilimo. Akija mkulima mmoja mkubwa akalima ekari 1,000 au hekta 2,000, ataajiri watu wengi sana na si ajabu hawa watakaoajiriwa pale watapata mapato makubwa kuliko aliyeajiriwa kwa jembe la mkono. Aajiriwe pale, apate mshahara na mapato mengine makubwa kuliko kama yeje angelima kwa jembe la mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi. Uvuvi ni sekta nyingine ambayo ilikuwa inaaajiri watu wengi sana. Wanajajiri wenyewe, wanavua, wanapata mapato. Sasa hivi kwa mfano pale Bukoba, tumezungukwa na ziwa. Tuna samaki wengi ndani ya ziwa mle, kwa miaka mingi wananchi walikuwa wanavua, wanajajiri wenyewe. Sasa wamezuiwa kuvua. Wameambiwa wanaharibu mazingira ya ziwa, mazalia ya samaki. Kwa hiyo, hakuna kazi. Kazi zilizoko zimeharibiwa, zimeuawa. Nilitegemea Wizara hii iwe na mpango madhubuti hawa wananchi wawezeshwe, waunganishwe vikundi vidogo vidogo, wapate elimu na mikopo. *TIB* inatoa mikopo, Wizara iwawezeshe, wanunue mitambo mizuri, maboti makubwa, injini waende maji marefu, wavue vizuri bila kuharibu mazingira. Ajira ziendelee kuwepo. Sasa hizo wameambiwa wasivue na hakuna njia mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufgaji. Mtu anaufuga ng'ombe mmoja, wawili, huku siyo kufuga, ni kuchunga na unasema umejajiri kwenye ufgaji. Huu siyo ufgaji, Wizara hii ingekuwa na mpango madhubuti kuboresha sekta ya ufgaji, wakulima waweze kuwa na ufgaji bora na waweze kupata matunda mazuri ya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ufundi. Amesema mmoja wa wasemaji, Mbunge mmoja kwamba tuna *VETA* 20 peke yake, nchi hii au pungufu ya hapo. Kuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika baadhi ya Wilaya. Hivi ni vyuo ambavyo vinatoa mafunzo ya ufundi stadi, ufundi mbalimbali, ufundi seremala, ufundi uwashi, ufundi magari, *welding* na kadhalika. Vijana wangekwenda wengi kule, vyuo viongezwe. Pale ambapo havipo vijengwe, vijana wasome kule ndani wapate mafunzo, waweze kuongeza fursa za ajira. Lakini pia suala la wageni limesemwa na Waheshimiwa Wabunge, wageni wamesambaa mpaka mitaani, wanaiza madukani, wanaiza karanga. Hili limesemwa sana, nisisitiza kwamba kwa kweli, katika hili hatua zichukuliwe, waondolewe wageni amba wameingia kiholela, wenyeji wachukue nafasi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna fursa nyingi za ajira kwenye soko la Afrika Mashariki. Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya milango imefunguliwa. Imekuwa wazi, nilitegemea Wizara hii iwe na mpango madhubuti kusaidia vijana hawa wenye stadi za ufundi na kadhalika waende huko watafute ajira katika nchi jirani. Pale Bukoba kuna vijana wengi sana wana ufundi mbalimbali, fundi uwashi kama nilivyosema, ufundi *welding*. Lakini kijana atoke pale aende Kenya atafute kazi mwenyejewa hawezi, hajui aanzie wapi. Kuna fomu za kujaza, kutafuta *passport*, vibali na kadhalika. Wizara iwawezeshe, iwashauri, iwafundishe, waende kule wapate nafasi hizo. Nafasi zipo na tuzitumie. Wenyejewa wamekuja huku, pale Dar es Salaam wamejaa Wakenya na Bukoba wamejaa Waganda. Wametumia fursa hizi, sisi tumekaa hatuzitumii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri tumeona amesema kwamba kuna baadhi ya Watanzania wamekwenda nje, wamepata kazi. Ukienda nchi kama Italia kuna Waphilipino milioni moja, wana mikataba, wanafanya kazi za ndani, kulea watoto, kupika, mkataba kati ya Serikali ya Philipino na Serikali ya Italia. Wizara hii ifanye mambo kama haya iwawezeshe. Tupeleke vijana nje watafute ajira huko wafanye. Ukienda Qatar wamejaa Wasudan wengi sana kwa mkataba maalum, Serikali ya Sudan ya zamani ile kabla haijatengana. Sasa kwa nini sisi tusifanye hivyo? Wizara hii ndio kazi zake hizo kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuzungumzia suala la wastaifu. Nashukuru baadhi ya Wabunge wamezungumzia pensheni kwa wazee wote. Ni jambo jema likifanyika, lakini hata wale watu wa pensheni wanaopewa sasa hivi ambao ni wastaifu wanapewa pensheni kidogo sana. Kuna wazee wamestaifu wameitumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa, kwa miaka mingi, hadi kufikia umri wa kustaifu kwa heshima. Hawakuiba wala hawakufukuzwa. Anapewa pensheni sh. 40,000/= kwa mwezi au sh. 30,000/= kwa mwezi, ataishije huyu mzee? Tunasema tunamtunza malipo ya izeeni. Haya siyo malipo ya izeeni ni utani huu! Huyu mzee anaishi pale ana mke wake, ana watoto anaishi nao, au watoto wake wengine wamefiwa analea wajukuu pale,

ataishije na shilingi 30,000? Hiki kiasi kiongezwe ili aweze kununua unga, mboga, mafuta ya taa na sukari. Pale Bukoba sukari kilo moja shilingi 2,300/=. Juzi hapa nilidanganywa na Waziri wa Viwanda kwamba, sukari itapungua bei itakuwa sh. 1,700/=, imepanda, sh. 2,300/= kilo moja. Sasa mzee mnampa shilingi 30,000, ataishije?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombi Wizara hii iangalie jambo hili la pensheni kwa wazee. Juzi nilikaa pale Bukoba, wanajeshi wastaa fu wengi kama 200 wamenialika. Walikuwa na kikao chao wakanialika. Kilio chao ni hiki, wanapata pensheni kidogo sana hawawezi kumudu maisha. Kwa hiyo, niombi sana hawa wenzetu tuisiwaue haraka, tuwape pensheni kidogo ambayo inaweza kukidhi maisha yao ili waweze kuishi vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa maelezo hayo nashindwa kujua kama niunge mkono hoja hii au nisiunge mkono, hakuna pesa humu, niunge mkono nini? Haina pesa, Wizara nzima inapewa billioni moja! Kwa hiyo, sijui kama niunge mkono au ninyamaze. Nisubiri labda majumuisho nitajua la kufanya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza. Waheshimiwa Wabunge kwa ratiba ya leo tunapaswa kuimaliza shughuli iliyio mbele yetu ya Wizara hii ya Kazi na Ajira na kwa hiyo wachangiaji wetu wachache lakini wametuwalishwa vizuri. Jioni tutapata nafasi ya mchangiaji mmoja tu halafu tutaendelea na utaratibu. Mheshimiwa Rebecca Mgodo kama ataweza kuwahi saa 10 kamili juu ya alama. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mpina anakumbushia tangazo la wale wawakilishi wa vyuo vikuu kukutana pale Ukumbi wa Msekwa saa saba hii kwa muda mfupi sana. Lakini niwatangazie Waheshimiwa wote kwamba kesho ni siku ambayo tumepanga shughuli nyangi, tutaanza na semina asubuhi, saa tisa kutakuwa na mpira wa miguu na netiboli kule uwanjani. Lakini saa moja jioni kutakuwa na tafrija fupi itakayofanyika katika viwanja vyetu vya Bunge ambayo imeandaliwa na *British Council*. Kwa hiyo, wote tunaalikwa kushiriki katika tafrija hiyo ya kesho jioni. Kwa hiyo, kesho ni siku ya shughuli nyangi tunawaomba tushiriki katika maeneo hayo tukikumbuka vile vile kwamba maonyesho ya Nane Nane hapa Mjini Dodoma yanaendelea na ni vizuri Waheshimiwa Wabunge kuyatembelea.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili leo jioni.

(*Saa 7.11 mchana Bunge lilitishwa hadi saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

HOJA ZA SERIKALI

(*Majadiliano yanaendelea*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Na kama nilivyoahidi kabla ya kusitisha shughuli za Bunge mchana wa leo kwamba Mheshimiwa Rebecca Mgodo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo. Baada ya hapo nitamuita Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, atafuata.

Mheshimiwa Rebecca Mgodo. (*Makof!*)

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, ambayo aliwasilisha Bungeni ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya mwaka 2011/2012. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ni chombo muhimu sana katika kuhakikisha maendeleo ya nchi yetu, lakini bado Taifa letu lina changamoto nyangi. Bado Taifa letu

linahitaji elimu ili tuweze kuondokana na hali ya umaskini tulionao, bado katika Taifa letu kuna watu ambao hawafanyi kazi kabisa. Wengine hawafanyi kazi kwa sababu pengine wamekosa kazi! Wengine hawafanyi kazi kwa sababu pengine wanaangalia kazi fulani kwamba ni kazi ya kike au ni kazi ya kiume na hivyo kuamua kukaa bila kufanya kazi na ndio maana nimesema kwamba elimu bado inatakiwa kwa sababu kwa kufanya kazi kwa bidii ndio njia pekee ambayo kila Mtanzania na kila mwanajamii wa nchi hii anaweza kujikomboa katika hali tuliyonayo ya umaskini na kupata maendeleo katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi unaosema kwamba asiyefanya kazi basi na asilie, lakini utakuta kuna watu wakishaona chakula kimeshaipuliwa wapo tayari kwenda kula na kazi hawajafanya na mimi nataka kuwatangazia kwamba waufuatilie usemi huu ya kwamba asiyefanya kazi na asile na hivyo wajitume, wafanye kazi kwa bidii, kwa sababu hatuvezi kuendelea kuwa Taifa la kuomba tu misaada. Tunapewa misaada ili na sisi wenyewe tuweze kufanya kazi zetu wenyewe na kujitegemea sisi wenyewe, ni muhimu watu wakafahamu kwamba kufanya kazi sio adhabu. Kufanya kazi kwa bidii inahitajika na hivyo tutaweza kupata mafanikio makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu za mwaka 2006 tunaambiwa kwamba watu ambao wana uwezo wa kufanya kazi wanafikia milioni 22 na takribani watu zaidi ya 800,000 kila mwaka wanaingia katika soko la ajira na ni ushauri wangu pia kwamba vyombo husika viweze kufanya utafiti sahihi ili pia tuweze kuwa na tafiti ambazo zinaendana na muda huu ambao tunao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi Watanzania au jamii kwa ujumla tunahitaji kufanya kazi katika mazingira salama ya kazi. Na wakala ambaye anahuksika na mazingira safi na salama ni OSHA ambao wanatakiwa kukagua sehemu za kazi na usalama wa wafanyakazi, kutoa ushauri wa kiufundi, lakini mara nyingi tumeona kwamba wameshindwa na nikitoa mfano wa kiwanda kimoja kinaitwa *Jambo Plastics* pale Dar es Salaam ambapo nembo ya OSHA ipo, lakini wafanyakazi wa kile kiwanda wanasema hawajawahi kuwaona OSHA wakija kukagua! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine hatuvezi kuwalaumu sana OSHA kwa sababu tunasikia kwamba hawapo zaidi ya 50 kwa nchi nzima na wanafanya kazi kwa Kikanda, hawana vitendea kazi, wana gari moja Mbeya, wana gari moja Arusha, wana gari moja Mwanza na magari matatu Dar es Salaam. Hivyo, ningependa kutoa ushauri kwa Serikali ya kwamba itenge fedha kwa ajili ya kuwawezesha OSHA ili waweze kufanikisha kazi yao na usalama kazini na afya kwa wafanyakazi iweze kuzingatiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi fulani Serikali imewaachia waajiri na waajiriwa na hajatoa mchango wake sana na ndio maana kwa mfano huu ambao nimeutoa, *Jambo Plastics*, utaona kwamba kwa muda mrefu wafanyakazi wamefanya kazi katika mazingira magumu bila kuwa na vitendea kazi na wakati mwingine hata chumba kile cha kazi hakuna mzunguko mzuri wa hewa na hivyo inaweza kusababisha wao kupata magonjwa ya kuambukiza kama vile *TB* na ndio maana nimeishauri Serikali iweze kuchukua hatua hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi hali ya kiwanda hiki ya usalama wa kazi haiendani kabisa na haki za binadamu. Milango yote hufungwa na kubakizwa mlango mmoja tu! Na endapo hatari ya moto itatokea ni kwa hakika kwamba wafanyakazi wa kiwanda kile wanaweza kupoteza maisha yao kwa sababu ya msongamano wa kujitahidi kujilokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2004, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilianzisha Sheria za Kazi; Sheria za Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Namba 7 ya mwaka 2004 madhumuni makubwa yakiwa ni kutoa muongozo wa kisheria kwa ajili ya mahusiano mazuri na ya haki ya kiajira na viwango vya msingi vya mazingira ya kazi. Pia kutoa muongozo wa majadiliano ya pamoja ya hiyari baina ya waajiri na wafanyakazi. Pia kutoa muongozo wa kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi, uamuzi na hukumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya sheria hiyo kuwepo bado kuna Watanzania ambao wanafanyishwa kazi kama watumwa katika nchi yao wenyewe! Ninaomba Sheria iweze kushika mkondo wake kwa sababu kama Sheria imetungwa ina maana inahitaji kuheshimiwa na waajiri na waajiriwa pia. Haiwezekani kwa kizazi hiki cha leo tusikie kwamba kuna wafanyakazi wanawekewa hata masharti ya mavazi! (*Makofii*)

Nitapenda kutoa tena mfano wa kiwanda hiki cha *Jambo Plastics* kwa sababu, wafanyakazi wanavalishwa vikaptura na ndala! Hawaruhuswi kuva suruali! Wafanyakazi wanafanya kazi zaidi ya saa zile ambazo zimekusidiwa bila hata Mkataba wa Ajira! Huu ni mgogoro ambao umeendelea kwa zaidi ya miaka sita! Na ningependa kujua ni kweli kwamba Serikali imeshindwa kabisa kutatua mgogoro umeendelea kwa miaka sita? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba aliyoitoa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema kwamba Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilitembelea kile kiwanda na mimi nilisikia kwamba baada ya Kamati ile kutembelea kile kiwanda badala ya mwajiri wa *Jambo Plastics* kufuata ushauri aliokuwa amepewa, badala yake alichukua polisi na akatumia msaada wa polisi kuwatoa wafanyakazi na kuwazuwa wasilingie ndani! Wafanyakazi ambao wanakaribia 400 na kwa sasa hivi tunasikia kwamba ameajiri wengine wapya bila kuwapa haki zozote za kimsingi wale walioachishwa kazi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sio haki hata kidogo, ni lazima Serikali ifuatilie jambo hili na ikiwezekana pia pengine kuna viwanda vingine vingi zaidi hapa nchini ambavyo vinafanya kama *Jambo Plastics* na sio sahihi kabisa ya kwamba wananchi wenzetu waendelee kuteseka na kudhalilishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa kuongelea kuhusu ajira kwa watoto, ni muhimu haki za watoto pia zikalindwa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa ule wa 10 naomba kunukuu, alisema kwamba; "Wizara inatekeleza mpango wa kutokomeza ajira mbaya ya mtoto katika Wilaya 18 za Tanzania Bara na Wilaya mbili za Tanzania Visiwani, chini ya mradi uliofadhilliwa na Idara ya Kazi ya Serikali ya Marekani." (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo lolote na ufadhili. Lakini mradi wa kutokomeza ajira mbaya kwa watoto na mazingira hatarishi ni mradi ambao umeendelea kwa muda mrefu sana! Mimi tangu nikiwa kwenye vyombo vya habari miaka 16 nimefanya kazi kwenye vyombo vya habari, tulikuwa tukiandaa vipindi vya kuelimisha wananchi kusudi ajira hizi zikomeshwe; kwa muda wote huu, kwa nini hii ajira haifiki mwisho? Au ni mradi wa watu kuendelea kukaa katika maofisi na kupokea mishahara minono huku watoto wetu wakiendelea kuteseka barabarani na katika mashamba na hata katika migodi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali ya kwamba iharakishe na iangalie kwamba hii ajira ya mtoto na mazingira hatarishi ya kazi kwa watoto pia; yanakomeshwa kwa sababu inawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida sisi Watanzania ni watu tunaokuwa na familia ndefu, Waingereza wanasema *extended family*, tunakuwa na familia ambapo kuna shangazi, kuna mjomba na kuna ndugu wengine. Pengine sasa ni wakati umefika Wizara itumie nguvu ya vyombo vya habari. Vyombo vya habari vina nguvu kubwa sana, vinaweza kuwafikia watu wengi kwa wakati mmoja. Hivyo basi, naishauri Wizara iweze kuwa na vipindi hata vya redio au vya television kuliko kusubiri siku ya Nanenane au siku ya maadhimisho, ndipo tunaona! Kwa mfano ukurasa wa mwisho hapa, tunaona OSHA wakiwa kazini na katika mazungumzo yangu nimesema hawana vitendea kazi! Lakini katika kitabu tunaoneshwa wako kazini! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusikae kusubiri maadhimisho ni lazima Wizara itumie nguvu ya vyombo vya habari, kuna watu wanaamini sana vyombo vya habari, wakisikia chochote kutoka chombo cha habari, wanaamini. Hivyo basi, tusipoteze hiyo nafasi, lakini ili kuwaokoa watoto wetu ambao ukifika Dar es Salaam wanaombaomba! Ukifika kule baharini kwenye mabaki yale ya meli wapo kule ndiko wanakoishi! Na sisi tutakaa tukisema kwamba tunangoja ufadhili, kila mwaka tunagoja ufadhili! Ninaomba jambo hili liweze kufikia mwisho wake na Serikali iweke nguvu katika

kutokomeza kabisa na kukomesha na huu mradi sasa ufile mwisho tuone kwamba jambo hili linamalizika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba niishie hapo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rebecca Mgodo, umetukumbusha enzi ulipokuwa kwenye habari kule.

Sasa kabla hatujaendelea naomba kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, ambao ni wanakijji 40 wa kijji cha Sanjaranda. Pale walipo naomba wasimame, karibuni sana, wanaongozwa na Diwani wa Kata ya Sanjaranda Ndugu Eliphasi Lwanji. Karibuni sana Bungeni na niwahakikishie Mbunge wenu Mheshimiwa John Paul Lwanji, anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni. Karibuni sana. (*Makofii*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ni muhimu sana kwa wafanyakazi wetu pamoja na vijana wetu wanaomaliza masomo yao na wale ambao hawajapata bahati ya kuendelea na masomo ya juu lakini wanahitaji ajira ili waweze kujipatia riziki za maisha. Katika Wizara hii ukisoma ripoti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha bado haijaaeleza kuhusiana na changamoto ambazo zipo kama vile kwanza wafanyakazi wa majumbani hawalipwi mishahara yao.

Pili, wafanyakazi wa majumbani wanalipwa mishahara midogo sana. Tatu, wafanyakazi wa mahoteli wanalipwa mishahara midogo pia hawana mikataba na nne, wafanyakazi wa baa hawalipwi mishahara yao hata wakilipwa ni mishahara midogo sana pia hwana mikataba ya kazi.

Tano, wafanyakazi wanaojiriwa katika makampuni binafsi hawana *job security* na wanafukuzwa kila wakati katika ajira zao, sita, ajira kwa vijana ni ngumu sana na saba, mishahara inaongezwa kwa kiwango kidogo sana katika mashirika ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa Wizara, kwanza kufanya tathimini ya vijana wanaojiriwa katika baa, mahoteli na wafanyakazi wa majumbani, pili, kufanya tathimini ya mishahara yao na tatu, kuweka viwango vya mishahara yao na nne, ku-*publish* tathimini katika magazeti na kwenye mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa hotuba nzuri na ya kina, fupi lakini iliyoeleweka vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa kuwa inasimamia sekta nyeti ya kazi na ajira na mambo yote yanayoambatana nayo kama vile sheria za kazi, haki za wafanyakazi, maslahi yao wakiwa kazini na baada ya kustaaufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza utaratibu wa kuwahuisha wakulima na wafanyabiashara na sekta binafsi kujiunga na kuchangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Pamoja na hamasa inayofanyika bado kwa wakulima kuna kikwazo kwa vile mapato yao ni ya msimu hivyo hawana uwezo wa kuchangia kila mwezi. Nashauri uwepo utaratibu maalum kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Wizara ya Afya unaelekeza kwamba mtoto anyonye maziwa ya mama yake kwa miezi sita mfululizo tangu kuzaliwa. Je, Wizara ya Kazi na Ajira imeweka utaratibu gani wa kuwawezesha wanawake wafanyakazi kunyonesha watoto wao kulinga na mwongozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya haki kwa kazi halali yanastahili kwa kila mfanyakazi. Ubaguzi katika malipo kati ya wafanyakazi wa aina moja unajitokeza sana katika viwanda na makampuni ya watu binafsi. Wafanyakazi wengi wazalendo hupewa malipo kidogo dhidi ya wale wanaotoka nje. Suala hili lichunguzwe na kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Waziri na Naibu wa Wizara utekelezaji mwema wa Bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABABAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Waziri wa Kazi na Ajira, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara yako kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Shirika la *NSSF* na hasa kwa uongozi madhubuti wa Dkt. Ramadhan Dau kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Dar es Salaam wanajua kwamba daraja litaanza kujengwa chini ya uongozi madhubuti wa *NSSF* na mimi nimeona picha yake kwenye viwanja vya Bunge ni zuri na linapendeza sana, lakini leo wakati wa majumuisho wananchi wa Dar es Salaam watafurahi sana wakisikia kauli yako daraja litaanza kujengwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mamilioni ya Kikwete, tunapongeza sana mfuko huo kwa kujali wajasiriamli, lakini mara ya kwanza zilipotolewa pesa hizi katika Jimbo langu wajasiriamli wengi hawakupata kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba katika Jimbo letu la Temeke, mamilioni ya JK yapitie *SACCOS* na *VICOBA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) kwa rehma na neema zake nyingi kwangu, sina budi kupiga magoti kwake (*Alhamdulillah*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ni muhimu sana kwa ustawi wa watu wetu na uchumi wa Taifa kwa ujumla, kazi ndio kipimo cha utu. Ni lazima kila mtu afanye kazi ili aweze kumudu kujihudumia yeye mwenyewe, lakini pamoja na familia yake au wale waliomlazimu kuwahudumia kwa mujibu wa sheria za nchi au za vitabu vitukufu vya dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ndio nguvu kazi ya nchi yoyote duniani ikiwemo nchi yetu Tanzania. Nchi yetu imejaalifa kuwa na rasilimali watu kubwa na hasa vijana. Rasilimali hii bado haijatumiwa ipasavyo kwani Serikali pamoja na kuwepo sheria lakini bado haijasimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ni tatizo kubwa katika nchi yetu, pamoja na jitihada za Serikali kuvutia wawekezaji bado kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wengi wa ndani na nje bado, bado hawajakubali kufuata sheria ya ajira. Sekta nyingi hizi za uwekezaji na za binafsi zinaacha kuwaajiri vijana wetu hata kama wana sifa zitakiwazo na wanaajiri wageni wenyе sifa za chini zaidi ya wazawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la aibu, fedheha na dharau kwa nchi hii na viongozi wake pale inapofikia hata meneja wa kawaida mahotelini asilimia kubwa kuwa ni wageni. Kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna zaidi ya hapo, hata mkatishaji vishina vya tiketi za boti pale bandarini Dar es Salaam anawekwa mgeni! Hii inaleta adha, usumbufu na dharau kwani mkatishaji vishina huyu anakuwa hajui hata lugha yetu na inasababisha afanye dharau kwa wazee wetu na hata viongozi wetu! Hii ni fedhaha!

Mheshimiwa Naibu Spika, hata pale inapokuwa ajira zimetolewa kwa wazawa wenye sifa sawa na wageni hawalipwi vizuri kama wazawa! Hili ni tatizo na Serikali sasa ni waketi na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni lazima ishirikiane vizuri na Idara ya Uhamiaji ili wageni wanaoomba vibali vya kazi nchini bila ya kuwa na sifa stahili kwa nini wanapewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu Serikali kupitia Wizara hii ya Kazi ifanye ukaguzi wa wafanyakazi ili kubaini wageni walioajiriwa ni kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika Serikali kufanya kazi za Serikali, ili kupunguza adha za ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. ZAHRA ALI HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwanza kuhusu wazee wa Tanzania wamejenga historia kubwa kwa kulifikisha Taifa hapa lilipo, wao ndio wanaoishi maisha magumu kupita kiasi, hivyo nakuomba Mheshimiwa Waziri iboreshe pensheni ya wastaifu katika sekta zote ili kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kulipiwa matibabu, bado kuna haja ya kulipa huduma nyingine muhimu za kijamii kama usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi na kwa kiasi gani tunawahamasisha vijana na kuwasaidia ili waweze kujitegemea na kuacha kujingiza kwenye makundi yasiyofaa kwa kuwapatia mitaji ambayo itawawezesha kufanya biashara ndogo ndogo badala ya kazi hizo kufanywa na wageni, tukiweza kuwasaidia ni kweli tutaweza kupanua soko la ajira. Vipi mfuko wa JK umewasaidiae vijana na mpaka sasa ni kiasi gani kimetumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya nami ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kuelekeza mchango wangu katika hoja zifuatazo:-

Kwanza, tofauti ya malipo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Act.2008*), pili, mafao ya Waziri wastaifu wa *East Africa Community* na tatu, hali ya ajira kwenye makampuni yanayopewa kandarasi mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tofauti ya malipo ya Hifadhi ya Jamii limekuwa tatizo sugu sana ambalo linaathiri morari ya utendaji kazi huku mtumishi au mwanachama wa mfuko akifikiria kuona mwisho wa ajira yake atapata kifuta jasho cha aina gani au kiasi gani. Sheria ilitlanguwa lakini mpaka sasa hajulikani kama kanuni hizi zipo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtumishi anayechangia mfuko huu kupitia *NSSF* anachotakiwa kwanza kulipwa mafao yake na pia anapolipwa bado ni kidogo mno ukilinganisha na mifuko mingine mfano *LAPF* na *PSPF*. Hapa tatizo ni nini? Kwa nini mamlaka husika ziliangalie suala hili kwa ukaribu sana? Mfuko huu wa *NSSF* unahudumia watu wanaofanya kazi kwenye taasisi na sekta mbalimbali mfano afya. Huyu mfanyakazi baadaye analitumikia Taifa hili mpaka kufikia hatua ya kustaifu anapata kiinua mgogo au mafao ambayo hayafikii hata milioni tano huyu mstaifu tunamtakia maisha yapi ya uzuri? Hebu mfuko huu urekebishe taratibu zake na kuanza kutoa mafao mazuri kwani mfuko unafanya biashara na unazalisha na hii na kupitia mtaji wa wanachama. Taratibu za mfuko huu ziangaliwe na ikiwezekana hata Mfumo wa Bodi ya Mfuko huu uwe na mwakilishi wa wanachama ndani ya bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa suala la mafao ya wazee halichukui hatma yake. Kila mara tunaambiwa shida ipo Hazina. Kwa nini Wizara isifanye utaratibu wa makusudi na wa

haraka kumaliza tatizo hilo la wastaafu? Watu hawa wamefanya kazi kubwa ndani ya nchi hii na wamefikia umri huo sasa ndio wanaanza kuhangaishwa. Tatizo ni nini? Hatuna kumbukumbu za idara walizokuwa wakifanya kazi? Mbona nchi za wenzetu majirani hata sisikii suala hilo. Ina maana Kenya hawakuwepo wafanyakazi hawa, Uganda hawakuwepo? Kwa nini hawa wetu wasumbuke kiasi hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Kazi na Ajira ifanye jhitihada za makusudi kushughulikia hili na pia watumishi wa Wizara hii watoke na watembelee sehemu mbalimbali ili wabaini matatizo na wayashughulikie ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ajira kwenye kampuni zinazopewa kandarasi hapa nchini ni shida tupu, vijana wetu wengi wanapata mateso makubwa sana. Vijana hawa wanafanya kazi zaidi na hawana mkataba wa kazi. Ajira inafanyika asubuhi na jioni inakuwa ndio mwisho wa ajira. Mfanyakazi huyu anapoumia inakuwa ndiyo sasa basi hapati huduma juu ya tatizo analokuwa amepata na hii hususan kwenye makampuni yanayojenga barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hizi hazijali afya ya wafanyakazi hawa, hata kampuni inapomaliza muda wake hakuna hatua ambazo Serikali inazifanya kufuatilia hali za afya za hawa watu, kazi hizi ni hatarishi sana kwa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali hiyo, napenda kuishauri Wizara kuwa inapitia mikataba hiyo na kuona mapungufu yaliyomo. Hii itasaidia kuwapa vijana wetu ajira yenye manufaa na mafao mazuri ya baadae na kulinda afya zao. Tukirebisha kanuni hizo natumaini ajira za vijana wetu sitakuwa zenye mashiko mazuri.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kushukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Bajeti hii ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuunda Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa *SSRA* utaivezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwa endelevu na itawezesha kuhakikisha kwamba mifuko hiyo inaendeshwa kwa kufuata kanuni na taratibu za kisheria. Itasaidia ajira, kuhakikisha wanachama wa mifuko hiyo amba ni wafanyakazi (kupata) taarifa za mifuko yao na pia kuhakisha mafao yanaboreshwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko yetu ina wigo finyu wa huduma ya Hifadhi ya Jamii nchini Tanzania huduma ya Hifadhi ya Jamii inafikia 3.5% tu ya Watanzania wote. Nguvu kazi ya Tanzania ni takribani watu milioni 20.6 na ni 6% tu ndiyo wanaopata huduma za Hifadhi ya Jamii. Wenzetu wa Kenya ni 15% na Uganda 8%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuongeza wigo wa Hifadhi ya Jamii kama inavyoelkezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Ibara ya 11 (c), mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 (Ibara ya 82(c) inayotamka wazi; "Kuchukua hatua za makusudi za kupanua wigo wa kinga ya Hifadhi ya Jamii ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na huduma za Mifuko ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana hususan kuhusiana na tofauti kubwa ya mafao ambayo imekuwa ikiwapata wafanyakazi mfano wahadiri wa Vyuo Vikuu na Vyama vya Wafanyakazi wamekuwa wakilalamikia tofauti kubwa sana katika utoaji wa mafao ya mkupuo na pensheni ya izeeni. Utakuta wafanyakazi wenye viwango sawa vya mishahara, muda sawa wa utumishi, lakini wanapostaafu, mtumishi mmoja anapata hadi mara tatu zaidi ya mwenzake aliye mwanachama wa mfuko mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya pensheni pia vinatofautina sana. Hivi ni kwa nini kusiwe na *formula* moja inayotumiwa na mifuko yote katika kukokotoa mafao hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko mingine inatoa mafao mengi na mingine inatoa mafao kidogo. Vilevile, mifuko mingine pia imekuwa ikitofautiana muda wa uchangiaji (*Qualifying period*) wengine miaka 10, wengine miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa pia na kuingiliana kwa mafao mfano mwanachama aliye NSSF na NHIF, mifuko hii miwili inatoa mafao ya afya, wakati huo huo mwanachama analazimika kuchangia mifuko yote miwili. Hii ni gharama kwa mwajiri na mwanachama mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo pia la muundo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kisheria. Nchini Tanzania, tunayo mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii ambapo mifuko hii inawajibika katika Wizara tofauti, mfano PSPF, GEPF na PPF wapo chini ya Wizara ya Fedha. NHIF wapo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, NSSF wapo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira na LAPF wapo chini ya Ofisa ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Hali hii ni kinyume na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 ambayo inaitaka mifuko yote iwe chini ya Wizara inayohusika na masuala ya Hifadhi ya Jamii yaani Wizara ya Kazi na Ajira. Hivyo basi, ninaishauri Serikali iiangalie upya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ili iendane na sera zote za Hifadhi ya Jamii zioanishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakapojuisha hotuba yake, atueleze endapo SSRA imekwishafanya tathmini ya matatizo yanayoikabili mifuko yetu kama vile matatizo ya ulinganifu wa mafao ya pensheni na kutathimini afya ya mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii imekuwa ikitabiliwa na gharama kubwa za za uendeshaji wa mifuko na hivyo kupunguza ubora wa mafao na imani ya wanachama kwenye mifuko hii. Wastani wa gharama za kuendesha mifuko hii ni 12%, kiwango hiki ni cha juu sana ukilinganisha na kiwango cha Kimataifa ambacho ni 5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuligusia ni kuhusiana na ukosefu wa Hifadhi ya Jamii kwa wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee katika jamii ni washiriki wenye umuhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi, inakadirisha kwamba 73% ya wazee ambao ni takribani milioni mbili bado wanashiriki katika shughuli za kiuchumi. Kwa mujibu wa tafiti za Shirika la Kazi Duniani na Taasisi ya Help Age, zimebainisha kwamba Hifadhi ya Jamii kwa wazee inawezekana kwa gharama isiyozidi 1.28% ya Pato la Taifa kwa kuwapatia shilingi 16,586 kwa mujibu wa tathmini ya mwaka 2010. Natoa wito kwa Wizara ya Kazi na Ajira kuharakisha uundwaji wa mfumo wa penshen kwa wazee wetu. Mfumo huu ukianzishwa utasaidia kuwapatia wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 na kuendelea, kutawapunguzia umaskini na Taifa kwa kiwango cha 11.9%.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni masuala ya hifadhi ya uzazi (*maternity protection*). Upo Mkataba wa Kimataifa Namba 183 wa mwaka 2000, lakini hadi kufikia hivi sasa mkataba huu bado haujariidhiwa na nchi yetu. Tatizo ni nini? Je, ni lini sasa nchi yetu itaridhia mkataba huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu ya Ajira na Mahusiano Kazini namba sita ya mwaka 2004 inakataza ubaguzi wa aina yoyote ile. Aidha, maeneo ya viwanda vya EPZ, vingi vimekuwa vikiajiri wasichana wadogo na inapotokea mfanyakazi huyu mdogo anapopata mimba, anafukuzwa kazi. Kwa kweli wamekuwa wakinyimwa haki za uzazi na ndiyo maana, ninazidi kuiomba Serikali iridhie mkataba huo ili kuwawezesha wafanyakazi wanawake kupata haki ambazo hazijaainishwa kwenye sheria yetu ya kazi. Ni lazima kuzingatia haki za uzazi ili kuhakikisha pindi anapojifungua anapata haki na marupurupu yote na kwamba akirudi kazini ataiuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunasifika tunazingatia masuala ya kijinsia lakini kwa wafanyakazi wanawake bado wanakosa haki nydingi na wengine wamekuwa wakibaguliwa kwa misingi ya jinsia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni wafanyakazi wa majumbani. Kundi hili la wafanyakazi ni muhimu sana katika jamii yetu lakini ndilo kundi lenye maslahi duni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Tanzania, kwa kuwa mionganoni mwa nchi zilizopitisha Mkataba wa Kimataifa Namba 189 wa kuwatambua wafanyakazi wa majumbani uliopitishwa kwenye Mkutano wa 100 wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wafanyakazi wa majumbani kwa hotuba yake nzuri aliyoitao tarehe 15/06/2011 Geneva, ambapo aliwatambua wafanyakazi wa majumbani kama watumishi halali wanaostahili haki zote za waajiriwa. Kupatikana kwa mkataba huu ni ushindi mkubwa kwa wafanyakazi wa majumbani ambao kabla ya hapo walikuwa wakichukuliwa kama watumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Sheria yetu ya Ajira na Mahusiano Kazini, inawalinda na kuwatetea, bado utekelezaji wake umekuwa ni tatizo. Mkataba huu ukisharidhiwa utatoa fursa kwa wafanyakazi kupata mikataba ya ajira na kulipwa haki stahiki za mfanyakazi kama vile aina ya kazi anazotakiwa kufanya mfanyakazi wa majumbani. Mazingira anayofanyia kazi, usalama wa afya zao kazini, ukomo wa saa za kazi, ili kuwapa fursa ya kupumzika na kuwasiliana na familia zao, fursa ya kujiburudisha na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi hawa wana dhamana kubwa katika familia zetu kama vile kulea watoto, kutunza nyumba, kupokea wageni na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wengi hawalipwi kabisa mishahara, hawana mikataba ya kazi na wengi wamekuwa wakifanya kazi kwa zaidi ya saa 18. Natoa wito kwa waajiri kuwachukulia wafanyakazi hawa kama sehemu ya familia kwa kuthamini utu na haki zao za msingi kama binadamu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ifanye kaguzi majumbani ili kubaini idadi halisi ya wafanyakazi hawa na kama wanatizimiwa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea ajira za wafanyakazi wa kigeni. Kumekuwa na tatizo kubwa la ajira za wafanyakazi wa kigeni ambao wengi wamekuwa wakipewa vibali bila kufuata utaratibu. Wengi wao wamekuwa hawana elimu wala ujuzi na kuna mara kadhaa ambao wengi wao walipoingia nchini walifundishwa kazi na wafanyakazi, lakini baada ya muda wageni hawa wamegeuka kuwa ma-supervisor. Wageni wengi wamekuwa wakifanya kazi ambazo kimsingi zinaweza kufanya na Watanzania (kwa mfano *Marmo Granito Mines (T) Ltd.*) iliyopo Mbeya ina si chini ya wafanyakazi 32 ambao wanafanya kazi za kawaida ambazo Watanzania wana uwezo wa kuzifanya na wapo wengi wapo mafundi mchundo si chini ya 12, walinzi wawili, mafundi chuma watatu, fundi seremala na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kumekuwa na uwiano usio sawa baina ya wafanyakazi wa Kitanzania na wale wa kigeni. Mfano *Barrick* kuna *Welder* Mtanzania analipwa shilingi 800,000/= wakati Mghana analipwa shilingi milioni 11 wakati, migodi mingine imekuwa hailipi kima cha chini kama kinapoainishwa na bodi za kisekta ambapo wanapaswa kulipwa si chini ya shilingi 350,000/= na wamekuwa hawawalipi kwa madai kwamba hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa pia na tatizo la baadhi ya waajiri kuanziahia mifumo mbadala ya mabaraza ya wafanyakazi kinyume na utaratibu. Baadhi ya taasisi hizi ni Mgodi wa Buzwagi na *Kibo Hotel* ambapo imeanzisha Baraza la Wafanyakazi la Buzwagi linalojulikana la (*Buzwagi Workers Forum*) ambapo wanachama wa vyama vyaya wafanyakazi na menejimenti hawaruhusiwi kuwa wajumbe na wamekuwa wakiwalipa wafanyakazi yote hii ni kuwanyamazisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kaguzi sehemu za kazi, eneo hili lina upungufu mkubwa na linakabiliwa na changamoto kubwa. Ni wakati sasa OSHA na Idara ya Ukaguzi wa sehemu za kazi, ukaongezewa fedha kwani Bajeti inayotengwa ni ndogo na idara hizi hazina vitendea kazi vyaya kutosha, rasilimali watu na uelewa wa masuala ya kaguzi za kazi ili kusimamia kwa makini

kaguzi hizo. Wakati mwengine afisa wa kazi amekuwa anapelekwa kufanya kaguzi kwa kutumia usafiri wa mwajiri ambaye ndiye anayeenda kukaguliwa, hivi atafanya haki kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia kwa wanaoumia kazini ni eneo lingine lenye matatizo makubwa, kitengo hiki ni vyema kikaangaliwa. Ni lazima wawe na takwimu za watumishi wanaoumia kazini na fedha zitengwe kwa idara hii ili waweze kulipa fidia kwa nini haki ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nashauri, mishahara ya *house girls* isiachwe kwenye soko huria, Wizara itamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni utaratibu upi unaotumika kuunganisha vijana na ajira? Mfano, *job agencies* katika miwa yote nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pensheni kwa wazee iwe rai kwa wazee wote Watanzania. Mfano, *compulsory education to all children aged seven years*. Vivyo hivyo nashauri pensheni kwa wazee iwe ni kwa wazee wote naomba maoni ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mpango gani kuongeza ajira kwa vijana?

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, pungezi kwa Waziri na Naibu Waziri kwa taarifa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo, kwanza Waziri atoe maelezo juu ya wafanyakazi wa kigeni wanaoingia nchini kinyemela hasa katika viwanda vya samaki Jijini Mwanza, mishahara inayotolewa kwa wafanyakazi wenye ajira inayofanana na kulipwa mishahara tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili sheria ya mifuko ya pensheni ni ya kikandamizaji kwa wafanyakazi na wachangiaji wengine. Uwekwe utaratibu wa wachangiaji wa mifuko hii kuwaruhusu watumie akiba zao kama dhamana katika benki ili waweze kupata mikopo. Haingii akilini kuona mtu ana akiba yake na hawezি kuitumia hadi azeke ndo apewe hizo pesa. Mtu huyu anakuwa amechoka na hana uwezo mzuri wa kutumia akiba yake. Kama haja kubwa ni kuwahakkishia *security* ya maisha baada ya kustaafu, ni vema kabisa wakapewa mitaji mapema ili waanzishe shughuli za kuendeshea maisha yao baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wizara ishughulikie mgogoro wa kazi wa waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha MWATEX kina Shaban Mkamba na wenzie 1,717 ambaa kesi wameshinda mahakamani (*Civil Case No. 59/2002*).

Mheshimiwa Naibu Spika, wameteseka sana na *CHC* haichukui hatua za kuwalipa baada ya utaratibu wa kubinafsisha kampuni hii kukamilika.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole Waziri na Naibu Waziri hasa katika kipindi hiki kigumu ambacho sekta ya uzalishaji inayumba na hivyo kuathiri ajira. Natambua Wizara hii ni mtambuka na kwani inategemea sana ufanisi wa sekta zingine kwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo, kwanza, bado Wizara ina ufanisi mdogo katika kutetea haki za wafanyakazi pengine kutoptana na matatizo ya kimfumo hasa kama nilivyozungumza hapo juu kwamba Wizara hii ni mtambuka. Naomba Wizara iweke mpango wa kisheria utakaosaidia kurahisisha Wizara kuratibu masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napenda kufikisha malalamiko ya wafanyakazi wa Mgodi wa Chumvi Uvinza iliyopo chini ya Kampuni ya *Great Lakes Mining* kwenye mgodi huu wamekataa

kufuata sheria zote za maslahi ya wafanyakazi hata waraka wa Wizara yako kuhusu malipo ya watumishi haufuatwi, nafikisha malalamiko haya, naomba uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mifuko ya hifadhi bado ni changamoto, napendekeza Wizara iongeze ukaribu katika kufuatilia maslahi ya mifuko hii hasa katika uwekezaji kwani matatizo katika mifuko hii ni hasara kwa maslahi ya wafanyakazi. Hapa naomba kuikumbusha Wizara juu ya uwekezaji wa mifuko ya hifadhi katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo zaidi ya shilingi trilioni moja zilitumika lakini mpaka leo hata *MOU* kati ya Serikali na mifuko hii bado hajatengenezwa achilia mbali kulipwa. Naomba kujua mpango wa Serikali kuhusu malipo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa takwimu. Bado kuna tatizo kubwa la kubaini kiwango cha ajira katika Wizara. Mara kadhaa hapa Bungeni Wizara imeshindwa kubainisha kiasi cha ajira hapa Bungeni. Sikubaliani na utaratibu wa Serikali kutambua walioajiriwa na waliojajiri kwa wahusika kujilandikisha. Nashauri utengenezwe mfumo wa uhakika kutambua suala hili kwa sababu hii kama tutashindwa kutambua ukubwa wa tatizo hili ni wazi hatuvezi kuwa kwenye mazingira ya kutatua. Ni bahati mbaya sana kwani hata ofisi yetu ya takwimu bado ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifuatilie suala la wanaohitimu/waliohitimu Vyuo Vikuu hasa *UDOM* kuhusiana na tatizo la wahitimu mwaka huu wamekosa mafunzo kwa vitendo (*field*). Matokeo ya tatizo hili ni kwamba vijana hawa hawataweza kupata ajira kwa kuwa hawana mafunzo kwa vitendo. Kuna malalamiko kwa vijana hawa naomba Wizara ifuatilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la Watanzania kukimbilia ajira za nje. Natambua suala hili ni mtambukwa, lakini ni muhimu kulifanya kazi kwa kuanza kutambua ukubwa wa tatizo na tofauti za maslahi ili Wizara inapoleta Bungeni mpango wake usaidie Wabunge kutambua. Kwa mfano ni muhimu Watanzania tujue kiasi gani cha Watanzania wenye taaluma mbalimbali wanafanya kazi nje ya nchi, pengine hili linagusa pia udhaifu wa taasisi ya takwimu. Nasema hili ni muhimu kwa sababu zaidi ya kutambua pia inaweza kusaidia kujua kama tatizo tulilonalo kwenye taaluma mbalimbali linaweza kuzibwa vipi na kama tungwarejesha watumishi hao waliopo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kupata maelezo ya Serikali kuhusu wafanyakazi wa Mgodi wa Chumvi, Uvinza ambaao tangu ubinafsishwe mwaka 1999 mpaka leo mwaka 2011 bado wafanyakazi hawa hawajalipwa mkono wa kwaheri hali *PSRC* ilitangaza mwaka 1995 kuwa wafanyakazi hawa wangepewa mkono wa kwaheri. Zaidi ya yote hata mapunjo katika mifuko ya hifadhi bado hawajapewa kwa kuzingatia kuwa kabla ya ubinafsishaji palikuwa na tatizo la michango ya watumishi hawa kufikishwa. *CHC* ndio baadae ilibeba dhamana hiyo, lakini hadi leo watumishi hawa zaidi ya 406 hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya Wizara, naomba sana.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake na namna alivyoiwasilisha vizuri. Pia nimeona ina mipango mingi mizuri kama ilivyo kawaida kwa Chama Tawala kuwa na mipango mizuri ya upande mmoja bila kujali utekelezaji na maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuongeza mishahara ya wafanyakazi, wafanyakazi kupata mishahara isiyokidhi maisha yao kwa mwezi mzima, tija haitapatikana na kamwe hatuvezi kujikwamua katika umaskini hata siku moja, tutaendelea kuwa maskini milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anajibu swaliliano papo kwa papo alisema wawekezaji hawapendi kuwaajiri Watanzania walio wengi eti kwa sababu Watanzania wengi ni wavivu na hawajitumi. Inawezekana ikawa kuna ukweli kiasi fulani katika majibu haya.

Mheshimiwa Waziri naomba nielezee kiasi kidogo juu ya maneno haya aliyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo anasema aliambiwa na baadhi ya wawekezaji alipotembelea

maeneo mbalimbali walipowekeza na alipouiza inakuwaje wanaajiri wageni hata kwenye kazi ambazo zingeweza kushikwa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufuatiliaji. Lakini mimi naona Watanzania si ni wavivu na hawapendi kujituma. Hii inasababishwa na kipato yaani mishahara wanayopata ni midogo mno kiasi kwamba wakitulia katika maeneo ya kazi watashindwa kuishi, kwa kuwa mshahara wanaolipwa hata kuishi kwa wiki moja tu hautoshi. Inabidi watafute mbinu za kuishi wanahangaika kufanya biashara za hapa na pale ili wajiongezee kipato, kibaya zaidi wanapofanya kazi zinazofanana na wageni, wageni wakapewa mishahara mikubwa wao wakabaki na kima cha chini ambacho kimependekezwa na viongozi wa Serikali yetu ama yao. Kwa kweli inatia uchungu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hawaoni umuhimu hata wa kuajiriwa matokeo yake wengine wengi wamekuwa wakijishikiza tu kazini lakini kipaumbele kwa wanaweka kwenye ajira zao binafsi ambazo zinawawezesha kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho hapa ni kuongeza mishahara, naomba uishauri Serikali ikubaliane na Kambi ya Upinzani kima cha chini kianzie shilingi 315,000/= ili tuongeze morari wa kufanya kazi, wafanyakazi wakipata mshahara ambao wenyewe wamependekeza baada ya kuiangalia hali halisi ya maisha tena kwa kujinyima sana. Tukitaka tija ya kazi lazima tuangalie ujira pia, tuwape heshima wafanyakazi kwa kujali maisha yao wapate mishahara itakayokidhi matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutasema mengi sana lakini kama hatutaweka utaratibu mzuri wa kufanya wafanyakazi wafurahie kazi na wawe na hamu ya kufanya kazi ni kazi bure. Zamani enzi za Baba wa Taifa watu walikuwa wanafanya kazi kwa bidii. Viwanda villileta ufanisi mkubwa kwa kuwa wafanyakazi walipata mishahara iliyowatosha na kuwawezesha kuishi kwa kutegemea ajira kuanzia tarehe moja hadi tarehe 30. Dawa ni kuongeza mishahara, tuanzie hapo tutafanikiwa, tija itaongezeka, rushwa itapungua na umaskini utapungua. Tuongeze mishahara, mambo mengine baadae, kama kweli tunakerwa na umaskini, rushwa na kutowajibika. Naomba kuwasilisha.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo, kuhusu ajira, watu wengi wanalamika hakuna ajira lakini na waliopo kazini hawafanyi kazi ipasavyo. Watu wengi walioajiriwa na Serikali hawafanyi kazi na kwa mantiki hiyo nchi hii haiwezi kuendelea kamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *private sector*, Serikali kwa nini hajifunzi kutoka *private sector*, wao wanafanikiwa kwa nini? Ni kwa sababu kila mwajiriwa amepewa malengo ya kufikia kwa kipindi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni vema Serikali itambue kuwa mwanadamu ni wa kusukumwa, maisha yake yote. Hivi sasa hakuna hata mkakati wa kufanya watu wawepo kazini kama ipasavyo hivyo basi lazima kuwepo utaratibu wa mtu kulipwa kadri afanyavyo kazi, viwepo vitambulisho vyta *punch in punch out*, hii itasababisha watu kukaa kazini na kila mtu apewe malengo ya kufikia kwa kila kipindi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wawekezaji hawachukui watu wa Tanzania au wafanyakazi wa Kitanzania kwa sababu ya kutokuwa na moyo wa kuwajibika bila kubadilika Watanzania, Mashirika binafsi huwezi kuwalazimisha wachukue watu wazembe. Wao wapo kutengeneza faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri wa Wizara hii, Naibu wake na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta binafsi hapa nchini zinaajiri Watanzania wengi sana kutokana na Serikali kutoweza kuajiri vijana wengi wanaomaliza elimu zao kutoka vyuo mbalimbali

kwa baadhi ya sekta binafsi kwa mfano viwanda, makampuni, mashirika na kadhalika. Wamiliki wake wamekuwa hawafuati sheria na taratibu za maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna unyanyasaji mkubwa, uonevu unaofanywa na wamiliki hawa wa sekta binafsi, mishahara inayotangazwa na Serikali kima cha chini hakifuatwi na sekta binafsi. Mfanyakazi akiumia akiwa kazini mwajiri wake hamjali wala kumthamini. Ikiwa atalazwa hospitalini kwa muda mrefu na hivyo kushindwa kurejea kazini ndani ya siku 60 hadi 90 basi atafukuzwa kazi akiwa hospitalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wakidai haki zao za msingi watatishwa na kama wataendelea kudai basi watafukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanaowanyanya waajiriwa wanawake kijinsia. Hili ni tatizo kubwa na pale anapokwenda kuomba kazi wanalamizishwa kuwa na mahusiano na mabosi kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uhaba wa ajira ndani ya nchi yetu wafanyakazi hawa wanalamizika kuendelea kuteseka ili waweze kuishi. Serikali inafanya utafiti gani kuona hali inayoendelea kwenye sekta binafsi na ni mipango gani iliyopo kulinda wafanyakazi wa sekta binafsi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa wageni, imekuwa ni utamaduni wa viongozi wa Serikali kuwaona wageni tena wenye ngozi nyeupe kuwa wao wanao uwezo mkubwa na ujuzi wa kufanya kazi zaidi kuliko Watanzania. Hili ni tatizo na tabia hii inasababisha Watanzania wengi kukosa fursa za kufanya kazi zilizo ndani ya uwezo wao na wanao ujuzi nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kulinda watu wake na vijana wake kwenye soko la ajira. Mahoteli yetu ya kitalii *management* zao zote zinaendeshwa na wageni kwa nini? Tunavyo vyuo vyetu vya utalii na *management* wahitimu wetu waende kufanya kazi wapi wakati ajira nzuri tunawapa wageni?

Mheshimiwa Naibu Spika, wageni wanalipwa mishahara minono mikubwa na marupurupu mazuri kwa ujuzi ule ule ambao vijana wetu wanao lakini wako mitaani. Ni vigezo gani vinatumia na waajiri kulipa mshahara shilingi 800,000/= kwa Meneja wa Tanzania wakati huo wanamlipa mgeni shilingi 11,000,000/= huo sio ukandamizaji wa wazalendo? Je, Serikali ina taarifa ya mambo haya yanapofanyika maeneo ya migodi ya madini? Je, ni hatua gani zinachukuliwa kwa waajiri wa aina hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwapo kasumba ya watendaji wa Serikali wakipewa dhamana kuwa na mahusiano na kuwalinda waajiri binafsi. Pale wafanyakazi wanapotaka mishahara iongezwe au watendewe haki wanayostahili kazini watendaji wa Serikali wanaungana na waajiri kukandamiza wafanyakazi hawa na badala ya kuwatetea wanawataka wakubaliane na atayotaka mwekezaji/mwajiri wao ili wasifukuzwe kazi. Hayo yanafanyika maeneo mbalimbali, haswa viwanda vya Dar es Salaam na viwanda vya samaki vilivyopo Mwanza. Huku ni kutowatendea Watanzania haki.

Msheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wengi wa viwanda vya samaki Mwanza wanatumikishwa kama vibarua kwa zaidi ya miaka saba. Je, Serikali inalijua hilo? Na kama linafahamika kwa nini tatizo limeendelea kuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi hawa wanatumikishwa mpaka saa 4.00 usiku. Hawapewi usafiri wala chakula cha mchana, wanapewa/wanalipwa shilingi 3,500/= kwa siku (wanalipwa kwa wiki). Mtu huyu ana familia, anasomesha, anapanga nyumba anasafiri, je, kwa hii pesa anaishije?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha watu wake/vijana wake wote wana ajira/wameajiriwa wenyewe ni kwa shughuli mbalimbali. Hili litawaidia kuondoa umaskini wa kipato uliokithiri mionganoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atueleze katika kutekeleza hilo ni mikakati gani iliyopo kwa kila sekta, kuhakikisha ajira zinakuwepo za uhakika?

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, kwani Wizara hii ni muhimu sana kwa Watanzania walio wengi. Nikianza na kazi, kuna vijana wetu wengi ambao wanafanya kazi kwenye viwanda binafsi na hata kwenye wawekezaji, lakini cha ajabu ni wafanyakazi hao wanafanya kazi kwa muda mrefu bila kuajiriwa. Wengine yafika miaka kumi hajaajiriwa na kuwa kibarua tu. Hii sio haki kwani wawekezaji hawa ni wazi inawanyonya sana vijana na wafanyakazi hao wa Kitanzania. Kibaya zaidi vifaa wanavyotumia ni duni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya samaki vilivyo Kanda ya Ziwa, wafanyakazi ambao hufanya kazi bila vifaa vya kujikinga. Mtu anafanya kazi kwenye chumba cha barafu, lakini hana kifaa cha kujikinga na baridi na baada ya hapo hapewi pesa ya maziwa, mayai, wala nyanya. Huku ni kuwauwa vijana wetu wakiwa hai. Ushauri wangu, kwanza kabisa ni kukomesha wafanyakazi kuwa kibarua zaidi ya miezi sita. Kama tatizo ni sheria ndio inakinza, basi iletwe na tufanyielekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni lazima kufuatilia zana za utendaji kazi ziwe bora na zinazomudu kazi inayofanyika na kwa kuwa OSHA wapo, ni lazima wafanye kazi kama OSHA kwani OSHA nao hawawaoni wafanyakazi hao wanavyotaabika. Angalia hata wale wazoa taka katika Jiji la Dar es Salaam hufanyishwa kazi bila vitendea kazi, hili nalo linahitaji tochi au OSHA hawalioni hili au tunahitaji mwelekezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ambazo wanapewa vijana wetu wengi ni mbovu kulingana na utaratibu kama nilioutoa hapo juu. Isije ikafikia mahala tukawa na vijana wagonjwa wengi na Taifa kuwa na wagonjwa watupu. Tunaiomba sasa Wizara hii kuangalia hili halihitaji tochi wala mtaalamu mwelekezi (mshauri).

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima sasa Wizara hii iweze kusaidia vijana kupata ajira, kwani ajira nyingi hapa nchini hasa za wawekezaji hufanywa na wageni. Naiomba Serikali wakati umefika wa kufanya sensa katika viwanda binafsi ambazo ndizo zenye ajira nyingi na kuwatambua Watanzania na wanapata nini yaani mshahara na sio posho. Pia Wizara hii ijitahidi kuwawezesha vijana katika vikundi na kuwapatia vifaa na sio pesa. Mfano wavuvi, wapewe nyavu na boti za kisasa, hata kama ni boti tatu kila ziwa na ziwe za mfano. Wakirejesha wakopeshwe wengine, huu utakua mpango wa kujajiri. Ahsante.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa mipango mizuri juu ya ajira kwa vijana wetu, ongezeni mipango zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itadhiliti ajira za watu wanaotoka nje ya nchi yetu wakati watu wetu wana ujuzi na utaalalm mzuri, tu kwa hiyo, naiomba Serikali juu ya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia maoni yangu katika Bajeti hii ya Wizara ya Kazi na Ajira 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tatizo kubwa la baadhi ya waajiri kubadilisha mikataba ya wafanyakazi kutoka mkataba wa muda mrefu au msimu na kuwa mkataba wa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika Wilaya ya Rufiji, Kijiji cha Ikwiriri kuna kampuni ya Wachina ambayo inajishughulisha na utafutaji wa mafuta na gesi ilipoanza kazi iliwaajiri wafanyakazi kwa mkataba wa muda mrefu na walikuwa wanapata haki zao kwa kuwekewa akiba katika Mfuko wa Akiba ya Jamii NSSF na wanapata nyongeza ya malipo kwa muda wa ziada na matibabu lakini tangu mwaka 2009 hadi sasa mwaka 2011 wafanyakazi hawa

wanachukuliwa kama wafanyakazi wa muda hivyo hawawekewi mafao yao *NSSF*, wanafanya kazi hadi Jumamosi na Jumapili na hawapati malipo ya ziada na wanatumikishwa hadi usiku kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Wizara iharakishe kufanya utafiti na kukamilisha kwa wakati malalamiko yote wanayoletewa kutoka kwenye makampuni yenye wafanyakazi wa Kitzanzania ili waweze kuwasaidia kwa wakati na si kwenda kuchukua rushwa kwa waajiri kama inavyolalamikiwa sasa badala ya kwenda kuwasaiia Watanzania wazawa na wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, takwimu zinaonesha idadi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini ikiwemo *NSSF*, *PPF*, *PSPF*, *LGPF* na mingineyo, lakini swalii la kujuliza, je, wanachama wa mifuko hii ya hifadhi wamenufaika vipi? Kwa kuwa tunaoneshwa jinsi Serikali inavyokopa bila ya kulipa kwa wakati katika mfuko wa *NSSF*, sasa je, wanachama wangapi ambaa wamenufaika moja kwa moja na kuwa uwazi katika mfuko huu wa *NSSF*, na mingineyo kama *PPF* na *PSPF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na mapendekezo yangu ni kuwa mgawanyo wa faida inayotokana na mifuko hii igawanywe kwa wanachama. Kwa mfano mifuko iwjibike kugawa robo tatu ya faida yote inayotokana na vitega uchumi viliviyotokana na kuwekeza fedha za wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa wanachama yakamlike kwa muda mfupi, mfano miezi mitatu ili mwanachama aweze kuijendesha katika maisha yake kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaunga mkono 100/100.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Wizara ya Kazi na Ajira kwa kazi nzuri inayofanya na *NSSF* hongera kubwa, kazi zinaonekana na wananchi wanaridhika. Je, Mashirika mengine mbona kimya au wanaendelea na mkakati wa semina, tathmini, uhamasishaji, uhakiki, upembuzi, mchakato na kongamano. Tunataka kitu kinachoonekana sio mambo hayo hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii, kuna mradi ulikuja unaitwa *youth mapping* ni mradi wa utambuzi wa vijana wa vikundi vya uzalishaji mali! Je, mradi huo umeshafika katika Mkoa wa Lindi ndani ya Wilaya zake Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Kilwa na Lindi? Naomba majibu. Sasa ni wakati muafaka wa kutambua shughuli za vikundi vya vijana (Uk.42 – (vi)).

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wapewe *pension* tafadhali (uk.42 (vi)). Tunaomba sasa nyumba za *NSSF* zijengwe mikoa maskini kama Mkoa wa Lindi na wilaya zake. Wakati Serikali inapopandisha mishahara Serikalini, waangaliwe pia wafanyakazi wa sekta binafsi, viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, misaada ya *ILO* haioneshi tija badala ya kuwawezesha vijana, wao wanalazimisha (semina, utafiti, michakato, uhamasishaji, kongamano na kadhalika.) Masuala hayo yamepitwa na wakati, wabadili msimamo, vinginevyo hatutaki hatutaki.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na watendaji wao kwa hotuba nzuri ya Wizara hii. Mimi sina zaidi ya kusema naunga mkono hoja hii kwa 100%, kinachonifanya niunge mkono hasa ni Shirika la *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika hili linaendelea kufanya vizuri kadri siku zinavyokwenda binafsi linanifurahisha, lakini niseme sifa hizi zisiwafanye wabweteke.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwa *PPF* na *NSSF*, ninachowashauri mimi wajaribu kushuka kwa wafanyakazi waliopo vijijini waweze kuwajengea nyumba kulingana na

mishahara yao ili waweze kuwakata kidogo kidogo kila mwezi, hili litawasaidia watumishi hawa kuwa na makazi mazuri wakiwa kazini na wanapokuwa wamestaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu watumishi wengi wamekuwa wakistaafu na kukosa hata pahala pa kuishi na kuweza kula *pension* zao vizuri. Nayashauri mashirika haya yaje Mkoa wa Shinyanga na kwa kuanzia waanzie Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi na naunga mkono hoja hii bila kigugumizi. Ahsante.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa masikitiko kabisa kuchangia katika Wizara hii ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika jambo la unyanyasaji wa wafanyakazi katika sekta binafsi na hasa zile za kigeni yaani *Foreign Investment* ambazo huwa owned na *Foreign Investors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji huu upo sehemu nyingi lakini nita-base sana katika Gazeti la *The African* ambalo lilitoka tarehe 1.08.2011 likionyesha ni jinsi gani kampuni ya *Barrick African Gold* inavyoweka matabaka na kuwanyanya wa fanyakazi wazawa kwa kuwafanyisha kazi muda mrefu na katika mazingira hatarishi na kwa malipo madogo sana bila kuwa hata na promotion. Napenda kujua tangu kutoka kwa taarifa hii na hata kabla, Serikali imechukua hatua gani katika kukomesha udhalimu huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje mgeni analipwa au analetwa nchini na kulipwa kwa kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya na ndio wanaofanya na credit kwenda kwa hao expatriate?

Mheshimiwa Naibu Spika, mzawa huyu analipwa dola 800 na kibaya zaidi kubadilishwa kwa exchange rate ya dola kwa shilingi 1000/= wakati kwa sasa exchange rate ni shilingi 1600/= kwa one dollar, swali hapa ni kwa nini hii exchange rate iwe fixed wakati inflation na factor zingine lazima ziwe factored in? Ajabu wageni (ma-expatriate) wanalipwa kwa dola tena kama minimum wages ya dola 7,000 kwa welders ambayo ni sawa na shilingi 11,200,000/= this is an absurd sababu tuna Watanzania wenye ujuzi wa welding, jamani hivi huyu anayetoa working permit huwa anasoma CV za hawa watu kweli au ndio rushwa inapindisha sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu wazawa wanafanyakazi na hasa experts hawafanyi hizi kazi lakini wanalipwa hadi shilingi 20,000,000/. Mbaya zaidi hawa wageni hawafanyi hizi kazi kama nilivyosema wazawa ndio hufanya hizi kazi lakini kuna extra allowance ambayo wafanyakazi wa Kitanzania hawapewi allowance bali ni wageni (experts) ndio hupewa dola 800 kwa wiki kwa ajili ya maziwa na mahitaji mengine na ku-exhale/neutralize toxic kutokana na materials wanazotumia wakati wa mining. Lakini Watanzania ambao wanaenda underground katika shughuli za mining wana-inhale toxic nyingi hawapewi allowance yoyote ile, licha ya kazi zao za uhatarishi (risky work) na zinazochosha sana. Hivi kweli Wizara haijui shughuli za mgodini ni very risky kwa afya za binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najuliza hivi sisi Watanzania tumelogwa na nani? Hivi hii mentality ya kuthamini wageni na kuachia rasilimali zetu (madini) na rasilimali watu kunufaisha Mataifa ya nje huku sisi tukipata mapango na labda Serikali inajivunia upatikanaji wa ajira kutokana na hiyo investment ya Barrick, labda na kamrahaba kadogo tunakopata kama Serikali, sasa kumbe hatupati income yoyote ile na Serikali inaruhusu expert kuja Tanzania wakati tuna geologist wengi tu, Mine Engineers wengi, welders etc. Maana huu uwekezaji kwangu mimi kama umekuwa ni vilio maana Barrick hii ambayo inamiliki Tulawaka, Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu uwekezaji umepelekea mauaji ya Watanzania aidha kwa kupigwa risasi kuwa wameenda kuokota mawe au wanawaita invader's, wanaathirika na hata kufa kutokana na uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na large scale mining operations

zinazofanywa na kampuni hizi, vilevile wakazi wa maeneo husika wamekuwa maskini maradufu kwani wengi hawajalipwa fidia na walilipwa fidia ni fidia mbuzi yaani *just permit* ambazo haziwezeshi *settlement* yoyote, ajira zimepotea kwa wale waliokuwa wakifanya uchimbaji mdogo mdogo. Sasa badala ya kupata neema wameishia kuona madini yetu yakibebwa, wao wanabaki kapuku na kupukutika kama utitiri kwa *toxication* na risasi. Mazao hayaoti wala shughuli za ufugaji hazipo tena sasa hata ajira ya kilimo haifai tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata majibu kwa haya. Naomba kuwasilisha.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza kwa hotuba nzuri na mikakati yote ya kufanikisha maendeleo ya nchi na uchumi. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Mashirika na Asasi zilizopo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ni kwa nini wafanyakazi wanaofanya kazi ngumu kama za ufagizi, kuzibua *ma-septic tanks* ya maji machafu hawalipwi kiwango kikubwa cha mshahara? Nimeona katika nchi kama Uingereza, kazi kama hizo zina malipo makubwa. Naomba jibu.

Pia *ILO Conventions* kuhusu mkataba wa usalama na afya kazini je, mkataba huo unafanya kazi yake? Kwani sioni kama wanaofanya kazi za usafi barabarani na kwininge kuwa na mazingira safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa msongamano wa watu mjini huletwala na watu wengi kukimbia vijijini kwa kutafuta ajira, je, Wizara inajipanga vipi kwa kushirikiana na Wizara zingine ili kuondoa tatizo la msongamano mijini kwa kuongeza ajira vijijini na mikoa mingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara inatambua kuwa kuna unyanyasaji wa kijinsia makazini kwa kuwa tu mwanamke amemkataa mkubwa wake kimpenzi na hivyo kupata adhabu ama ya kufukuzwa kazi au kutopandishwa cheo au kuhamishwa au kutopatiwa fursa ya kuijendeleza na kadhalika? Wizara ina mkakati gani kukomesha hali hiyo? Na kwa kuwa mambo hayo ni siri mtu anakosa pa kutolea taarifa mara apatapo adha hiyo kuna mkakati gani ya kuwanasa mabosi wa namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza watendaji wote kwa jitihada wanazozifanya hapo Wizarani. Naomba kupata majibu kwamba ni kwa nini wageni wanalipwa pesa nyngi zaidi *in terms of* mishahara na *benefits* nyngine, kuliko wazawa? Mfano mzuri ni wafanyakazi kwenye sekta za uchimbaji wa madini ambako Serikali imeruhusus idadi isiyo na ukomo la *expatriates!* Na *expatriates* hao wanalipwa zaidi ya mara kumi ya mfanyakazi wa ndani mwenye sifa zile zile au za kufanana?

Mheshimiwa Naibu spika, mfano *Barrick Gold* inamlipa *expatriate* wa kutoka Ghana shilingi milioni 11 kwa mwezi wakati *counterpart* wake wa Kitanzania analipwa shilingi 800,000/= tu! Pamoja na uozo mwengine kwenye sekta hii, basi jamani walau tufaidike na ajira kwenye miradi hii! Barrick hiyo hiyo inawalipa wageni *in USDs*, wakati Watanzania inawalipa katika viwango vya *USD* moja sawa na shilingi 1000/= kwa nini? Ni kwa nini Serikali isibane mirija kwa makampuni haya kuleta *expatriates* ili na sisi tufaidike?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madaktari wamehamishwa na Serikali kwenda sehemu nyngine bila mazungumzo nao, kwa nini? Tutaendelea kuwakandamiza wataalamu wetu mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, waraka wa kuwaongeza viwango vya pensheni wastaafu wa Serikali ulipitishwa na Rais kusaini Sheria hiyo, kwa nini malipo rasmi hayafanyiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Nzega hawapati ajira mgodini, Lusu, Serikali inaliangalia vipi hili suala?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Dada yetu Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga kwa kuwasilisha Bajeti yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa Shirika la NSSF Bwana Ramadhan Dau kwa kazi kubwa inayofanyika. Mifuko ipo mingi kwa nini kila ikitajwa mifuko ya kukopesha Serikali utajwe huu? Ni kwa sababu inafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mkurugenzi huyo kwa kutuwezesha katika kilimo cha uyoga. Baada ya kushauriana na wadau tuliona bora tuanze ujenzi wa maabara badala ya darasa kwa vile tulipata sehemu ya kusomea jirani na mjini. Jengo hilo la maabara limekamilika, sasa kuna mambo madogo ya kumalizia na sasa tunawasiliana na COSTECH ili watununulie na kutufungia *machine* za kutengeneza mbegu za uyoga. Jengo lipo Mkuse, Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira, ni kweli maelezo yaliyotolewa na Wabunge wanaowakilisha wafanyakazi Mheshimiwa Angella Kairuki na Mheshimiwa Zainabu Kawawa maana tulikutana na viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na wakatufahamisha hayo. Nami nayaunga mkono na nashauri yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unyanyasaji wa watu kuwa *middle people* na kuchukua pesa kwa niaba ya wenzao ipo hata kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa nini Serikali isiwalipe moja kwa moja madereva wa Wabunge na badala yake kusaidia kutoa ajira zenye utata? Mimi naona sio haki hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwa na sehemu mbalimbali za kupitisha ajira za wageni nazo zinachangia kutoa mwanya wa wageni kutumika hata kwenye kazi za kawaida. Mfano kwa *T/C*, Utumishi, Kazi na Ajira kwa nini isiratibiwe sehemu moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, walemau hawasaidiwi katika kijiwezesha hasa katika kupata vitendeua vya kazi na masomo. Nimeshuhudia walemau wakipigwa mnada vifaa vyao na *TRA*, hii si haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya ajira ya watoto na mazingira hatarishi. Naipongeza Serikali kwa mpango wa kutokomeza ajira za watoto na mazingira hatarishi, naamini kazi hii nzuri italeta *data sahihi* za ajira za watoto na utumikishwaji watoto katika mazingira hatarishi. Ipo haja kwa Serikali kupitia Wizara hii kwa kushirikiana na wadau na taasisi mbalimbali, kuziangalia sheria mbalimbali zinazomgusa mtoto na changamoto zinazomkibili kwa sasa na baadee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kuna sheria ngapi ambazo zinatoa tafsiri ya umri wa mtoto. Mila na desturi zinashiriki vipi katika kuchangia uendelezaji wa ajira za watoto. Haki za watoto zinapokosekana kwa sababu mbalimbali kama familia duni, mayatima, ulemavu na kadhalika, ni Wizara gani itawajibika kuwasaidia watoto kupata haki zao, zikiwemo za kupata elimu, afya, kuishi, kusikilizwa na kushirikishwa, kuendelezwa, kulindwa dhidi ya unyanyasaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumeshuhudia watoto ndio watumishi katika majumba ya kuishi, je, ni chombo gani kinachowasaidia kwa kuwatambua walipo, kazi wanazofanyishwa na ujira wanaolipwa, kwa nini watumishi wa majumbani wasitumiwe watu wazima?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira zisizo katika mfumo rasmi, kwa kuwa kundi hili ni kubwa na hadi sasa hakuna utaratibu wa hifadhi ya jamii uliobuniwa kwa ajili yao. Je, hatuoni ni

muda muafaka kwa kundi hili kuanzishiwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kulingana na mazingira ya ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi za dhati sana kwa Wizara nzima, kwa juhudzi za kuongeza ajira nchini. Aidha, napenda kutoa ushauri juu ya pensheni kwa wazee wetu wa Tanzania (Bara), naisihi sana Serikali itathmini na kukubali wazo la kuwapa *pension* wazee (*60 year and above*) wote wa Tanzania Bara kwa kuheshimu michango waliyooita kwa nchi yetu wakati wa ujana wao. Faida zitokanazo na uamuzi wa kuwapa *pension* wazee wetu ni hizi zifuatazo:-

1. Wazee wengi ndiyo wanaolea watoto yatima na wengi wao ni wale waliotokana na wazazi wao kuaga dunia kwa tatizo la UKIMWI. Vema Serikali nayo ikatoa mchango wa kuwaunga mkono wazee hawa.

2. Maadili mema yanaanza kwa wazee wetu. Maadili hayo yatapata nguvu ya kusikilizwa na kuzingatiwa na watoto wanaolelewa na wazee hao pale wanapokuwa na nguvu za kiuchumi.

3. Kuwapa *pension* wazee kutawawezesha kuitumia pesa hiyo kununua mbolea kwa ajili ya kilimo chao cha kujikimtu.

4. Kuwapa *pension* wazee kutaongeza mzunguko wa fedha nchini kwani wazee hawana starehe zilizotopea. Wengi wao watazitumia pesa hizo kununua mahitaji ya msingi tu kwenye maduka yaliyo jirani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira ya vijana na watu wazima pia mafunzo ya ujasiriamali, naunga mkono hoja. Ajira hasa kujiajiri ni muhimu sana na hasa kwa vijana wetu wenye umri wa kujiajiri wakipewa stadi za maisha. Kwa kutumia rasilimali zilizopo Jimboni, Wizara itusaidie ili stadi zkipatikana vijana wajiajiri. Mkoani Tabora fursa hizo zipo naomba *ILO* na taasisi nydingine zitusaidie.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa Tanzania kwa ujumla inashuhudia wimbi kubwa la ajira za wageni wakiwemo hasa Wahindi, Wachina, Wasomali na Kadhalika. Mbaya zaidi mshikadau mkubwa ni Kampuni za *Mohamed Enterprises (METL)*, ambayo ina asilimia 80% ya Wahindi wakifanya kazi katika viwanda na makampuni yake na Serikali kuwa kimya kana kwamba ni halali. Je, ni hatua zipo Serikali inachukua kwa ukiukwaji wa sheria na taratibu. Hivyo sitaunga mkono hoja mpaka nipate jibu la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa hoja hii yenye kero na kukandamiza ajira za Watanzania na kupuuza agizo la Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuwa halina maana, napenda kuwasilisha.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Kazi. Hata hivyo, kuna haja kubwa ya kuangalia namna bora zaidi ya kuhakikisha kuwa haki za wafanyakazi zinalindwa. Udhibiti ufanyike kuhakikisha wageni hawapewi vibali hovyohovyo na Watanzania waelimishwe umuhimu wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu *VETA*, napendekeza kuwa Taasisi ya *VETA* irejeshwe Wizara ya Kazi na Ajira. *VETA* ina mahusiano ya moja kwa moja na kupunguza tatizo la ajira nchini. Taasisi hii huko ilipo haipati mkazo unaotakiwa. *Tracer studies* zinazofanywa na *VETA* zinasaidia sana kujua namna ya kushughulika na tatizo la ajira nchini. Kwa uzuri kabisa, nashauri *VETA* irejeshwe Wizara ya Kazi mara baada ya Bunge hili la Bajeti. Wizara ipeleke ombi hili la Wabunge Vijana kwa Mheshimiwa Rais ili kuiwezesha Wizara kutengeneza ajira vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, *SSRA*, nawapongeza sana kwa kuanza vizuri kazi. Nadhani ni vema *SSRA* isaidie Mifuko ya Pensheni iunganishwe na kubakia mitatu (Umma, binafsi na isiyo rasmi) na yote iwe chini ya Wizara moja. *SSRA* isaidie Mifuko ya Pensheni kuwekeza kwenye miradi inayosaidia kukuza uchumi na hivyo kutengeneza ajira (hivyo tuungeze idadi ya wanachama wa mifuko). Kamati ya Bunge ya *POAC* ilielekeza Mifuko iwekeze kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme. Ni matarajio yangu kuwa *SSRA* itakuwa chachu ya kusaidia suala hili badala ya kuwa kikwazo. Naomba *SSRA* isaidie miradi hii badala ya kuipiga vita. *SSRA* iwe *facilitative*. Uwekezaji kwenye umeme na gesi ndio *future* ya mifuko kwani inazalisha ajira na kuongeza *members*. *SSRA* wawe *open minded*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, *NSSF*, ukurasa wa 24 (iii) umezungumzia kuhusu vitega uchumi Kigoma. Bodi ya *NSSF* ilipitisha mradi wa ujenzi wa Stendi Kijiji Mwendiga kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Mpaka sasa hakuna lolote linalotajwa. Ukurasa 40(vi), umeendelea kutaja Kigoma bila mradi huu. Naomba majibu ya Wizara katika jambo hili vinginevyo nitaipinga Bajeti ya Wizara hii na kuondoa shilingi. Kigoma napo ni Tanzania. Haiwezekani miradi iwe Dar es Salaam, Arusha na Mwanza tu. Hili sitakubali. Naomba *commitment* ya wazi kabisa ya suala hili vinginevyo katika Kamati ya Matumizi nitazuia makadirio ya Wizara.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni umuhimu wa Serikali kuiwezesha kikamilifu Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini. (*Occupational Safety and Health Authority - OSHA*) ili iweze kutekeleza jukumu lake muhimu la kulinda nguvu kazi ya Taifa kwa ajili ya kuchangia ipasavyo maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la msingi la *OSHA* ni kupitia Sheria ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2003 na kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa nchi hii wanapokuwa katika shughuli zao mbalimbali za ujenzi wa Taifa, wanahakikishiwa usalama wa mili yao na maisha yao wawapo kazini na baada ya kuacha kazi lakini inaonesha kwamba lengo hili haliwezi kufikiwa kwani Wizara ya Kazi imeshindwa kuiwezesha Mamlaka hii kufanya kazi zake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wa takribani miaka 10 sasa tangu kuanzhishwa kwa *OSHA* tarehe 31/8/2001, Wizara kupitia bajeti ya Serikali imekuwa ikiipatia *OSHA* fedha za kujidhesha (*OC*) kwa viwango tofauti kati ya Tshs.0, Tshs.60,000,000 na mara moja tu Tshs.120,000,000 ambazo zilitumika kununua gari la Mtendaji Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha shilingi 60,000,000 yaani shilingi 5,000,000 kwa mwezi wanazopatiwa *OSHA* hazitoshii hata kulpia gharama za umeme. Mahitaji ya *OSHA* kwa mujibu wa *Business Plan* yao ya mwaka 2011/2012 ni Sh. 3,646,577,310. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/2011 kufikia Mei, *OSHA* walikuwa wamepewa Shilingi 14,000,000,000 tu kati ya Shilingi 60,000,000 walizotakiwa kupewa. Kwa hali hii *OSHA* haiwezi kufanya kazi zetu kwa ufanisi hata kwa robo ya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya *OSHA* kutokuwezesha ni kutoa vibali au leseni ya kukidhi matakwa ya sheria (*compliance licence*) kila mwaka bila hata kufanya ukaguzi wa eneo husika. Mfano, benki fulani inahitaji cheti/leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Kazini, inapeleka orodha ya matawi yake nchini kwa Mtendaji Mkuu wa *OSHA*, naye anasema "Mungu Mkubwa" wanatoa kibali/vyeti husika kwa matawi yote, bila hata ya kuyatembelea kwani fedha hizo walikuwa wanazihitaji ili kulpia bili ya umeme, maji, simu, mtandao na kadhalika. Sheria inaitaka *OSHA* ifike kukagua sehemu inayoombewa cheti ama cha usajili au cha kukidhi matakwa ya sheria ili kujiridhisha kabla cheti husika hakijatolewa. Watifikaje kwa *OC* ya Shilingi 0? Matokeo yake ni majumba kuperomoka, watu kupata ulemavu au hata vifo na hata fidia hawafidiwi. Mpaka sasa *OSHA* imetoa vibali 5000 tu kati ya zaidi ya 20,000 vya sehemu za kazi zinazotakiwa kupewa vibali. Hivyo sehemu zote hizo zinafanya kazi bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, pamoja na Rais kuridhia Sheria mpya ya Fidia kwa wafanyakazi (*Workers Compensation Act 2008*) iliyopitishwa na Bunge, Wizara ya Kazi bado inasuasua kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wakati Wizara ikijua fika *OSHA* hawana uwezo kufika sehemu za kazi kukagua mazingira ya kazi, ni dhahiri wafanyakazi wengi wanaumia na kupata magonjwa kazini au yanayosababishwa na kazi wanazozifanya. Kama tujuavyo magojwa ya kazi hayatibiki, hivyo fidia ndiyo njia pekee ya kumliwaza huyu mfanyakazi aliyeathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa lingine ni Serikali kupitia Wizara ya Afya haina wataalam wa magonjwa yatokanayo na kazi. Sheria ya zamani ya Fidia ambayo ndiyo inatumika inaonesha kwamba *maximum compensation* ni shilingi laki moja na nane (108,000/=) kwa mtu aliyeumia na shilingi 83,000/= kwa kifo. Je, kiasi hiki ni nini kuweza kulipwa kama fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iunde Idara kamili kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Hifadhi ya Jamii. Kutokana na upungufu ulioainishwa katika Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003, ni dhahiri kwamba tunahitaji Idara kamili kwa ajili ya kusimamia Sera hii kikamilifu. Kwa sasa Sera inasimamiwa kupitia Sehemu (*Section*) ya Idara ya Kazi, mwendo amba si rahisi kuleta ufanisi unaotarajiwa. Hata Mheshimiwa Rais alipokuwa anaunda Serikali iliyopo, aliondoa majukumu ya vijana ili kuipa Wizara muda wa kushughulikia masuala ya kazi, ajira, hifadhi ya jamii na masuala ya wastaafuli, ni vizuri nia nzuri ya Rais ikatafsiriwa kwa vitendo kwa kuainisha Idara kamili ya Hifadhi ya Jamii chini ya Wizara ya Kazi na Ajira. Kuanishwa kwa Idara kamili ya Hifadhi ya Jamii kutasaidia pia kusukuma baadhi ya mambo yanayosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Idara kamili unapaswa kwenda pamoja na Serikali kutoa maamuzi ya kuiweka Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii na Pensheni (*PPF, PSPF, GEPF* na *NSSF*) chini ya Wizara moja, yaani Wizara ya Kazi na Ajira. Inashangaza kuona kuwa Sera ya Hifadhi ya Jamii pamoja na *SSRA* ukiwa chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, lakini Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Pensheni ikisimamiwa na Wizara zaidi ya moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuiweka Mifuko yote chini ya Wizara ya Kazi na Ajira (Wizara moja) kuna haja ya *SSRA* kuhakikisha kwamba ile Mifuko ya lazima kujunga (*Marketing Schemes*) itakuwa miwili na mwingine kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta binafsi. Ni vizuri pia *SSRA* wakajikita kusimamia *Supplementary Schemes* ambazo ni muhimu ziwepo kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na wale watakaopenda kuwa na hifadhi ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka (MB), aliyoiwasilisha Bungeni juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira ni nyenzo muhimu katika kudumisha na kukuza maendeleo ya nchi yetu. Kila Mtanzania akipata mwamko wa kufanya kazi basi kwa muda mfupi, Watanzania tutaweza kuondoka na hali ya umaskini uliokithiri ambao unaitesa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama na afya mahali pa kazi, ni jambo la msingi katika kufanya kazi katika mazingira salama. Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi wanashindwa kufanya kazi yake vizuri, kazi za ukaguzi kwani idadi yao hawazidi hamsini (50) kwa nchi nzima. Ni kwa nini Serikali haiboreshi na kuongeza idadi hiyo ili kazi ifanyike kwa ufanisi.

Pamoja na hayo, hawana vitendea kazi. Kazi inafanyika kikanda, Dodoma, Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza. Mwanza wana gari moja tu, Arusha gari moja, Mbeya gari moja na Dar es Salaam magari matatu. Kwa vitendea kazi hivyo vichache vyta usafiri, ni wazi kwamba Wakala hataweza kufanikisha kazi zake kwa ufanisi unaotakiwa. Ili *OSHA* ifanye kazi yake vizuri ya ukaguzi, basi vitendea kazi viongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki za msingi za kazi na ajira zizingatiwe, hii ni pamoja na sheria kushika mkondo wake kwa kutokomeza ajira mbaya kwa watoto, kazi za shuruti na ubaguzi sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ifuatilie wageni wanaofanya kazi nchini bila vibali vya kufanya kazi, kwa mfano Kiwanda cha Jambo *Plastics*-Dar es Salaam ambapo kuna Waasia 40 wasio na vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha hoja.

MHE. PEREIRA AME SILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii. Nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji mzuri. Pamoja na pongezi hizo, napenda nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kukuza ajira kwa vijana. Naelewa jitihada za Wizara hii katika kukuza ajira. Hata hivyo, ni lazima tukiri kwamba jitihada hizo bado hazitoshii kutokana na mahitaji yaliyopo. Ni budi tuzidishe juhudii zilizopo na tuangalie mbinu mbadala katika kulitekeleza hili. Nashauri elimu ya amali na ufundi ipewe nafasi kubwa. Hapa elimu ya kubadilisha "mind sets" za vijana kuhusu nini ajira na kwa nini wasitegemee ajira maofisini na hata kuajiriwa ni lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tija ya wafanyakazi. Nchi yetu ni moja kati ya nchi ambazo watumishi wake wanazalisha kwa tija ndogo sana na kupelekea sehemu za kazi hasa za Serikali kuwa vijiwe vya mazungumzo. Umaskini tulio nao pamoja na mambo mengine unasababishwa na tija ndogo jambo linalopelekea hata ujira/malipo yaye madogo. Hii haikubaliki. Hatua za ziada ni lazima zichukuliwe. Elimu ya tija na uzalendo inahitajika na wafanyakazi wetu walio kazini na vijana waliopo shulenii budi watayarishwe ili wazalishe zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni pensheni. Hali za maisha za wastaa fu zinakatisha tamaa. Mfano pamoja na huduma zinazotolewa na Mifuko yetu bado hazilingani na mahitaji ya maisha ya wastaa fu. Katika hali ya sasa, bado ni Watanzania wachache mno wanaonufaika na mipango iliyopo ya hifadhi za jamii na kuwaacha Watanzania wengi nje ya huduma hii. Katika hili nashauri kupanua huduma zinazotolewa na Mifuko na kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii ili uwaingize Watanzania wengi zaidi ikiwemo sekta isiyo rasmi, wafanyabiashara binafsi na muhimu kabisa wazee ambaao wengi wanaishi katika maisha chini na kujuta kuzaliwa. Nashauri tarifi zilizotajwa zifanywe haraka ili pensheni za wazee zianze kutolewa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze *NSSF* kwa kazi kubwa inayofanya ya kuleta maendeleo ikiwemo miradi mikubwa. Kazi yao ni nzuri na wanastahili kupon gezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Waziri wa Kazi, Ajira pamoja na Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kupunguza migogoro katika sehemu ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wanawake wengi wanadhalilishwa na baadhi ya waajiri wao wa kazi, lakini kwa kutokujua haki zao basi wanashindwa kuwafungulia mashtaka au kuwaripoti sehemu zinazohusika. Hivyo basi, nashauri Wizara hii ifanye semina au mikutano kwa wanawake ili waelewe haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Wizara hii fanye kaguzi za mara kwa mara katika sehemu za kazi ili ione namna Sheria za Kazi zinavyotekelizwa. Pale inapobainika kuwa kuna baadhi ya waajiri wamekiuka Sheria za Kazi basi wachukuliwe hatua ili kuzuia ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzuia migogoro, chuki na fitna kwenye sehemu za kazi na kuleta mahusiano mazuri baina ya waajiri na waajiriwa, kuna baadhi ya wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye viwanda ambavyo vinatumia kemikali katika shughuli zao. Watanzania hawa wanaathirika sana na kemikali hizi na baadhi yao hupata maradhi ya ngozi, wengine

hukohoa sana na wala waajiri wao hawajali maisha ya wafanyakazi hawa. Naomba Serikali iwashughulikie sana ili watu hawa wapate haki zao kwa waajiri hawa.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Pamoja na pongezi hizi, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, programu ya kukuza ajira nchini. Nimepitia *details* za maeneo muhimu yote manne (i) to (iv), page 13 kuhusu maeneo yaliyoainishwa kuongeza ajira na nimeona bado kunahitajika msukumo zaidi. Kwa mawazo yangu, ili kuwa na uhakika vijana wetu wanapata fursa za kuajiriwa, ni muhimu mambo yafuatavyo yashughulikiwe na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza Vyuo vya Ufundu Stadi (*VETA*). Vijana wengi wakipata *skills* za kutenda kazi watapata fursa za kujitegemea wenyewe kwa kutenda kazi za uzalishaji wa huduma mbalimbali zinazotakiwa na jamii. Vilevile watapata fursa kubwa ya kuajiriwa maeneo mbalimbali kwa kutoa huduma ya kazi walizojifunza. Utaratibu huu umetumika sehemu mbalimbali duniani na umeleta mafanikio makubwa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamasisha taasisi binafsi kuchangia elimu ya ufundi nchini ili teknolojia na ufundi ukue haraka nchini. Kuna haja ya kuhamasisha uwekezaji wa watu binafsi katika kufungua Vyuo vya Ufundu na Serikali kutoa motisha ya punguzo la kodi kwa wawekezaji hawa. Pia kushirkiana na Wizara zingine kubainisha fursa mbalimbali za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa nchi nzima kuwa na Takwimu za Kina (*Detailed Economic Potentials*) za maeneo mbalimbali nchini ambapo shughuli mbalimbali za uzalishaji (*macro, small, micro and medium enterprises*) zinaweza zikaanzishwa kwa kutumia vijana waliofunzwa katika Vyuo vya Ufundu. Serikali kwa kusaidia hili inaweza kufanya yafuatayo:-

1. Kutenga bajeti kwa ajili ya miundombinu ya msingi.
2. Kutafuta masoko ya kuuza vifaa au huduma zitakazozalishwa na makundi hayo.

MHE. NAOMI M. KAIHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii ya Kazi na Ajira. Wizara hii ina umuhimu wa pekee uliojificha kwa sasa lakini ni bomu la hatari sana. Kwa nini? Kwa vile kwanza linaigusa jinsia ya vijana ambayo ni zaidi ya nusu ya idadi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kipindi sasa Serikali iliyo madarakani yaani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kabisa kutengeneza ajira za kuwapatia vijana wanaomaliza Vyuo, Sekondari, Darasa la Saba na kadhalika. Serikali imeshindwa hata kuwapa elimu ambayo ingewawezesha vijana kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwamba Serikali imeshindwa kubadilisha mitaala na kuifanya iendane na hali halisi ya nchi, kutohana na kwamba idadi ya vijana wanaostahili kujitegemea na kujajiri ili waweze kujikumu inaongezeka kwa kasi mno. Serikali hii pia imeshindwa kuzuia au kulinda ajira kwa ajili ya vijana na Watanzania. Si hivyo tu bali pia Serikali hii imeidumaza Sekta ya Kilimo na Sekta ya Viwanda na Blashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kuhusu jinsi ya kusaidia kutatua tatizo hili sugu ni kwanza kurekebisha mitaala kuanzia Shule ya Msingi hadi Vyuo. Marekebisho haya yalenge kugeuza mitaala ya kikoloni iliyokuwa ikikazia (*White-collar jobs*) kazi za kuajiriwa maofisini badala ya kujajiri. Mitaala ilenge kuhamasisha watoto kuipenda sana nchi yao na kuwa tayari kuihindia kwa hali yoyote ile na pia kutambua kuwa kilimo siyo dhambi wala laana kama walivyokuwa wamelelewa kuamini hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ya kulikabili tatizo hili ni kuhimiza vijana kujunga katika vikundi vya kuzalisha mali. Hili litawezekana pale tu ambapo Serikali itakuwa makini jinsi gani ya kuwapatia *settlements* ambazo Serikali zimewawekea miundombinu ya msingi mfano maji,

nyumba ambapo wasaidie kuzijenga wakiwa wamepatiwa vifaa vya msingi kama cement, mabati na kadhalika. Katika *settlement* hizi watakuwa na uwezo wa kulima, kusindika mazao na hata kuvifungasha vizuri vitu vyao (*packaging*). Kuchukua hatua kama hizi zinasaidia sana kuwafanya vijana wamiliki ardhi, kuondoa msongamano wa kutaka kuishi mijini. Watapenda kuishi Vijiji badala ya kukimbilia Mijini na kuishia kuwa Machinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inapaswa kuwalinda vijana wake dhidi ya uporwaji wa ajira zao kutokana na majirani zetu ambao inaelekea wametayarishwa vizuri zaidi kukabiliana na wenzi wao katika mashindano ya soko la ajira la Afrika ya Mashariki. Tusijidanganye wala kulichukulia kirahisi suala hili la ajira kwa vijana wetu inapokuja kushindania ajira. Nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na kadhalika vijana wao wametayarishwa vyema zaidi mfano lugha ya Kiingereza ambayo hutumika katika usaili (*interview*) wenzetu wana uwezo zaidi kuliko vijana wetu. Ziwepo sheria za makusudi za kuwawekea ajira hawa vijana katika nchi zao hadi hapo watakapowezeshwa na mitaala iliyorekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala hili, pia Wizara ya Mambo ya Ndani inahusika sana katika kuona kuwa nchi yetu haivamiwi na wageni wasio halali (*illegal labour migrants*) ambao kwa sasa wamejaa kwenye ajira za *salon*, kiosks, hoteli na kadhalika. Wizara yetu iwe makini katika kukagua mara kwa mara makazi ya watu na kutambua wageni wasio halali na kuwaondoa haraka sana kama vile wafanyakyo wao kwao huko, kufukuza Watanzania bila huruma na upelelezi huu uwe ni wa kudumu na ufanyike mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu nasisitiza kuwa viongozi wote waachane na utamaduni wa kusema na kuandika mambo mazuri, waachane kabisa na uzembe na umangimeza. Watanzania tufanye kazi kwa juhudhi na maarifa na kuwa wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kuwasilisha.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Serikali kuiwezesha kikamilifu Mamlaka ya Usalama na Afya Kazini ili iweze kutekeleza jukumu lake muhimu la kulinda nguvu kazi ya Taifa kwa ajili ya kuchangia ipasavyo maendeleo ya nchi. Ni busara kutumia sehemu ya mapato ya mfuko kuzuia wafanyakazi wasipate madhara kuliko kusubiri wapate madhara eti kwa vile mfuko utawalipa fidia kutokana na madhara waliyopata.

Kutokana na umuhimu wa Mamlaka ya Usalama na Afya kazini (*Occupational Safety and Health Authority – OSHA*), ni vizuri Serikali ikatafakari upya suala zima la kuiwezesha *OSHA* kutekeleza majukumu yake ipasavyo, kwani mchango wa *OSHA* ni muhimu sana katika kufikia malengo ya kujenga na kukuza uchumi wa nchi, waongezewa fedha. *OSHA* iwezeshe na Serikali badala ya kuendeleza na hali hii isiyordhisha katika kulinda usalama na afya ya nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema pia na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF, PPF, PSPF, LAPF, GEPF*) nayo ikaungana na *Workers Compensation* katika kusaidia *OSHA* kuititia utaratibu rasmi kwani nao wana mafao ya ulemavu (*work-related disease and injury and disability benefits*) yanayotolewa kwa wanachama wao kutokana na kuumia na kupata magonjwa yatokanayo na kazi au ulemavu. Ili hii mifuko ifanye kazi au kutekeleza vizuri majukumu yake ni wakati Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii itakapokuwa chini ya Wizara moja, yaani Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafao duni baada ya kustaafu kwa wafanyakazi waliokuwa katika *Social Security Schemes* mbalimbali bado ni changamoto ambayo ni vema Serikali ikaanza kwa dhati kuishughulikia kwa kuwa wastaafu huhangaika na kukosa huduma muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji unaofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii haujamsaidia mfanyakazi/mwanachama wa mfuko mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna makundi ya wafanyakazi waliokuwa katika Mifumo ya *Provident Fund* ambao walichangia sawa na wenzao waliokuja kuwa katika mifumo ya *Pension*

Fund, lakini mifumo ya *pension* ilipoanza wakasahaaulika na sasa wanateseka sana kwani hawapati *pension* ya kila mwezi mfano wale wa Vyuo Vikuu waliokuwa katika mfumo wa SSSS ambaao ni 400 hivi walishastaafu na wameachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya SSRA inaruhusu (Ibara 30) mfanyakazi kuchagua mfuko wa kujiunga kati ya ile ya lazima (*Mandatory Schemes*). *Mandatory Schemes* kwa sasa ni PSPF, PPF, NSSF, LAPF na GEPF. Ingekuwa busara kama wangepewa uhuru wa kuchagua ili kuonyesha kwa vitendo utawala wa sheria. Mifuko hii inalalamikiwa sana na wanachama wake kwa kuwa na mafao duni hasa fao la wategemezi.

Wizara sasa iangalie jinsi ya kupunguza adha wanayoipata watumishi katika maeneo yao ya kazi. Mfano ajira za viwandani, ajira ya Mashirika binafsi, ajira ya wafanyakazi wa majumbani na ajira Serikalini. Ni vema kuangalia usalama wao katika maeneo wanayoishi. Mfano Walimu wanaopelekwa Vijijini ambako hakuna nyumba, shule zingine majengo yake yanatisha, karibu yanaanguka, yote haya yatiliwe maanani.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Pia bila kuwasahau Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi nchini na wafanyakazi wote nawapa pole kwa kazi ngumu wanazozifanya za kuinua uchumi wa Taifa letu. Wasikate tama, waendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi, mimi nitachangia katika hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

1. Ajira kwa ujumla.
2. Wageni wanaoingia Tanzania na kufanya kazi.
3. Mafao ya wafanyakazi.
4. Vyama vya Wafanyakazi.
5. Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ajira. Upatikanaji wa ajira ni tatizo nchini Tanzania pamoja na kuwa na mashirika mengi na Kampuni binafsi nyigi lakini sidhani kama Serikali leo ikiambiwa itoe takwimu kama tutapata takwimu sahihi. Hali ya ajira ni tete na hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Vijana wengi wanatoka katika Mikoa mbalimbali wanakuja Dar es Salaam kufuata ajira. Hali hii inatusababishwa mrundikano wa vijana Jiji. Ajira ziko nydingi sana Dar es Salaam lakini tatizo haziko wazi. Utakuta watu wanafanya kazi hatujui zilitangazwa lini na wapi? Hali hii inasababisha vijana kuwa wanyonge na kugawanyika katika makundi ya wale waliosoma mjini na wa vijijini kujiona wao hawana uwezo wa kukabiliiana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikija kwa wale walioajiriwa bado Serikali inakabiliwa na changamoto ya viwango vya chini vya mishahara na hasa wafanyakazi wa Serikalini. Naomba sasa Serikali yangu sikivu ifanye mpango wa kukutana na Kamati zake za Ajira kuangalia kwa uso wa huruma na upendo viwango vya mishahara ya wafanyakazi wake kwa hiari pasipo migogoro yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mafao ya wafanyakazi. Wafanyakazi wengi baada ya kuacha kazi wanakuwa na maisha magumu sana kutokana na sababu ya kukosa fedha ambayo inatokana na matumizi mabaya ya mafao hayo. Naishauri sasa Serikali pamoja na mashirika yanayotoa mafao watoe mafunzo kwa wateja wake jinsi ya kutumia mafao hayo pindi watakpostaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kulipwa mafao ya pensheni kwa wafanyakazi miezi mitatu ni tatizo kubwa. Wizara iangalie malipo ya pensheni yawe mazuri na yalipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wageni wanaoingia Tanzania kufanya kazi. Raia wa nchi za kigeni wamekuwa wengi sana na hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Wageni kutoka China, Kenya, Congo na hata nchi nyingine za jirani wanaingia kwa wingi kuja kazi nchini

Tanzania. Je, Serikali yetu inatambua hali hiyo? Je, kweli hao wote wanaoingia wana vibali vya kufanya kazi? Kama si hivyo, Serikali yangu ijpangie kuanzia sasa kutafuta njia ya kukabiliana na changamoto hiyo. Mfano Wakandarasi wa barabara wa Kichina wanajaa mfano *Kilwa Road* hata wachimbua mifereji na waongozaji ni Wachina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Vyama vya Wafanyakazi ni kimbilio na roho ya wafanyakazi wote nchini Tanzania. Vyama vya Wafanyakazi visiingie katika siasa badala yake wasimamie wafanyakazi katika maslahi na matatizo yao. Nataka nitoe masikitiko yangu na kuonyesha kuwa ni mhusika lakini sasa Vyama vya Wafanyakazi vimetugawa. Viongozi wa kitaifa na hasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano aheshimiwe kwa kuwa sisi ndiyo tumemchagua, tumeona anatufaa. Kama Chama cha Wafanyakazi kina Rais wake wa Jamhuri mwingine asubiri atakapotawala naye apewe jukumu tuone kama ataweza. Tunaomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri pamoja na changamoto zilizopo tumpe nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie katika Mifuko ya Mafao. Napenda nipongeze Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa kazi kubwa ambazo imekuwa ikizifanya. Shirika hili kwa kweli ni mfano wa kuigwa, kwa jinsi linavyowajibika kwa kutoa huduma mbalimbali. Tumeona kazi nydingi sana zinazofanywa na *NSSF* ikiwemo zile za Chuo kikuu Dodoma na nyumba za Mtoni Kijichi na majengo mengi sana Jijini Dar es Salaam. Nikiwa kama Mbunge wa Mkoa wa Dar es Salaam nitakuwa mkosefu wa fadhila nisiposhukuru *NSSF*. Nasema hongereni sana *NSSF* na ahsanteni sana kwa kutuwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nishauri Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. *NSSF* inatoa fedha nydingi katika miradi hivyo Serikali ijitahidi kurudisha mikopo yote wanayotupa ili tuweze kujengewa miradi mingine na Shirika liweze kuendelea. Serikali isiporudisha mikopo hiyo, Shirika tutaliangusha, tujitahidi, isijeonekana kwamba wao hawako makini kumbe mikopo hairejeshwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%. Ahsante sana.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inafanya kazi nzuri na napongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwanza kuhusu *NSSF*. Shirika linao wanachama wao pale Mbinga na kwa sasa mradi wa Makaa ya Mawe ikiwa ni pamoja Mitambo ya Kufua Umeme kujengwa kule Ntunduwao – Ruanda, Shirika lijpange kujenga ofisi zao pale Mbinga na pengine ofisi ndogo katika Makao Makuu ya Tarafa – Ruanda. *NSSF* itakuwa na wanachama zaidi na hivyo inatakiwa iwe karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wizara ifikirie kumpeleka Ofisa Kazi (*Labour Officer*) pale Mbinga kufuatia maendeleo niliyotaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa vile wafanyakazi wana matatizo ya makazi, napendekeza na kuwaomba *NSSF* kujenga angalau jengo la ghorofa tatu pale Mbinga na kupangisha wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ajira za kufundisha na Mahotelini zinachukuliwa na wageni. Naiomba Wizara itafakari na kupata mkakati wa kujua kwa nini Watanzania hawapati kazi hizo na tuenze kuwaandaa Watanzania kwa kurekebisha mtazamo wa Watanzania kuhusu kazi lakini kupenda kusoma.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna malalamiko makubwa ya wananchi kuwa kazi ambazo zilipaswa kufanywa na Watanzania sasa zinafanywa na wageni.

Aidha, wageni hao pengine wengine wana vibali na wengine hawana vibali ambaa ndio wengi. Wageni aina hii wanaonekana sana kwenye mahotelii na biashara za bidhaa za madukani. Hata zile kazi wanazodai za kitaalam kwa hao wenye kazi hizo basi utaalamu mwingine Watanzania wanao. Nadhani umefika wakati Wizara kwa kushirikiana na Idara ya

Uhamiaji kufanya msako nchi nzima ili kuwatambua wahalifu hao na kuchukua hatua za kisheria zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwepo Sheria ya Mtoto bado ajira mbaya kwa watoto ipo na badala ya kupungua ajira hizo zinaongezeka. Hali hiyo iko hivyo kwa sababu hakuna utekelezaji wa dhati wa kuondoa tatizo hilo. Watoto wanaoomba katika Miji mfano Dar es Salaam wanaonekana hadharani lakini hakuna hatua yoyote inayochukuliwa, ziko habari kuwa wengi wa watoto hao hutumiwa na wazee wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* na Mifuko mingine inafanya kazi katika kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali. *NSSF* imeshiriki katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na Mifuko mingine. Ipo habari kuwa Serikali mpaka leo hajatoa uthibitisho kwa Mfuko huo juu ya ujenzi wa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Hapa inatia wasiwasi ikiwa uthibitisho huu Serikali ina kigugumizi je, malipo ya fedha itakuwaje? Nadhani umefika wakati Serikali ithibitishe ili Mfuko huo wapate cha kutegemea na ushahidi wa ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya waajiri binafsi wana tabia ya kuwanyanya wa wafanyakazi wao. Aidha, mishahara yao wanayotoa wakati mwingine hailingani na viwango vinavyowekwa. Nadhani ipo haja Wizara kuwa karibu sana na ajira binafsi ili manyanyaso yaliyopo yaondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko sehemu za kazi baadhi yake hawataki kuweko Vyama vya Wafanyakazi. Hali hiyo inaonekana katika migodi na baadhi ya viwanda. Ukosefu wa Vyama vya Wafanyakazi katika maeneo hayo ni dhahiri kutakuwa na uonevu mkubwa wa haki za wafanyakazi. Wizara ipo haja kufutilia sehemu hizo ili Vyama hivyo viwepo na kuwatetea watusika. Ahsante.

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichangie katika Wizara hii ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika kipindi cha mwanzo cha kampeni ya uchaguzi wa mwaka 2005 alitangaza ajira 1000. Je, hadi kufikia kipindi hiki cha 2011, ni waajiriwa wangapi wamefaidika na ajira hizi wakiwemo vijana ambao ni Taifa la Tanzania na ni nguvu ya mabadiliko ya nchi hasa inayoendelea kama hii yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alikiri kwamba Watanzania wavivu, hawapendi kusoma majorida lakini pia starehe tunazipenda. Sasa ili kuboresha sekta hii ya kazi, ni lazima Serikali na Wizara ipange mikakati madhubuti ya kuwafanya wafanyakazi wajali kazi zao.

Kwanza, kuboresha mishahara yao. Pili, kuboresha vitendea kazi maofisini. Tatu, kuunda mpango mkakati wa kazi yakiwemo mafunzo kwa wafanyakazi. Nne, kuweka motisha katika kila Wizara ili wapate kufanya kazi kwa ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kuboresha mazingira ya kazi na vitendea kazi. Kuna Idara nyininge za kazi kuna magari yamenunuliwa toka mwaka 1988 mwisho wa gari hilo limepelekwa Wilayani na ukiliona gari jipya *No.DFP* basi hilo ni la msaada. Mheshimiwa hivi kweli katika hali kama hii kutakuwa kuna wafanyakazi hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika (*ILO*) yaani *International Labour Organization*, Makao yake Makuu yapo Geneva Uswisi. Nataka kujua kuhusu misafara ya kwenda mikutano ya *ILO*, je, Zanzibar inashirikisha vipi? Pia kulikuwa na tatizo Watanzania wanaofanya kazi Oman na nchi za Arabuni kuhusu mikataba ya kazi kuzuiwa. Je, ni hatua gani Serikali ya Tanzania imechukua ili kumaliza tatizo hill?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba, ukurasa wa 13, kipengele cha 28, imeelezwa Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kushughulikia matatizo ya ajira kwa kutekeleza programu ya kitaifa ya kukuza ajira kwa kuhamasisha uwekezaji wa umma kwa kupitia

Serikali Kuu, upanuzi wa Vyuo vya Mafunzo, ukuzaji wa ajira na mengineyo. Haya yote ni mipango tu lakini ajira hapa bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isijenge viwanda na kufufua vilivyopo hapa nchini na kila Mkao? Hapa Tanzania kuna rasilimali zake na kuna kila aina ya nafaka, kwa nini tusianzishe ubunifu mpya kila Mkao ujengewe viwanda, hizo ni ajira, nchi isiyo na viwanda ni maskini wa mwisho.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tatizo katika maeneo ya kazi kwa baadhi ya viwanda binafsi katika maeneo mbalimbali kama vile:-

- (1) Waajiri kutokutoa mikataba kwa wanaowaajiri jambo ambalo linawanyima stahili nyingi wanaofanya kazi.
- (2) Kukosekana kwa vifaa vya kukabiliana na maeneo ya kazi (maeneo ya uzalishaji) katika viwanda husika.
- (3) Usalama wa afya katika eneo la kazi kwa watumishi.
- (4) Kutoheshimu viwango vya mishahara kwa wafanyakazi (mishahara haizingatii muda mrefu wa utumishi) na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama vile wawekezaji hawapewi masharti yoyote juu ya kuwajali watumishi wao na kwamba waajiri wanaongozwa na hisia na mapenzi yao, jambo ambalo linaleta dhana ya Serikali kuititia Wizara kuonekana kwamba hajali wananchi wake na ndio maana haiweki masharti yoyote kwa mwekezaji katika kulinda haki za mfanyakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi (*OSHA*) ndiye aliyepewa dhamana ya kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika maeneo yote ya kazi na kwamba pia aweze kusimamia haki na stahili za wafanyakazi, lakini pia *OSHA* kwa kiwango fulani ndio suluhisho la matatizo baina ya mwajiri na walioajirisha. Inatia shaka kwamba *OSHA* haiwajibiki ipasavyo na ndio maana matatizo mengi yanaonekana kuibuka au kuibuliwa na waajiri kutokana na kutoheshimu haki za wafanyakazi wao na huku wakiwa wanajiamini kabisa kama vile hakuna chombo chochote ambacho wao kinawatia hofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya waajiri katika baadhi ya viwanda huamua kuwafukuza wafanyakazi baada ya kuona tu kwamba wanakabiliwa na jukumu la kulipa fedha nyingi kwa wafanyakazi wao na hivyo kuwafukuza kazi watumishi (wazalishaji) bila kuwalipa stahili yoyote na kwa jeuru ya maneno kwamba (nendeni popote mimi hamnishughulishi na sina wasiwasi wowote). *OSHA* yanafanyika yote haya ikiwa inafahamu lakini inafumbia macho mambo haya kama vile yanayofanyika ni haki kwa wanaofanyiwa, jambo ambalo linafanya tuijulize, kuna nini katika ya *OSHA* na baadhi ya wawekezaji (baadhi ya wenye viwanda)?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sana *OSHA* yenyewe ikachunguzwa juu ya utendaji kazi wao lakini pia namna ambavyo wanawafumbia macho waajiri ambaao wanawadhalilisha wafanyakazi wao na bila kujali haki za wafanyakazi wao. Pamoja na jitihada za Chama au Vyama vya Wafanyakazi mahali pa kazi kulalamika na kutoa taarifa juu ya manyanyaso wanayopata kutoka kwa mwajiri, lakini *OSHA* bado wanabaki kimya bila kuchukua hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mimi hili ndio liliikuwa kero kubwa kwangu nikizingatia kwamba wanaofanyiwa ni Watanzania wenzangu na ambaao ni wanyonge sana, unyonge wao isiwe ndio sababu ya wao kunyanyasika kiasi cha kudhalilisha utu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia kwenye mambo yafuatayo:-

(i) Kumekuwa na kero kubwa ya watu wanaoomba ajira kutakiwa vyeti vyao kufanyiwa *verification* suala ambalo linachukua muda mrefu. Tunaitaka Wizara iongeze wafanyakazi ili zoezi hili liweze kufanyika kwa siku moja au mbili.

(ii) Ajira kwa watoto. Kumekuwa na wimbi kubwa hasa maeneo ya mijini watoto wengi wamekuwa wakijajiri ili kukidhi mahitaji yao, hasa maeneo ya Morocco Jijini Dar es Salaam, watoto wanaosha magari yakiwa kwenye foleni na kupewa ujira mdogo, wakati mwingine hawapewi kabisa.

(iii) Kuna suala tete na changamoto inayoikabili nchi kutohana tu na hii *protocol* ijulikanayo kama *East African Common Market Protocol*. *Protocol* hii itaruhusu nchi wanachama kufanya kazi sehemu yoyote. Je, nchi tunaweka mikakati gani bora itakayohakikisha vijana wetu wanapata ajira za kutosha hata katika sekta binafsi kama vile mahoteli, mabenki na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 60% ya Watanzania ni vijana ambao wengi wao hawana kazi na wengine wana kazi za kususua tu ambazo hazina mwelekeo wa uendelevu na wengine hujishughulisha angalau kwa kupata mkate wao wa siku tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi ni Wizara ambayo ni uti wa mgongo kwa vijana na watu wazima ambao wengi wao wanaiangalia kwa macho makubwa katika kuendeleza maisha yao. Ingawa Wizara imejikita katika shughuli mbalimbali za kazi, Sheria na mafao ya wafanyakazi wake, lakini pia juu ya kuwapa ushauri vijana wake “counselling” juu ya namna gani ya kupata kazi, lakini ni vijana wangapi wanaojua au wanaokwenda Wizarani au kuelewa kwamba Wizara ina jukumu kama hili? Ni vizuri Wizara ikaelimisha vijana kwa kutumia njia mbalimbali kama magazeti, redio, TV, mikutano ya hadhara na vikundi vya sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wengi wanaozalishwa katika Vyuo mbalimbali hukosa kazi kwa sababu kazi ni kidogo au kukosa uzoefu au hawana sifa. Vijana wengi wanaohitimu Chuo Kikuu, wanashindwa kupata ajira kwa kuwa hawana sifa zinazotakiwa. Hii inatokana na kwamba Vyuo vingi vinazalisha wahitimu wasio na sifa na ndio maana wanashindwa kupata ajira katika soko la ushindani, kutohana na ukweli kwamba mafunzo yao yanaendeshwa kinadharia pasipo kufanya mazoezi ya kivitendo. Serikali ichukue hatua ya kuinua kiwango cha elimu nchini ili vijana wanaohitimu Vyoni wakubalike katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala inayofundishwa iwe na mada ambazo zinahitajika katika mazingira ya sasa ya soko la ajira, hiki ndio chanzo cha Kampuni na Mashirika kutowaajiri. Ni vyema Wizara ya Elimu, Kazi, Biashara na Viwanda kukaa pamoja na kujaribu kutengeneza mitaala itakayowawezesha vijana kujituma mara tu watapomaliza mafunzo/masomo yao. Aidha, elimu ya ujasiriamali ienezwe katika mashule ili wanafunzi waweze kuijendeze wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya wafanyakazi katika Mashirika, Makampuni mfano hotelini, wafanyakazi wao ni vijana kutoka nje na hasa Kenya, Zambia, Uganda, hii inawafanya vijana wa Kitanzania kukosa kazi. Kama Wizara wanachukuliaje jambo hili ambalo hata bado hatujakubaliana kisawasawa katika soko la Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna tatizo kubwa la uwajibikaji kazini, tunadharau katika sehemu zetu za kazi, ama kwa kucheleva kufika, kutoroka au kuondoka mapema. Pia inaweza kutokea au kutohana na vitendea kazi, kutokuwa wabunifu, wavivu au kupata kazi kwa ujamaa na ujomba. Sekta binafsi na Mashirika ya Umma hufanya kazi kwa tija kutohana na sheria zinavyofanya kazi ukilinganisha na Serikali. Hivyo uzalishaji haudorori, kazi zinafanywa kwa mpango na uendelevu na tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadili ya pahala pa kazi ni muhimu, ni vyema wafanyakazi wawe na maadili mazuri ili waweze kufanya kazi kwa uangalifu, lugha, tabia na mavazi yawe mazuri ili utendaji wa kazi uwe mzuri. Kila mfanyakazi awe na *ethics* na kuzifuata katika eneo la kazi ili kudumisha siri za pahala pa kazi lakini kuna baadhi ya wafanyakazi ambao wanakwenda

kinyume na *ethics*, hutoa siri au *documents* ambazo hazistahili kutolewa, je, Serikali inachukua hatua gani kwa watu wa aina hii, ina mikakati gani kwa wafanyakazi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri anapokuja kwenye majumuisho alieleze Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, migomo inayopelekea kutowajibika vyema katika kazi. Serikali ifanye kazi kubwa ya kuwatekelezea wafanyakazi haki zao ili migomo ipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri yafuatayo:-

(i) Serikali na Viongozi wa Vyuo watambue kuwa Vyuo Vikuu katika nchi zilizoendelea vimepanuliwa kuridhisha soko la ajira, kwa kuhakikisha kuwa mitaala ya Vyuo hivyo inatayarishwa na kuelekezwa katika hali ya kuitkia mahitaji ya viwanda na kampuni za biashara. Hivyo wahitimu wanajajiri wenyewe au wanaajiriwa kirahisi kwa sababu tayari wanakuwa na maarifa, elimu, ujuzi na umahiri katika fani husika.

(ii) Ni vema maofisini kuwe na *punch card* ambayo itasaidia wafanyakazi kufika mapema na kuendelea na kazi vyema.

(iii) Vijana wawezeshwe katika mikopo kwa mpangilio mzuri ili waweze kujiendeleza kimaisha, hasa wale wa Vijiji.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira kwa wageni. Kumekuwa na uajiri wa wageni wengi katika Kampuni za Kigeni. Waajiriwa hawa huwa wanafanya kazi za kawaida ambazo Watanzania wana uwezo wa kuzifanya. Sheria ya uwekezaji inasema kuwa mwekezaji anaruhusiwa kuleta wataalamu wasiozidi watano kutoka nje ya nchi. Tunalolishuhudia hivi sasa ni kuwa wanaletwa wafanyakazi wa kawaida kuja kufanya kazi Tanzania. Tunamtaka Waziri achukue hatua thabiti ya kudhibiti suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uachishwaji kazi holela. Wafanyakazi wanaofanya kazi katika taasisi za watu binafsi na viwanda wanafukuzwa kazi bila sababu za msingi. Haki za waajiriwa hazizingatiwi kwa mujibu wa sheria ya uajiri. Hali hii hasa hutokea katika viwanda. Mifano mizuri katika hili ni Urafiki, *Geita Gold Mine*, *Jambo Plastic* na Kadhalika. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie ukiukwaji huu wa haki za wafanyakazi kwa karibu zaidi, kwa azma ya kuwapatia haki zao wafanyakazi wote wanaofukuzwa kazi kiholela.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na watumishi wote kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu wa kuboresha Wizara hii. Nianze na *OPRAS*. Mfumo huu wa upimaji utendaji wa kazi ni mzuri kwani haumuonei mtumishi. Pia una lengo zuri la kuongeza tija kwa watumishi wa umma lakini tangu uanzishwe umekuwa unasuasua ni kama haupo. Naomba Wakuu wa Taasisi, Idara zote na wafanyakazi wapewe mafunzo ili waelewe utekelezaji wake. Naomba uanze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifuatilie ajira katika makampuni ya wawekezaji. Ajira ndogondogo ambazo zinaweza zikafanywa na wazawa (Watanzania) zinafanywa na watu toka kwao au wanaajiri toka Malawi, Zambia na Kadhalika. Mheshimiwa Waziri hili linasemekana lipo, kwa nini wasiajiri kutoka ndani ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri elimu ya Afya ya Jamii itolewe ili wananchi waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la ajira hapa Tanzania. Kama nilivyosema, ajira wapewe vijana Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana Wizara ina Makaimu wengi. Nashauri hizo nafasi waajiriwe wale wenye sifa stahili badala ya kuweka Makaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu vigezo vya ajira. Baadhi ya vigezo vinavyotumika katika sifa ya kupata ajira vinatakiwa viangaliwe upya. Moja ya kigezo kinachotumika katika ajira na kufanya vijana wanaomaliza masomo yao wakose kazi ni sifa ya uzoefu katika kazi. Ni moja ya kigezo kinachopaswa kuangaliwa upya. Kwa kutambua kuwa uzoefu unapatikana baada ya mtu kufanya kazi, je, uzoefu utapatikana mashulen?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni upendeleo katika ajira. Upendeleo katika kutoa ajira ni moja ya udhaifu unaosababisha kuwa na watumishi wasio na sifa na wasiowajibika kutokana na kuwa na uwezo mdogo. Hali hii hufanya watumishi hao kutowajibika na kuleta malalamiko ndani ya jamii na kuleta hasara katika Taifa letu kwa kuzorotesha ufanisi wa shughuli mbalimbali za Serikali au Taasisi mbalimbali na hasa Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa wazawa. Katika ajira mbalimbali na hasa kwa wawekezaji, moja ya kifungu katika mikataba ya wawekezaji iwe ni kutoa ajira kwanza kwa wazawa na Serikali iratibu ajira hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwajibikaji. Watumishi wengi wa Serikali wamekuwa hawawajibiki, hivyo kuiletea Serikali hasara kwa kuwalipa mishahara ambayo hawakuifanyia kazi. Serikali inabeba mzigo wa kuwalipa mishahara watumishi ambao hawazalishi kitu chochote kazini, wanakaa maofisini kwa kusubiri mwisho wa mwezi ufike wapate mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya ajira ya watoto. Vita hii inakuwa ngumu kufanikiwa kwa sababu viongozi ndio wanaoajiri vijana wadogo kuwa watumishi ndani ya nyumba zao kwa ajili ya kulea watoto, kuwa wapishi na wengine kufanya kazi ya kuchunga mifugo yao. Hivyo, Serikali katika kupiga vita jambo hili ianzie kwetu viongozi na liundiwe sheria na sifa mojawapo ya kiongozi iwe ni kuepukana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufund. Vyuo hivi vikianzishwa katika kila Wilaya, vitasaidia sana katika kupata mafunzo ya Ufund Stadi ambayo yatawezesha vijana wengi kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria za Kazi katika sekta ya migodi hapa nchini umekuwa legelege. Baadhi ya waajiri katika migodi wanakiuka Sheria za Kazi bila kuchukuliwa hatua zozote kwa mujibu wa sheria hizo. Je, Serikali inajua hili kwani kuna Maafisa wa Kazi wa Mikoa na hatua gani zitachukuliwa kurekebisha hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama kazini bado ni tatizo kubwa nchini. Eneo hili bado linahitaji juhud mahsusili wafanyakazi wasipate madhara kutokana na kuathirika na mazingira ya kazi mfano viwanda vya mbao, viwanda vya kusindika vyenye dawa mbalimbali na vingine vingi. Je, Serikali inawavezeshaje Maafisa kukagua viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya kuijunga na Vyama vya Wafanyakazi inakiukwa katika baadhi ya migodi kwa kuanzisha 'forum' zingine zichukue nafasi ya Vyama vya Wafanyakazi. Je, Serikali inajua?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inafanya kazi nzuri lakini ni vema iwe chini ya Wizara moja tu na hasa Wizara ya Fedha.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri. Hata hivyo, napenda kutoa maoni katika maeneo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni likizo ya uzazi (*Maternity Protection*). Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Na.6 ya 2004, kinatoa haki ya likizo ya uzazi na maslahi ya fedha kwa wanawake wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa licha ya uwepo wa Sheria hii, bado kuna baadhi ya waajiri hasa katika sekta binafsi ambao wanawanyima wanawake haki yao ya likizo ya uzazi na malipo. Je, Wizara ina mikakati gani mahsus ya kuhakikisha wanawake Watanzania wanaofanya kazi, wanafaaidi (*enjoy*) haki yao ya likizo ya uzazi hasa wale walioajiriwa katika sekta binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia Wizara kutoa hamasa na elimu kwa wanaume/kina baba juu ya umuhimu wa kuchukua likizo ya uzazi (*paternity leave*) pale wake zao wanapoifungua kama Sheria inavyowapa stahili hii. Hii itasaidia kupunguza mzigo/kazi kwa wake zao katika kipindi cha uzazi na pia kutoa fursa kwa kina baba kuchangia malezi ya watoto wao kuanzia siku za mwanzoni mwa kuzaliwa watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ajira mbaya kwa watoto. Napongeza jitihada za Wizara katika kupambana na tatizo la ajira mbaya kwa watoto hapa nchini. Hata hivyo bado tatizo hili ni kubwa sana kwa sababu watoto wengi wanaajiriwa katika kazi/sehemu mbalimbali kama vile katika migodi, bandari na maeneo ya uvuvi. Je, Wizara imefanya sensa katika miaka ya hivi karibuni kujua idadi halisi ya watoto walioajiriwa/wanaofanya kazi katika mazingira hatarishi? Je, Wizara ina mikakati gani ya kuwaondoa watoto hawa katika ajira mbaya na kuwawezesha kuendelea na masomo? Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja iliyotolewa leo hii asubuhi na Mheshimiwa Kabaka, inayohusu mada niliyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kulipongeza sana Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa kazi kubwa inazofanya katika miradi mikubwa ya maendeleo hapa nchini. Shirika hili ambalo kwa kiasi kikubwa linafanya kazi zake kwa uadilifu mkubwa limeendelea kuwa ni chachu ya maendeleo kwa nchi yetu hii ya Tanzania. Miradi kama ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Jamii hapo *UDOM*, ni kielelezo tosha kuwa shirika hili lipo kwa ajili ya wanachama wake bali pia ni kwa wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa chuo hicho, shirika pia linaendelea kujenga majengo mbalimbali kama yalivyoainishwa kwenye kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa 23 hadi 25. Miongoni mwa miradi mikubwa inayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 ni ujenzi wa daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, michoro kwa ajili ya daraja hili tayari imekamilika, hii ni hatua kubwa. Kazi ya kumtafuta Mkandarasi inaendelea na mwishoni mwa mwaka huu ujenzi wa daraja hilo utaanza rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya ujenzi wa daraja hili imeanza muda mrefu uliopita bila utekelezwaji. Bajeti za miaka ya nyuma nyingi zilikuwa zinazungumzia matarajio yake ya ujenzi bila mafanikio. Ahadi zinatolewa lakini hakuna utekelezaji, hali kama hii inawakatisha sana wananchi kwa kuiona Serikali yao inawaongopea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, basi naiomba Serikali kufuatilia kwa makini ili ahadi hii iliyotolewa leo hapa Bungeni inatekelezwa kwa kuanza ujenzi wa daraja hili kwa wakati. Naiomba Serikali ikishirikiana na *NSSF* waweze kutimiza ahadi hii ili ile ndoto ya ujenzi wa daraja la kisasa pale Kigamboni iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nyingi nilizotoa kwa shirika hili niliombe pia liweze kuangalia uwezekano wa kujenga makazi ya Askari Polisi ambao kwa kiasi kikubwa hawana makazi. Mfano, katika Jimbo la Kibiti ambalo lina Askari Polisi 36, askari hao wote hawana makazi wala ofisi. Ofisi iliyokuwepo (Kituo cha Polisi) ipo katika hifadhi ya barabara ni mita tano tu kutoka kwenye mabega ya barabara kuu ya Kilwa na hivi sasa imewekewa alama ya X (Bomoa).

Watumishi hawa wanaishi maisha magumu kwa kupanga uraiani jambo ambalo linahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Serikali ya Kijiji cha Kibiti A kwa kutoa eneo kubwa la ardhi kwa kujenga siyo kituo tu bali pia nyumba za askari zaidi ya mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweze kukiangalia Kituo hiki cha Polisi ili kama kuna uwezekano waweze kuingia mkataba na NSSF ili ujenzi wa majengo hayo uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana kuwateua Makamishna wote wa *CMA* mapema iwezekanavyo kwa kuwa muda wao wa kuitumikia *CMA* (ambao walipo) muda wao umekwisha (*expired on 3/2011*). Ahsante.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kazi na ajira ni la kidunia lakini hapa Tanzania ni kubwa zaidi. Je, Serikali ina mpango gani endelevu utakaopunguza ukubwa wa tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wawekezaji wanaotoa malipo madogo chini ya kiwango kilichowekwa na Serikali lakini pia wapo waajiri ambao siku zote wanaajiri wafanyakazi wa muda tu hata kama mfanyakazi yupo pale kwa miaka ishirini. Uchunguzi umebaini kuwa waajiri hao wanakwepa kulipa kiinua mgongo ikiwa watakuwa waajiriwa wa kudumu.

Je, Serikali imefanya utafiti wa kuwatambua waajiri wa aina hiyo na imewachukulia hatua gani? Lakini hiyo haitoshi wapo pia waajiri wanaowakata wafanyakazi wao fedha za NSSF lakini hawazitumi kunakohusika, matokeo yake ni kuwa mfanyakazi anapostaafu kazi na kwenda NSSF kuchukua pesa yake anakuta pesa hizo haziko yaani hazijapelekwa NSSF. Je, katika hali kama hiyo, Serikali inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inawasaidiae Watanzania kutumia fursa ya ajira za nje kwani kuna tetesi kuwa Zanzibar wameanza kuwatafutia Wazanzibari ajira za nje kwa makubaliano maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wanafanya kazi ya kubabaisha tu, hawana hakika ya maisha yao ya kesho. Ni lini Watanzania ajira zao zitakuwa za uhakika, kwa sababu viwanda ni vichache ambavyo vingeweza kuajiri watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Machinga *Complex*, jengo la Machinga *Complex*, Dar es Salaam limejengwa kwa nia safi ya kuwapatia vijana kazi, lakini ni kwa nini majengo hayo hayatumiki ipasavyo, kuna tuhuma ya kuchukua rushwa katika kutoa nafasi tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali yafuatayo:-

(a) Ijenge viwanda vya kusindika mazao au bidhaa za kilimo na kadhalika kwa kuziongezea thamani lakini pia kwa kutoa ajira.

(b) Kushawishi vijana wetu kujiajiri katika kilimo, ajira ambayo haina mashaka yoyote.

(c) Mishahara ya wafanyakazi wa Serikali na sekta binafsi ipandishwe ili ilingane na kupanda kwa garama za maisha.

(d) Wamachinga wasaidiwe kwa mikopo midogo midogo na maeneo yasiyo na kero ili waweze kujiajiri wenyewe.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa uhai unaoniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu ya Kibunge ya kuchangia hoja mbalimbali zinazowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa mipango ya mwaka 2011/2012 iliyopelekea uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kimaandishi nitauelekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni bajeti finyu ya maendeleo ya mwaka 2010/2011. Nimesikitishwa sana na kitendo cha Serikali cha kutoipatia Wizara hii Mtambuka bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa sita, kiasi cha bilioni 2.143 sawa na asilimia 32.52 katи ya bilioni 6.590 ndio zilizopokelewa na Wizara. Jambo hili sio la kujivunia kwa kuwa Wizara hii inategemewa sana katika suala zima la kuongeza ajira kwa Watanzania hususan vijana ambao wana nafasi kubwa ya kuongeza pato la Taifa kupitia nguvu kazi ya vijana hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuhakikisha kuwa, fedha zote zilizopitishwa na Bunge hazina budi kupelekwa mapema kwa Wizara husika kama ilivyokusudiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni hifadhi za jamii. Kwa namna ya pekee nipongeze kazi nzuri inayofanywa na Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa kazi nzuri ambayo Mifuko hii inafanya. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wake nilipongeze sana Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa kazi kubwa na nzuri inayofanya hapa nchini kwetu. Shirika la *NSSF* limechangia sana katika shughuli za maendeleo ya nchi yetu kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali mfano ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa nyumba Kijichi, ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi, ujenzi wa daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nipongeze mpango kazi wa mwaka 2011/2012 wa Shirika la *NSSF* hasa katika kutekeleza kazi zifuatazo pamoja na kazi zingine kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 38:-

(i) Kukamilisha utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Umeme wa megawati 300 katika eneo la Mkuranga. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Pwani na hususan Wilaya ya Mkuranga kwa uwekezaji huu mkubwa uliofanyika katika Mkoa wetu wa Pwani. Ni imani yangu kuwa, mshauri mwelekezi amepatikana, basi utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa haraka ili kuweza kuchangia katika kutatua tatizo la umeme linaloikabili nchi yetu ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kudorora kwa ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lililo dhahiri ni kwa Shirika la *NSSF* linao uwezo mkubwa wa kutekeleza miradi ya umeme, hivyo, naishauri Serikali kuangalia upya uamuzi wake wa kutafuta mkopo wa kutekeleza mradi wa Mchuchuma, Liganga wenye uwezo wa kuzalisha megawati 400 na badala yake mradi huu wapewe Shirika la *NSSF* kama walivyoomba ili kuепusha gharama za riba za mikopo hiyo.

(ii) Mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni, Hospitali ya Appolo, Jijini Dar es Salaam, Chuo cha Nelson Maendeleo na kadhalika. Kwa miradi hii inaonesha ni jinsi gani Shirika hili liliyodhamiria kuchangia maendeleo ya nchi yetu na uboreshaji wa huduma za kijamii mfano, afya, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la *NSSF*, Dokta Ramadhani Dau kwa uongozi wake thabiti, wenye ubunifu na weledi wa hali ya juu. Mafanikio yote ya shirika hilo yamechangiwa sana na umahiri wa Mkurugenzi wake Mkuu Dokta Ramadhan Dau namwomba Mwenyezi Mungu amjalie uhai na afya njema ili mipango yote iliyopangwa itekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kukuza ajira. Kwa vile Serikali imeshindwa kumwajiri kila mtu, naishauri Serikali kujenga mazingira mazuri ya wawekezaji wa nje na ndani, tuwashauri wawekezaji ili waweze kujenga yale maeneo ambayo yanaweza kuajiri watu wengi na tuwe na mkataba nao katika kutoa ajira ya asilimia 70 kwa Watanzania. Kwa kuwa wao huja na wataalam kutoka huko wanakotoka tuwaeleze na sie tunao wataalamu wa kutosha ili waweze kuwaajiri hawa tulionao Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni mishahara. Kwa mazingira ya hivi sasa mshahara ni kidogo sana, maisha yamepanda sana na wananchi hasa wale wenyewe kipato cha chini wanashindwa kumudu maisha yao.

Naishauri Serikali wakati wa kupandisha hii mishahara wale wa chini wapewe ongezeko kubwa kuliko wale wenyewe kipato cha juu kama inavyofanyika hivi sasa ikiwa mtaamua kuongeza mshahara 100,000/= basi kwa wale wenyewe mshahara wa chini waongezwe 200,000=/. Pamoja suala hili liko kwenye mazungumzo naishauri Serikali mazungumzo yamalizike haraka kwa wafanyakazi wanazidi kuteketea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni kuhusu wastaafu na haki zao. Kwa kuwa kila Wizara wanazo kumbukumbu zao za kujua lini kila mfanyakazi anastaifu, kwa hivyo, Wizara hii husika imtengenezee huyu mstaifu mafao yake siku ile ile anastaifu, akiondoka tu aondoke na *cheque* yake, huo utakuwa utaratibu mzuri kuliko ule unaotumika hivi sasa kumhangisha mfanyakazi kila siku kuja ofisini kupata mafao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni malipo ya pensheni. Mfumo unaotumika unawasumbua sana wafanyakazi muweke tarehe maalum ambayo hiyo *pension* inatiwa benki ili isiweze kumhangisha mwananchi. Hizi *pension* muwe mnazipitia kuendana na wakati isiwe mstaifu wa mwaka 1960 ambapo wakati huo walikuwa wanalipwa 2,000/= na mpaka hii leo awe analipwa hizo hizo 2,000/=.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata wasaa huu ili niweze kutoa mchango wangu wa maandishi. Nazipongeza hotuba zote zilizotolewa na Waziri kwa niaba ya Serikali, Kamati ya masuala ya jamii pamoja na ile ya Kambi ya Upinzani. Serikali izingatie sana maana yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani ili kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira ni pana sana na hasa ikizingatiwa kwamba linagusa karibu maeneo yote ya maisha ya mwanadamu. Kwa kuwa binadamu anahitaji ajira iwe ni ya binafsi au rasmi ili kuweza kukidhi mahitaji muhimu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la wageni ambao wamekuja kujajiri hapa nchini, hali hii imewaweka katika mazingira magumu wazawa wa nchi hii kupata ajira. Tunaitaka Serikali kuhakikisha Watanzania wanapata ajira katika maeneo ambayo wawekezaji wanakuja kuwekeza katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuwashakikishia usalama wa ajira yao, malipo yao pamoja na stahiki zao zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walioajiriwa migodini wanafanya kazi katika mazingira magumu, afya zao na ajira zao zimekuwa zikiashiria utata mkubwa kwa maana kwamba haziko sawa. Tunaitaka Serikali kuititia kwa Waziri wa Kazi kutoa tamko lenye matumaini juu ya wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wafanyakazi ambao wamekuwa wakipata matatizo makazini mfano, ajali zinawasababishia ulemavu, tunaitaka Serikali iongeze viwango vya fidia kwa wafanyakazi hawa sambamba na kwa waajiri wao kutoa taarifa zilizo sahihi sehemu stahiki ili

waweze kuhudumiwa haraka, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kuyamudu maisha yao mapya wakiwa ni walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro na migomo iliyokithiri katika maeneo ya kazi tumeshuhudia ikiongezeka kila iitwapo leo, hii ikiwa ni kiashiria tosha kwamba kuna matatizo mengi katika maeneo ya kazi. Tunaitaka Serikali pamoja na kuwepo Mabaraza ya Usuluhihi Makazini, iingilie kati tabia hizi kwani kuna baadhi ya waajiri wengi ambao hawafuati masharti ya kazi na hivyo kushindwa kudhibiti changamoto hizi ambazo zimekujwa zikilitia aibu Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi duni, kutosikilizwa, uongozi kutofuata taratibu sambamba na upendeleo makazini ni mionganoni mwa kero ambazo zimekuwa zikilalamikiwa. Pia wazee wakumbukwe, kama Serikali ilivyoahidi tunataka isimamie kauli yake wazee walipwe pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti kati ya nchi maskini na tajiri sio umri wa nchi, kama ilivyo katika maisha ya mtu mmoja mmoja. Hii inaweza kulinganishwa na nchi kama India na Misri ambazo zina umri wa miaka zaidi ya 2000, lakini ni nchi maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Canada, Australia na New Zealand, nchi hizi miaka 150 iliyopita ziliikuwa hazijulikani leo ni nchi zinazojulikana kama zilizoendelea na tajiri duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti kati ya Tajiri na Maskini haitegemeani na uwepo wa maliasili au la! Mfano mzuri ni nchi kama Japan ambayo ina 80% ya milima katika nchi hiyo, maeneo haya hayafai kwa kilimo au ufugaji, lakini ni ya pili kwa uchumi mkubwa duniani. Nchi hii inaagiza malighafi kutoka duniani kote na inauza bidhaa za viwandani duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mifano hiyo, ni lazima tujichunguze ni namna gani Wizara ya Kazi inavyoweza kuchangia maendeleo katika nchi yetu. Tanzania kama nchi nyingine za Kiafrika ina tatizo kubwa katika Wizara hii ya Kazi na Ajira. Tofauti kubwa kati ya nchi zilizoendelea na maskini ni mtazamo (*attitude*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunagundua kuwa watu wengi katika nchi zilizoendelea wanafuata kanuni hizi zifuatazo katika maisha yao:-

- (a) *Ethics (maadili).*
- (b) *Uaminifu (Integrity).*
- (c) *Uwajibikaji (Responsibility).*
- (d) *Kuheshimu sheria na taratibu.*
- (e) *Kuheshimu haki za raia wengine.*
- (f) *Kupenda kazi.*
- (g) *Kupenda kuweka akiba na vitega uchumi.*
- (h) *Kufanya kazi kwa kiwango cha juu.*
- (i) *Kutunza muda.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi kama Tanzania ni watu wachache wanafuata hizi kanuni za msingi katika maisha ya kila siku. Tanzania sio maskini kwa sababu hatuna maliasili au *nature was cruel to us!!* Ili Wizara hii itoe mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu, ni lazima Wizara ifanye kila linalowezekana kubadili mtazamo wa Watanzania na kuanza kufuata na kuzingatia kanuni hizo hapo juu, kuziishi na kuzifundisha. Matokeo yake tutapata mfumo imara katika taratibu za Kiserikali (*Government regulation*). Wananchi wakifuata kanuni hizo ikitanguliwa na Wizara malalamiko mengi yatapungua kama sio kuondoa tatizo.

MHE. DKT. SEIF S. RASHID: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudi za Serikali katika kuwasilisha bajeti yenyewe mwelekeo wa matumaini makubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze juhudhi na mafanikio ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa nafasi ya pekee niipongeze NSSF kwa michango yake katika miradi mingi yenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kwanza kuunganisha mifumo ya taarifa ya kazi nchini ili Watanzania popote pale wapatiwe nafasi za kazi au ajira kwa msingi madhubuti ya Mtanzania kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuongeza kuwawezesha Watanzania katika miradi mikubwa ya uwekezaji na kuondoa kabisa ukaribishwaji wa wawekezaji wageni ambao kwa namna moja au nyine ni kupunguza utegemezi wa wageni kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa maendeleo yoyote yale ni nidhamu na uwezo wa waajiri kusimamia waajiriwa na kuona malengo ya chombo hicho yanafikiwa. Wakati umefika kwa Serikali kuonesha haya kwa vitendo, kwa kuanza kuwajibisha watendaji wake wakiwemo Wakurugenzi wa Wilaya ambao ni wazembe, wabahirifu au wale ambao wameshindwa kutekeleza kazi na kufikia malengo yaliyoainishwa katika mipango ya maendeleo ya Halmashauri husika, ni lazima waondolewe kazini kwa haraka na bila ya kusita. Hii itakuwa ni fundisho kwa wafanyakazi wengi na tabia hii itahamia katika nyanja za watu binafsi ya kumtaka kila Mtanzania kufanya kazi kwa nidhamu, uadilifu na uwezo wa kufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuongeza utaratibu wa kuiwezesha NSSF, LAPF na Mifuko mingine kuwekeza katika nyanja ya kilimo, kwa kuanza kuwakopeshwa wateja wao, sio tu katika nyumba bali katika miradi ya uvezeshaji kiuchumi kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Baba wa Taifa aliamini ukombozi wa kudumu ni kujikombua kutoa ujinga, umaskini na maradhi. Hivyo, alihimiza watu kufanya kazi kwa bidii, kupata ufumbuzi wa matatizo yao ndani ya nchi yao, kutumia rasilimali walizonazo badala ya kutegemea misaada kutoka nje. Alisema inawezekana timiza ahadi yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitabu cha Mpango wa Miaka Mitano ukurasa wa 68 umebainisha kuwa *High skilled level picture* kwa nchi yetu ni asilimia tatu tu (3%) na *Low skill level picture* ni 84%. Hii inamaanisha kuwa tunahitaji sana mafunzo zaidi (*training*) katika nchi yetu ili kujenga uwezo wa rasilimali watu ili wakidhi thamani ya kazi yao ndani ya nchi yetu na thamani kwenye *global labour market* Serikali ina mikakati gani katika kutimiza azma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha umaskini ni ujinga. Kwa hiyo, siyo rahisi kutokomeza umaskini na maradhi bila kwanza kutokomeza ujinga. Elimu ndiyo nyenzo muhimu inayomwezesha mtu kutumia rasilimali zinazomzunguka na alizonazo kujikwamua kiuchumi. Elimu ndiyo inayompa mtu uwezo wa kuweka thamani na ubora katika rasilimali zake ili ziweze kupata bei kubwa, hatimaye kupata pato kubwa ili kuboresha maisha na kuinua uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujinga kuwa chanzo kikuu cha umaskini kuna mambo mengine:-

- Watu kutoheshimu kazi – Watanzania ni wavivu
- Kutothamini kazi

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ama Wizara hii ina wajibu wa mambo yafuatayo:-

- Kuwawezesha wananchi walio wengi kupata maarifa na uwezo wa kuziwekea rasilimali walizonazo thamani.

- Kuelimisha watu ili wazalisho bidhaa bora na nyingi kwa ajili ya kupata soko na pato kubwa. Ukinipa unga wa kula leo, kesho nitaomba tena, lakini ukinielimisha kulima kwa utaalami nitajitegemea.
- Kutayarisha wahitimu wa vyuo vyetu Tanzania kumudu ajira ya kuondoa umaskini na pia wawe ni wahitimu wanaomudu ushindani katika soko la ajira nchini, la sivyo ajira zetu zitakwenda kwa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali haya, je, Wizara hii ya Kazi na Ajira inajielekeza vipi kuiboresha:-

- (a) Sekta ya kilimo inayoajiri 81% ya Watanzania.
- (b) Sekta isiyo rasmi inayoajiri 9%.
- (c) Sekta binafsi 4%.
- (d) Sekta ya nyumbani 3.6%.
- (e) Sekta ya Umma inayoajiri 2.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kubuni mikakati mipyaya kukuza ajira na kuinua kazi hapa nchini. Hotuba ya Bajeti ya mwaka huu imefanana kwa kiasi kikubwa na taarifa ya 2010. Tuwe wabunifu kuboresha mikakati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara pamoja na Waziri wake na watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri yenye matumaini kwa wafanyakazi na waajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu kuendeleza vyuo vya VETA kwa kila Mkoa ikiwezekana hata Wilaya ili vijana wapate ujuzi na waweze kujajiri na kwa upande wa pili wa Muungano mtuletee vyuo hivi angalau viwili ili tuweze kuinua uwezo wa elimu na kujajiri kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza uajiri wa wageni katika sehemu ambazo vijana wetu wa Kitanzania wanaweza kufanya hivyo. Wizara iharakishe na kufanya jitihada za makusudi za kushirikiana na wadau wengine katika kushughulikia matatizo ya ajira ili kutekeleza program ya Kitaifa ya kukuza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwe na mikakati maalum kuhakikisha wafanyakazi wanawajibika ipasavyo ili Serikali ipate tija zaidi na kuweza kuwalipa wafanyakazi mishahara na marupurupu muhimu na yenye maslahi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha kwa kuunga mkono hoja.

MHE. JUMA S. JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa vijana. Ni muda mrefu sasa vijana wa Tanzania wamekuwa wakizurura ovyo mitaani, aidha, kadhaa hiyo inatokana na utaratibu mbaya wa upatikanaji wa kazi nchini. Hivyo, nashauri ni vema Serikali ikaweka utaratibu maalum utakaowezesha kutatua ajira kwa vijana. Sambamba na hilo utaratibu huo uwe katika Makampuni yote ya ujenzi ikiwa barabara au majumba na kadhalika iwe ni lazima wachukuliwe vijana. Pia Serikali kuwapelekea vijana katika vyuo Amali, VETA na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wafanyakazi, naishauri Serikali ikaweka utaratibu na mikakati maalum kwa kila Taasisi kuwashirikisha umoja wa wafanyakazi katika

maamuzi mbalimbali ili kupata ule msimamo wa pamoja wa *collective leadership*, kwani utaratibu huu ni mzuri na unaondosha malalamiko katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dokta Milton Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara ya Kazi na Ajira kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu wafanyakazi na vibarua wanaofanya kazi kwenye Makampuni ya Wachina, wanaojenga barabara, wamekuwa hawapewi vifaa vyta kuwasaidia wakati wanapokuwa kazini mfano, nguo, kofia na viatu. Mfano, hivi karibuni wakati Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete alipofanya ziara Mkoani Kigoma kwa ajili ya kuzindua Miradi ya Barabara, wafanyakazi walionekana wamevaa nguo (ovaroli, kofia na viatu) vyote hivyo vikionekana kuwa vipyta, hii inaonekana kuwa Wachina walitoa vifaa hivyo ili wasiweze kuumbuka kwa sababu siku nyingine wafanyakazi hao huwa wanafanya kazi bila hata kuwa na *gloves* wanapokuwa wanachomelea madaraja na kadhalika. Naomba kuanzia mwaka huu Wizara kwa kusaidiana na wasaidizi wa Wizara walioko Mikoani, kufuatilia maslahi ya wafanyakazi wa makampuni ya ujenzi wa barabara ili kuweza kubaini matatizo wanayokumbana nayo wafanyakazi wa kampuni za Wachina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuunga hoja hii mkono asilimia mia moja.

MHE. RAMADHAN HAJI SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba na kuweza kutujalia kuwa wazima wa afya siku hii ya leo. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira kwa hotuba yake, ni nzuri ambayo imejaa matumaini kwa Watanzania ambao wana hamu ya maendeleo katika nchi yao tulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba hii nikijikita upande wa ajira. Ajira katika nchi yetu ya Tanzania bado imekuwa tatizo, hali ambayo inapelekea maisha kuwa magumu, katika hali hii ya ugumu wa ajira nchini, naiomba Wizara ilipe kipaumbele suala hili ili vijana ambao wamemaliza vyuo vikuu waweze kupata ajira na kuweza kuendesha maisha yao vizuri. Pia naomba nichangie upande wa usalama mahali pa kazi. Bado kuna matatizo makubwa katika viwanda na makampuni juu ya usalama wa wafanyakazi. Waajiri ambao wanaajiri watu katika sehemu za viwanda pamoja na makampuni wamekuwa hawazingatii afya za wafanyakazi hao hali ambayo inapelekea kuhtarisha maisha yao kuwa hatarini, waajiri hao hawaweki hata huduma ya kwanza katika viwanda hivyo na pindi ikitokea mfanyakazi ameumia basi anaambiwa ajitegemee kutafuta matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini hali hii inaweza kuondoka ikiwa yeye ndio mhusika mkuu wa jambo hilo. Sekta ambayo imepewa ishughulikie usalama mahali pa kazi (*OSHA*) kulingana na utendaji wao wa kazi bado haujaridhisha na namwomba Mheshimiwa Waziri awachukulie hatua watendaji hao kwani wafanyakazi wengi wa viwandani na kwenye makampuni wanalamika sana Mheshimiwa Naibu Spika, kama hawa (*OSHA*) hawakuchunguzwa vizuri au kupewa mikakati migumu kwa ajili ya utendaji wao wa kazi, wanaweza kuitia aibu Wizara yako na kuweza kukuweka mahali pabaya, kumbe wewe mwenyewe ni mtendaji mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naamini kuwa wengi ambao watapata kuchangia hotuba hii watajikita katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri, na Mheshimiwa Dokta Makongoro Mahanga, Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu ingawa umuhimu wake haujatambuliwa na wengi. Vile vile nawapongeza watendaji wakuu wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Eric Shitindi na Bibi Edna Mangesho, Kamishna na Wakurugenzi wa Wizara pamoja na viongozi wa Taasisi na watumishi wa idara zote kwa kazi wanayofanya kusimamia sheria za kazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu bajeti ya matumizi na maendeleo. Nimepitia bajeti ya Wizara hii na kuona kuwa fedha zilizotengwa ni kidogo sana kulinganisha na majukumu iliyokabidhiwa. Bajeti ya maendeleo kifungu kwa kifungu ni kidogo sana kulinganisha na mahitaji halisi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa. Nashauri Serikali ifanye uchambuzi wa majukumu ya Wizara hii na kupima umuhimu wa nafsi yake katika jamii na kutenga fedha za kutosha. Ileweke kuwa kazi ya kusimamia utekelezaji wa sheria hususan inayohusisha tajiri (mwajiri) dhidi ya mtumishi (mwajiriwa) inahitaji motisha binafsi (*Intrinsic motivation*) ili kuepuka vishawishi vinavyotolewa kwa maafisa wanaosimamia utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhusu pensheni kwa wazee. Maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, 2010 juu ya kupanua wigo wa pensheni ili kujumuisha wazee, wakulima, wafugaji na wafanyabiashara itekelezwe ili kuwapunguzia wazee hao mateso wanayoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni uwekezaji wa fedha za *NSSF*. Hivi karibuni *NSSF* imekuwa ikipanua wigo wa uwekezaji kiasi kwamba kama tahadhari isipochukuliwa iko hatari Mfuko ukawekeza kwenye miradi ya hasara. Ni vizuri kuwa kabla ya uamuvi wa kuwekeza kwenye miradi mikubwa kama vile miradi ya kufua umeme wanachama kuitia wawakilishi wao washirikishwe kuititia semina ili kupata maoni na ridhaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ni ajira kwa wageni. Wageni wengi toka nchini Kenya na nchi za Asia wamekuwa wakiingia na kuajiriwa nchini kwenye nafasi ambazo Watanzania wa kawaida wanao ujuzi na uwezo wa kufanya kazi hizo. Hili ni jambo la aibu kwani linakosesha wananchi wetu ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwa ukaguzi uimarishwe kwa kuunda Kamati itakayojumuisha Maafisa au Wakaguzi wa kazi, Uhamiaji, Polisi na TAKUKURU kwa kila Wilaya ili kubaini waajiri wanaoajiri wageni kinyume na sheria na kuchukua hatua dhidi ya mwajiri na mwajiriwa pale ambapo kampuni ni ya mgeni, basi afungiwe biashara na kufukuzwa yeze na aliowaajiri toka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waziri wa Kazi na Naibu wake pamoja na watendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo unahusu tatizo la ukosefu wa uaminifu kwa wafanyakazi wa Kitanzania katika maeneo mbalimbali mfano, wawekezaji wengi kutoka nje na hata wale wa hapa nchini wamekuwa wakilalamika kufanyiwa vitendo vyta ukosefu wa uaminifu. Hali hii imekuwa ikisababisha kutokuwa na imani kwa vijana wetu, hivyo tatizo la ajira kukosekana kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa vijana wengi na Watanzania wengi wamekuwa wakilalamika ukosefu wa ajira je, Serikali itakuwa tayari kubainisha matatizo ambayo yanasa babishwa na tabia zetu za kukosa uaminifu? Hata hivyo, kutohana na suala hili kujulikana kwa chinichini (haliko wazi), Serikali itakuwa tayari kulizungumzia suala hili kwa uzito unaostahili ili wakati Watanzania tunalalamika lakini tuje pia na wajibu wetu kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna budi kulisemea suala hili kwa nguvu na uzito ili Serikali isiendoolee kuonekana haitili maanani suala la upatikanaji wa ajira. Serikali inalaumiwa sana. Suala hili liwekwe wazi kupunguza lawama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kusema kuwa, utawala bora na demokrasia ya kweli ni nguzo imara katika kujenga Taifa lillo imara na lisilotetereka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufanya ukaguzi sehemu za kazi. Viongozi wengi kwa maana ya waajiri wamekuwa hawana ukaribu na wafanyakazi wao kwa kuwanyima haki zao za kimsingi. Kama vile kusuluuhisha migogoro inayotokea kazini na waajiri kuelemea upande na hivyo kusababisha migogoro kukua katika maofisi. Kiongozi bora hatakiwa kufungamana na upande mmoja kwani watumishi wote wapo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadili ni jambo la kuzingatia katika kazi. Maadili haya yanasis mama katika lugha, mavazi na usafi. Kiongozi anatakiwa kuwa na lugha nzuri na ya kueleweka. Lakini kuna viongozi wamekuwa na lugha za kihuni ambazo hazijengi utumishi bora pia mavazi mengine kwa watumishi yamekuwa hayazingatii maadili mema ya kazi bali kupotosha jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia kwa waajiri ya kuendekeza rushwa mahali pa kazi, mfano, mtu anapoomba ajira, anatozwa rushwa ndipo apatiwe nafasi ya kazi au kama ni mwanamke huombwa rushwa ya ngono ndipo apate kazi. Huu ni unyanyasaji na uonevu, Serikali ipige vita tabia kama hii kwa waajiri ni kulikwamisha Taifa katika utendaji mzuri, pia ni hatari katika kutoa nafasi kubwa ya kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia kwa wafanyakazi. Pamoja na Wizara kukamilisha uundaji wa Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Act*) bado haifuatwi, kwani watumishi wengi hawanufaiki. Kumekuwa na upendeleo wa ulipwaji, Serikali isimamie sana suala hili la kulipana fidia kwa upendeleo hasa kwa wafanyakazi wa sekta binafsi kama wafanyakazi wa baa, hoteli na wafanyakazi wa majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vita dhidi ya ajira ya mtoto na mazingira hatarishi ya kazi. Serikali isimamie sana hili kwani mpaka sasa watoto wenye umri chini ya miaka 15 wamekuwa wakiajiriwa katika kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini ukizungukia sehemu za stendi za mabasi utawaona watoto ndio wabebaji wa mizigo. Uchungaji wa ng'ombe na uchekechaji wa dhahabu. Hii sio hadithi nimejionea stendi za mabasi Sumbawanga na Mbeya watoto wakibeba mizigo. Uchimbaji wa madini nimeona watoto wakijihuisha na uchekeshaji wa madini Mpanda na Ibindi pamoja na mashamba ya tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikemee sana suala hili la utumikishwaji wa ajira hizi kwa watoto wadogo hawa wanaopaswa kwa wakati huu kuwa shule wakisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu mabilioni ya J.K. Miaka mitano iliyopita Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa bilioni 21, maarufu kama mabilioni ya J.K. kwa ajili ya kuongeza ajira kwa vijana na watu wa chini, lakini mpaka sasa taarifa ni tofauti maana kwa tafiti nilizofanya katika Jimbo langu la Mbozi Magharibi hakuna wananchi waliofaidika na mabilioni hayo. Hivyo basi, wananchi wa chini au wanyonge wa Mbozi Magharibi wanauliza ni kwa nini wanatengwa na Serikali yao wakati wao ni sehemu ya nchi. Mheshimiwa Waziri naomba maelezo

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mikakati ya ajira kwa wahitimu wa vyuo na vyuo vikuu. Katika miaka ya hivi karibuni Taifa limekumbwa na ukosefu wa ajira hususan kwa wahitimu wa Vyuo mbalimbali na Vyuo Vikuu nchini, ili hali Taifa letu bado linahitaji wasomi kwa ajili ya uendelezaji wa Taifa. Sasa Wizara itueleze nini mikakati yake ya kuwawezesha wasomi wote waliohitimu kuanzia mwaka huu wa fedha 2011/2012 ili tusiwe watu wa kupoteza rasilimali watu na fedha kwa kusomesha watu ambao hatuji kuwaajiri nchini. Hivyo basi. Wizara itueleze ni namna gani inaweza kuondoa wimbi la ukosefu wa ajira na wa uhakika kwa Watanzania. Maana mikakati iliyoainishwa katika hotuba ya Waziri tumeizoea na kuisikia kila bajeti mpya inapofikia au kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunjaalia kuendelea kuwepo katika dunia hii na kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekumbwa na wimbi kubwa la vijana waliokosa ajira, hili ni tatizo na ni janga kwa Taifa letu. Hali hii imezidi kuwa mbaya kwani kuna ongezeko kubwa la vijana wanaomala shule na hawana kazi, hawana pa kwenda. Vijana hawa mara nyangi natumbukia katika dimbwi la ujambazi, wizi na utumiaji wa madawa ya kulevyia. Ni vema Serikali ikalatifikia vizuri tatizo hili ili kulinusuru Taifa na tuweze kujenga Taifa bora la baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu vijana wengi wako vijiji, nashauri Serikali iweze kujenga mazingira mazuri ya ajira binafsi za vijana hawa ili kuhakikisha tunawadhibiti vijana wetu. Aidha, nashauri Serikali iboreshe Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili ziwe za kileo na ili sekta hizi ziweze kuchukua vijana wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbi hili la vijana ni muhimu kwa Serikali kutafuta mikakati mahsusini ya kuweza kuwadhibiti vijana hao kwa kuwapatia ajira ambazo zitawashughulisha katika maisha yao. Ni muhimu sana kuwajengea uwezo vijana katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Hayo yanaweza kufanya sanjari na mafunzo ya stadi za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kushukuru tena na naomba kuchangia hoja. Nashukuru.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii na hivyo kutoa mwanga wa kutosha kuhusu mambo muhimu ambayo yanatekelezwa katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dokta Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira kwa msaada mkubwa anaompa Mheshimiwa Waziri na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu sisi wananchi wa Siha ni kuiomba Serikali itukumbuke katika mgawo ule wa mabilioni ya J.K. Tuko vijiji na ukiangalia tathmini mbalimbali, wananchi waishio katika maeneo haya hawajanufaika na Mfuko huo. Tunaomba wizara isitusauhau.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Kazi na Ajira. Awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii. Pamoja na kuzisajili hifadhi sita za jamii, nashauri mamlaka hii iwe na madaraka ya kuziwekeea mwongozo hifadhi hizi hasa kwenye maeneo ya gharama za Bodi zao kuwa kubwa sana na pia kutolingana wakati fedha za Mfuko hii ni mali ya wanachama ambao sasa wanategemea kuwa mamlaka hii

itawatetea na kulinda fedha hii ya umma. Malipo ya mafao ya pensheni kwa mashirika mengi yanachelewa sana na pengine kutolipwa kwa wakati kutoptaka na urasimu na ukiritimba hasa Shirika la PSPF. Watumishi wengi huwa hawana barua za kuajiriwa pamoja na rekodi ya kuwasilisha michango ya mishahara yao kwa zaidi ya miaka 15. Sasa kama komputa zipo, hivi ni kweli ni lazima kwa dunia ya leo mtu atake barua hizo wakati *data* zote zimeingizwa kwenye kompyuta? Viwango vya mafao kwa watumishi wa Umma viwe sawa na viunganishwe kuwa chini ya Shirika la Jamii moja na wale watumishi wa sekta binafsi, ni vema wawe na shirika moja la jamii.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira inasimamia masuala muhimu kwa uchumi wa nchi na maisha ya wananchi ya ajira na hifadhi ya jamii. Matatizo ya ajira na ujira yasipofanyiwa kazi kwa uzito unaostahili yana athari kubwa kwa tija katika Taifa na usalama wa nchi kwa ujumla. Hivyo, ni vema Wizara hii ikapewa uzito unaostahili ikiwemo bajeti yake kuongezwa kujadiliwa kwa siku mbili badala ya siku moja kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku kwa ajili ya Mamlaka, Taasisi na Wakala chini ya Wizara hii ziwekewe mfumo thabiti wa utekelezaji na tathmini kwa kurejea kifungu 18 cha Sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act*, 2001). Hii inahusu Fungu 65 – Kifungu 2001, Kasma 270400 na Kifungu 2002, Kasma 270700. Aidha, utekelezaji wa miradi yenye kutoa fursa ya ajira na ujira bora ikiwemo kwenye *Volume IV*, Fungu 65, Kifungu 1003, Kasma 4901, izingatie matokeo na vigezo maalum vya kupima ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukuzaji wa ajira na ujira bora, Wizara inapaswa kuweka mkakati maalum kwa kushirikiana na Tume ya Mipango ili kuwezesha rasilimali za umma zinazotolewa kuititia zabuni na mikataba mbalimbali zinatumika kwenye mfumo wa ndani na kuchangia kwa kiwango kikubwa zaidi katika kuongeza ajira. Aidha, Wizara ieleze mafanikio mahususi yaliyofikiwa katika kutekeleza mkakati wa ajira kwa vijana, hatua za haraka zisipochukuliwa hili ni bomu la wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika mwaka wa fedha 2011/2012, ifanikishe uanzishwaji na uiimarishaji wa Kamati za kutoa ajira kwa Wilaya ya Kinondoni. Pia itekeleze mradi wa kazi nje kwa vijana katika Jimbo la Ubungo. Aidha, naiomba Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ichukue hatua maalum kuititia vyombo vyake ikiwemo Wakala wa Usalama na Ajira Mahali pa Kazi (*OSHA*) na Tume ya Usuluhishi na Uamuvi (*CMA*) kuhusu matatizo ya wafanyakazi katika Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Ubungo ambayo yamedumu kwa zaidi ya miaka kumi (10). Malalamiko hayo yapo kwenye mamlaka zote za Kiserikali. Hata baada ya wafanyakazi kwenda Mahakamani na kushinda kesi mbalimbali bado Serikali haijaweza kutekeleza wajibu wake na Kikatiba na kisheria na kuhakikisha wanapata haki zao. Baadhi ya malalamiko hayo ni pamoja na kutokulipwa kwa mafao ya kuachishwa kazi kwa wafanyakazi 92 na kampuni hiyo toka 1999 ya bilioni 1.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, (rejea barua ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya 11 Julai, 2011, yenye Kumbukumbu Namba J/C.60/4/2512 na ya Ofisi ya Rais (Ikulu) ya 29 Novemba, 2010 yenye Kumb. Na. CEA/110/404/II/01 kwa wafanyakazi wanaoendelea na kazi wana mgogoro wa muda mrefu na kiwango duni cha mishahara pamoja na maslahi mengine ya wafanyakazi kutokuzingatiwa, malalamiko ambayo mamlaka ya Kiserikali inayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani toka mwaka 2009 *Tanzania Union Industrial and Commercial Workers (TUCO)* waliwasilisha malalamiko kuititia barua yenye Kumb. Na. TUC/FTC/VM/13/2008 kwa Kiwanda toka 2007 kilikuwa kinalipa kima cha Sh. 65,000/= tu tofauti na GN. 223 ambayo ilielekeza Sh.150,000=/. Hata baada ya GN nydingine kutolewa 2010, bado kiwanda hakijazingatia matakwa ya wafanyakazi na Serikali kama nilivyothibitisha nilipokwenda kutembelea kiwanda mwaka huu 2011 na kukutana na menejimenti, viongozi wa wafanyakazi na wafanyakazi. Pia Serikali itoe kauli kuhusu madai ya wafanyakazi wa migodini kama nilivyotaja tarehe 15 Julai kwenye hotuba ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe kauli kwa mujibu wa wajibu wa kisheria na kikatiba ina lengo la kuongeza kwa kiwango gani idadi ya Watanzania kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii kutoka asilimia sita tu ya sasa. Aidha, Bunge liteupe na kujadili taarifa za uchambuzi wa

uendelevu wa mifuko (*Actual Studies*) toka mamlaka ya udhibiti (SSRA) ikiambatana na mikakati ya kupunguza garama ya uendeshaji na kuongeza mafao na ushiriki wa wafanyakazi.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pondezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri inayoleweka, ila hofu yangu ni kuhusu utekelezaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, natoa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu ukosefu wa ajira kwa watu wenyewe ulemavu nchini. Natambua kuwa Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Menejimenti na Utumishi ndizo zinazohusika na masuala ya ajira rasmi nchini. Hata hivyo, kwa upande wa watu wenyewe ulemavu hasa wale waliosoma na kukidhi vigezo wameendelea kuhangaika kutafuta kazi rasmi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wachache wanapata bahati kuitwa kwenye usaili, habari huishia hapo, kwani wakionekana tu katika hali zao wanaachwa kwa kisingizio cha ulemavu wao. Kwa msingi huo, nashauri Serikali ifanye utafiti wa kina na kupata takwimu za wenyewe ulemavu walioajiriwa katika sekta binafsi na rasmi ili kutatua changamoto inayowakabili wana jamii hawa nchini. Zaidi nashauri Serikali ihmize utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya 2010 katika vyombo au makampuni yanayoajiri. Kwa kukosa ajira rasmi na zisizo rasmi kwa wenyewe ulemavu ni kudumisha umaskini kwa wenyewe ulemavu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuhusu ajira za wageni nchini. Kwa vile mpaka sasa wageni kwa kutumia mianya mbalimbali ya kisheria wanaingia nchini na kushika ajira hata zile ambazo Watanzania wana ujuzi nazo. Jambo hili hukatisha tamaa vijana wetu na wataalam wetu. Pindi Watanzania wanapoajiriwa hasa na sekta binafsi mishahara yao wanapunjwa, mazingira ya kazi katika maeneo mengi ni magumu na kadhalika. Ni muhimu kwa Wizara kufanya utafiti juu ya suala hili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo, naunga mkono hoja.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya. Pia kwa nafasi hii, nimshukuru Waziri wa Kazi na Naibu wake, Katibu Mkuu na timu yote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeendelea kuwasomesha Watanzania wa jinsia na rika mbalimbali na kila mwaka Wizara au Idara mbalimbali imekuwa ikipata wahitimu mbalimbali katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania katika *level* ya Kata, Vijiji, hata Wilaya kumekuwa na upungufu mkubwa wa wataalam kwa ajili ya kufanya kazi na jamii. Ni rai yangu basi Serikali kuhakikisha inawaajiri wahitimu au wataalam hawa kwenye Kata na Vijijini, lakini yakiandaliwa mazingira rafiki kwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu pia kuwa Serikali iangalie kupandishwa vyeo kwa muda muafaka lakini ikizingatiwa mabadiliko ya *scheme of service* na mabadiliko ya mishahara. Wafanyakazi wasilimbikisiwe madai ya posho zao mbalimbali kama posho ya likizo, uhamisho, matibabu na kadhalika. Natoa rai yangu kwa Serikali, kutoa mafao ya watumishi wanapostaafu *immediately* na mafao mengine yanayofuatia.

Mheshimiwa Spika, wastaaafu hawa ndio wamekuwa wafanyakazi thabiti na wamechangia maendeleo, uchumi, amani, *stability* ya nchi, wamekuwa na michango yao mizuri kiuchumi, kijamii, kiutamaduni katika nchi yetu, ni vizuri Serikali isiwasahau lakini iwaenzi hata kama ni kwa *level* yao, kama vile viongozi wa Serikali Kitaifa wameendelea kuenziwa hata baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie ni kwa jinsi gani itadhibiti wimbi kubwa la wafanyakazi wanaokimbilia nje ya nchi kwenda kufanya kazi, lakini vile vile Serikali irudie utaratibu wa zamani wa kuwafanya wataalam wanapokaribia kuhitimu hata kabla hawajapewa vyeti wasaini mikataba kuwa watafanya kazi popote pale hapa hapa nchini pindi watakapopangiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imepewa pesa kidogo sana katika bajeti ya maendeleo, ni shilingi bilioni moja tu, zile nyingine bilioni tano zinatazamiwa kutoka nje (*forex*), zisipopatikana hizo basi. Kwa hiyo, pesa yetu ya ndani tumeabajeti shilingi bilioni moja tu, lakini majukumu ya Wizara hii yanatakiwa yawe makubwa, hasa kutengeneza fursa za ajira. Kwa sababu hii ukiangalia mafungu katika kitabu cha bajeti (*Volume IV*) ukurasa 135, hakuna pesa. Mafungu muhimu kama *subvote 2001 item 6243, Supports Employment Creative Program*), pesa ni zero (sifuri). *Item 5417, Fourth Employment Creative Programme*, sifuri. Wizara haitimizi majukumu yake muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ijikite kuboresha kilimo. Tuachane na kilimo cha jembe la mkono, tuachane na kuchunga ng'ombe tufuge kisasa. Wavuvi wawezeshwe katika vikundi wavue kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaofanya kazi hapa kinyume na sheria na hivyo kuziba nafasi za wazawa waondolewe.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira inayo dhamana kubwa ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata kazi na ajira zenye tija. Wizara hii ni lazima iandae sera mjarabu ambazo utekelezaji wake utawapatia fursa Watanzania kufurahia matunda ya uhuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha azma niliyoeleza hapo juu, napenda kuishauri Serikali kwamba Wizara ya Kazi na Ajira ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili watayariske mitaala ambayo itawapatia *Entrepreneurship Skills*, Watanzania waweze kujajiri wamalizapo masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wakipata ajira zenye tija kuna faida nyingi kwa Taifa letu. Kati ya faida hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali itaongeza mapato yake kwa njia ya kodi ambazo wafanyakazi wanapaswa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, familia zenye kipato cha uhakika zitatumia kipato kusomesha watoto wao lakini pia Watanzania kujivekeea akiba hivyo kuwa na *Social Security* ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kupunguza kwa wimbi la uhalifu linalotokana na vishawishi vya umaskini na hivyo kutafuta kukidhi mahitaji ya kijamii kwa njia zisizo halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa watoto wa kike wanapokuwa wana vipato vya uhakika hawatojiingiza kwenye vishawishi vya ukahaba ili kupata mapato ambayo mwisho wa siku huwapelekea kupata maambikizo ya maradhi yakiwemo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara hii isaidie kuanzishwa kwa Taasisi za Kifedha ambazo zitatoa mikopo kwa wananchi bila ya masharti magumu ili mikopo hiyo iwasaidie wajasiriamali waanzishe *SME's (Small and medium enterprises)* kwa lengo la kupanua wigo wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili dira ya Taifa ya 2025 na Mpango wa Maendeleo wa 2011/12 – 2015/2016 viweze kutekelezeka kwa ufasaha, ni lazima Wizara hii ijenge ajira za kutosha kwa kuweka sera mahsus ambazo zitasaidia sekta binafsi kustawi na kufanyakazi kama inavyotarajiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inahitaji kulifahamu ipasavyo tatizo la ajira na nguvu kazi iliyopo hapa nchini. Mipango yetu haiwezi kufanikiwa kama hatujui ukubwa wa tatizo la ajira.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Kazi na Ajira kwa namna nzuri ya uwasilishaji wa hotuba yake. Wizara iendelee na utaratibu wa kuongeza ajira na kusimamia sheria za nchi, mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Wizara kuchukua hatua zaidi katika sekta binafsi hasa wafanyakazi wa makampuni binafsi yakiwemo makampuni ya uchimbaji madini ambayo kwa kiwango kikubwa kuna unyanyasaji mkubwa, ubaguzi mahali pa kazi, matokeo yake wazawa wananyimwa haki za msingi, wananyimwa haki ya kuanzisha Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, progamu ya ukuzaji ajira nchini kama mtoa hoja alivyobainisha hasa kwa kuhamasisha uwekezaji katika uwezo wa kufufua fursa nydingi zaidi za ajira. Kuviimarisha ujenzi wa vyuo vya VETA na upanuzi wa vyuo vyenye kutoa mafunzo na matumizi ya teknolojia. Pia kukuza ajira kwa kuimarisha uwekezaji wa umma kwa kupitia Serikali kuu, Serikali za Mitaa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iendelee kuimarisha usimamizi wa taasisi zote zilizo chini yake. Vinginevyo Wizara hii itapunguza aibu yake machoni pa wafanyakazi na wafanyakazi watarajwa. Hata hivyo, Wizara pia iwe na wajibu wa kuwasimamia wafanyakazi kwa kupitia sheria ili nao watimize wajibu wao wa kuachana na masuala ya uvivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niyapongeze Mashirika ya Hifadhi ya Jamii (hasa hasa NSSF kwa mfano, wote tunawashukuru kwa kazi nzuri wanazozifanya nchi hii kwa kuwekeza katika mambo ya msingi mfano, miundombinu ya majengo ya Chuo cha UDOM).

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kuyataka mashirika ya namna ile ile ya NSSF, yaige mfano.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya sababu kubwa inayochangia kuwa kikwazo kwa vijana wanaomaliza Chuo Kikuu kukosa ajira hasa Serikalini, ni kigezo cha uzoefu kazini, lakini vijana hao kiuhalisia hakuna sehemu wanayoweza kupata uzoefu zaidi ya kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo pindi wanapokuwa chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kwamba huu ni muda muafaka wa kuondoa kipengele hicho cha uzoefu kazini ili vijana wengi wanapomaliza elimu ya juu waweze kuajiriwa bila kuwepo kikwazo hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya wageni wanaokuja hapa nchini kuwekeza, wamekuwa wakija na watu wao ambao wanafanya kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya, hivyo kukiuka taratibu za makubaliano, lakini pia kufanya Watanzania wasinufaice na uwekezaji huo kwa kukosa ajira au vibarua. Maeneo mengi yanayolalamikiwa ni Sekta ya Barabara, Makampuni ya Simu na Hoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi karibuni malalamiko yaliyotokeza dhahiri katika Kampuni ya Simu ya Zantel kwamba wageni wamekuwa wakifanya kazi ambazo Watanzania wana uwezo wa kuzifanya, mbali na baadhi yao kuendelea kuishi nchini bila kuwa na kibali.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja naipongeza pia Wizara kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ambayo ninaiomba Wizara kutilia umuhimu.

Mheshimiwa Naiu Spika, kwanza, kuna tatizo la viwanda vingi kutokuwa na mikataba na wafanyakazi. Hili ni tatizo kubwa sana, tunaiomba Wizara hii kufuatilia jambo hili kwa karibu.

Pili, ukaguzi wa maeneo ya kazi hasa viwanda, hapa pana tatizo kubwa sana, *OSHA* hawana vifaa au vitendea kazi vya kuwawezesha kukagua usalama mahali pa kazi, hivyo usalama kwa wafanyakazi kuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tubadilike, tusimamie kanuni za kazi. Umangimeza wa watendaji nao ni kikwazo kikubwa katika usimamizi wa kazi. Ahsante sana.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Gaudentia Kabaka – Waziri wa Kazi na Ajira, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Makongoro Mahanga, na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichangie kidogo kuhusu Wizara hii. Kwa kuwa ongezeko kubwa la ukosefu wa ajira linawahusu vijana na kwa kuwa wengi wanaishia Elimu ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa pendekezo kwamba Elimu yetu ya Msingi kwa wale ambao hatakwenda Kidato cha kwanza, wapate nafasi ya kusoma miaka miwili ya Ufundu ili wakimaliza iwe rahisi wao kuajiriwa au kujajiri wenyewe. Kwa kidato cha nne, wapewe mwaka mmoja wa madarasa ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatakiwa kuanzisha maonyesho ya kila mwaka ya kitaifa ya kazi za vijana ili kuibua vipaji vya Watanzania wale ambao wanafanya vizuri Serikali iwe inawapa msaada kuwapa moyo wa kujituma na hii itasaidia Serikali kuwatambua vijana ambao ndio nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajira nyingi kwa vijana hazitambuliki rasimu na Serikali, hivyo kupelekea vijana hao kunya yasika kwa kutopewa ajira, mfano Serikali yetu inaingiza pato kubwa la kodi kupitia pombe na bia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza, wauzaji wale au mawakala wa kukusanya kodi hiyo, yaani *Bar maids* hawana ajira wala mishahara. Sasa ifike mahali Serikali iseme au itoe kauli kuhusu hili la ajira. Je, wanajua hawa mawakala wa kukusanya kodi wanywaji wanalipwa shilingi ngapi? Pia ningependa kujuu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linatia uchungu ni hili suala la wageni ambao wamefika Tanzania hasa wengi wakiwa Raia wa Kichina. Sasa hivi wamekuwa wamachinga, wanauzu kadi, maua, *ice cream* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli sisi tukienda nchi nyingine tutapewa fursa hii? Ningombwa Wizara hii itoe fursa hiyo. Ningombwa Wizara ya Mambo ya Ndani wakomeshe hili ili Wizara wafanye kazi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii mara ngapi imeunda sehemu kama Magereza ambako ndiko kuna vijana ambao Wizara hii ikishirikiana na Magereza wangebuni mambo ya pamoja ya kuwasaidia vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yangekuwa ni Vyuo vya Mafunzo ili vijana wakimaliza vifungo vyao waweze kupatiwa mitaji wajajiri ili kubadili tabia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ajira ya vijana wanaofanya kazi za ndani, yaani *house girls* au *house boys*, ajira hii haina mikataba kati ya mwajiri na mwajiriwa. Kutokana na hilo, vijana wengi sana wananyanyasika. Ningombwa Serikali itoe kauli, pia kima cha chini kitambulike. Naunga mkono hoja.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa umahiri na uwasilishaji wake mzuri, lakini pia kwa utendaji wake makini. Hata hivyo, nampongeza Naibu Waziri kwa uwajibikaji na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Bajeti hii kujibu karibu kila eneo, naomba nami nichangie hapo kwa uchache. Lipo tatizo la ajira kwa wazawa ambaao wanabaguliwa bila sababu za msingi. Kimsingi, pamoja na ujuzi walionao, bado inaonekana haitoshi wao kupata nafasi za ajira katika maeneo hasa ya wawekezaji wa kigeni na hata wa hapa ndani ambaao wana asili ya nje ya nchi. Naitaka Serikali sasa ichukue hatua madhubuti ili kuthibiti hali hii ya unyanyasaji kwa raia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ajira lina uwiano sawa na lile la uvamizi wa wageni kwa visingizio tu nya ujuzi. Naitaka Serikali kwa kushirikiana na Taasisi zake, kwa mfano, Uhamiaji, *TIC*, *TCU* kuhakiki uhalisia wa ujuzi kwa watu hawa ambaao mara nyangi siyo kweli, wana ujuzi kuliko Watanzania. Ufanyike ufuatilaji wa vyeti vyao pia kwa maana ipo dhana kuwa wana -forge hivi. Katika ajira pia kuna tatizo kubwa sana la unyanyasaji wa hali ya juu kabisa katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ya watoto bado inasumbua sana katika nchi yetu, hasa ukizingatia lipo wimbi la watoto wengi wa Mitaani ambaao hawana namna ya kujitafutia maisha. Sheria zifuatwe kwa kuwabana wazazi au walezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro katika ajira imekuwa sugu sana kutokana utatuzi wake, inachukua muda mrefu sana katika mabaraza husika. Iwekke wazi sasa kwamba ni muda gani mashauri haya yanastahili kupata uamuzi? Wananchi wanakaa muda mrefu wakisubiri haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo la uwekezaji kwa kuwapa fursa wawekezaji kuamua nani wa kuajiri na kuweka mfumo mzima wa ajira. langaliwe upya sasa namna bora ya utatuzi na ufumbuzi wa kudumu. Mara zote wawekezaji wamekuwa wakandamizaji kwa wazawa. Tujiweke sawa, tupambane nao ili tuweze kuondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujira mdogo kwa waajiriwa, hasa viwandani linatia aibu kwa Taifa letu. Serikali isimamie kwa umakini zaidi sheria zilizopo kwa maana zinakiukwa bila sababu za msingi. Tuhakikishe kuwa waajiriwa wanapewa mikataba kwa kazi zao pamoja na elimu ili wajue haki zao za msingi, na waelimishwe umuhimu wa kuheshimu kazi na mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii adimu kumpongeza Mheshimiwa Gaudentia Mgosi Kabaka - Waziri wa Kazi na Ajira kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano kushika wadhifa wa Waziri wa Wizara hii. Ni ukweli ulio wazi kuwa Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kwa kumteua Mheshimiwa Kabaka kushika nafasi hii. Hii inajidhirishwa wazi kwa namna Mheshimiwa Kabaka anavyojitahidi kushughulikia migogoro ya wafanyakazi na kutafuta usuluhishi wa haraka wa migogoro hiyo. Hakika huyu mama anaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Kabaka – Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga - Naibu Waziri wa Kazi na Ajira pamoja na watendaji wote wakuu wa Wizara husika kwa kuandaa bajeti yao vizuri. Pia nawapongeza kwa umakini wao wa kuongoza Wizara, Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi natamka hadharani kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pamoja na shukrani hizo zote na kwa kuunga hoja mkono kwa asilimia zote, mchango wangu utajikita katika vipengele vifuatavyo:-

- Suala la Ajira mchini Tanzania;
- Suala la migogoro kazini;
- Suala la ukaguzi sehemu za kazi;
- Bodi za mishahara za kisekta;
- Fidia kwa wafanyakazi;

- Usalama mahali pa kazi;
- Ajira hatarishi kwa watoto;
- Programu ya kukuza ajira nchini;
- Ajira kwa vijana; na
- Suala la NSSF.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira nchini Tanzania linaweza kuwekwa kwa mitazamo tofauti. Kwanza, kuna ajira kwa wazawa. Pili, kuna ajira kwa wageni. Pia kuna vigezo vya elimu, ujuzi, uzoefu hata itikadi. Pamoja na mitazamo hiyo ya wazawa na wageni au vigezo vya elimu, ujuzi, uzoefu na itikadi, bado kuna tatzizo kubwa la ajira hapa nchini Tanzania. Binafsi, napenda zaidi kuangalia mtazamo wa kuajiri wageni hapa nchini Tanzania kwa visingizio kwamba wana uzoefu na ujuzi kuliko Watanzania. Aidha, kigezo cha lugha ya Kiingereza nacho huwa kikwazo kwa Watanzania kupata ajira. Naishauri Wizara kufanya ukaguzi wa kina katika viwanda, Taasisi na mashirika binafsi, katika migodi, na kadhalika ili kubaini ni Watanzania wangapi wameajiriwa katika sekta hizo pia linganisha na ajira kwa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio dhahiri kuwa viwanda vingi, hasa vya Wahindi na Waarabu kwa kiasi kikubwa huajiri wageni toka nchi zao na kuwaacha Watanzania wakitaabika kwa ugojwa uitwao "Ukosefu wa Ajira Nchini." Hii ni aibu kwa nchi yetu inayotimiza miaka 50 ya Uhuru. Tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Waziri wa Kazi na Ajira za kutatua migogoro kazini, bado ifahamike wazi kuwa kuna migogoro mikubwa katika sehemu za kazi. Kwanza kabisa, kuna unyanyasaji wa wazi wa kitabaka. Tabaka la viongozi au waajiri kuwanyanyasa watumishi/waajiriwa. Hali hii inathibitika katika viwanda, sehemu za migodi, katika Taasisi na hata Mashirika ya Umma. Ni vizuri ifahamike wazi kuwa migogoro inapozidi kazini, ufanisi wa kazi huwa ni mdogo sana. Ushauri wangu kwa Wizara husika ni kuongeza jitihada za kutatua migogoro kazini. Katika utatuzi wa migogoro hiyo, masuala ya uonevu, unyanyasaji, udhulumaj, ulaghai na mikataba isiyo na tija kwa wafanyakazi iangaliwe kwa umakini. Vitendo hivyo vya udhalilishaji na hata ubaguzi, vikomeshe mara moja. Wizara ihakikishe inajenga upendo, amani, umoja na mshikamano mahali pa kazi. Wizara ihakikishe kuwa mahali pa kazi hakuna chuki, fitina, uhasama na dhuluma. Tukiamua, tunaweza. Sasa tuamue.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza wizara kwa kufanya kaguzi 3,003 katika sehemu mbalimbali za kazi katika nchi nzima, lengo kuu la kaguzi hizi likiwa ni kutoa elimu ya sheria za kazi, ukiukwaji wa sheria, kuzuia migogoro pamoja na kuboresha mahusiano mema mahali pa kazi. Swali langu ni: Je, hadi sasa ni waajiri wangapi wameonekana wanakiuka sheria za kazi? Ni hatua zippi zimechukuliwa dhidi yao? Swali lingine: Je, Wizara imewahi kutembelea mgodi wa *North Mara* (Nyamongo) ulioko Wilayani Tarime kwa lengo la kuona ukiukwaji wa sheria za kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mishahara za Kisekta. Naipongeza Wizara kwa kulitambua hilo na kuamua kuunda Bodi kumi na mbili za mishahara za kisekta, katika fani za ujenzi, mawasiliano, shule binafsi, afya, maji, viwanda na biashara, ulinzi binafsi, majumbani, mahotelini, kilimo, usafirishaji pamoja na Sekta sugu ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie kwa makini suala la mishahara katika sekta zilizotajwa hapo juu na kuhakikisha kuwa kuna uwiano mzuri wa mishahara kati ya waajiriwa wageni na wale waajiriwa wazawa. Kwa ufupi ni kuwa, hadi sasa waajiriwa wazawa wanaonewa na kunyanyaswa katika sekta hizo. Tuzidi kufikiri zaidi, hasa katika Sekta ya Madini, Mahotelini, Ulinzi Binafsi, Viwanda na Biashara bila kusahau wafanyakazi wa majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza tena Wizara kwa kukamilisha waandaaji wa Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Act*) Na. 20 ya mwaka 2008 ambayo inakusudia kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi. Naishauri Wizara kusimamia utekelezaji wa mfuko huo. Mfuko huo uhakikishe wafanyakazi wanaoumia, wanaopata magonjwa, ajali na hata kufariki wakiwa kazini kuwa wanalipwa fidia halali na siyo kifuta jasho kama ilivyozoleka kuwa mtu akiumia au akifariki akiwa kazini anapewa kifuta jasho. Ondoa kifuta jasho, sasa weka fidia halali kwa yejote anayepata matatizo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kumpongeza Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Gaudentia Kabaka kwa juhudi za dhati anazoonesha kwa kupigania haki za wafanyakazi. Kwanza amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba kuna Bodi za Mishahara kisekta, kuna kaguzi sehemu za kazi, pia kuna fidia kwa wafanyakazi wanaopata matatizo mbalimbali wakiwa kazini. Kwa umakini huo huo, naiomba Wizara ihakikishe kuwa inashughulikia usalama na afya mahali pa kazi. Napenda kumwuliza Waziri: Je, usalama wa afya za wafanyakazi wazawa wanaofanya kazi katika viwanda mbalimbali nya Wahindi na Waarabu ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiuliza Wizara ya Kazi na Ajira, swali moja tu: Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ajira zinazotolewa kwa watoto wadogo ambazo zinawadhalilish? Hatua zipi zimechukuliwa katika Wilaya ya Tarime ili kukomesha hali hii? Elimu ya Kuzuia ajira kwa watoto itatolewa lini Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara, napenda kuikumbusha Wizara kuwa ni bora itilie mkazo kwa kujenga mazingira ya kujajiri kwa watu binafsi toka ngazi ya familia, Kijiji hadi Taifa. Kazi yoyote ile halali anayoifanya mtu binafsi ikiba inamwingizia kipato iwe ndio ajira yake. Kazi ya ukulima, ufugaji, uvuvi, biashara binafsi, na kadhalika ziwe ndizo ajira kwa wanaofanya kazi hizo. Kazi za ofisini au viwandani ziboreshw, lakini ifahamike wazi kuwa ajira isiyi rasmi hasa ya kilimo itasaidia kwa kiasi kikubwa kukuza ajira. Namwuliza Waziri, mradi wa kazi nje utaendeshwa lini Wilayani Tarime ili kuwasaidia vijana wengi wa Tarime wanaotaka kuwa wajasiriamali ili waweze kujajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Ajira kwa vijana, napendekeza kuwa Wizara ishawishi vijana wengi wafanye kazi za kujajiri. Lakini ili hayo yote yakamilike, naishauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili kuhakikisha kuwa Wizara hizi zinajenga Vyuo vya Ufundu (*VETA*) kwa kila Wilaya hapa nchini Tanzania. Pia, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vihusishwe kwa manufaa ya kutayarisha vijana ili waweze tayari kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza vijana wetu wapewe mafunzo ya namna ya kujajiri kwa kuwajengea mazingira mazuri ya kuendesha shughuli zao za kuwapatia kipato. Je, Waziri wa Wizara husika ana mpango gani wa kuwawezesha vijana wa Tarime kujajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napongeza juhudi zinazofanywa na Shirika la *NSSF* katika nchi ya Tanzania. Kwa ruhusa yako, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali yafuatayo:-

- Je, miradi inayofadhiliwa na *NSSF* inazinufaishaje Wilaya zilizo duni kimaendeleo kama vile Tarime?
- Ni utaratibu gani unaotumika kwa *NSSF* kutoa ufadhili kwa baadhi ya maeneo?
- Je Shirika la *NSSF*liko tayari kupokea maombi ya wana Tarime ya ufadhili wa miradi ya Maendeleo ya kijamii?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, narudia kumpongeza sana Waziri wa Wizara ya Kazi na Ajira kwa umakini wake wa kuiongoza Wizara. Pia naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wimbi kubwa la watu ambaa hawana ajira huko Mitaani, na hii inachangiwa na kuongezeka kwa idadi ya wahitimu kutoka vyuo mbalimbali wakati huo huo nafasi za ajira ni chache na haziongezeki kwa uwiano sawa na idadi ya wanaohitaji nafasi hizo. Kwa kuwa hili ni tatizo kubwa na lenye kuleta machungu kwa wananchi, namwomba Waziri anieleze, kama kuna mikakati iliyoifanywa ili kuongeza ajira kwa lengo la kutatta tatizo la ukosefu wa ajira, hasa ikizingatiwa kwamba ukosefu wa ajira huongeza kiwango cha uhalifu na mambo mengine mengi ya uvunjifu wa amani na sheria za nchi mbalimbali duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa kwamba nchi yetu ipo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na inajiaandaa kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati, hali ambayo itapelekea kuwepo na ushindani mkubwa sana katika soko la ajira. Hivyo basi, namwomba Waziri anieleze, ni kwa namna gani amewaandaa wanafunzi waliomaliza Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) ili wamudu ushindani katika soko la ajira, wakati huo huo hawana uzoefu na mbaya zaidi, hawana hata mafunzo kwa vitendo licha ya kwamba ilikuwa ni haki yao kwa Serikali kuwapatia mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na Mungu awabariki sana.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu ajira kwa vijana. Ni takriban zaidi ya vijana 700,000 watakaomiliza vyuo, lakini wanaotegemea kupata ajira siyo zaidi ya 40,000. Lakini pia pamekuwepo na matatizo ya vijana kupata ajira zaidi. Moja ya sababu ya kupata kazi, ni uzoefu usiopungua miaka mitatu mpaka mitano. Je, vijana hawa watapataje kazi ikiwa uzoefu utahitajiki? Je, Serikali haioni ni busara kuwasaidia vijana hawa kwa kutoa kigezo hicho cha uzoefu ili vijana hawa waweze kupata ajira? Je, kwa hao vijana waliobakia karibia 650,000 Serikali ina mikakati gani nao? La sivyo, tutakuwa tunajenga Taifa lenye wasomi, lakini wanaishia kuwa majambazi au kujingiza katika biashara chafu ya madawa ya kulevyta kitu ambacho siyo kizuri kwa Taifa letu. Je, Serikali haioni kuna kila sababu ya kuwawezesha vijana hawa kwa mafunzo ya ziada ili waweze kujajiri wenye kama ujasiriamali?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwepo na Vyama vya Wafanyakazi ambavyo husimamia maslahi na haki za wafanyakazi. Swali: Je, mwajiri anazo kinga gani? Kuna baadhi ya wafanyakazi huwa wanawanyanya sana waajiri wao: Je, Serikali inalijua hili hasa katika sekta binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wengi wamekuwa wakilipia *NSSF*, lakini ningependa kujua, kwa mfanyakazi anayelipia, anaweza kupata mkopo wa riba nafuu ili aweze kujenga nyumba ya bei nafuu ili afaidike na makato hayo? Ni kwa kiasi gani wananchi/wafanyakazi wanaolipia *NSSF* wanajulishwa pindi fedha zao zinapotumika kwa ajili ya miradi mbalimbali? Je, ni riba kiasi gani wanachama wanayopewa kwa faida zipatikanapo na miradi mingi mingi *NSSF* walioingia kwa niaba ya wanachama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya kazi nyingi tu zinafanywa na wageni kutoka nje na kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania, kwa mfano, kuna karakana nyngi sana za kichina zilizopo mjini. Unakuta kuna Wachina wanakuja nchini wanafanya kazi hata za kukwangua rangi magari. Siyo hilo tu, kuna *Supermarket* iliyopo Dar es Salaam *Shoppers Plaza* iliyopo *Old Bagamoyo Road*, unakuta kuna baadhi ya wafanyakazi kutoka Asia (Indian) ni walini, wanasi mama nyuma ya Till kulinda wasiibwi.

Swali: ni kweli hapa Tanzania hakuna wananchi wenyewe kuweza kufanya kazi hizo? Kwa mtindo huu vijana wetu watapata wapi kazi? Je wizara hii na wizara ya Mambo ya Ndani kitengo cha Uhamiaji kuna ushirikiano kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wanalinda ajira za wananchi wake? Hivi kuna Mtanzania anaweza kwenda India au China kufanya umachinga au kazi za kupiga rangi au kazi zisizohitaji ujuzi? Wakijulikana, *the next day* wanarudishwa Tanzania. Kwa nini hapa kwetu mambo ni tofauti?

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna waajiriwa wengi wa wafanyakazi wa majumbani hawatendewi haki, wananyanyaswa na kulipwa mshahara mdogo pamoja na kutokutumia mikataba kwa maelewano kwa wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kufanya utafiti juu ya tatizo hili na kufanya tathmini ili kujua ukubwa wa tatizo na kuipatia ufumbuzi thabitili ili kuweza kuondoa tatizo na kupelekeea wafanyakazi hao wa majumbani kufanya kazi zao kwa hali ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna tabia ya kuwafanyisha kazi watoto wadogo katika kazi ngumu za mashambani kama vile mashamba ya kahawa, miwa, pamba na kadhalika, waajiri wamefanya makosa makubwa kuwatumikisha watoto wadogo katika mashamba haya, jambo ambalo linatakiwa haki za watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kufanya utafiti juu ya jambo hili ili iweze kuchukua hatua zinazofaa kwa maana ya kuwanusuru watoto na tatizo hili na hasa tukitilia maanani kwamba watoto wana haki zao za msingi, wanawajibika kuzipata kama vile elimu, afya, muda wa kucheza na kulindwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu aliye niwezesha kuchangia bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka 2011/2012. Pia napenda kumpongeza Waziri kwa kuandaa bajeti hii iliyoingatia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Bajeti hii imemeanisha mipango ya kuratibu na kusimamia sheria za kazi mahali pa kazi, kusuluhiha migogoro ya kazi sehemu za kazi na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za Hifadhi za Jamii, na Fidia kwa Wafanyakazi, walioumia kazini, kuangalia shughuli za Vyama vya Wafanyakazi, Usalama na Afya ya Wafanyakazi, na majukumu mengine mengi ya kuongeza ajira na kuhakikisha wafanyakazi wanafanya kazi kufuatana na mikataba yao na mwajiri anatoa haki pamoja na mazingira mazuri ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuweka mipango mizuri na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kwa madhumuni ya kutoa haki na wajibu kwa wafanyakazi na waajiri ili kuongeza tija, ufanisi na uhusiano mwema katika sehemu za kazi, lakini bado kuna pengo kubwa kati ya haki wanayopewa wafanyakazi kutoka kwa waajiri wao. Wizara hii inatakiwa kuhakikisha wanakagua sehemu za kazi na kutoa miongozo kuona kwamba wafanyakazi wanalipwa mishahara kufuatana na sheria za viwango vya kima cha chini cha mishahara vinavyopangwa na Serikali, pia kuangalia mazingira ya kufanya kazi, uwiano wa mishahara na marupurupu kati ya wafanyakazi wa ngazi zote. Waajiri wahakikishe wanatumia sheria ya kazi katika kuadhibu au kuwarekebisha wafanyakazi wanaofanya makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajiri wengine ni wawekezaji wa nje ambao hawawezi kuelewana luga na wafanyakazi, pengine sheria na mazingira ya nchi walizotoka ni tofauti na mazingira na sheria za kazi za hapa nchini. Wengine ni wakorofi na wanafiki, kwa kuwa nchi yetu ni maskini, basi wafanyakazi inabidi wakubali kufanya kazi katika mazingira magumu. Mara nyangi utakuta kutokana na hali ya umaskini ya mfanyakazi inamlazimu kufanya kazi katika mazingira yoyote yale bila kulalamika kwa kuwa hana namna nyingine ya kupata ajira nyingine au anaogopa mamlaka. Hili ni tatizo kubwa sana linalowaumiza wafanyakazi hasa wa viwandani na migodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii kwa kushirikana na wadau mbalimbali wa Wizara nyingine zinazoshughulikia uwekezaji na biashara katika sekta mbalimbali, iwe Madini, Viwanda, Kilimo, Mifugo, Ujenzi na kadhalika, kupanga mikakati ya kuhakikisha wawekezaji hawa wanaelimishwa kuhusu sheria za kazi za hapa Tanzania na pia mara kwa mara wataalamu wa Wizara wawe wanaandaa semina kwa wafanyakazi na hasa viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi ili watambue haki na wajibu katika ajira zao na namna ya kuwakilisha wafanyakazi wenzao kwa kutenda haki pande zote. Kwa kufanya hivi kutapunguza migogoro ya kazi kati ya wafanyakazi na waajiri ambayo hayaleti tija. Mwekezaji atavutiwa kuwekeza katika nchi ambayo anaona wafanyakazi wake wanafuata taratibu za kazi, kuna amani na utilivu. Vinginevyo hawezikuchukua hatua zitakazohatarisha mtaji wake na mali zake. Hayo mazingira ya amani kazini ni kigezo kimoja kitakachoongeza ajira na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana ukipita Mikoani na kuangalia Ofisi za Watendaji wa Wizara na hasa Ofisi za Kazi majengo yake ni ya kizamani sana, mengi yana ufa, hayapakwi rangi, hakuna vyoo na mengine hata ndani *ceilingboard* zimeliwa na panya na siyo jambo la kushangaza unapopishana na panya anakimbiza kipande cha karatasi kinachotoka katika jalada la mashauri yanayoshughulikiwa. Mifano michache ni ofisi ya Kazi ya Mkoa wa hapa hapa Dodoma, Kilimanjaro, Shinyanga, Ifakara Morogoro, Kigoma na kadhalika. Aidha, vyumba vya kutunza mafaili viko katika hali mbaya kiasi kwamba kupata faili la shauri liloahirishwa baada ya mwezi mmoja ni shughuli kubwa. Naomba sana majengo haya yapewe kipaumbele, yakarabatiwe na kuwa katika hali nzuri na mfano kwa waajiri wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mazingira ya kufanya kazi kwa maofisa wanaosimamia mashauri ya migogoro ya wafanyakazi na waajiri ni magumu sana. Katika Ofisi za Kazi hakuna vitendea kazi kama kompyuta, magari, kalamu, makaratasi na mafaili ambavyo ni vitu muhimu sana kwa wafanyakazi. Hali ni mbaya sana kwa ofisi ya Tabora ambayo mpaka sasa wanatumia *typewriter* kuandika muhtasari ya mashauri. Pia kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi na mfumo pia ni mbaya. Kwa mfano, Ofisi ya Morogoro na Tabora ambapo mhudumu/*messenger* ndiye mlinzi wa ofisi. Sasa mfanyakazi huyu analipwa mshahara kufuatia vigezo vipi? Kila kazi ina majukumu yake na hasa ulinzi ni kazi inayohitaji mtu acae macho kulinda mazingira ya usalama wa ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, haki na wajibu havipo, japo ndiyo mamlaka ambayo inadhamana ya kusimamia. Ikumbukwe kwamba, maofisa wa kazi wana wajibu wa kwenda kukagua mazingira ya kufanya kazi katika sehemu mbalimblai vikiwemo viwanda na maofisi. Je, kama hali za kufanya kazi maofisini mwao ni duni kiasi hiki na hazifuati sheria, kweli wataweza kuchanganua mazingira mazuri ya kufanya kazi na mazingira duni ya kufanya kazi? Je wataweza kuwaita waajiri ambao wamekiuka amri ya kuwawekea wafanyakazi wao mazingira mazuri ya kufanya kazi wakati wao kitu cha kukalia kimeliwa na panya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa ajira hapa nchini ni tatizo kwa karne hii. Vijana wetu wanaomaliza Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Sita na hata wahitimu wa Vyuo Vikuu mbalimbali hapa nchini ni tatizo kupata kazi. Hata pale soko huru linapotangaza nafasi za kazi wanaweka sharti la uzoefu wa miaka kadhaa. Masharti haya hayawapi nafasi vijana hawa kujaribu katika ushindani wa kupata kazi, kwani hata wakiandika barua za kuomba kazi zinawekwa pembeni kwa kigezo cha kukosa sifa. Katika mikakati ya kuzalisha ajira mpya, vijana hawa wamejikuta pia hawawezi kuajiriwa wala kujajiri kwa kukosa sifa ya uzoefu, stadi mbalimbali, mitaji na dhamana za kupatia mikopo. Nashauri Wizara ijitahidi kuhakikisha Vyuo vya Stadi vinachukua vijana hawa kuwapa mafunzo ya stadi za kuwasaidia kujajiri wenyewe. Katika mikakati hii ni pamoa na kuanzisha mfuko wa dhamana wa mikopo kwa vijana kama ilivyo kwa wanawake wajasiriamali wadogo ili kuwawezesha kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ni warithi wetu au kwa maana nyiningine, ni Taifa la kesho na wana majukumu ya kuendeleza kizazi hadi kizazi. Endapo wataachwa bila kujengewa uwezo na mazingira ya maendeleo, tutakuwa tunazalisha Taifa la umaskini uliokithiri zaidi, kwani wengi wao kwa sasa hivi wanaondoka vijijini kwenda katika miji mikubwa kutafuta ajira na wanapokuta hali ni mbaya hakuna ajira anajjingiza katika vitendo vya ujambazi, uzururaji, na madawa ya kulevyo. Hii ni kwa sababu ya kukata tamaa ya maisha.

Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijiini walio wengi, hali zao ni duni na wanajitahidi sana kufanya shughuli ndogo za ujasiriamali, lakini wanakumbana na vikwazo vya kutoweza kuandaa bidhaa zao na ukosefu wa soko na mbinu za biashara. Aidha, sehemu za kuajiriwa ni ndogo, kwani Jimbo ni changa. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa roho ya imani aangalie jinsi ya kusaidia wananchi hawa. Kwa kuhakikisha mfuko wa dhamana na mikopo kwa jina la mamilioni ya JK zinawafikia, kwani wanawenza kukopeshana kwa sababu wengi wao ni wakulima na wafugaji na wanajitahidi sana katika shughuli hizo. Wakiwezesha, wanawenza kujihusisha na biashara ndogo ndogo, ufugaji wa kuku, nyuki, ufundu seremala, uchongaji wa vinyago, usukaji wa ukili, ufugaji wa samaki, uchomaji matofali kwa ujenzi wa nyumba bora, kilimo cha bustani za mboga, ushonaji wa nguo na kadhalika.

Pia naomba kuwe na mipango ya kutoa mafunzo kwa vijana ili nao waweze kujijendeleza na kuwa katika soko la ajira pamoja na kujajiri wenyewe. Serikali itakapopata wafadhili wa kusaidia vijana, naomba wakumbuke Jimbo la Kibaha Vijiji katika kuwajengea Chuo cha Ufundu na Stadi za Mikono ili kuwawezesha nao kupata ujuzi wa kujajiri na kuchangia kikamilifu katika uchumi na shughuli za maendeleo. Naunga mkono hoja.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Kazi na Ajira, ishirikiane kwa ukaribu sana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuhakikisha kwamba miradi ya Liganga na Mchuchuma inaendelezwa. Kuendelezwa kwa Miradi ya Liganga na Mchuchuma kutotoa ajira tele kwa vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi ishirikiane kwa karibu na iihamasishe Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha viwanda vya chuma vinajengwa Ludewa ili vijana wa Tanzania wapewe ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaisihi sana Wizara ya Kazi ishirikiane na Wizara nydingine ili kuhakikisha ajira nyingi zinapatikana kwa vijana wetu.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri na ninampongeza Waziri, Naibu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi nzuri ilizozifanya na inazoendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Waziri Kabaka kwa kuweka utulivu, maelewano na kupunguza migogoro katika Vyama vya Wafanyakazi tofauti na hali ilivyokuwa huko nyuma. Hii inajidhihirisha kuwa yapo maelewano kati ya Serikali na wafanyakazi hali iliyopeleke Mheshimiwa Rais kualikwa kwenye Sherehe za Mei Mosi zilizofanyika Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na ninaomba mazungumzo ya mara kwa mara yawe yanafanyika ili kupunguza kama siyo kuondoa migogoro na maandamano ya wafanyakazi kwenye vyama vyao. Madai ya walimu na wengine yanayodaiwa yahakikiwe haraka na utaratibu wa kulipa ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza *NSSF* kwa kulipa mafao ya wafanyakazi kwa muda, tofauti na miaka ya nyuma ambapo ndani ya Bunge, kila Mkutano wa Bunge yalikuwa hayakosekani maswali yaliyokuwa yanaihusu *NSSF* za malalamiko, lakini siyo tu Bungeni hata kwenye Vyombo vya Habari (magazeti) ambapo kwenye ukurasa wa maoni ya msomaji mara kwa mara *NSSF* ilikuwa ikilalamikiwa kwa huduma isiyoridhisha na ucheleweshwaji wa kulipa mafao. Endeleeni kuboresha zaidi huduma ili mwendelee kuwa kioo safi cha Mfuko wa Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri, kuangalia utaratibu wa mifuko kuiunganisha kama mamlaka ya usimamizi wa udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Hii itasaidia kuondoa mkanganyiko kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie wafanyakazi viwandani. Nashauri Idara ya Ukaguzi katika viwanda ufanyike mara kwa mara ili kuona na kushauri uongozi namna bora ya kuwalinda wafanyakazi hasa wanaofanya kazi kwenye viwanda vinavyotoa kemikali kali. Uongozi wa baadhi ya viwanda imekuwa haiwapi wafanyakazi "vizuia" *gloves, mask, gumboot*, maziwa na kadhalika lakini mazingira wanayofanya kazi hayaridhishi kwa baadhi ya viwanda, wafanyakazi wanatumikisha kama siyo binadamu. Hivyo, naomba sana Idara hii ifanye kazi yake kama ilivyokuwa zamani kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi cha *TUICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kwa kusema, nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi, hivyo Wizara hii ndiyo mhimili mkubwa wa kusimamia wafanyakazi wote nchini. Wizara muda wote ishirikiane na Chama cha Wafanyakazi nchini TUCTA ili kuondoa migogoro ya wafanyakazi nchini. Migogoro haijengi, inaharibu sifa ya nchi. Najua umahiri wa Waziri kwa kushirikiana na Naibu wake kwa pamoja na Katibu Mkuu ndugu Shitindi, ni watu makini. Utatu ukitumika vizuri, utaondoa migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kutoa maoni yangu kwa Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ambayo ni mionganini mwa Wizara mama. Ni tegemeo la ujenzi na maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote ambayo haina kazi na ajira kwa wananchi wake itabaki kuwa duni, isiyo na mwelekeo, yenye matukio mabaya ya uporaji, wizi na hata ujambazi wa kutumia silaha, jambo ambalo huhatarisha maisha ya raia wake. Nchi ambayo haina kazi na ajira mara nyingi hukabiliwa na majanga kama vile njaa, maradhi na utapiamlo; hukabiliwa na umaskini wa kutisha, hubakia kuwa Taifa la omboomba na hujikita katika kutumia vyombo vyadola katika kuijwekeea madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina maeneo mengi ya kazi na ajira. Hata hivyo, kazi na ajira zilizopo katika nchi yetu hazitoshii na maeneo mengi ya kazi hizo hakuna tija na hatimaye hata hiyo kazi ya kijungujiko haipatikani kutokana na maeneo hayo ya kazi, hayatoi tija.

Mheshimiwa Spika, kuna majanga na maafa mengi yanayojitekeza katika maeneo ya kazi ambayo wananchi huwa wanajajiri wenyewe, kwa mfano, maafa yaliyotokea katika machimbo ya Mererani, *MV Bukoba*, *MV Kabul* iliyotokea Tanga kuelekea Pemba na kwa sababu hakuna utaratibu wa kuwawekeea Watanzania hawa Bima ya Maisha, hatimaye watu wetu wanajituma kutufuta maisha yao, lakini lilitokeea la kutokea, hakuna fidia yoyote wanayopatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wa Tanzania wanamaliza masomo yao, lakini kutokana na ukosefu wa ajira Serikalini huishia kufanya biashara za kutembeza maji, *juice* na biskuti barabarani jambo ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya nchi yetu, kupoteza raslimali ya vijana ambaa wangeweza kulinyanyua Taifa kiuzalishaji, kielimu na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Waheshimiwa Wabunge hupiga kelele na kusema kwamba maeneo mengi ya Mikoa yetu na wilaya zetu hususan vijiji, hakuna walimu wa kufundisha watoto wetu mashulenii na mara nyingi shule nzima inaweza ikawa na mwali mu mmoja. Je, ile ahadi ya Serikali kuweza kunyanya viwango vya elimu kwa Watanzania ni kwa maeneo maalum, mijini tu? Serikali kuwakosesha uwezo wa kujipatia maendeleo Watanzania walioko vijiji kwa kupata ajira kutokana na kukosa elimu: Je, siyo kuwabagua? Je, siyo kuwakosesha haki zao kama Watanzania wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania bado ina upungufu mkubwa wa ajira kutokana na kwamba kuna uchache wa viwanda, mashirika na hata ajira za Serikali. Kwa upande mwingine wawekezaji wa viwanda, mashirika na makampuni mara nyingi huajiri watu au vijana kutoka katika nchi zao wanazotoka na hivyo kuwakosesha vijana wa kitanzania ajira wakati katika nchi zao ajira hazitolewi kwa wageni, lakini Serikali ya Tanzania imekaa kimya kama haipo. Kuna mahoteli ambayo hata kuchemsha yai, mchemshaji anatoka nje. Mfano, *White Sand Hotel* iliyoko nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, *Pearl Hotel* iliyopo jijini Dar es Salaam kwa sasa. Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba kazi za ajira zinapatiwa Watanzania wazawa na siyo wageni?

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Wizara hii mambo makubwa mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu wafanyakazi wa Mtibwa wamekuwa na tatizo la kucheleweshewa mishahara. Wastaafu wanadai mafao yao hasa michango yao ya *PPF* ambayo haikuwasilishwa na mwajiri. Wizara inatoa tamko gani juu ya tatizo hili la kucheleweshewa mishahara na mafao yao kutolipwa na michango yao ya *PPF*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Wafanyakazi *TRAUWU* kwa muda mrefu kimekataliwa na Kiwanda kuingia mkataba wa hiari. Hili ni tatizo, linapelekeea wafanyakazi kulipwa stahili zao likiwemo mishahara midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Menejimenti imepunguza wafanyakazi zaidi ya 2000 kutoka katika ajira ya msimu ambapo walikuwa wakilipwa mishahara na michango yao ya *NSF*, hivi sasa wanawekwa vibarua wiki tatu tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itoe tamko, matatizo haya ya wafanyakazi yatashughulikiwa lini? Kwa kuwa Waziri wa Kilimo na Chakula ameahidi kwenda Kiwanda cha Mtibwa kuongea na wafanyakazi, Menejimenti na wadau wa miwa: Je, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii haioni umuhimu kwamba kuna haja pia ya kufika Mtibwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu. Naunga mkono hoja.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika siku ya leo katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na nawatakia kheri Waislam wote wanaofunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kuwasilisha bajeti yao na pia kwa utekelezaji mzuri wa kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi Serikali imejipanga kwa kutengeneza ajira kwa vijana/wanawake walioko vijijini kwa kushirikiana na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na *VETA* ili kupata vijana ambao watakuwa na taaluma yenye vyeti? Ni vipi Serikali itawezesha vikundi (*resources*) viajiri kwa kuangalia Wilaya/Kijiji kina raslimali gani za kutosha? Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuyathamini mashirika ya hifadhi ya jamii na kuwapa kazi mbalimbali za ujenzi wa maendeleo ya nchi hii. Nchi nyingi duniani zinayashirikisha mashirika ya hifadhi ya jamii kuendesha miradi ya umeme, barabara na kadhalika. Hivyo Mheshimiwa Rais hajakosea, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Shirika la *NSF* kwa kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais na kujenga majengo mbalimbali ikiwa vitega uchumi, Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho ni chuo pekee Afrika Mashariki na hata Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali na *NSF* kwa ujenzi wa Daraja la Kigamboni, tunaoutarajia kuanza mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama Malaysia, imetoa nafasi kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii kuendesha miradi wa umeme na wamefanikiwa. Hivyo basi, kwa kuwa *NSF* imeomba na uwezo wanao na kwa kuwa Serikali ina kila sababu ya kuwapa *NSF* mradi wa umeme wa gesi ambao ni wa uhakika (kuliko kutegemea maji/mafuta). Je, Serikali imeweka utaratibu upi (*time frame*) kuanzia kwa mradi huu ili usichelewe? Kwani tatizo la umeme ni kubwa sana nchini na hali hiyo ikiendelea, uchumi wa nchi yetu utadorora sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipatiwe majibu, ni vipi Serikali ilivyojipanga na ni lini *NSF* wataanza mradi huo? Naomba majibu kwani tumeona jinsi gani mradi wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni ulivyojukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya dhahabu kwa sasa ni dola 1600 kwa *ounce* moja. Wakati Makampuni ya dhahabu walivyoanza uchimbaji wa dhahabu ilikuwa dola 250. Mishahara ya Watanzania toka miaka hiyo bado ni midogo, Wizara inachukua hatua gani? Kwanini wawekezaji wasipewe *rate* za mishahara na Serikali? Kama hawaweki waondoke. Mbona sheria hii nchi nyingine wawekezaji wanazifuata?

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya. Hata hivyo, ninayo machache ya kuchangia na kuboresha hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) umepokea michango mbalimbali ya watumishi na waajiri wao kwa ajili ya kutoa mafao ya uzeeni (*pension*). *Pension* hii hutolewa mara baada ya mtu kuzeeka na fedha (akiba) yake inakuwa tayari imeshaharibika na kukosa thamani kutokana na mfuko wa bei. Riba inayotolewa ya kati ya 2% - 3% ni kidogo sana ukilinganisha na riba nzuri au nafuu ya 5% - 7% inayotolewa na mfuko wa *LAPF* (*Local Authority Provident Fund*). Kwa maana hii, watumishi wote waliojunga na *NSSF* wananyonywa sana. Nashauri sheria na kanuni za *NSSF* zibadilishwe haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imejipanga kusomesha vijana kuanzia Shule ya Msingi hadi Vyuo Vikuu. Vijana wetu hawa wanaomiliza vyuo, wengi wao hawana ajira na kwa kuwa elimu ni lazima iwekwe kwenye maarifa, vinginevyo elimu itapoteza maana. Ni kwa nini Serikali isijipange vizuri na kuwatafutia ajira vijana wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi hizi za kisekta ziliundwa kisheria ili zisimamie kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Madini, hoteli, majumbani, viwandani na kadhalika. Bodи hizi zilizinduliu na aliyekuwa Waziri wa Kazi wa wakati ule Mheshimiwa Zephania Chiligati na Bodи hizo zilifanya kazi kwa kipindi cha mwezi mmoja tu. Baada ya hapо, hazijaweza kufanya kazi tena. Kwa kuwa Bodи hizo tayari zilishapendekeza kima cha chini cha mishahara, lakini Bodи hazikujulishwa kama mapendekezo haya yalikubaliwa na Serikali. Je, Bodи hizo zilishamaliza muda wake? Kama zimemaliza muda wake, ni lini zitajulishwa kwa maandishi na kupewa marupurupu yao, yaani (*Directors fees*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa limefanya kazi nzuri sana ya kujenga nyumba na kuziua. Ombi langu ni kwamba shirika hili llongeze kasi na liende Mikoani na Wilayani. Nyumba za kuuza ziwepo muda wote ili mtu anunue Mara apatapo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi kujenga jengo la Machninga *complex*, lakini hadi sasa tunashuhudia Machininga wengi wakitembeza bidhaa zao Mitaani. Mojawapo ya sababu za wamanchinga kurandaranda ni kutokana na kukosa nafasi katika jengo la machininga *complex*. Ni kwanini wamachinga hawana nafasi katika jengo lao na kama zipo, ni kwanini hawaendi huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wachina kufanya biashara Kariakoo limepigiwa kelele siku nyingi, na Serikali iliahidi kulifanya kazi suala hili, lakini hadi sasa hatuoni lolote liliofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kupongeza kazi zinazofanywa na Waziri na Naibu Waziri katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Naomba yafuatayo yafanyiwe kazi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kigezo cha uzoefu kwa maeneo mbalimbali ya kada za kazi kiweze kutolewa isipokuwa kazi maalum za kimenejimenti ambazo zinahitaji uzoefu maalum. Jambo hili litawasaidia sana vijana wetu wanaomiliza vyuo kupata ajira na hivyo kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashirika ya kimataifa na makampuni mbalimbali hapa nchini ambayo yanatumia wafanyakazi wa kutoka nchi za nje wakati watu wenye sifa kama hizo wapo hapa nchini. Kuna mashirika ya kimataifa ambayo kwa nafasi ya menejimenti huwa wanatumia wageni pekee. Hii haikubaliki hata kidogo, kwani jambo hili linakatisha tamaa wataalam wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana wetu wengi ni tatizo kubwa na wengi wao wanabangaiza kwa kuuza vitu ambavyo havina tija wala thamani ambavyo vingi vyao vinaingizwa kutoka nje ya nchi. Sasa suluhisho ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu wakiwa tayari kuwa wajasiriamali, basi mabenki yakubaliane, wapatiwe mikopo ya riba nafuu (au hata isiwe na riba) ili waanze kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi mahsusizi zifanyike kuwakusanya wale wanaotembeza vifaa duni kwenye makutano ya barabara (wamanchinga) ili waweze kuwa wabunifu, watengenezaji na wachuuzi wa bidhaa zao wenyewe na pia mabenki yahamasishwe kuwapatia mikopo nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Tanga Mjini kuna vikundi vya vijana mbalimbali ambavyo tayari wanajishughulisha na mambo mbalimbali. Je, Wizara ina mipango gani yakuvisaidia vikundi kama hivi ili viweze kupata mitaji ya kuendelezea shughuli za vikundi hivyo na kama vile cha *cockcraft*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BENARDETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara, Waziri na Watendaji kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni kati ya nchi zinazosomesha vijana wengi sana katika Shule za Sekondari na Vyuo Vikuu. Wengi wao ni vijana, na wakimaliza hawapati ajira ya Serikali. Ninatambua kuwa Serikali haina uwezo wa kuajiri wahitimu wote. Wengine wataajiriwa kwa kuwa Wizara yako inatambua kuwa wahitimu wamezalishwa wengi sana kuititia mpango mikubwa sana ndani ya Wizara ya Elimu, ikiwemo MMEM, MMES na mpango wa maendeleo ya elimu ya juu. Hivyo, kwa kutumia utaratibu wa kawaida, siyo rahisi kuwaajiri. Je, Wizara haioni kuna haja ya kuweka mikakati/mipango mikubwa na ya kuzalisha ajira ili kupunguza wimbi hili kubwa la wasomi? Nasema ni lini Wizara nayo itakuwa na mipango mikubwa kama MMEM na MMES ya kuzalisha ajira? Kama ipo, ni ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kagera kuna vijana wengi waliohitimu Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo, lakini hawana kazi. Hawa wanakosa mambo mawili, elimu ya ujasiriamali na vifaa vya kuanzia na mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi na Ajira imejipangaje kuwasaidia hawa? Je, tutazalisha wimbi la wazururaji na vibaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa elimu wa Tanzania unawaandaa wanafunzi wote, kana kwamba wote wataendelea na Elimu ya Upili na Vyuo Vikuu. Inawasahau wanaoishia Darasa la Saba, *Form IV* na *Form VI*. Utaratibu uliokuwepo wa kuwafundisha stadi za kazi, kilimo, biashara, Sayansikimu, upigaji chapa, ujasiliamali na kadhalika, masomo ambayo yangemtayarisha mhitimu ambaye haendelei na elimu ya juu, ili stadi hizi zimwezeshe kujajiri: Je, kuna mipango gani kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuhakikisha mitaala inawezesha haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kabisa, napenda kufahamu tatizo la ajira kwa watu wenye ulemavu. Ni la muda mrefu: Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hilo tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia ya watu wenye ulemavu wenye ajira ni 0.7%: Je, Serikali inasema nini kuhusiana na asilimia hii kwa kuwa ipo chini sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa umezuka mtindo wa baadhi ya wawekezaji hapa nchini, kutoa ajira kwa wageni katika kazi ambazo nyngi zingeweza kufanywa na Watanzania. Limekuwa jambo la kawaida sasa kuona katika mahoteli, kazi kama za ulinzi, upishi, wahudumu zikifanywa na raia kutoka nje ya nchi, kwa vyovoyote huu ni ukiukaji wa sheria amba Serikali haina budi kuchukua hatua stahiki kwa manufaa na ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara, marupurupu na mafao ya wastaifu katika sekta binafsi, ni kilio kikubwa sana kwa wananchi. Makampuni mengi hapa nchini yanawatumikisha wafanyakazi kupita kiasi, lakini hata hivyo, kiwango cha stahili zao ni chini kuliko kima cha chini kilichowekwa na Serikali. Pia hayachangii katika mashirika ya pensheni. Serikali haina budi kuwabana ili watekeleze sheria ya mikataba ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuoanisha mafao ya wastaifu kwa taasisi zote kuwa na *formula* moja ya malipo sawa. Rais aliagiza Wizara ya Kazi pamoja na *Regulator*, miaka ya sasa yapata minne kufanya kazi mafao ya wastaifu kwa kuhusisha Taasisi za *PPF*, *PSPF*, *LAPF*, *NSSF* na kadhalika. Kupata *formula* moja itakayolipa mafao sawa kwa wastaifu wote. Pia Rais alirudia hili agizo katika Sherehe za Mei Mosi mwaka huu ili mchakato huu uharakishwe na utumike mara moja.

Sambamba na hili, Rais aligiza pia Tume hiyo iangalie upya mafao ya wazee walistaifu yarekebishwe ili yaendane na hali halisi ya gherama za sasa za maisha za Mtanzania aliysteaifu. Ni vizuri sasa wananchi wakalelewa wazi, kwani ni muda mrefu kuwa amewadanganya wastaifu na wanaotarajia kustaifu. Tunaomba Waziri kwa faida ya bajeti hii atoe tamko sahihi, ni lini hayo marekebiso yatarekebishwa ili kuleta matumanini kwa wastaaifu wote?

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudzi zake za kutengeneza ajira kwa vijana, lakini pia kwa kuongeza ajira kwa wanawake kiasi cha kufikia asilimia 36 ya wanawake wenye nafasi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iendelee kubuni mikakati ya kuwapatia ajira vijana. Idadi ya vijana nchini ni kubwa. Kutokuwa na ajira ni athari kubwa hasa kwa Serikali ya Chama kinachotawala (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iwe na mkakati thabitii wa kuhakikisha kuwa vijana wengi wanajunga na *VETA* ili kupata ustadi wa kuweza kuajiri (haja ya kuwa na mazungumzo na Wizara husika, mfano, Wizara ya Elimu) ili uwepo mkakati thabitii wa kutangaza nafasi za masomo *VETA* na pengine Wizara ya Kazi iande namna ya kuwajulisha vijana kwa vile sio wote wanasona magazeti na sio wote wanaangalia *television*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *information is power*. Ziko nafasi nyngi zinatangazwa na *international organizations*, mfano Shirika la Ndege la *Emirates*, *Qatar* na kadhalika wanatangaza kazi na Wakenya wengi wanafanya kazi katika mashirika hayo. Mimi nilishuhudia mwenyewe *Qater Airline*, *Dar es Salaam* kwenye ndege hata ofisi zao *DOHA*. Nilipouliza, waliniambia nafasi zinatangazwa katika *internet*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wakati wa Ajira (*employment Agents* wa Wizara) waangalie nafasi hizo na kuwatangazia Watanzania ili nao wajipatie ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania imejiunga na Soko la Afrika Mashariki. Ajira zitakuwepo katika nchi zote za Jumuiya hii. Iko haja wakala wa ajira awaandae Watanzania, vijana wa Kitanzania ili nao washindane katika mchakato wa kupata ajira katika nchi za Afrika mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia sita ya *Development Skills* inayotozwa na Serikali kwa kila mwajiri mwenye zaidi ya wafanyakazi wanne, ina-discourage ajira *the more staff one has, the more he/she pays*. Iko haja Serikali ipunguze asilimia sita, angalau iwe asilimia tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako *labour officers* Mikoani ambao wanaripoti kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Kazi. *Labour Officer* anatoa taarifa kuwa *RAS*. Migogoro ni mingi, lakini hakuna mahusiano ya *Labour Officers* wa Ofisi ya *RC*. Nashauri Serikali ipitie upya sheria hii ili *labour officer* aliyeko Mkoani aripoti kwa *RAS*, na hivyo *RAS* atawenza kushughulikia matatizo ya ajira na kuishauri Wizara. Uzoefu unaonyesha Serikali haiwezi kushughulikia migogoro hiyo, ni mingi, na Katibu Mkuu yuko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iliamua kupeleka madaraka Mikoani ili wananchi waweze kupanga na kuamua kirahisi mambo yao ya maendeleo yaani “*D by D*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha madaraka hayo Wilayani hasa kwa upande wa ajira kwa maana kwamba Kurugenzi husika zifanya kazi hiyo hasa kwa ajira za kada ya chini na kat?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha suala la jinsi katika ajira linatafutiwa ufumbuzi? Kwani kumekuwa na malalamiko na upendeleo katika ajira hasa kwa nafasi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko katika baadhi ya Taasisi hasa za Elimu ya Juu kwamba ajira nyingi zimekuwa zikitolewa kwa undugu (*undugunization*) urafiki na upendeleo bila kuzingatia vigezo husika. Je, Serikali inasemaje kuhusu hill? Je, Serikali ina mikakati ipi ili kupambana na hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaangalia vipi suala la vijana kuhusu ajira? Serikali ina mpango gani sasa kuweza kuwasaidia vijana hasa wale wenye elimu ya chini na kat ili waweze kujajiri na kuweza kuondokana na umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inasema nini kuhusu wimbi la Wachina waliopo Dar es Salaam wanaofanya shughuli za umachinga kwani fursa hizo ni za Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Sasa nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri, Kazi na Ajira. Mheshimiwa Dokta Milton Makongoro Mahanga. Karibu sana Mheshimiwa, una dakika 20. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia uhai na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. Nikushukuru sana wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Kazi na Ajira na niseme toka awali kabisa kwamba naunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kiniamini na kunituea kuwa Naibu Waziri, kwa miaka sita sasa. Kwanza kama Naibu Waziri wa Miundombinu kwa miaka miwili na nusu na baadaye katika Wizara hii ya Kazi na Ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Mawaziri wote wanne niliofanyanao kazi katika Wizara hizi mbili, kwa kunijenga kiuwezo na kiuzoefu. Nimshukuru sana Waziri wangu wa sasa, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, ambaye amenipa ushirikiano mkubwa sana katika majukumu yangu ya kumsaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Segerea, kwa kunichagua kwa mara ya tatu mfululizo mwaka jana, kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu na katika kusaidiana nao kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Katika miaka zaidi ya 10 tuliyofanya kazi pamoja, karibu kila mtu anayepita katika Jimbo la

Segerea, analionea gere Jimbo letu kwa mafanikio makubwa na maendeleo na hasa katika sekta za miundombinu na elimu. Nataka niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Segerea kwamba baada ya juhudhi kubwa tulizofanya mwaka jana kuligawa Jimbo la Ukonga na sasa kuwa na Jimbo dogo kiasi la Segerea na kwa mipango mizuri iliyopangwa na Serikali, maendeleo makubwa katika Jimbo la Segerea katika miaka mitano ijayo sasa yatakuwa kama kumsukuma mlevi na hasa katika kero sugu za maji, miundombinu na kupunguza umaskini hasa wa akinamama na vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu katika kuhitimisha shukrani zangu, nataka niishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa Florence, watoto wangu na wajukuu zangu kwa kuendelea kunipa moyo na kunivumilia katika kutimiza majukumu yangu ya kikazi. Kwa kweli miaka 33 ya ndoa na Florence, yeye na mimi bado tunadai kama mnavyoona bado vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo sasa naomba nichangie kidogo katika hoja hii huku nikjaribu kujibu na kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, hoja nyininge zikiwemo za kisera, atakuja kujibu Mheshimiwa Waziri. Aidha, tunaahidi kutolea majibu kwa maandishi, hoja zote zilizotolewa na Wabunge, pamoja na zile ambazo hatutapata muda wa kuzijibu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nianze kwa kueleza masuala yanayohusiana na Hifadhi ya Jamii. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la pensheni kwa wazee wakiwemo Mheshimiwa Mtutura Mtutura, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Dokta Antony Mbassa, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye na wengine wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikubaliane nao kwamba umuhimu wa pensheni ya wazee ni suala ambalo hata Serikali sasa imeona kuna umuhimu wake na nieleze tu kwamba suala hili limekuwa likifanyiwa kazi na Serikali kwa muda sasa na kwa sasa tafiti ambayo inaendelea ambayo inafanyiwa na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*), Wizara ya Kazi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Fedha, utafiti huu utakamilika mwisho wa mwaka wa fedha huu ambaa tumeuanza baada ya hapo tutawenza kuona sasa ni namna gani tuanze kutoa hii pensheni ya wazee kama ambavyo vilevile hata Waziri Mkuu aliwahi kuahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wabunge wengi wamezungumzia kuoanisha na kuboresha mafao ya wastaafu kwa kutumia *formular* moja. Waheshimiwa wengi wamezungumzia akiwemo na Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Dokta Antony Mbassa na wengineo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nieleze tu kwamba Mamlaka yetu ya *SSRA* tayari imempata mthamini yaani *actuary* ambaye anafanya tathmini ya mifuko yote ili kuainisha *formular* zote za mafao. Zoezi hili tunategemea likamiliike mwisho wa Disemba, 2011. Hii itatuwezesha sasa kuainisha *formular* za mifuko hiyo, pamoja na kuangalia uwezekano wa kuboresha sasa thamani ya pensheni ambayo inaitwa *indexation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wabunge vilevile wamezungumzia kuunganisha mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii akiwemo Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum na Mheshimiwa Pereira Ame Silima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba jambo hili ni jambo ambalo tunalionia kwamba ni zuri na kwa sasa *SSRA* imeanza kufanya tathmini ya afya ya mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo matokeo yake sasa yataonesha ni kwa namna gani suala hili sasa tunaweza tukalishughulikia. Lakini tukumbuke tu kwamba mifuko hii kila mmoja umeanzishwa kwa Sheria yake na inatoa masharti tofauti ya kunufaika na mafao mbalimbali yanayotolewa. Kwa hiyo, marekebisho ya Sheria yatakayokuwa yanafanyiwa ya mifuko hii itatuwezesha kufikia lengo hili ambalo kama nilivyosema, sisi tunaona ni zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane vilevile na Waheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Dokta John Charles Tizeba, kwa suala la kwamba kuna umuhimu wa kuwekeza fedha za mifuko hii katika miradi ambayo itanufaisha wanachama wake na kwa sasa ni kwamba *SSRA* tayari kwa kushirikiana na Benki Kuu, inaandaa utaratibu wa uwekezaji (*Investment Guidelines*) ambazo zitatakiwa zifuatwe na mifuko hii katika kuchagua vitega uchumi salama na vyenye tija kwa manufaa ya wanachama. (*Makofii*)

Mimi ninaamini baada ya hili kufanyika tutakuwa sasa na uwezekano wa kufuatilia nani anawekeza wapi na je, ina matokeo mazuri kwa wanachama au hapana! Na pale ambapo inabidi kuzuia pale ambapo uwekezaji mbaya unataka kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningeweza kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba ukiangalia kifungu cha 38 cha Sheria Namba 8 ya mwaka 2008, hii ya Hifadhi ya Jamii inaruhusu wanachama wa mifuko kutumia mafao kama *collateral* kwa ajili ya mikopo ya nyumba za makazi. Sasa hili litakalokuwa limekamilika kwa maana ya kuweka *guideline* ya hizo *collateral* likianza na hakika kwamba wanachama watafaidika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala vilevile la mifuko kuwa chini ya Wizara moja na Wizara hiyo Wizara ya Kazi na Ajira, ni wazo zuri kama alivyosema Mheshimiwa Rose Kamili Sukum na Mheshimiwa Angellah Kairuki, ni kwamba ukiangalia hata Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii inaipa mamlaka Wizara inayohusika na Hifadhi ya Jamii ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira, kusimamia shughuli zote za Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini ikiwepo mfuko. Kwa hiyo, marekebisho ambayo sasa tunafanya kwenye sheria mbalimbali za mifuko mbalimbali itatuwezesha tufike katika hatua ya kuona kwamba je, mifuko yote iwe chini ya Wizara moja ya Kazi na Ajira na hilo tutafahamishana na tutaleta hapa kwa uamuji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watumishi kuchangia mara mbili katika *energy, NHIF, NSSF*, suala hili limeanza kwenye *circular* ya Serikali baada ya Serikali kutoa *circular*, kuwaelekeza watumishi wake kuchangia kwenye bima ya afya bila kujua kuwa kuna watumishi ambao tayari walikuwa wanachangia kwenye Mfuko wa *NSSF* ambao tayari unatoa fao la huduma za afya, hii ilisababisha watumishi hawa kujikuta wanachangia mara mbili kwa huduma hiyo hiyo. Serikali imelitambua hilo na imeweka mkakati mathubuti wa kusimamisha mchangiaji mmoja. Kwa maana hiyo uchambuzi kuhusu suala hili unaendelea na mradi utakapokamilika Serikali itatoa maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za uendeshaji wa mifuko zipo juu, hili ni suala ambalo tathmini ambayo inafanyika itawenza kuangalia katika tathimini hiyo ni gharama za uendeshaji ziweje. Tathmini hii itategemea kukamilisha kabla ya mwisho wa mwaka huu na suala la wigo vilevile wa hifadhi la jamii nalo ni mojawapo na mambo ambayo yanaangaliwa. Suala la *Senior Staff Superannuation (SSSS)* na *scheme*, aliyozungumza Profesa Kahigi, suala hili kwa kweli ukiangalia limechukua muda mrefu na lina historia ndefu lakini niseme tu kwamba kwa sasa Serikali imeshakubali kwamba wale wote katika kupata suluhisho la tatizo hili wanachama wa *SSSS*, Serikali imeamua kuchukua wote ambao hawajastaafu na kuwaunganisha katika taratibu za *PPF*. Sasa hawa tayari Bajeti yao ni kama shilingi bilioni 9.3, kwa sasa tumeishia hapo lakini nieleze tu kwamba Serikali inaendelea kuangalia wale wengine ambao walishastaafu kabla, je, utaratibu gani ufanyike, utakapokuwa tayari tutawenza kulizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya *TaESA* na OSHA, nieleze kwamba wengi walikuwa wanadhani labda *TaESA* na OSHA labda wako Dar es Salaam, lakini niseme tu ukiacha Dar es Salaam wapo kwenye kanda, Kanda ya Ziwa kuna ofisi zao Mwanza wote wawili, kati Dodoma vilevile wote wawili wapo, Kaskazini kule Arusha wapo wote na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wapo Mbeya na Kkanda ya Kusini wapo Mtwara, wote OSHA na *TaESA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba katika suala OSHA limezungumzwa sana, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ameizungumzia sana kwamba OSHA imeweka mwanya mkubwa kwa wafanyakazi kushindwa kutoa taarifa ya uvunjifu wa kanuni za afya na usalama kazini. Niseme tu kwamba wala mlolongo si mrefu sana ukiangalia kifungu Na. 99(1)(d) na (e) mlolongo siyo mrefu kwa sababu mfanyakazi anatoa taarifa kwa mwakilishi wa Kamati ya Afya na ambaye anamuarifu mwajiri, mwajiri akishindwa kutekeleza basi mfanyakazi anaweza kwenda

moja kwa moja kwa mkaguzi. Kwa hiyo, nadhani (c), (c) hii tunaweza tukaboresha tukiona kwamba hali hiyo bado inaleta matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafanyakazi wanapotoa taarifa ni kama wamejifukuzisha kazi, inaweza kuwa kweli, lakini ukiangalia Sheria Namba 102 inakataza kwa kweli mwajiriwa kwa sababu yoyote ile kumfukuza mfanyakazi kwa sababu tu ametoa taarifa ya uvunjifu wa sheria hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wengi akiwemo Mheshimiwa Said Mtanda, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Zainabu Kawawa, Mheshimiwa Ali Mohamed na Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe wote kwa kweli wamezungumzia tatizo la uwezo mdogo wa OSHA, kwa maana ya vitendea kazi na hata watu (rasilimali watu).

Mheshimiwa Naibu spika, nataka kusema tu kwamba pamoja ni kwamba upungufu wa fedha umefanywa hali hiyo ikawepo sasa hivi kwenye Bajeti tumejitahidi ili OSHA ipate nguvu zaidi na iweze sasa kufanya kazi zake za ukaguzi vizuri. Katika mwaka ujao wa fedha, mtatusikia tu na mimi nimewambia Wazirii wangu anipe OSHA nitembee nao kwenye viwanda na maeneo mengi ili tuhakikishe kwamba watu wanafuata sheria na ikiwemo tatizo la *Jambo Plastic* ambalo Mheshimiwa Wazirii atalielezea, lakini nieleze katika tatizo la vifaa katika *Jambo Plastic*, tulilliona na limeshafanyiwa kazi na OSHA na sasa *Jambo Plastic* wanatoa vifaa vinavyofaa kwa ajili ya wafanyakazi wale kuweza kuvivaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa John Mnyika, wamezungumzia suala la kuimarisha ukaguzi wa afya salama sehemu za kazi na hasa kwenye sekta ya ujenzi wa barabara na sekta nyingine na mimi nakubaliana nao na kama nilivyoahidi, OSHA itaendelea kufanya kazi hizo na tutaendelea kuwapa uwezo zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Martha Mlata, amezungumzia masuala ya wanaozibua mifereji, nikuhakikishie Mheshimiwa Martha Mlata kwamba hili tumeshalionna na tayari makampuni 50, yanayofanya kazi hizi za kuzibua mifereji wamepewa mafunzo na OSHA, katika hali ya kuhakikisha kwamba wanatekeleza sheria na hata Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, viwanda vile vya samaki, tayari vimekaguliwa na ushauri wa kitaalam umeshatolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu *NIP* au Shirika la Tija, umuhimu wa Tija katika uzalishaji kwenye maeneo ya kazi na kwenye maeneo ya huduma. Mimi nataka nikubaliane nao wote waliozungumzia suala hili akiwemo Mheshimiwa Regia Mtema, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Pereira Ame Silima na wengine wote kwamba umuhimu huo tunaona na kuna haja ya kuweka mkakati wa kuiwezesha zaidi Shirika letu la *NIP* na kwa sababu sasa hivi tunajandaa kuandaa Sera ya Taifa ya Tija, basi tutazingatia yote haya ambayo mmeyasema, na kuhusu jengo lao lile kwamba liendelezwie tayari wana mkataba na *NSSF*, kwa ajili ya kulijenga jengo kisasa kabisa katika eneo lile la *Maarifa House* na ujenzi huu utaanza katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, yote haya yatakuwa katika kuwezesha Shirika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya tija kama alivyoeleza Mheshimiwa Pereira Ame Silima ni muhimu na hili tatalizingatia, ingawa tayari programu za kuboresha tija katika maeneo ya kazi Serikali tayari imeshaanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi vilevile wamechangia kuhusu suala la haki ya kuijunga na vyama vya wafanyakazi, ukichukulia Mheshimiwa Ali Self, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Zainabu Kawawa, wamezungumzia sana umuhimu wa vyama vya wafanyakazi.

Mimi naweza kusema kwamba ukiangalia Sheria ya Kazi, vifungu vile vya 45 mpaka 58 vyote vinaeleza namna umuhimu wa wafanyakazi katika maeneo yote ya kazi kuanzisha na kuijunga na vyama vya wafanyakazi bila kuzuiliwa na waajiri. Eneo la kazi lenye wafanyakazi kumi au zaidi panaweza kuundwa Tawi la Chama cha Wafanyakazi, kwa hiyo, ni wajibu wa wawakilishi

wa Vyama vya Wafanyakazi kuzingatia tu taratibu zinazotakiwa na kusimamia taratibu hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna waajiri ambao wanajaribu kudidimiza juhudzi za wafanyakazi kuunda mabaraza au kuyafanikisha lakini hili tukilipata tutakuwa tunachukua hatua zinazostahili na tayari tumeshachukua hatua maeneo mbalimbali kwamba masuala ya kisiasa yanaingizwa kwenye Vyama vya Wafanyakazi kwa kweli nia ni kwamba hakuna chama chochote kinachoruhusiwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na mahusiano kazini kujihusisha na masuala ya kisiasa. Chama chochote cha wafanyakazi, kinachojihusisha na masuala hayo kinatenda kinyume cha sheria na illyotajwa na ikibainika inaweza kufutiwa katika daftari la usajili wa vyama na mimi nitoe wito hapa kwamba kweli tusiingize siasa kwenye masuala ya kazi na vyama vya wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kulikuwa na masuala ambayo yamezungumzwa kuhusu SMA au Tume ya Usuluhihi na Uamuvi, mengi yamezungumzwa kuhusu mkataba wa hali bora na wafanyakazi kiwanda cha Sukari cha Mtibwa dhidi ya uongozi wa Mtibwa.

Sasa Wizara kwa sheria ya kazi ambayo ni Sheria ya Kazi Namba 6 ya mwaka 2004, sheria hiyo inatoa muongozo wa namna ya kujadiliana na kufunga mkataba wa hali bora mahali pa kazi, mimi nataka tu nitoe wito kwa Mheshimiwa Amos Makalla, kukaa na viongozi wa vyama vya wafanyakazi pale kuangalia kwamba taratibu hizi zinafuatwa ili kweli kuwe na hali bora na sisi tupo tayari kwenda na Mheshimiwa kutumia idara yetu ya vyama vya wafanyakazi kusadiana na Mheshimiwa Mbunge kuona kwamba hali hiyo inakuwa inatekelezwa pale Turiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mmezungumzia matatizo ya vitendea kazi kwenye SMA, hili tumeliona, lakini kwa kweli tunajitahidi na Serikali imekuwa ikijitahidi kutoa sasa fedha za kutosha ili chombo hiki kiweze kufanya kazi. Imefanya kazi kubwa sana na kuzuia masuala mengi ama kwenda kwa Waziri kama ilivyokuwa zamani au kwenda mahakamani yamekuwa yakimalizwa na SMA na mimi nataka niwapongeze sana wenzetu wa SMA kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Murtaza Mangungu naye alizungumzia kuhusu muda unaotumika kutoa maamuzi au mashauri ya mgogoro wa kazi mbele ya tume, kama kila kitu kimetekelezwa kwa maana ya kuwasilisha taarifa zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya mwaka 2004, siamini kwamba itachukuka muda mrefu kutatua maamuzi ya mgogoro. Sasa katika kifungu 88(9) kinaleza kuwa uamuvi utelewe ndani ya siku 30, mara baada ya pande mbili husika kufanya majumuisho mbele ya maamuzi, *arbitrate*, kwa hiyo, mimi nadhani kwamba haya yakitekelezwa wala maamuzi hayawesi kuchelewa na wameona wengine kwamba maamuzi yamekuwa yakitolewa mapema tu katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ni mengi ambayo yamejitokeza kwa muda mdogo niliokuwa nao nimeweza kujibu haya ambayo nimeyajibu, pengine yaliyobaki yakiwepo yale yanayohusu Shirika letu la NSSF, lakini hasa ya sera kuhusu ajira na migogoro ya kazi. Mheshimiwa Waziri atakuja hapa kuweza kuyatolea majibu na kama nilivyoahidi toka mwanzo tutajitahidi tutoe majibu kwa hoja zote zilizotolewa na Wabunge kwa maandishi na kwa kuzungumza humu ndani ili tuweze kupata nini hasa msimamo wa Serikali kuhusu suala hili au Sera za Ajira, Kazi pamoja na Hifadhi za Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba naunga mkono hoja hii ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Waziri una dakika 55. (*Makofi*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi nyingine jioni hii ili niweze kutoa maeleo na kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza katika michango ya Waheshimiwa Wabunge katika hoja niliyoasilisha leo asubuhi. (*Makofi*)

Nipende kuwashukuru kwa moyo wa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia hoja hii kwa kuongea na wengine kwa maandishi na kufikisha jumla ya wachangiaji 182 ikiwemo ni pamoja na wale waliochangia kwenye hotuba zilizopita mpango wa miaka mitano, hotuba ya Waziri Mkuu, hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango yote hiyo nimeijumlisha ni 182. Hii ni ishara tosha kuwa eneo hili la kazi na ajira ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu na kwa kweli michango yenu tunaithamini na tunaahidi kuizingatia katika utekelezaji wetu wa kazi na kuboresha shughuli zetu za kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi ambaye tayari ameshatoa ufanuzi na kujibu baadhi ya hoja kwa umahili kabisa nami nitaendelea kutoa maelezo pale ambapo ameishia, kwa yale yaliyosalia. Lakini aliyosema na mimi nirudie kutokana na muda mfupi na hoja kuwa nyngi sidhani kama tutawenza kumaliza zote tukiwa tumesimama hapa na kama ilivyo ada kama aliyosema tutawaletteeni majibu ya hoja zote kwa maandishi kwa mtindo wa bango kitita yaani *matrix*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ilivyo tabia njema niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba hizo za nyuma na wale waliochangia leo, kama ifuatavyo, nikianza na wale waliochangia katika hotuba za nyuma nilizozitaja, tunao Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Salim Barwany, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Freeman Mboge, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Zainabu Kawawa, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mariam Msabaha, Mheshimiwa Mohamed Mgimwa, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, naona yamerudiwa haya majina. (*Makofii*)

Wachangiaji katika hotuba ya leo na naanza na wale waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuataao, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa *Engineer Athumani* Mfutakamba, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Suleiman Jafo, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa *Engineer Ramo* Makani, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Desderius Mipata. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Freeman Mboge, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Abas Mtemvu, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashidi, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Sabrina Sungura, Mheshimiwa Ummy Ali Mwalimu, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, Mheshimiwa Mtutura Mtutura, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa *Engineer Gerson* Lwenge, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Margareth

Mkanga, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis na Mheshimiwa Esther Matiko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Christowaja Mtinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hapa nakosa *list* ya wale waliochangia kwa kuongea lakini nitawataja baadaye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naifikiri sasa ndiyo dakika 55 zinaanza, kama hiyo ndiyo kweli naomba nianze kama nilivyosema kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochangia humu ndani na wengine wamechangia huko nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo limechukua hisia kubwa za wachangiaji ni eneo la ajira na hasa hasa ajira za vijana wetu. Nakubaliana nao kwani tatizo la ukosefu wa ajira ni kubwa hapa nchini na hususani kwa vijana. Hii siyo kwetu tu bali ni duniani kote na madhara yake ni makubwa kwanza kwa kijana mwenyewe, jamiili na Taifa kwa ujumla. Baadhi ya madhara hayo ni vijana kuijingiza katika shughuli mbadala kama vile biashara haramu, biashara za ngono, utumiaji wa dawa za kulevyta na mengine mnayoyafahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa ajira tunalifahamu, nydingine zimetajwa katika hotuba ya Kambi ya Upanzani na mimi naomba niongezee kwamba lingine ni pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa nafasi za ajira katika uchumi ukilinganisha na nguvukazi inayoingia katika soko la ajira kila mwaka na hawa ni vijana wa rika zote na viwango vyote vya elimu. Vijana kutokana na uzoefu wasiokuwa nao wa kazi na unaohitajika katika baadhi ya kazi au *gap* iliopo kati ya ujuzi walionao na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo lingine la ukosefu wa ajira ni vijana wetu kuchagua kazi. Lingine ni miradi midogo walijonayo au ukosefu wa mitaji kabisa, lakini pia lingine ni kwamba vijana wengi wanafikiri ajira ni kuajiriwa tu kuliko kujiajiri mwenyewe. Pia kuna mambo mengi ambayo kila mtu anaweza kusema yanasantabisha ukosefu wa ajira. Serikali inafanya nini? (*Makofii*)

Kwanza Serikali inasema suala la ajira ni suala mtambuka ambalo kila Wizara na kila Taasisi ya Umma na Taasisi binafsi zinapaswa kutambua na kuchukua hatua za kuangalia fursa za ajira zilizopo katika mipango yao yote. Hii itasaidia kuwa na taarifa za ajira ngazi zinazotarajiwa katika mwaka husika, Wizara yangu kwa kushirikiana na *ILO* tumekwishiwezesha Wizara sita tayari kuchambua baadhi ya sera zao kama nilivyosema katika hotuba yangu nikirudia kuzitaja hizi Wizara ni Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha na kwamba katika mipango yao ya maendeleo waweze kuibua aina za ajira zinazoweza kupatikana kwa walengwa katika maeneo haya ni vijana kati ya miaka 15 na 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ielevweke kwamba mahitaji ya vijana kulingana na viwango mbalimbali vya ajira yanatofautiana, kwa hiyo, jambo kubwa ni kuwajengea uwezo vijana ili waweze kujiajiri na kuajiriwa. Kwa sababu vijana wengi wanaingia katika soko la ajira bila ujuzi wowote na hivyo wanapata wakati mgumu kuweza kujiajiri na kuajiriwa na hii ipo katika taarifa ya ajira ya mwaka 2007 yaani *National Employment Report* ambayo inaonyesha kuwa 37.2% ya nguvukazi isiyi na ajira hajawahi kupata mafunzo yoyote au stadi za kazi. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo Serikali tumeliona na tumechukua hatua kabisa kuhakikisha tunakuwa na programu ambayo itawawezesha vijana kupata uwezo wa kujiajiri na kuwaajiri wengine. (*Makofii*)

Hii itakuwa ni programu ya miaka mitano ambayo itahusu kuwajengea vijana uwezo na tunapendekeza kwamba ianze katika maeneo ambayo yatakuwa na matokeo ya haraka kwa mfano maeneo ya kilimo, uvuvi na ufugaji, sekta ya nguo labda, usindikaji, *TEKNOHAMA* na ujasiriamali mdogo mdogo, lakini pia sanaa, utamaduni, michezo na kadhalika. Yote haya ni maeneo ambayo yana uwezo wa kuwaajiri vijana na kuwasaidia kuwaajiri wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Freeman Mbewe ameniletea karatasi hapa ya mchango ni fupi sana lakini amesema michezo ni ajira, michezo ni burudani, michezo ni afya na michezo ni uchumi. Nakubaliana naye na sisi tumeshaona haya maeneo ni maeneo ambayo yanaweza kuleta fursa za ajira. (*Makofii*)

Aidha, Serikali inachukua hatua za kuboresha sheria, kanuni na mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia wawekezaji zaidi watakosaidia kuongeza fursa za ajira. Tunafanya hii kwa kutumia mradi lakini pia tunatumia pesa zetu wenyewe. Sasa tunasema vijana hawa wapo katika maeneo ya vijijini na sisi tusingependa watoke katika maeneo hayo na kuja kutafuta ajira au fursa tunazozizungumza mjini.

Kwa hiyo, tutawawezesha huko huko walipo na kwa hali hiyo Wizara yangu imeanza kuunda Kamati za Kukuza Ajira katika mikoa nane. Tutaanza na mikoa nane ambayo ina jumla ya Wilaya 48 na ni matarajio yetu kwamba katika mipango ya maendeleo ya kila Halmashauri ya Wilaya hizi basi kutakuwepo na fursa za ajira katika maeneo ya kilimo, viwanda na hata elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majina ya mikoa na wilaya hizo ninayo lakini kwa ajili ya muda naomba nisizitaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imeona ni vizuri kuimarisha mfumo wa kukusanya na kusambaza taarifa za soko la ajira yaani *Labour Market Information System* kwa kushirikiana na ILO tumeandaa mfumo ambao utasaidia kupatikana kwa taarifa mbalimbali za ajira ili kuwaunganisha watafuta ajira na waajiri wenyewe na nafasi za ajira. Lakini najua Serikali kuititia Wizara ya Elimu pia inaboresha mfumo wake wa elimu, inaweka sasa hivi programu za ujasiriamali ili kuwaandaa vijana wanaotoka katika hasa elimu ya juu ili waweze kujajiri na kuajiri wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaamini kwamba sekta binafsi ina nafasi kubwa ya kuchangia kupunguza tatizo la ajira mbali ya kuwa waajiri wanaweza kushirikishwa pia katika utoaji wa mafunzo ya stadi mbalimbali yaani *practical training* ili kuwapa vijana uzoefu. Pia taasisi za fedha zinaweza kutusaidia kutoa mikopo yenye masharti nafuu na mitaji kwa wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala hili nimeamua kulitolea maelezo kidogo kwa sababu wengi tunafikiria kwamba ajira lazima ipatikane katika Ofisi za Serikali. Lakini Serikali ina sehemu yake na sekta binafsi ina sehemu yake. Lakini matatizo tumeona vijana hawana stadi za kujajiri, hawana mitaji na hawana uwezo na kwa hiyo, Serikali tutafanya tutakachoweza na tunaomba pia na sekta binafsi kwa kuboresha mazingira ambayo sasa Serikali inafanya hasa kuititia mpango wa maendeleo wa miaka mitano tuweze kuongeza ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa kwa hisia pia ni masuala ya waajiri binafsi hasa masuala ya kuwanyanyasa wafanyakazi na masuala ya kutowapa haki na kutowasaidia wafanyakazi kupata kazi za staha. Wengi wame-sight viwanda mbalimbali hasa kiwanda cha *Jambo Plastic*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kusema hivi, sasa hivi Sheria yetu ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu ni sheria mpya inayokidhi mahitaji ya mfumo wa kiuchumi na kijamii tulionao sasa hivi hapa nchini. Hii ni sheria ambayo sasa inakuza maendeleo ya kiuchumi na kazi ya kijamii, inatoa mwongozo wa kisheria kwa ajili ya uhusiano mzuri na haki ya kiajira na viwango vyta msingi vyta mazingira ya kazi. Pia inatoa mwongozo wa majadiliano ya pamoja ya hiari baina ya mwajiri na mfanyakazi, inatoa mwongozo

wa kutatua migogoro ya kazi kwa njia ya usuluhishi, uamuzi na ikishindikana kwa njia ya hukumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *Jambo Plastic* nimekitembelea, tulikuwa kwanza na Kamati lakini pia nimetuma wataalam. Tatizo kubwa la kiwanda kile ni wafanyakazi kutoelewa sheria mpya ya ajira na uhusiano kazini na kutokana na hilo wamejihusisha katika mgomo isyo halali. Migomo kweli ni haki kwa kila mfanyakazi kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani na mimi nakubaliana naye, ipo katika kifungu cha 80 cha sheria hii lakini mgomo huo pamoja na kuwa ni haki ni lazima uwe halali. Lakini pia kifungu kile sehemu ya kwanza inatamka kwamba kama mgomo ni halali lazima uwe ni mgomo wa kimaslahi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa pamoja na hayo nisingependa kuendelea zaidi ya suala hili la *Jambo Plastic*, lakini ilipofikia sasa hivi ni hatua ambayo hatuwezi kuizungumzia kwa sababu ya baadhi ya wale wafanyakazi kufukuzwa wamekwenda *CMA*. *CMA* ni sehemu ya Mahakama na ndiyo maana nimesema masuala mengi katika sheria hii migogoro ya mwajiri na mfanyakazi inatatuliwa kwanza kwa njia ya usuluhishi, ikishindikana ni lazima iende kwenye uamuzi na kazi hizi za usuluhishi na uamuzi zinahanyika kwenye *CMA* yaani *Commission for Mediation and Arbitration*, itakapokuwa imeshindikana basi watapelekana Mahakama Kuu ya Kazi. Sasa kutokana na hilo na sheria yako inasema kwamba hatutazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama, basi naomba tusubiri sheria ichukue mkondo wake kuhusiana na wafanyakazi wa *Jambo Plastic*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna viwanda vingi vimezungumzwa kama kiwanda cha Mtibwa ambacho pia amekizungumza Mheshimiwa Amos Makalla, alikizungumzia wakati wa Bajeti nafikiri ya Mambo ya Ndani na amekizungumzia leo na kweli leo ndiyo mahali pale kwa sababu hotuba ya leo inahusu wafanyakazi. Lakini tunachosema ni kwamba katika taratibu za *CMA* mtu ye yeyote anayekuwa ametendewa isivyo haki awe mwajiri au mwajiriwa lazima shauri la mgogoro wa maslahi alipeleke kwanza likatolewe usuluhishi au uamuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla ya kufanya hivyo tunashauri na kanuni za sheria zinashauri kwamba ni vizuri mwajiri na mwajiriwa wakakaa katika makubaliano yaani wakasuluhishana kwanza ili kwamba suala la kupelekana *CMA* liwe la mwisho. Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alikubali atakitembelea kiwanda hicho, naomba basi na mimi niseme kwamba nitakitembelea kiwanda hicho ili kuangalia hali halisi ya masuala ya wafanyakazi yaliyopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilirozungumzwa ni suala la vibali yaani vibali vinavyotolewa kwa wawekezaji na watu amba si Watanzania. Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997 imeainisha idadi ya wageni wanaoruhusiwa kufanya kazi katika kampuni za wawekezaji hapa nchini. Idadi hii inaweza kuongezeka kutokana na umuhimu wa mahitaji yatakayothibitishwa na mamlaka zinazosimamia uwekezaji nchini.

Aidha, Wizara inaweza kuwakatalia kuwapa vibali wageni wanaoomba nafasi za kazi zinazowenza kufanya na Watanzania katika soko la ajira la ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongezee kwa kusema mamlaka zinazotoa vibali vya kazi sasa hivi katika nchi ni vya aina tatu. Tuna mamlaka inayotoa kibali cha *grade A* ambacho hicho kinatolewa na *TIC* lakini kuna *class B* ambayo inatolewa na Wizara yangu au kibali cha ukazi ambacho kinatolewa na Idara ya Uhamiaji. Kwa hiyo, tuna mamlaka tatu zinazoshughulikia vibali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana katika mamlaka hizo watu wanatumia ujanja wanatoka kwenye mamlaka moja kwenda kwenye mamlaka nyingine wanapata kibali cha ukaazi na hicho kibali cha ukaazi kinatumika kama kibali cha kazi. Serikali tumeshagundua utata uliopo na siku ya Mei Mosi Mheshimiwa Rais wakati wa hotuba yake alituagiza mimi na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani tufuatilie jambo hili na tulifanyie kazi na ninashukuru kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba tuko karibu sana na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya

Ndani ya Nchi, tumekubaliana mambo kadhaa ambayo tutayafanya ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayetumia mwanya wowote katika kutafuta vibali hivi. (*Makof*)

Kwa hiyo, tutatenganisha vibali hivi vya ukaazi na vibali vya kazi ili kusudi kiwe ni kibali kimoja, huwezi kupata kibali cha ukaazi mpaka kwanza umepata kibali cha kazi. Pia tunajua kwamba wafanyabiashara wengine wanapoingia Tanzania kuja kutafuta uwekezaji wanakuja na watu wao watano lakini anatumia fursa hiyo kuwaingiza watu wengine kwa kutumia kitu kinachoitwa *carrying on temporary assignments*. Kwa hiyo, anaingiza watu wengine kama dereva, mpishi na watu wengine kwa kutumia kipengele cha *carrying on temporary assignments*. Sasa hawa ndiyo mnaowakuta mahotelini, hao ndiyo mnaowakuta *Zantel* na hao vilevile ndiyo mnaokuta kwenye maeneo mengineyo. Suala hili tumeshalitambua Serikalini na tunalifanyia kazi na tunaomba mtuamini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina orodha kwa kuonyesha tu jinsi tulivyo makini katika utoaji wa vibali, nina uthibitisho mdogo kuhusiana na watu tunaowapa vibali, orodha ni ndefu lakini nichukue mfano wa watu waliomba kazi inayoitwa *Medical and Health Professionals*, waliomba watu watu 55, walikataliwa na tukampa mtu mmoja. Kuna watu waliokuja wanaomba kazi inayoitwa *Life Science Professionals* walikuja watu 15, tuliwakatalia wote. Alikuja mtu anaomba kazi inayoitwa *Database Designers and Administrators*, kuna wengine walikuja kama *Cooks and Chefs* watu 49, tuliwakatalia na tukampa mtu mmoja. Kwa kweli Wizara tunajitahidi kuhakikisha kwamba zile kazi ambazo zinaafanya na Watanzania, watu wa nje hawapewi lakini kama mnawaona huko katika maeneo basi wametumia ujanja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja iliyojitokeza ya wafanyakazi kuzuiwa kijiungu na kushiriki kwenye vyama vya wafanyakazi kinyume na sheria ya ajira mfano kwenye mgodi na hasa *Geita Gold Mining* pamoja na viwanda na rai hii ilitolewa na wengi wakiwemo Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mariam Kisangi pamoja na Mheshimiwa Zainabu Kawawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yake ni kwamba sheria ya mahusiano kazini inatoa uhuru na haki kwa wafanyakazi katika maeneo yote ya kazi, kuanzisha na kijiungu na vyama vya wafanyakazi bila kuzuiliwa na waajiri. Hii inatoa haki kwa eneo la wafanyakazi *at least* kumi pale ambapo kuna wafanyakazi kumi na wanataka kijiungu na chaama cha wafanyakazi au kuanzisha tawi lao wanaruhusiwa.

Ni wajibu wa wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi katika ngazi za juu kama ni wilaya au mkoa kuzingatia taratibu za kuingia eneo la kazi kwa kujaza fomu zilizoainishwa kisheria ili waweze kusajili wanachama wenzao. Mwajiri anayezuia wawakilishi wa vyama kusajili wanachama au kufanya shughuli za chama katika eneo la kazi anatenda kosa na wahusika wanawenza kufungua shauri la mgogoro katika tume ya usuluhishi na uamuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hakuna mwajiri yejote anayepaswa kuanzisha *forum* tofauti na Chama cha Wafanyakazi katika eneo la kazi kwa ajili ya kufanya kazi za chama cha wafanyakazi. Wizara yangu itaendelea kufutilia na kubainisha waajiri wenye tabia hiyo na kuchukua hatua stahiki, lakini kwa kuwa mmeshanieleza kuhusu suala la *Geita Gold Mine (GGM)* na maeneo mengine, basi tutafanya hiyo, lakini tumeshaanza na tumeshakagua maeneo mengi kama nilivyosema kwenye hotuba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni suala la *Mohamed Enterprises* kuajiri wageni kwa asilimia themanini ya wafanyakazi wote siyo kweli. Kutokana na taarifa zetu kampuni ina kampuni tanzu zipatazo kumi na tisa na zina matawi karibu nchi nzima. Wana jumla ya wafanyakazi wazalendo 11,228, wazawa 11,062 na wageni ni 166. Idadi hiyo ya wageni siyo asilimia themanini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kampuni zinazoshughulika na kilimo, biashara, mawasiliano na fedha, utafutaji mafuta na usafirishaji, kampuni nyingine kama vile *21 Century Textiles* ipo chini ya EPZ na hii ina wageni 30, A1- 14, Afrilex tisa na Equalfill wapo 11. Wastani wa

wageni wote kwa wazawa ni asilimia 14.8 na idadi ya wageni ni kubwa kwa vile viwanda vingi vipo kwenye ngazi za upanuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *Marmo Grantal* ya Mbeya, ukaguzi uliofanyika tarehe 20 Mei, 2011 ulibaini kwamba kuna wageni kumi kwenye fani za *General Manager, Finance Manager, Construction Manager, Electrical Technicians, Quarry Manager, Production Manager* na *Security Manager*. Ilibidi kumwajiri huyu baada ya kutokea wizi wa mara kwa mara bila kudhibitiwa. Wageni hao ilibidi waendelee kuwepo baada ya wazalendo waliopata mafunzo kuondoka na kwenda kuendesha shughuli zao. Wanazo pia ofisi zao Temeke- Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha Sukari cha Mtibwa tumeshazungumzia. Kulikuwa pia na swali la muda unaotumika kutoa uamuzi wa mashauri ya migogoro ya kikazi mbele ya tume. Sheria inayozungumzia imeweka muda wa kutoa uamuzi wa kutatua mgogoro katika kifungu cha 88(9) na hizi na siku 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, endapo itatokea kuna ucheleweshaji kabla ya uamuzi kutolewa kwa mara ya kwanza, hili linatokana na pande husika kuomba kuahirisha shauri kwa sababu mbalimbali. Pia ucheleweshaji huo unatokea kutokana na sababu mbalimbali zinazowahusu wadau wote wawili katika suala hilo. Aidha, tume ya usuluhishi imekuwa ikijitahidi kutatua migogoro ya kikazi kwa wakati na itaendelea kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la kuwa na utaratibu maalum kwa kila taasisi wa kuwashirikisha wafanyakazi katika kufanya maamuzi mbalimbali kuondoa malalamiko sehemu za kazi. Hyo tunasema ni kweli, ni vizuri taasisi kwanza zianze kujadiliana na kutatua migogoro yao kwa majadiliano, kabla hawajafika katika vyombo vyya kisheria vyya kutatua migogoro yao chini ya programu ya uboreshaji wa huduma za umma (*public service reform programme*) kila mtumishi anapaswa kushiriki katika uandaaji wa mpango wa kazi wa sehemu anayofanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee na hapa kuna suala la *NSSF*. Hili lilitolewa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambayo ilishauri kwamba Serikali iangalie namna ya kuboresha mafao ya wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jmii. Tunasema Serikali kupitia *Social Security Regulatory Authority (SSRA)* inafanya tathmini ya mifuko yote ya hifadhi ya jamii kwa nia ya kuongeza wigo na kuboresha mafao. Kwa upande wa mafao ya *NSSF*, kuna mafao ambayo yamegawanyika katika makundi mawili, mafao ya muda mrefu na yale ya muda mfupi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya muda mrefu ni haya yafuatayo, pensheni ya uzeeni ambayo inalipwa kwa mwanachama anayestaafu na kutimiza masharti yanayohitajika. Pia kuna pensheni ya ulemavu ambayo hulipwa kwa mwanachama ambaye atakuwa amepoteza uwezo wa kujitafutia kipato kutokana na ulemavu wa mwili au akili na kuna pensheni ya urithi ambayo hulipwa kwa waliokuwa wakimtegemea mwanachama aliyefariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya muda mfupi ni yale ambayo hulipwa kwa kipindi kifupi kwa muda maalum kama ilivyoainishwa katika sheria. Mafao haya ni manne, kwanza ni msaada wa mazishi ambao hutolewa kwa fedha taslimu kwa mtu aliyeghamramia mazishi ya mwanachama aliyefariki, mafao ya uzazi ambayo hutolewa kwa mwanachama mwanamke kabla na baada ya kujifungua na mafao ya uzazi ambayo yanajumuisha matibabu na fedha taslimu na hutolewa kwa mwanachama kila baada ya miaka mitatu. Hata hivyo, mafao mengine yataendelea kuboreshwa kadri Mdhibiti wa Hifadhi ya Jamii atakavyokuwa anafanyakazi hasa baada ya sheria yake kuhuishwa na zile sheria zilizoanzisha mifuko mingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *NSSF* tumeitaja. Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali iondoe kodi kwenye mapato yatokanyo na uwekezaji (*investments*) ili fedha hizo zitumike kuboresha mafao kwa wanachama. Tunaupokea ushauri huo na *NSSF* itaufanya kazi ushauri huu ili kutokana na vitega uchumi vyake basi wanachama waweze kufaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya, pia alihoji iwapo *NSSF* inaweza kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wanachama wake? Sheria mpya ya *SSRA* inatoa ruhusa kwa wanachama wa *NSSF* kutoa hadi asilimia hamsini kama dhamana (*security*) kwa mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja juu ya namna ambavyo wanachama wanajulishwa kuhusiana na fedha zao zinavyotumika katika uwekezaji. Wanachama hujulishwa kuitia bodi ya wadhamini wa *NSSF* ambayo ndio inafanya maamuzi yote ya uwekezaji. Kati ya wajumbe tisa wa bodi wanaoteuliwa na Waziri, wanachama wanawakilishwa na wajumbe sita amba ni sawa na asilimia 66%. Pia shirika linatoa taarifa ya hesabu za utekelezaji wa shughuli zake kila mwaka (*annual report and accounts*) ambayo inawasilishwa Bungeni. Aidha, mwaka huu shirika limefanya mukutano wa mwaka wa wadau ambapo katika mukutano huo taarifa za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa ya hesabu zilijadiliwa na mukutano huu utakuwa unafanywa na wanachama kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachama wanafaidikaje na miradi inayofanywa na *NSSF*? Jibu ni kwamba wanachama wananufaika kutokana na vitega uchumi mbalimbali kwa kupata mafao saba. Mafao haya ni mazuri kuliko mafao yanayotolewa na mfuko wowote wa hifadhi ya jamii, Kusini mwa Jangwa la Sahara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zaynabu Vullu anatoa pongezi kwa *NSSF* kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na *UDOM*. Pongezi zimepokelewa, Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu gani kuiwezesha *NSSF* kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa bomba jipya la gesi kutoka Kusini kwenda Dar es Salaam. *NSSF* kwa kushirikiana na kampuni ya mafuta (*TPDC*) inakamilisha taratibu za kuwekeza katika ujenzi wa bomba la gesi kutoka Songosongo – Somanga – Dar es Salaam. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* itawezeshwaje na Serikali katika utekelezaji wa mradi wa umeme ili kuondoa mgawo wa umeme amba ni tishio kwa Taifa? *NSSF* ipo katika mchakato wa kuwekeza katika sekta ya nishati. Uwekezaji katika sekta hii muhimu utakamilika kabla ya mwezi wa Desemba mwaka huu. Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, ametoa pongezi kwa *NSSF* kwa ufanisi wa shughuli zake, pongezi zimepokelewa. Miradi inapotekeleza na *NSSF* inazinufaishaje Wilaya duni kama vile Tarime? Jibu ni kwamba miradi inayotekelwa na *NSSF* inafanywa katika misingi ya kibashara (kuwekeza ili kupata faida inayotumika kuboresha mafao ya wanachama) matokeo ya uwekezaji huu ni faida kwa jamii kwenye maeneo ambayo miradi inatekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni utaratibu gani unaotumika kutoa ufadhili kwa baadhi ya maeneo? Jibu ni kwamba ufadhili hutolewa kusaidia huduma za jamii kufuatana na Bajeti ya ufadhili inayowekwa kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maswali mengi sana kuhusiana na *NSSF*. Mheshimiwa Gosbert Blandes, anasema riba ya asilimia mbili mpaka tatu inayotolewa na *NSSF* ni kidogo sana ukilinganisha na asilimia tano mpaka saba inayotolewa na *LAPF*. Jibu ni kwamba *NSSF* hutoa mafao ya pensheni ambayo huzingatia mapato ya mwisho ya mwanachama kwa kuchukua wastani wa miaka mitano ya mwisho. Pia mafao ya *NSSF* yanafanyiwa mapitio na marekebisho ya kila mwaka (*udjustment*) kufuatana na tathmini ya mfuko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Richard Ndassa amepongeza kwanza kwa kulipa mafao kwa muda mfupi zaidi ukilinganisha na siku za nyuma, pongezi zimepokelewa. Mheshimiwa Pereira Ame Silima amepongeza pia, pongezi zimepokelewa. Mheshimiwa Mariam Kisangi, amepongeza, pongezi zimepokelewa. Lakini pia amesema Serikali ijithadi kulipa fedha za *NSSF* kwa muda ili kutoathiri mafao ya wanachama. Hili ilmezungumzwa pia na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii. Serikali itazingatia ushauri huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto wa Kigoma Kaskazini, ameuliza ni kwa nini *NSSF* hajatekeleza mradi wa ujenzi wa stendi mpya katika eneo la Mwandiga hata baada ya mradi huo kuitishwa na bodi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wa stendi ya kisasa eneo la Mwandiga kwa ubia kati ya *NSSF* na Halmashauri ya Kigoma bado haujapitishwa na bodi. Mradi huu upo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Iwapo upembezi huu utaonesha kwamba mradi huu una manufaa kiuchumi kwa mfuko basi watawekeza katika mradi huo. Pia Mheshimiwa Mbunge ameuliza ni kwa nini miradi yote ya *NSSF* inakuwa Dar es Salaam, Mwanza na Arusha tu? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu tu kwa kusema kwamba miradi ya *NSSF* iko katika mikoa mbalimbali zaidi ya hii ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Miradi mingine ya *NSSF* imetekelezwa katika mikoa ya Kigoma (jengo jipya la kitega uchumi) na pia kuna mradi Kahama, Njombe na sehemu nyaginezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi amepongeza, pongezi zinapokelewa. Anasema pia *NSSF* ijenge majengo ya vitega uchumi katika mikoa maskini kama Lindi na wilaya zake. Niseme kwamba *NSSF* itafanya tathmini na ikiona kwamba vitega uchumi vitaleta faida basi itajenga, lengo ni kujiridhisha ili fedha za wanachama zisije zikapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Subira Mgusu naye ametoa pongezi kwa *NSSF* kwa kutekeleza miradi muhimu kama UDOM, nyumba za Polisi, nyumba za Mtoni Kijichi. Pongezi zimepokelewa. *NSSF* iharakishe mchakato wa uzalishaji wa umeme wa *MW300*. Niseme tu kwamba mshauri ameteuliwa na anaendelea na upembuzi yakinifu. Serikali iangalie uwezekano wa kuwakabidhi *NSSF* miradi ya makaa ya mawe na uzalishaji wa umeme wa Liganga na Mchuchuma kwani sasa ni muda mrefu umepita na hakuna kitu. Niseme kwamba ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, anasema *NSSF* iweke tarehe maalum ambayo pensheni itakuwa inaingizwa kwenye akaunti za wastaafu, hii itasaidia kuondoa usumbufu kwa wastaafu. Ukiphasikia "S" unafikiri ni "C". (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Hiyo ndiyo sawa sawa kabisa! Endelea tu Mheshimiwa Waziri! (*Kicheko*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF*inalipa pensheni kwa wastaafu wake kuitia Benki au Posta tarehe 25 ya kila mwezi. Pia Mheshimiwa Mbunge anasema viwango vya pensheni vinavyolipwa kwa wastaafu viwe vinafanyiwa marekebisho ili viwe vinaendana na hali halisi ya maisha. Hii ni kweli *NSSF* inafanya marekebisho (*Indixation*) ya mafao kwa wastaafu wanaopata kima cha chini. Shirika linafanya tathmini ya mfuko (*actuarial valuation*) kila baada ya miaka mitatu na kutokana na zoezi hilo, pensheni za wastaafu huboreshwa. Kwa mfano, tathmini ya mwisho ilifanyika mwaka ulioshia 2009 na hivyo kuongeza pensheni kwa wastaafu wote kwa asilimia 52%. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdul Marombwa ameipongeza *NSSF*, pongezi zimepokelewa. Lakini pia amesema Mkandarasi wa Daraja la Kigamboni apatikane haraka. Jibu ni kwamba, mkandarasi atateuliwa mwezi Oktoba mwaka huu na ujenzi wa daraja ambalo mmeliona leo kwenye picha hapa utaanza mwezi Desemba mwaka huu. Pia amesema kwamba *NSSF* ishirikishwe katika kujenga vituo vya kisasa vya polisi na makazi ya askari kama vile eneo la Kibiti ambalo sasa halina kituo cha polisi na nyumba za askari. Serikali imekuwa ikishirikiana na *NSSF* kujenga majengo kwa ajili ya makazi ya askari kama vile *Kilwa Road*. Juhudi zinafanywa kwa kuwashirikisha jeshi la polisi na *NSSF* ili kutekeleza miradi hiyo kwa taratibu zilizowekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Azza Hamad anaipongeza *NSSF*, pongezi zimepokelewa tunashukuru. *NSSF* na *PPF* waende vijijini hasa Shinyanga Vijijini kuwajengnea wanachama wao nyumba kufuatana na mapato yao ili waishi vizuri watakapostaafu. Ushauri umepokelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye anazungumzia *NSSF* kuwa na uanganifu mkubwa katika uwekezaji ili isijikute inaingia katika miradi ya hasara. Nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutahadharisha namna hiyo, lakini nimwambie pia kwamba *NSSF* inayo sera ya uwekezaji yenye vigezo vyote muhimu katika kutoa maamuzi ya uwekezaji. Zaidi ya sera

hiyo upembuzi yakinifu hufanywa kwa kila mradi kabla ya maamuzi kufanyika. Hata hivyo, tunashukuru kwa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge. Anaendelea kusema kwamba NSSF iwashirikishe wanachama wake katika maamuzi makubwa ya uwekezaji kwa njia ya semina ili wapate mawazo zaidi na ridhaa ya wanachama. Ni kweli wanachama wanashirikishwa katika maamuzi ya uwekezaji kupitia wawakilishi wao katika bodi na bodi ndiyo inayowawakilisha wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa ajira nchini nimelizungumzia kwa kirefu lakini limechangiwa na watu wengi. Mheshimiwa Athumanzi Mfutakamba, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mwanamirisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Agripina Buyogera. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Ni kweli hii ni changamoto kubwa sana katika nchi yetu, lakini kama nilivyosema Serikali peke yake haiwezi kuajiri nguvu kazi ambayo inaingia kwenye soko la ajira, kwa hiyo, ni lazima tushirikishe sekta binafsi. Serikali inachofanya ni kuandaa mazingira kwa kuboresha sheria zake ili zisiweze kuwapa taabu wale wanaokuu kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na masuala mengine aliyozungumzia Mheshimiwa Angellah Kairuki hasa ubaguzi ambalo nimeshalizungumzia. Pia alizungumzia suala la kutoridhia mkataba ambaa unahu masuala ya akinamama (wanawake na uzazi). Ni kweli tumeshasaini mkataba kama wanachama wa *ILO*, isipokuwa hatujauridhia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaridhia mkataba huo kwa sababu bado tunaangalia vipengele vile ambavyo haviendani na taratibu zetu. Maana tunaweza tukaridhia mkataba wote au vile vipengele ambavyo tunafikiri vinaendana na taratibu na sheria zetu hapa nchini. Kwa hiyo, huo ndiyo mchakato ambaa tunaendelea nao. Hata hivyo, hiyo peke yake haituondoi katika taratibu za kuwahudumia akinamama wafanyakazi wajawazito na hao wanaopata watoto kwa sababu sheria yetu vipengele vya 33 na 34 vinazungumzia waziwazi kuhusu mwanamama ambaye anataka kupata mtoto kuchukua likizo ya uzazi na anaweza kufanya hivyo kuanzia wiki ya nne. Imezungumzwa wazi katika kipengele cha 33(2)(a) na kipengele cha 33(2)(b) kinasema anaweza akachukua hata hiyo likizo ya uzazi tarehe yoyote itakayothibitishwa na daktari kwamba lazima achukue likizo mapema hata kabla ya wiki ya nne. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 33(3) kinaeleza kwamba hakuna mwajiriwa atakayefanyakazi ndani ya wiki sita baada ya kujifungua. Kwa hiyo, mama mjamzito ambaye anatarajia kujifungua analindwa vizuri na sheria hii ya ajira na mahusiano kazini. Pia ni vyema kutambua kwamba siyo mama tu, lakini sheria hii imemjali hata baba. Kipengele cha 34 kinasema kwamba baba wa mtoto aliyezaliwa anaweza pia akachukua likizo ya uzazi ya siku tatu ndani ya siku saba za mama kujifungua. Kwa hiyo, sheria hii inatosheleza kabisa mahitaji ya mama anayejifungua na kutohana na kutoridhia ule mkataba, haituondolei hiyo haki kwa sababu sheria yetu inatambua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wafanyakazi wa majumbani sheria imewatambua na imewaundi bodi ya kima cha chini. Tumeusaini mkataba ule mwezi wa Juni kama wanachama wa *ILO* na tunausubiri utakapokuja tutauleta kwenu Waheshimiwa Wabunge ili mpate kuuridhia. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge naomba niungane naye kwamba wafanyakazi hawa wa majumbani ni kama wafanyakazi wengine. Ni waajiriwa, kwa hiyo tunaomba kima cha chini kilichowekwa kwa ajili yao kiweze kutolewa. Kuna viwango kwa wale ambaa ni Waheshimiwa au Mabalizi. Kwa hiyo, hii kwa kweli na mimi nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba umefika wakati tuwa-treat kama wafanyakazi wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo sheria ambayo inazuia ajira kwa mtoto wa miaka 14, lakini sheria hiyo hiyo inazuia ajira mbaya kwa mtoto wa miaka 18. Miaka 18 ni ajira kama za migodini, ajira kama za baharini na katika mashamba, ambazo zitamfanya mtoto aweze kuteseka

kisaikolojia na kumharibia makuzi yake na hasa zile ajira ambazo zinamwondoa katika elimu yake ya msingi.

Programu tulioizungumza au mradi tuliozungumza wa kukomesha ajira ya watoto, sina hakika Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza yeye alikuwa anazungumzia *project* gani, lakini hii ni *special project* ambayo inafadhiliwa na *ILO* ambayo Tanzania tumepata sifa kubwa kwa kuiendeleza na kuitekeleza kwa sababu kwa programu ile tumeshawenza kuwaondoa zaidi ya watoto 500 katika ajira mbaya na watoto hawa tumewarudisha mashulen. Lakini pia familia wanazotoka wale watoto, tumeziwezesha kwa sababu tatizo kubwa ni kwamba mtoto anapokwenda kutafuta kazi au ajira, maana yake kule nyumbani hana hata hela ya kununua daftari ukiacha kwamba familia pia haina chakula.

Kwa hiyo, mradi huu umeweza kuwezesha familia zenyne watoto hawa pamoja na kuwaondoa mashambani au katika hizo ajira mbaya na kuwarudisha mashulen. Hatujawafuatilia, labda ambacho angetushauri tuwafuatilie watoto hawa tuone wamefikia kiwango gani cha elimu, siyo ajabu wengine sasa wanaelekea Chuo Kikuu. Kwa hiyo, ni mradi mzuri na Mheshimiwa Mbunge naomba asichoke nao. Tunaendelea nao na sasa hivi tunaendelea kwa ufadhili wa Serikali ya Brazil.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwalimu na sipendi kugongewa kengele ya pili, naomba nimalize kipindi kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Najua sikuweza kumaliza hoja zote, lakini naomba Waheshimiwa Wabunge katika bajeti hii tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba kaguzi mahali pa kazi zinafanyika kwa ustadi, kwa ufasaha na hii itatusaidia kupunguza migogoro ya kazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka. Umetoa hoja na hoja hiyo imeungwa mkono.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 65 – Wizara ya Kazi na Ajira

Kif. 1001 – *Administration and General*.....Sh.3,084,400,000/=

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza. Katika mchango wangu wa maandishi niliongelea suala zima la wafanyakazi wa Kiwanda cha Mtibwa, lakini Waziri amenijibu kwa maana tu ya kuhusu mkataba wa hiari.

Katika suala la wafanyakazi niliongelea juu ya madai ya wastaafu na michango ya *PPF* ambayo mpaka sasa hawajalipwa toka Kiwanda kibinafsishwe. Lakini pia hivi karibuni kuna wafanyakazi 2,000 tunavyoongea wamebadilishiwa ajira kutoka ajira ya msimu kuwa vibarua, maana yake michango ya *NSSF* sasa hawapati. Waziri amesema kwamba atakwenda Mtibwa, namshukuru, lakini kwa sasa hivi kwa hao wafanyakazi ilitakiwa zichukuliwe hatua za haraka. Je, hayuko tayari sasa hivi akiwa hapa hapa Bungeni atume wataalam kutoka Wizarani kwake na ikibidi hata Kamati ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii iende Mtibwa ili kujionea hali hii? Naomba majibu.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifiki akisikia kwamba anakwenda mwenyewe ataridhika zaidi kuliko kutuma wataalam. Basi nitatuma wataalam wakaangalie suala hilo, lakini pia tuna Ofisi zetu za *CMA* pale Morogoro. Kwa hiyo, tutatuma mtaalam mmoja kutoka Makao Makuu ataungana na wa *CMA* pale Morogoro wata-study hilo tatizo na watatusaidia kutoa ushauri.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa kukosa uwajibikaji kwa baadhi ya wafanyakazi nchini kumepelekea wageni kuleta wafanyakazi kutoka nje wakiwemo wahudumu: Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kubadilisha mfumo wa kulipa wafanyakazi, badala ya kuwalipa kwa mwisho wa mwezi walipwe kwa masaa wanayofanya kazi?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama Mheshimiwa Mbunge anazungumzia wafanyakazi wa Serikali, Sekta ya Umma au Wafanyakazi wa Sekta Binafsi. Lakini wafanyakazi wa Sekta Binafsi kuna mikataba ambayo wanalipwa kwa masaa, wengine wanalipwa kwa siku, na wengine wanalipwa kwa wiki na wengine kwa mwezi.

Sasa hili kama ni la Sekta ya Umma hilo liko katika taratibu nyininge za *standing orders*. Hatuwezi tukasema kuanzia leo walipwe kwa saa. Lakini ninachoweza kusema kuhusu uwajibikaji, ni kweli hii ndio inapelekeea kwa kweli wawekezaji wengi wakubali kuchukua watu wa nje hata kwa kazi ndogo na kuwaacha Watanzania kutokana na *attitude* yetu ya kazi. Tunaambiwa kisayansi kwamba sasa hivi mwajiri anapochukua mfanyakazi, anaangalia *skills*. *Skills* zinachukua asilimia 20, lakini uwajibikaji unachukua asilimia 80. Kwa hiyo, hii ni kigezo kwamba Watanzania tunapoingia katika Soko la Afrika Mashariki tuwe macho tuanze kuwajibika zaidi kuliko hii chenga chenga tunayopiga sehemu za kazi.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiiti, ahsante sana. Mimi suala langu ningependa nijibiwe kuhusu wafanyakazi wa *Jambo House, Jambo Plastic*. Tulipokwenda *Jambo Plastic* tuliona watu wale siyo wanadamu. Walikuwa wamevalishwa kaptula, wamevalishwa ndala, wako katika mazingira magumu na wanafanyakazi katika vyombo vya hatari. Mtu mwanamke na mwanamume wote wamevaa kaptula! Mimi naomba kuuliza Wizara hii tulipokwenda pale na badala ya kutatua tatizo wamefukuzwa kazi. Hivi kweli sisi tukiwa tunakwenda kwenye sehemu za kazi ni kuwasaidia au ni kuwaharibia? Maana Idara yetu tulipokwenda, tulipokuwa pale walitueleza matatizo yao na tuka-*sympathize* nao, badala yake, nyuma yake mwenye Kampuni akawafukuza kazi na kuwa-*treat* vibaya. Mimi naomba kuuliza mwisho wa wafanyakazi wa *Jambo Plastic* utakuwaje?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu sehemu moja ya maswali ya Mheshimiwa Mshama kwa sababu hili la kufukuzana kazi liko tayari Mahakamani kwa maana ya *CMA*, hatutaliingilia. Labda nilisemee ilie ambalo ni la kuwa na vifaa stahili vya kufanya kazi. Ni kweli baada ya pale, *OSHA* wamekwenda kufanya ukaguzi wakagundua udhaifu katika vifaa vinavyotakiwa na nguo zinazotakiwa zivaliwe na wale wafanyakazi na wakatoa maelekezo kwa Mwajiri ambaye alirekebisha tatizo hili na wafanyakazi, wakaanza kuvaan nguo na vifaa vinavyohitajika kwa mujibu wa sheria.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi ambao Mheshimiwa Waziri hakunitambua, nillishauri Wizara kuwa karibu sana na kufuatilia hivi vyombo vya fedha kama *TIB* ina fedha nyangi sana ambazo *policy* yake ni kuitisha kwenye *micro finances* kusudi wasaidie *VICOBA* na *SACCOS*. Kwa mfano, awamu ya pili ya mabilioni ya Rais Kikwete, yamepitia kwenye *micro finances* kama vile *PRIDE* kuhakikisha kwamba hizi Taasisi za fedha ambazo zimepewa fedha hizo ifike kila Wilaya na kwa mfano Ngara hatukufaidika na mabilioni ya Rais Kikwete awamu ya kwanza yaliyopita kwenye *NMB*, lakini sasa nimeambiwa zinapita kwenye *micro finances*.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwanza kumtambua Mheshimiwa Ntukamazina, lakini pia naomba niseme ushauri wake tutauchukua Serikalini.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa mara ya kwanza niliibua tuhuma na unyanyasaji mkubwa na ukiukwaji wa wafanyakazi wazawa katika Kampuni ya Simu ya ZANTEL. Lakini pia nilizungumzia suala la wafanyakazi wageni ambao wanaishi kinyume na taratibu na napenda kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani. *Immigration* walikwenda na waliwakamata wafanyakazi 20. Lakini pia kuna taarifa kwamba kuna wafanyakazi nane ambao wanatarajiwa kuingia Jumatatu kutoka nchi za Umoja wa Nchi za Kiarabu, Wafanyakazi watatu ambao watafanyakazi katika *Department ya Marketing*, wafanyakazi wanne kutoka India na mmoja *Atlantic* ambao watafanya kazi katika Huduma kwa Wateja ambapo wafanyakazi wazawa wanazo sifa za kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wafanyakazi wazawa kwa upande wa Zanzibar wamefanya kazi kwa kipindi cha miaka sita bila ya kupatiwa ajira na wanapajaribu kudai haki yao wamekuwa wakitsishwa na wengine kufukuzwa kazi na wafanyakazi hawa ni walinzi ambao wanalinda katika minara ya ZANTEL huko Zanzibar. Je, Mheshimiwa Waziri atachukua hatua gani kukomesha unyanyasaji wa wafanyakazi wazawa katika Kampuni ya Simu ya ZANTEL?

MWENYEKITI: Ufanuzi Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za ZANTEL tunazo na Ofisini tumeshakubaliana kuzifanya kazi. Kwa hiyo, naomba watupe nafasi. (*Makof*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia tatizo la Wafanyakazi katika Mgodi wa Chumvi Uvinza, ambapo nilizungumzia matatizo ya aina mbili. Kuna wafanyakazi ambao walistaafu, lakini kutokana na uzembe wa Wizara zaidi ya miaka sita, madai yao yalikuwa chini ya Wizara hii, lakini hawakuweza kupata majibu. Kwa mujibu wa sheria, imekuwa ngumu kufikisha Mahakamani. Lakini kwa upande wa pili, wafanyakazi ambao wanaendelea kwa maana ya tangu mwaka 1999 baada ya mgodi ule kubinafsishwa, yamekuwepo malalamiko mengi kiasi kwamba mwaka 2007 Waziri Mkuu wakati ule akiambatana na Naibu Waziri walipopita walipewa malalamiko, lakini mpaka sasa hakuna ambacho kimejibiwa, hakuna ambacho kinaendelea. Kwa hiyo, nikawa nimependekeza pengine Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kuwatazama wafanyakazi hawa ili kusudi suala hili lifikie mwisho.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikusikia hiyo sehemu ya kazi vizuri. Lakini kama ni kiwanda cha mtu binafsi, tumeeleza taratibu zinazotakiwa kwamba ni yule mlalamikaji kupeleka malalamiko mahali panapohusika hasa *CMA*. Lakini kama ulivyoomba, naomba basi tulichukue, lakini tuwasiliane zaidi kama unaweza kutupa *documents* zaidi tuweze kulifanya kazi, kuwasaidia waendelee na taratibu za kisheria.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati nilipokuwa nachangia bajeti ya Waziri Mkuu, nilizungumza hii kadhia ya wageni wanaojipenyeza na wanaopenyezwa kufanya kazi Tanzania na ikaonekana dhahiri Wizara yako Mheshimiwa Waziri, Uhamiaji na *TIC* kuna matatizo na inaonekana hakuna *proper co-ordination*, kiasi kwamba watu hawa wanaajiriwa hasa katika Sekta ya Utalii na mahotelii na nikatoa ushahidi wa wafanyakazi 29 ambapo 27 ni wa kigeni na kazi wanafundishwa na wale wale wao wamekuwa pale kama Wanyapara, sasa nilitaka kujua wakati Watanzania wanapata taabu wakienda nje na watu wanaondoka na *PhD* yao wanapewa kazi za kuosha vyombo mahotelini, hapa wanakuja watu hawana elimu yoyote na wanapewa kazi nzuri, watu wetu wanakosa kazi: nataka unifafanilie mtalifanya kazi namna gani suala hili pamoja na hii *co-ordination* ya Uhamiaji na *TIC* na hawa wote ambao wapo nchini sasa hivi waondolewe na kazi hizi wachukue wananchi wa Tanzania?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo limekuja juzi juzi na naomba tulipokee na tunaahidi tutalifanya kazi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi, niliomba kauli ya Serikali kuhusiana na namna iliyoshughulikia masuala ya wafanyakazi wa Kampuni ya Urafiki ambayo matatizo yamedumu kwa zaidi ya miaka kumi na niliomba kauli ya Serikali kwa kuwa kiwanda hiki kilichopo Dar es Salaam kinamilikiwa kwa hisa

asilimia 49 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa masuala haya yana sura mbili. Kuna malalamiko ya wafanyakazi 92 walioachishwa kazi na amezungumzwa vilevile na Mheshimiwa Esther Matiko ambao wanatakiwa kulipwa shilingi bilioni 1.8 na walikwenda Mahakamani wakashinda kesi mara kadhaa pamoja na Serikali kukata rufaa. Lakini kwa miaka kumi mpaka leo hawajalipwa.

Lakini pili, wafanyakazi walioko kwenye kiwanda hivi sasa ambao wana malalamiko ya muda mrefu ya aina nyangi ikiwemo ya kulipwa kima cha mshahara kisichoendana na agizo *GN Notice* ya Serikali ambayo nimeandika kwa kina kwenye maelezo yangu, sasa naomba kauli ya moja kwa moja ya Serikali kwa sababu naeleta malalamiko haya yapo kwenye mamlaka husika na kulikuwa na barabara vilevile ya lkulu ya kuelekeza masuala haya kushughulikiwa na yamalizike. Kwa hiyo, naomba kauli thabiti ya Waziri kuzingatia kwamba humu kuna bilioni 4.5 ambazo zinakwenda kutumikia masuala ya malalamiko. Naomba kauli ya moja kwa moja ya Waziri kuhusiana na namna ambavyo Serikali itamaliza matatizo ya wafanyakazi wa kiwanda cha Urafiki ambayo yanahatarisha uhai wa kiwanda sasa hivi hata uzalishaji wa nguo umesimama kwa muda mrefu sana na hali ya kiwanda ni mbaya sana.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kujua kama hiyo kesi bado inaendelea na yeze anasema hukumu imeshatolewa na Serikali ndiyo hajatimiza waliyoamuliwa. Kwa sababu kama hukumu imetolewa, basi inatakiwa yule ambaye hajatimiziwa akakazie hukumu Mahakama Kuu ya Kazi. Kwa hiyo, mimi naomba nipate hiyo taarifa kusudi tuweze kujua kinachotakiwa, halafu tuchukue hatua stahiki.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi naomba ufanuzi tu. Kwa vile sasa changamoto ya ajira nchini imekuwa ni tatizo na kwamba nchi inasisitizia kwamba angalau ajira zinaweza zikapatikana kwenye sekte binafsi kuliko sekte ya umma na rasmi, naomba kufahamu, baada ya kuwezesha watu wenye ulemavu, Serikali itachukua hatua gani kuweza kushawishi hao waajiri binafsi waweze kuajiri wenye ulemavu ambao sasa hivi wanadharaulika kwa kuonekana kwamba hawawezi kuzalisha?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini iko wazi. Haitakiwi kumbakuwa mfanyakazi kutokana na jinsia, ulemavu, ugonjwa, hata mwenye virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo, kama kuna ubaguzi na umeonekana dhahiri, yule ambaye amebaguliwa apeleke taarifa mahali panapohusika hata kama akileta ofisiini kwetu tutalichukulia hatua.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mheshimiwa Waziri afafanue kwamba hawa *OSHA* ambao tunawatengea fedha leo, hawaoni kuwa mbali ya kutotimiza wajibu wao wa kuhakikisha kwamba mahali pa kazi panakuwa salama, lakini pia wanarudisha nyuma viwango vya bidhaa zinazozalishwa katika viwanda.

Katika Viwanda vidogo vya korosho Mkoani Mtwara, hakuna kabisa vitendea kazi na wanawake wanaofanya kazi katika viwanda hivyo vidogo wanabangua korosho kwa mikono na wote tunatambua mashine zinazotumika bado ni ndogo, kwa hiyo mikono yao inachubuka na sidhani kama wakifika hapa. Kuna mmoja anaweza akathubutu kuwapa mikono, lakini zaidi ya hilo, kwenye viwanda vidogo kunatakiwa kuwe na huduma ya kwanza, hakuna hilo. Lakini lingine pia hakuna hata *mask* kwa sababu wanatumia mitambo fulani ya kuchemsha zile korosho. Hawa *OSHA* hawaoni kwamba wanaturudisha nyuma Mtwara na Mikoa mingine ambapo kuna viwanda?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama tulivyosema na sisi kwamba *OSHA* imekuwa haijapata vitendea kazi vya kutosha kufanya kazi na uwezo wa nguvu kazi. Lakini tumekuwa tukiongeza uwezo huo. Lakini napenda kusema kwamba *OSHA* haijafanya kazi. Nitoe mfano kwa mwaka jana, *OSHA* ilifanya kaguzi 5,312 ambayo ilikuwa karibu asilimia 76 ya lengo lao.

Katika mwaka huu fedha inategemea kufanya kaguzi 7,000 na tunadhani watafikia lengo kutokana na jinsi ambavyo Serikali sasa imeamua kuwasaidia zaidi. Lakini ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo bado wanatakiwa waendelee na kaguzi na moja ya maeneo ambayo tayari

tumeshawapa maagizo waende ni kwenye kiwanda cha korosho cha Mtwara. Mimi naamini baada ya maagizo hayo na baada ya bajeti hii watakwenda wakaangalie kile kiwanda kwa makini, watoe maelekezo ya nini cha kufanya ili wafanyakazi wale wapewe vifaa na nyenzo za kufanya kazi ili wasiathirike kiafya.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa kuna wafanyakazi 40 wenye asili ya kiasia wanaofanya kazi katika kiwanda cha *Jambo Plastic Dar es Salaam* na hawana kibali cha kufanya kazi na wemekuwa na tabia ya kujificha mara Maafisa wa Uhamiaji wanapofika kiwandani hapo, napenda kuja: Je, Wizara ya Kazi na Ajira inatoa kauli gani?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli tunayotoa ni kwamba kama kweli wapo na sio halali waondoke warudi makwao. Lakini ninachosema ni kwamba kaguzi tunafanya, kama mtu amejificha mahali ambapo hatuwezi kuona kama walivyokwenda watu wa Uhamiaji wakashindwa kuwaona, basi naomba tuahidi kwamba tutalifanya kazi hilo suala ili tuweze kugundua. Lakini tunakubali kwamba kweli kuna viwanda ambavyo tumeshapata taarifa na siyo *Simba Plastic* peke yake, ndiyo nasema kama hao watu wapo na hawapo kihalali na hawana vibali wawaondoe warudi makwao.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kuhusu kuwalinda wenyе vipaji maalum, wale vijana wetu ambao ni wengi hapa nchini na wengine wako nchi za nje. Hivi karibuni, mwaka huu kuna msichana mmoja ambaye anajulikana kama Dr. Zairini ambaye alimaliza shahada yake ya kwanza ya Udaktari nchini China na huyu msichana alifaulu vizuri sana akavunja rekodi ya ufaulu, kwamba katika kipindi chote cha miaka mitano alichosoma nchini China hakuna ambaye aliwahi kufikia ufaulu wa zaidi ya asilimia 90 kama ye ye alivyokuwa amefaulu, na matokeo yake wachina wale wameahidi kumsomesha Shahada ya Pili ambazo ni ya Uzamili. Sasa katika marekebisho ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja kwamba italetwa, nilikuwa nauliza: Je, Serikali itakuwa tayari kuzingatia na kuweka kifungu ambacho kitawalinda na kuwatambua na kuwfakiria kipekee vijana wetu wote ambao wana vipaji maalum ili kusudi wasiweze kushawishiwa kwenda nje, hususan madaktari?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunachosema tunafurahi kusikia Watanzania wanapata kazi iwe ndani au nje ya nchi. Lakini pia tunasema zile fani ambazo tunazihitaji kama Udaktari, Uhandisi na nini, tungeomba Watanzania wazalendo wanapomaliza masomo yao warudi waitumikie nchi yao. Kwa hiyo, naomba kwa kupitia Mheshimiwa Wambura kwanza atupelekee pongezi zetu kwa huyo msichana ambaye amefaulu vizuri sana na tunaomba kama akipenda arudi kwa sababu sasa hivi tuna maeneo mengi na tunaboresha maslahi ya wafanyakazi nchini.

MHE. REV. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilijaribu kutoa maoni yangu na kuainisha sababu zinazosababisha tuendelee kuwa maskini na ukizingatia kwamba ajira na kazi ni uti wa mgongo wa Taifa, lakini nilia nisha baadhi ya mambo kwamba kama Taifa tunatakiwa tubadilishe mtazamo kwa sababu tumekuwa na mtazamo hasi. Nikaorodhesha baadhi ya mambo kwamba tunakosa maadili, uaminifu, uwajibikaji, kuheshimu sheria na taratibu sehemu za kazi, kuheshimu haki za raia wengine, kupenda kazi, kupenda kuweka akiba na vitega uchumi, kufanya kazi kwa kiwango cha juu na kutunza muda. Sijapata ufanuzi kwamba kama Wizara ya kazi ina mikakati gani iliyoweka ili kulibadilisha Taifa tuwe na mtazamo chanya namna ya kuleta tija katika Taifa letu.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tungependa tija mahali pa kazi iwepo. Mikakati tuliyonayo kwanza ni kutoa elimu. Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) ni wataalam katika kutoa mafunzo na semina kuhusu masuala ya uwajibikaji ili kuongeza tija. Kwa hiyo, kwa kutumia Shirika hili, kwanza tunawaomba wote ambao ni waajiri waweze kulitumia ili kusaidia kuongeza tija mahali pa kazi. Lakini pili, niseme Watanzania wajenge *attitude* ya kuwjibika. Isiwe ni tabia ya Watanzania kutofanya kazi. Kwa hiyo, tunatakiwa tujenge *attitude*, ndiyo tanatakiwa tujenge kuanzia sisi wenyewe tunapokaa hapa mpaka huko tunapokuwa maofisini tusaidie watu wajenge *attitude* ya kupenda kazi na kukaa mahali pa kazi mpaka saa za mwisho za kazi.

MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua tu, hivi hawa wawekezaji kutoka nchi za nje wakija hapa nchini, mishahara wanajipangia wenyewe au kunakuwa na utaratibu maalum wa kupewa au masharti ya mishahara? Hivi ni kwanini Serikali inashindwa kuwaambia wawekezaji kama hawawezi kulipa kwango maalum kwa mfano kima cha chini cha laki tatu na nusu, waondoke? Mfano mdogo ni hawa wawekezaji wenye kuchimba dhahabu, walipokuja nchini, dhahabu ilikuwa dola 250 kwa *ounce*. Leo ni dola 1,600 na ushahe, mpaka leo mishahara ni ile ile. Hivi Serikali inasema nini kuhusu hilo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Zungu kwamba pale ambapo tija ni kubwa kwa maana kwamba faida inapatikana, basi na wafanyakazi waweze kufaidika na ndiyo maana katika suala la vima vya chini vya mishahara tumeweka Bodi mbalimbali za kisekta. Lakini Bodi hizi ziko kisekta zaidi kuliko kusema ziwe kwa maana ya kwamba mwekezaji kutoka nje au mwekezaji kutoka ndani. Kwa hiyo, zimepangwa kisekta. Kama ni Sekta ya Madini, Sekta ya Mawasiliano, Sekta ya Ujenzi na kadha wa kadha. Ninaamini baada ya bajeti hii, hizi Bodi za kisekta zitakapoanza kukaa na kuangalia upya kima cha chini cha mishahara, basi tutaona Sekta ya Madini ambayo hasa ndiyo ameigusia, inaweka kwango gani cha chini cha mshahara na kwa sababu wadau watahusishwa, tunaamini kima kitakachowekwa kitakuwa ambacho kinakidhi haja.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Moja ya kazi za Wizara hii ni kuratibu programu mbalimbali za kukuza ajira hususan ile ya kukuza ajira kwa vijana. Nilipochangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, nilifanua kwa kina kabisa na nikaainisha mpaka mifano ya nchi za wenzetu namna ambavyo wameweza kutengeneza programu mahsus za kukuza ajira kwa vijana, lakini vilevile kutenga bajeti mahsus katika programu hizo. Sasa niliomba pia na sisi kwenye bajeti yetu tufanye hivyo lakini kinachonisikitisha ni kwamba hapa tumetengwa *zero budget* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Ni kwanini programu hii haijatengewa fedha yoyote?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua zamani Wizara hii ilikuwa inahusisha pia vijana. Kwa hiyo, kipengele hiki kimehamishiwa katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ndiyo Wizara ambayo vijana wanatengewa bajeti. Lakini sisi tunayo ya *employment creation* na tuna milioni 136.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye michango yangu yote ya kuongea na wa maandishi, nilichangia kuhusiana na wafanyakazi wa *Barrick* kuhusu afya zao kwamba hawapewi stahiki ya posho kama wanavyopewa wageni na inasemekana kwamba katika shughuli za uchimbaji wa madini wanaathirika kiafyu kutohana na zile *chemicals* wanazotumia kitu ambacho wanapelekea kuharibika kwa mapafu kutohana na ile *crystalline silica* lakini vilevile wafanyakazi hawa hufanya kazi kwa muda mrefu na inasemekana kwamba wanapata kitu kinachoitwa *spinal stenosis*, kitu ambacho kwa wafanyakazi wa kiume kinasababisha kushindwa hata kushiriki tendo la ndoa na inasababisha pia wanapewa talaka na wake zao. Nauliza Wizara husika je, inautaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wale wanachekiwa afya zao ili kujua kwamba wameathirika na kazi zile wanazofanya au la?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther athari nyingine hizi unazifahamuje? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda athari nyingine nitashindwa kujibu, lakini niseme kwa ufupi kwamba, suala la *Barrick* kwanza limechukua sura ambayo kuna timu kubwa ya mazingira ambayo imeshakwenda kule na ambayo imeshaleta ripoti yake na inaangalia mambo mengi pamoja na athari ambazo wafanyakazi wanazipata pale na sisi ripoti ile ambayo imeshakuja tunaipitia ili sisi twende kama Wizara na kuangalia kwa ujumla matatizo ambayo yako pale *Barrick* kwa maana ya masuala ya kazi, lakini vilevile na hayo masuala ya mazingira na afya za wafanyakazi katika maeneo ya kazi. Nadhani baada ya pale, tutaona sasa tunashauriana vipi tukiwa na wataalam wa afya na hawa wa *OSHA*. Mimi nadhani hili tutalishughulikia mara moja baada ya Bunge.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nzega naomba niseme tu kwamba hususan vijana ambao wamejithidi sana kujielimisha

katika hizi *vocation training institutes* kama VETA ya Shinyanga ili waweze kuwa ma-operator wa mitambo mbalimbali katika mgodi na bahati mbaya sana pamoja na kujikusuru kwa kile kidogo walichanacho kwenda kupata elimu ya ufundi ili waweze kupata ajira, wamekuwa hawapati ajira katika mgodi ule na matokeo yake wamekuwa ni watazamaji wa mgodi ambao upo katika eneo lao.

Katika historia ya ule mgodi wakati Serikali inakuja kuwashawishi wananchi wa Nzega kwamba mgodi uwekezwe katika eneo lao, iliwaambia kwamba watafaidika kwa kupata ajira. Lakini bahati mbaya sana mpaka leo hii ni Wananzega chini ya 100 ambao wamewahi kuajiriwa katika mgodi wa uchimbaji dhahabu wa *Resolute*. Sasa Serikali inatoa tamko gani ili niweze kwenda kuwaambia ndugu zangu Wananzega ambao wametumia muda wao na *resources* zao kujelimisha katika fani mbalimbali za ufundi ili waweze kupata ajira na ambazo hawazipati mpaka leo hii?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi kumwamulia mwekezaji binafsi aajiri au amwajiri nani, *unless* ni katika masuala ya ubaguzi ambayo tunasema kisheria hayatakiwi. Lakini kama ni suala la kuajiri, yeye anaangalia ni nani atakayeleta tija? Ni nani ambaye ana *skills* zile ambazo anazihitaji? Kwa hiyo, ninachowea kusema na kuwashauri hao vijana waendelee kutafuta maeneo mengine ambayo wanawenza wakaajiriwa kwa zile *study* ambazo wamejelimisha nazo au wao wenye wakajinga katika kikundi, basi wakatafuta mahali labda na Mheshimiwa Mbunge akawasaidia wakajajiri wao wenye.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Wakati nachangia hoja ya Waziri kwa maandishi nilimwomba sana Waziri kuja na mpango mbadala ambao utawawezesha watoto ambao ni chini ya miaka 18 wasiendelee kuajiriwa, nikimaanisha kwamba watoto hawa, wengi wao huwa wanakwenda kwenye ajira za kufanya kazi au biashara kwa sababu ya hali duni sana iliyopo katika familia zao. Wengi wao wamefiwa na wazazi wao wawili, kwa hiyo, wanaishi na babu zao au bibi. Kwa hiyo, inawalazimu kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba Serikari au Waziri aje na mpango mbadala ambao utawasaidia zaidi hao watoto kiuchumi.

NAIBU WAZIRI KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwaiposa, Mbunge niliyemgawia Jimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sidhani kwamba kuna mpango mbadala unaoweza kushinda sheria ambayo ipo, kwa maana ya sheria ya kazi na mahusiano kazini kama tulivyosema mtoto wa chini ya miaka 14 haruhusiwi kufanya kazi, hata yule wa miaka 18 katika kifungu cha tano cha sheria hiyo. Kuna maeneo kama mashambani, migodni ambapo haruhusiwi vile vile kufanya kazi. Jambo la msingi hapa ni kusisitiza utekelezaji wa sheria ile na kufanya kaguzi ili kugundua wale wanaokiuka sheria hii na hatua kuchukuliwa. Kwa hiyo, ninachowea kumuahidi, sisi kama Wizara ni kuendelea kufanya kaguzi hizi. Kama anayo maeneo hasa ambayo ameyalenga, basi atupatie tufanye kaguzi ili tuchukue hatua zinazotakiwa.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Vijana wengi wa Vyuo Vikuu wanapomaliza masomo yao wanakosa ajira kwa kuwa kuna kipengele kinachosema kwamba uzoefu kazini, na wanafunzi wengi wanakuwa hawana uzoefu kazini. Hiki kipengele kwa watumishi wa umma kingefutwa, maana yake hata Mawaziri na Wabunge hatuna kipengele kinachosema kwamba tuwe na uzoefu. Tunaingia Bungeni na unapata Uwaziri bila uzoefu. Sasa watoto wanatoka chuoni, wanakaa nje miaka mitano bila kazi. Wanapata wapi uzoefu?

MWENYEKITI: Hilo ni swali la siku ya leo. Waziri, majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba suala la uzoefu kama anavyosema Mheshimiwa Kessy limekuwa tatizo na hasa unapozungumzia uzoefu wa muda mrefu. Kwa hiyo, sisi kama Wizara na kwa kweli kuna maelekezo hata kutoka kwa Rais kwamba tuwe na mawasiliano na Chama cha Waajiri ambao tunao hapa, ili waajiri kwanza wazingatia kwamba kuna wahitimmo wanaomaliza vyuoni na wanatakiwa waajiriwe moja kwa

moja. Kwa hiyo, pale hakuna cha uzoefu. Lakini hata kazi za *middle senior officers*, basi uzoefu huo usiwe mkubwa kiasi cha kuzuia vijana wetu kukosa ajira kutokana tu na kwamba wameweka uzoefu wa 10, au miaka 20 wakati ambapo watu wanataka ku-retire.

Kwa hiyo, mimi nadhani nitaendelea kulisimamia hili. Nami nachukua nafasi hii kuwaomba waajiri kuzingatia hilo kwamba wakubali vijana wetu wapate uzoefu wakiwa kazini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nami naongeza kwamba uzoefu ni muhimu, wapiga kura 2015 mwachague Wabunge hawa hawa, maana yake wana uzoefu tayari. (*Kicheko*)

MHE. ABDULLAH JUMA ABDULLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na Naibu Waziri, lakini kwa nafasi ya pekee nimpongeze Dkt. Dau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia sana suala la vijana. Vijana ni Taifa la kesho. Tusipowaandaa leo vijana hawa, tutatengeneza Taifa maskini. Je, Serikali ina mpango gani katika kuwaandaa vijana hawa ili waweze kutumia raslimali zilizopo vijiji ili waweze kujiajiri wenye?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba, tumeeleza na hata katika ufanuzi nimejithidi kueleza kwamba tumetambua hilo. Lakini tumetambua pia kwamba kuna changamoto kutokana na vijana kutokuwa na *study zinazotakiwa*. Kwa sababu tunapozungumzia nguvukazi ya vijana ni kuanzia Darasa la Saba, wanaomaliza *Form Four na Form Six* na Elimu ya Juu, wanatofautiana. Hizo tofauti pia ni changamoto. Kwa hiyo, Serikali tunachotaka kufanya ni kutambua uwezo na *study mbalimbali* za hawa vijana na tunesema tunaanzisha programu ya miaka mitano ambayo tutawasaidia kupata *study* za ujasiriamali kutokana na maeneo yao, kwa maeneo yele ambayo ni rahisi kupata ajira, eneo la mifugo, kilimo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa tumeanza hiyo hatua ya utekelezaji wa programu hii, naomba vijana wajitokeze, lakini tutaomba pia wawe katika vikundi ambavyo wengine wameshaanzisha. Kwa hiyo, ni juu ya vijana wenye vijana uhalali wa kujitafutia kazi au kujiajiri lakini pia kutumia fursa hizi ambazo Serikali inaandaa.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilikuwa nataka kuongelea suala la likizo ya uzazi kwa akina mama ambapo kwa sheria hii iliyopo, inasema angalau mama kama atajifungua mtoto mmoja, basi apate angalau siku 84 kama likizo ya uzazi. Lakini kwa kuwa malezi ya mtoto yanategemea sana pia uwepo wa Baba: Je, sasa Wizara haioni umuhimu sasa kuifanyia marekebisho sheria hii ili basi iweze kuwafanya na akina baba waweze kupata likizo ndefu ya *maternity* ili waweze kulea pamoja wale watoto. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Opulukwa pamoja na vijana ambaa bado wanapata watoto, nijibu kwamba kwa mujibu wa kifungu Na. 33 ambayo inampa likizo ya uzazi mama aliyezaa, kifungu kinachofuata cha 34, kweli kimetoa siku tatu tu kwa baba na hizo siku tatu azichukue ndani ya siku saba za mkewe kujifungua. Anachosema ni kwamba, siku tatu hizo ni chache ziongozwe. Sisi hatuna matatizo, kama tutakubaliana turudishe hiyo sheria ili tuongeze siku hapa, lakini mimi nadhani kilichoangaliwa hapa ilikuwa ni kipindi hicho cha wiki ya kwanza ndiyo kwa kweli wazazi wote wawili wanahitajika kutoa huduma. Baada ya pale, mama anaanza kuwa sasa katika hali ambayo angalau baba anaweza akaenda kazini na kuweza kupata ujira wa kumsaidia hata huyu mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wote watakaa tu nyumbani kwa muda mrefu, inaweza ikawa shida kidogo.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuendeleza suala lililokwisha sasa hivi. Nilikuwa naomba kufahamu Wizara inawasaidia vipi wanawake katika kutunza watoto baada ya kujifungua kwa sababu mwongozo wa Wizara ya Afya unasema kwamba mtoto anyonye mfulululizo miezi sita bila kula kitu kingine chochote. Wanawake walio wengi wanafanya kazi mbali na makazi yao. Wanawake hawa wanasaidiwa

vipi ili waweze kunyonyesha watoto wao kwa mfululizo wa miezi sita bila kuwapa kitu chochote watoto hao?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira bado inasimamia tu Sheria ile ya Kazi na Mahusiano Kazini ambayo ndani yake kuna suala la likizo kuhakikisha kwamba kweli likizo inatolewa kwa mama na ile ya baba. Lakini kuhusu hilo analolisema sasa kwamba wapate sasa msaada, Sheria inachosema ni kwamba Mwajiri atamruhusu Mwajiriwa kunyonyesha mtoto wakati wa saa za kazi kwa wastani wa saa mbili kwa siku, lakini kwa madhumuni ya kifungu hiki, cheti cha Daktari anayekubaliwa na mwajiri kukubalika hatakuwepo pasipo sababu ya msingi. Kwa hiyo, kuna masuala ya kisheria hapa ambayo akipata cheti cha Daktari basi anaweza kupata huduma ya mwajiri, lakini siyo ya Serikali kama Serikali ni mwajiri.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu, nilizungumzia tatizo zima la ukosefu wa uadilifu katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ni sekta muhimu sana katika kuisadia Serikali kukabiliana na tatizo kubwa la changamoto ya ukosefu wa ajira hapa nchini, lakini wawekezaji wengi wa ndani lakini vile vile pia hata wawekezaji ambao wametoka nje wamekuwa wakitumia kisingizio cha ukosefu wa uaminifu katika maeneo ya kazi kwa sisi Watanzania kama moja ya sababu ya kutukosesha ajira vijana wengi na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, Wizara hii imefanya jitihada gani katika kuhakikisha kwamba inajua uzito na ukweli wa tuhuma hizi ili kupata majibu mawili? Kwanza, kama ni kweli kuhakikisha kwamba inarudi nyuma na kututahadharisha sisi vijana ili wakati tunalalamikia tatizo la ajira, lakini tujue na sisi tuna wajibu kwenye hizo ajira. Pili, kama siyo kweli, basi hao wawekezaji wasitumie kisingizio cha kuweza kutudhalilisha sisi na kuleta wafanyakazi kutoka nje kwa ajili ya kufanyakazi ambazo zingeweza kufanywa na Watanzania. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili suala analouliza Mheshimiwa Mayenga limejibowi mara nyingi hapa. Tumesisitiza kwamba ni kweli tunahitaji Watanzania tuwajibike, tuwe waaminifu, tuchape kazi kwa bidii ili tuweze kushindana katika utandawazi na hasa kwenye hii *regionalisation* ambayo sasa tunakwenda kwenye Afrika Mashariki na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge ameuliza kwamba kama ni kweli, vijana waweze kupewa huo ukweli. Mimi ningeweza tu kurudia maneno yake kwamba vijana wa Kitanzania tuwajibike, tufanye kazi ili tuweze kushindana. Kusema kwamba siyo kweli, hii imethibitishwa kwa sababu hata wakati wa *interview panel* ambapo Watanzania na wenye wapo wameshuhudia Watanzania wenzao wakishindwa *interview* kutokana na kutowajibika na kutoweza kujibu maswali, lakini vile vile, wale wanaochukuliwa wameonekana wameshindwa kazi kwenye maeneo. Kwa hiyo, natoa wito kwamba Watanzania vijana tuchape kazi kwa kuwajibika kwa bidii na tusiwe wadokozi.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2000 kiwanda cha Sukari Kilombero kilibinafsishwa na wakati wa zoezi la mchakato kuna baadhi ya wafanyakazi walipunguzwa lakini mpaka leo bado hawajapata stahili zao;

Ningependa kupata kauli ya Serikali, ni lini wafanyakazi hao watapata stahili zao?

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo rahisi kutoa ufanuzi katika suala ambalo tunalisikia kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, lakini kama tungeletewa mazingira mazima ya hilo suala, basi tungeweza kujua ni sheria ipi imevunjwa na kumlazimisha mwajiri kupitia vyombo vyaa sheria viliviyowekwa, aweze kuwalipa hawa wafanyakazi stahili zao. Kwa hiyo, tunaomba tupate maelezo ya ziada kuhusiana na suala hilo la wafanyakazi wa Kilombero.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, aasante. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa NSSF kwa kazi nzuri wanayofanya katika kujenga majengo

mengi hapa nchini. Lakini pia katika mchango wangu, nilizungumzia ni namna gani vijana wengi wanakimbilia Mijini kwa ajili ya kwenda kutafuta ajira. Labda mimi niwasemee vijana wa Mkao wangu wa Singida kwamba: Je, sasa Waziri pamoja na Mkurugenzi Mkuu NSSF mnawenza sasa kutuletea jengo zuri sana kubwa pale Singida kwa ajili ya wawekezaji wengi ambao wameshaonyesha nia ya kuja kuwekeza katika Mkao wa Singida ili kuwafanya vijana wote wa Mkao wa Singida waweze kupata ajira Mkoani kwao Singida? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlata, kwanza nikupongeze kwa vazi lako zuri, na mimi nitamwomba Mheshimiwa Malima anitafutie kanzu. (*Kicheko*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mlata kama ifuatavyo:-

Kama tunavyofahamu, Shirika hili la NSSF linaweka fedha kwa ajili ya wanachama wake, na pale inapobidi wanawekeza. Kwa hiyo, linawekeza kwa kupata faida. Kwa kuwa Mkurugenzi wa NSSF yupo, basi atawatuma watu wake wafanye utafiti, wataangalia kama kweli wakiwekeza Singida hawataweza kupoteza fedha ya wanachama wao. Hilo ndilo linaloweza kumwambia. Lakini kama itaonekana haiwezekani, naomba Mheshimiwa Mbunge asipate matumaini sana.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Kwa kuwa leo wanachama Wabunge ambao ni ma-champion wa uzazi salama, walikutana na Wakunga na wakafahamishwa sababu ambazo zinawafanya kushindwa kutoa huduma yao vizuri, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na uwezekano wa kufanya kazi katika kigezo cha ILO cha Mkunga mmoja kuhudumia mtu mmoja, na kwa kuwa jambo hili linasababisha vifo vingi nya akina mama pamoja na watoto, kuna haja ya kufanya haraka sana kuwezesha wakunga wengine kuititia Vyuo na kadhalika.

Je, Waziri haoni kwamba ni vyema akaishauri Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba Wakunga wanasomeshwa bure ili kupata Wakunga wengi zaidi na katika vyuo husika?

NAIBU WAZIRI, KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani wazo lake linaweza likatafakariwa na Serikali na hasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu kuona kwamba: Je, sera hii inawezekana? Kama itakuwa hivyo, basi tutaleta hapa ndani ili turidhie.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo. Kwanza kabisa naishukuru Wizara na Serikali kwa kuanza kuona umuhimu wa kulipa pensheni kwa wazee wetu wote katika nchi yetu ya Tanzania. Suala hilo linaungwa mkono sana na Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme jambo moja, Kamati yangu katika kufanya kazi na Wizara hii, hakika imekuwa ikipata shida kubwa sana moja, na shida hiyo ni migogoro isiyokwisha ya upatikanji wa haki za wafanyakazi katika sekta binafsi na maeneo mengi ya namna hiyo. Natambua kazi nzuri inayofanywa na CMA, imekuwa ikitoa hukumu za mashauri mbalimbali katika viwanda na maeneo mbalimbali ya kazi. Lakini utekelezaji wa hukumu hizo umekuwa ukitumia hata miaka kumi wananchi wetu wanyonge wa Tanzania hawapati haki zao.

Nini nafasi ya Wizara katika kusimamia maamuzi ambayo yamekwishaamuliwa na CMA na hayatekelezeki miaka kumi, miaka ishirini na Watanzania wanaendelea kupata shida katika maeneo hayo ya ajira. Naomba kufahamu nafasi ya Wizara katika kusimamia jambo hilo ili tuwaokoe hawa Watanzania wanyonge wasiokuwa na mtu wa kuwatetea miaka hiyo yote wanapoumia katika ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba maelezo.

NAIBU WAZIRI KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, concern ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ni nzito kama alivyoitao, lakini niseme tu kwamba jambo la msingi sana hapa ni sheria. Kama yule ambaye hukumu imekubaliwa ama katika ngazi ya usuluhishi ama ngazi ya maamuzi na upande mmoja haujatekeleza, inatakiwa mara moja ndani ya muda uliowekwa kwenda

kukazia ile hukumu kwenye Mahakama ya kazi. Tatizo ni kwamba watu wengine wanakuwa wazito, unachelewa kwenda kukazia hukumu, mimi nadhani ni suala la elimu. Watu wajue haki zao, sheria inasemaje na ikishafika kwenye Mahakama ya kazi ni suala sasa la kisheria na ambalo sasa litafuata mkondo wa kawaida wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani suala ni kufuata sheria na kutoa elimu.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge 40 walismama kutaka kuzungumza katika kipindi hiki. Waziri majibu ya nyongeza.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ninukuu sheria hii ambayo inahusu Tume ya Usuluhishi na Uamuvi ambayo ilianzishwa na Bunge lako Tukufu chini ya Sheria za Taasisi za Kazi Kifungu Na. 15 kinasema kwamba, Tume itakuwa (i) Idara huru ya Serikali na (ii) Katika kutekeleza kazi zake, haitakuwa chini ya mwongozo na udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote (iii) haihusiani na chama chochote cha siasa, chama cha Wafanyakazi, shirkisho la Vyama vya Wafanyakazi au Jumuiya ya Waajiri. Kwa maana hiyo, Wizara kama Serikali haitawenza kuingilia maamuzi yoyote yaliyotolewa na CMA kwa sababu zamani CMA ilikuwa chini ya Wizara na ilikuwa chini ya Wizara kwa sheria ya zamani ya usalama kazini ambayo ilikuwa inaruhusu Serikali au Waziri kuweza kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya sheria hii ambayo nimeisoma, kwamba sheria mpya sasa inakwenda kisheria, haimruhusu Waziri, Naibu Katibu Mkuu au mtu yeoyote kwenda kushughulikia migogoro nje ya utaratibu huu uliowekwa ambaa unaanza CMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilifikiri hili tulielewe na sheria hii sasa imetafsiriwa Kiswahili na nafikiri Wizara ya Kazi ndiyo imekuwa ya kwanza kutafsiri sheria katika Kiswahili. Tunazipitisha kwa wafanyakazi sasa hivi tumeshafundisha Mikoa mingi, tunaelimisha wafanyakazi ili waweze kujua taratibu hizi za kutafuta haki zao bila kufikiri kwamba wanawenza kupitia kwa Waziri akamuamuru Mwajiri akafunga kiwanda na akawaamuru wafanyakazi waliofukuzwa ambaa wameandamana isivyo halali kwamba warudi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili ni muhimu.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kama nilivyosema, walismama Wabunge 40, Wabunge 30 tumejitahidi wameweza kupata nafasi na Wabunge kumi hawakupata nafasi. Mtapata nafasi wakati mwingine na wakati hauko upande wetu. Katibu tunaingia katika utaratibu wa *guillotine*.

Kif.1002 <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 237,718,000/=
Kif.1003 <i>Policy and Planning</i>	Sh. 331,838,000/=
Kif.1004 <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 109,682,000/=
Kif.1005 <i>Procurement Mgt Unit</i>	Sh. 296,706,000/=
Kif.1006 <i>Information, Education Comm. Unit</i>	Sh. 113,520,000/=
Kif.2001 <i>Labour</i>	Sh. 6,711,892,000/=
Kif.2002 <i>Employment Division</i>	Sh.1,188,238,000/=
Kif.2003 <i>Registrar of Trade Unions</i>	Sh. 130,117,000/=
Kif.5001 <i>Youth Development</i>	Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 15 - TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI

Kif. 1001 *Administration and General*.. Sh. 1,810,280,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 15 - TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI

Kif. 1001 *Administration and General...* Sh. 1,004,500,000/=

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 65 - WIZARA YA KAZI NA AJIRA

Kif. 1001 *Admnistration and General...* Sh. 275,000,000/=

Kif.1003 *Policy and Planning.....* Sh.5,084,920,000/=

Kif.2001 *Labour.....* Sh. 144,000,000/=

Kif.2002 *Employment Division.....* Sh. 440,955,000/=

Kif.5001 *Youth Development.....* Sh. 0

(*Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilitrudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kazi na Ajira ya mwaka 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofii*)

(*Hoja illitolewa iamuliwe*)

(*Hoja illamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, yalipitishwa na Bunge*)

NAIBU SPIKA: Nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa, na tunawatakia kila la kheri Wizara hii ya Kazi na Ajira katika utekelezaji wa bajeti hii vizuri katika mwaka ujao wa fedha.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo madogo tu ya kuwakumbusha ambayo nilitangaza tangu asubuhi, kwamba kesho saa 4.30 asubuhi katika ukumbi wa Msekwa kutakuwa na Semina ya Wabunge wote kuhusiana na masuala ya UKIMWI, saa 9.00 jioni kutakuwa na mechi za mpira wa miguu na *netball* katika uwanja wetu wa Jamhuri. Tunaomba Wabunge wote na wananchi wa Dodoma, mnakaribishwa uwanja wa Jamhuri kwenye mechi kati ya Bunge na *British Council*, lakini vile vile saa 1.00 jioni kesho katika viwanja vyetu vya Bunge kutakuwa na tafrija nzito kabisa ambayo imeandaliwa na ndugu zetu wa *British Council* kwetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, saa tatu asubuhi.

(*Saa 12.28 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 9 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi*)